*Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

**BUNGE LA TANZANIA**

______________

**MAJADILIANO YA BUNGE**

_________________

**MKUTANO WA KUMI NA TATU**

**Kikao cha Kumi – Tarehe 8 Novemba, 2013**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua*

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati ifuatayo iliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:**

Taarifa ya Mwaka ya Chuo Kikuu cha Dodoma kwa Mwaka 2011/2012 (*The Annual Report of The University of Dodoma for the Financial Year 2011/2012).*

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 107

**Kuzipatia Majengo Shule za Msingi za Kamukole na Ruzila**

**MHE. JASSON S. RWEIKIZA** aliuliza:-

Katika Kata ya Rukoma iliyopo Bukoba kuna Shule za Msingi za Kumukole na Ruzila ambazo zimesajiliwa, zina wanafunzi na zinapatiwa Mitihani ya Taifa lakini hazina hata jengo moja na badala yake zina mabanda machache yaliyojengwa kwa miti na kuezekwa kwa nyasi:-

*Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

*[MHE. J. S. RWEIKIZA]*

(a) Je, Serikali haioni kwamba hali hii ni aibu na hatari kwa watoto?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuzipatia majengo shule hizi?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jasson Samson Rweikiza, Mbunge wa Bukoba Vijijini, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia. Hivyo, Serikali huwa inaweka bajeti kila mwaka ya fedha na inapeleka fedha za ruzuku ya maendeleo kwenye Halmashauri kila mwaka na kuziachia Halmashauri zenyewe kupanga matumizi yake kutokana na vipaumbele vyao, Elimu ikiwa mojawapo.

Mheshimiwa Spika, Shule za Msingi Kamukole na Ruzila ni shule zilizoanzishwa kutokana na kuwasaidia Wananchi wa Kata ya Rukoma, ambao ni jamii ya wakulima na wafugaji wa kuhamahama. Mpaka sasa Shule ya Kumukole ina jumla ya wanafunzi 195 na Shule ya Ruzila ina jumla ya wanafunzi 255. Shule zote zina vyumba vya madarasa vitano na upungufu wa vyumba vya madarasa manane. Aidha, kupitia fedha za ruzuku ya maendeleo kwa upande wa Elimu, Halmashauri ya Wilaya ya Bukoba ilipata jumla ya shilingi milioni 442.5 kuanzia Mwaka wa Fedha wa 2010/11 hadi 2012/13 na Mwaka wa Fedha wa 2013/14 zimetengwa jumla ya shilingi milioni 169 kwa ajili ya ukarabati, ujenzi na maendeleo ya Elimu.

Mheshimiwa Spika, Shule hizi kupitia fedha za maendeleo, kwa Mwaka wa Fedha wa 2010/11 hadi 2012/13, zilepelekewa jumla ya shilingi milioni 48.4. Kwa Mwaka wa Fedha wa 2013/14, Halmashauri imetenga shilingi milioni 11.6 kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya shule hizi.

**MHE. JASSON S. RWEIKIZA:** Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Waziri, lakini pamoja na matatizo mbalimbali tunayopata katika Sekta ya Elimu, kuna Kata nyingine inaitwa Kata ya Kemondo, pale Kemondo umekuwa mji na watu wengi na kuna shule moja ya msingi inaitwa Kemondo, ina wanafunzi wengi sana, waliorundikana madarasani na shule nafasi haitoshi.

Wananchi wamejitahidi wamechanga changa wameanzisha shule nyingine jirani inaitwa Omujure, wameiomba Halmashauri isaidie kujenga Shule hii ili ipunguze msongamano Shule ya Komondo, lakini hawajapata majawabu wala msaada wowote.

Je, Serikali haioni kwamba ni muda mwafaka sasa na hao Wananchi wa Kemondo wakasaidiwa ili Shule ya Omujure nayo isajiliwe na kujengwa?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Rweikiza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyotangulia kusema kwamba, kazi ya Serikali Kuu ni kuzipelekea pesa Halmashauri na Halmashauri zenyewe zinapanga kufuatana na kipaumbele chao. Kwa hiyo, ninachomwomba Mheshimiwa Mbunge, ashirikiane na Halmashauri yake, kuona umuhimu wa kupeleka pesa katika Shule ya Kemondo. Kwa sababu sisi kama Serikali Kuu hatuwezi kupanga kila shule ipate kiasi gani, wajibu wetu ni kupeleka pesa tu katika Halmashauri, Halmashauri yenyewe ndiyo inapanga.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa Serikali hupeleka fedha za ujenzi kwenye Halmashauri kwa uwiano. Je, kama kuna Halmashuri ambazo Wananchi wanakusanya nguvu zao na kujenga

majengo mengi, Serikali itakuwa tayari kumalizia hayo majengo yote bila kujali uwiano?

**SPIKA:** Bila kujali nini?

**MHE. DIANA M. CHILOLO**: Bila kujali kile kiwango kinachopelekwa kwenye Halmashauri.

**SPIKA:** *Okay,* ahsante. Mheshimiwa Waziri wa Nchi!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Diana Chilolo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nadhani sisi wenyewe humu ndiyo tunaopanga hizo bajeti na vigezo vya kugawana pesa kwa kila Halmashauri tumepanga wenyewe. Kwa hiyo, kama Serikali, hatuwezi tukafanya maamuzi hayo, isipokuwa kama Bunge litapendekeza kwamba sasa hivi tusiangalie uwiano, tupeleke tu kulingana na mtu anavyofanya kazi, nadhani tutatekeleza.

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

Kumekuwa na jitihada kubwa sana kwa Wananchi kujitolea kujenga shule hizi, lakini kuna tatizo la kupata usajili wa shule hizi za msingi; kwa mfano, katika Kata ya Kipatimu pale Shule ya Msingi Ngingama, Nambuju kule Mkarango pamoja na Manzese pale Somanga, wanaomba maombi ya kusajili hizi shule lakini kunakuwa na masharti magumu yanayotolewa na Viongozi wa Wilaya na Mkoa kuweza kupatiwa usajili.

Nini tamko la Serikali katika usajili wa Shule za Msingi?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, imegawa vipeperushi na imeainisha kabisa sifa za usajili wa

*Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*



shule za msingi na sekondari kwa Halmashauri zote na kwa watu binafsi wanaoanzisha shule. Sifa hizo ni pamoja na kuwa na majengo ya kutosheleza. Kama ni *hostel* basi mabweni hayo yawe ya watoto wa kike na wa kiume. Vilevile kuwe na maabara, majengo ya maktaba, vitabu na walimu wenye sifa.

Mheshimiwa Spika, akishakamilisha sifa hizo, Mheshimiwa Mangungu, alete tu maombi yake tuone kama ana sifa ili tuweze kusajili shule hizo.

**MHE. MWIGULU L. N. MADELU:** Mheshimiwa Spika, nilitaka kuuliza swali ambalo ameuliza Mheshimiwa Mangungu.

**SPIKA**: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na swali linalofuata ambalo litaulizwa na Mheshimiwa Herbert Mntangi.

Na. 108

**Fedha Zilizochukuliwa Kutoka Akaunti za Shule za Vijiji**

**MHE. HERBERT J. MNTANGI** aliuliza:-

Mwaka 2011 Benki Kuu ya Tanzania iliagiza kufungwa na kuchukuliwa kwa fedha kutoka Akaunti za Shule za Msingi na Serikali za Vijijini ambazo zilikuwa hazitumiki kwa muda mrefu:-

(a) Je, ni kiasi gani kimechukuliwa Kitaifa na kwa Wilaya ya Muheza?

(b) Kwa kuwa fedha hizo zilikuwa kwa ajili ya Ujenzi wa Madarasa na Nyumba za Walimu. Je, kuna utaratibu gani wa kuzirudisha na mwongozo na ushauri wa matumizi yake ukoje?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Herbert J. Mntangi, Mbunge wa Muheza, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, mwezi Oktoba, 2010, jumla ya Akaunti za Shule za Msingi 10,511 zilizokuwa katika Matawi ya *NMB* kote nchini, zenye kiasi cha shilingi bilioni 1.1 zilifungwa na fedha zake kurejeshwa Benki Kuu. Uamuzi wa kufungwa kwa Akaunti hizi ulifikiwa baada ya kutofanya kazi kwa muda mrefu. Hivyo, jumla ya Akaunti za Shule za Msingi za Serikali 186 katika Wilaya ya Muheza, zenye kiasi cha shilingi milioni 21.2 zilifungwa katika zoezi hilo.

(b) Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, baadhi ya akaunti zilikuwa na fedha kwa ajili ya ujenzi wa madarasa na nyumba za walimu. Kwa kuwa akaunti hizo zilikuwa na fedha ambazo hazikufanyiwa kazi iliyopangwa kwa muda mrefu, fedha hizo zilirejeshwa Benki Kuu ya Tanzania, *Commercial Bank Dormant*. Jukumu la kuzifufua akaunti hizo lipo chini ya Afisa Masuuli wa Halmashauri husika. Kwa akaunti ambazo zilifungwa zikiwa na fedha na kuhamishiwa Benki Kuu, urejeshwaji wa fedha hizo zinaombewa kibali kwa Katibu Mkuu Wizara ya Fedha ili ziweze kukamilisha kazi iliyokusudiwa.

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Spika, ninayo maswali mawili madogo ya nyongeza kama ifuatavyo:-

(i) Kwa nini usiwepo utaratibu mzuri wa kutoa notisi kabla ya akaunti hizo na fedha hizo kuchukuliwa kutoka katika Serikali hizo za Vijiji?

(ii) Ningependa kufahamu; hapa takwimu inaonesha kwamba, zilikuwepo shilingi bilioni 1.1. Je, fedha hizo bado zipo katika akaunti hizo ili kuwezesha sasa Halmashauri kuomba kibali cha kurejeshewa fedha hizo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Mntangi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, pesa ambazo zilifungwa na kurejeshwa Benki Kuu, zilikuwa zimekaa kwa zaidi ya miaka mitatu bila kutumika. Sasa kama mtu alikaa zaidi ya miaka mitatu bila kutumia fedha, nadhani ukimpa notisi sasa unampa azitumie kwa kitu chochote kile, mradi tu ameziondoa katika akaunti ile. Ndiyo maana Serikali ilifanya maamuzi ya kuzichukua ili pale watakapokuwa tayari, waweze kurejeshewa fedha hizo. Kwa hiyo, utaratibu upo, fedha hizo zipo, kibali kikiombwa pesa zitawezwa kurejeshwa.

**MHE. RIZIKI OMAR JUMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa Serikali imeweka kila Halmashauri kuwa na akaunti sita tu, jambo ambalo kumekuwa na matatizo katika matumizi ya fedha za Mfuko wa *CDCF*. Je, ni lini Mfuko wa *CDCF* utakuwa na akaunti yake ili kuondoa Upinzani huu uliopo?

**SPIKA**: *CDCF* tena, haya!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Riziki Omar Juma, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli ni utaratibu wa Serikali kuanzisha hizo akaunti sita na lengo ni kuhakikisha kwamba tunadhibiti matumizi ya fedha za Serikali. Mimi ni Mbunge pia, ninao huo Mfuko wa *CDCF* kwenye Halmashauri yangu na hakuna utata wowote ambao unazuia fedha zisitumike kwa sababu ya akaunti sita. Labda Mheshimiwa Mbunge hakueleza ni tatizo la aina gani, lakini hakuna tatizo lolote

*Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

na sasa hivi ndiyo tunaweza kudhibiti zaidi kuliko tulivyokuwa na akaunti zaidi ya 34.

**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED:** Mheshimiwa Spika, nataka nitofautiane kidogo na Mheshimiwa Waziri; tatizo ni kwamba, fedha zile zinaingia katika akaunti ya fedha za miradi ya maendeleo na hapo ndiyo *loophole* ambapo Watendaji wa Halmashauri wanazitumia fedha zile kwa kuzipanga wao wenyewe, kitu ambacho ni kukinzana na Sheria ya Mfuko ule. Mfuko ule una Sheria zake tofauti.

Je, ni lini Mfuko ule utakuwa na akaunti yake tofauti?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Rajab, kama ifuatavyo:-

Mfuko wenyewe unaitwa Mfuko wa Kuchochea Mendeleo. Sasa sioni kama kuna tatizo kuingizwa fedha hizo kwenye Akaunti ya Miradi ya Maendeleo na katika Mfumo wa *EPICA 9.05.*

Labda nimwombe Mheshimiwa aje pale TAMISEMI ajielimishe, aone mfumo unavyofanya kazi. Pamoja na kwamba, zote zinaingia katika akaunti moja, kila matumizi yana *item* yake, kwa hiyo, nimwombe tu Mheshimiwa aje tumwelimishe.

Waheshimiwa Wabunge hapa ni mashahidi, waniambie kama kuna Mbunge ambaye ameshindwa kutoa pesa yake kwenye akaunti kwa sababu ya kuwa na akaunti sita; nadhani iletwe tutalifanyia kazi.

Na.109

**Uvamizi wa Msitu Kansay na Kambi ya Faru**

**MHE. MCH. ISRAEL Y. NATSE** aliuliza:-

Watu wachache walivamia Msitu wa Kijiji cha Kansay na Kambi ya Faru na kufungua mashamba ambayo yameharibu msitu huo. Wanakijiji walidai watu hao kuachia Msitu wao kwa muda mrefu bila mafanikio hadi walipoamua kujichukulia sheria mkononi kwa kufyeka mahindi yote na kubomoa makazi yao, jambo ambalo pia ni ukiukwaji wa Haki za Binadamu hata kama kuna upungufu:-

Je, Serikali inawaambia nini Wananchi wa Kijiji cha Kansay, Kambi ya Faru na Watanzania kwa ujumla kuhusu hali hiyo ambayo sasa imekuwa jambo la kawaida karibu kila mahali?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mch. Israel Yohana Natse, Mbunge wa Karatu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Msitu wa Jamii katika Kijiji cha Kansay ni sehemu ya Msitu wa Jamii ambao upo katika Vijiji vya Buger, Kansay, Ayalaliyo na Kambi ya Faru, ambao una ukubwa wa hekta 750.8, kufuatana na upimaji wa mipaka ya vijiji uliofanyika mwaka 1997, ambao ulibainisha mipaka ya misitu uliotengwa tangu mwaka 1936, enzi za Ukoloni. Msitu huu ni muhimu sana kwa hifadhi ya vyanzo vya maji na hifadhi ya mazingira.

Mheshimiwa Spika, uvamizi wa Msitu huu ulianza mwaka 1987 na wavamizi walichukua hatua mbalimbali za kisheria, ikiwa ni kutozwa faini na kijiji na kuamriwa kuondoka katika msitu huo na kwenda kwenye maeneo yao ya halali ambayo walipewa na kijiji. Baada ya kuondoka, wavamizi hao walianza kurudi tena kimya kimya na kuanza kulima na

kujenga makazi ambapo waliitwa katika Ofisi ya Kijiji na kutozwa faini na kuamriwa tena kuondoka mwaka 2003 kwa kutumia Sheria Ndogo ya Kijiji ya Mazingira.

Mheshimiwa Spika, wavamizi waliokaidi walipelekwa katika Mahakama ya Mwanzo Endabash, ambapo kijiji kilishinda kesi, wavamizi walikata rufaa Mahakama ya Wilaya ya Mbulu na kushinda kesi. Baada ya hukumu, Kijiji kilikata rufaa Mahakama Kuu Arusha, ambapo kesi hiyo inaendelea kusikilizwa tangu mwaka 2005 hadi sasa bila hukumu kutolewa.

Mheshimiwa Spika, Wananchi wanaendelea kulinda na kufanya doria ya mara kwa mara katika maeneo ya Misitu ya Kansay na Kambi ya Faru, kwa kushirikiana na Hifadhi ya Ziwa Manyara, kuhakikisha kuwa wavamizi hawaendelei kufanya shughuli yoyote katika maeneo ya msitu.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kesi inayohusu wavamizi katika Msitu wa Kansay ipo katika Mahakama Kuu Arusha, nawaomba Wananchi wavute subira kungojea hukumu hiyo.

**MHE. MCH. ISRAEL Y. NATSE:** Mheshimiwa Spika, nina maswali madogo mawili ya nyongeza.

(i) Ni wazi kwamba karibu kila mahali sasa kuna migogoro na migogoro hii inanishawishi niamini kwamba, Serikali ndiyo kiini cha migogoro hii yote inayotendeka; kwa sababu tangu mgogoro unaanza kidogokidogo Serikali haichukui hatua mpaka inafikia mahali Wananchi wananchukua Sheria mkononi. Je, Serikali inatoa kauli gani kuhusu migogoro yote inayoendelea kwa kukaa kimya bila kuchukua hatua? *(Makofi)*

(ii) Kama Waziri alivyojibu, kesi ipo Mahakamani tangu mwaka 2005 hadi leo bila hukumu kutolewa na Wananchi wanaendelea kupata matatizo. Serikali inatoa

kauli gani kwa vyombo vyetu vya sheria kuweza kutoa hukumu mara moja bila Wananchi kuteseka?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Natse, kama ifuatavyo:-

Wakati najibu swali, nimeelezea historia ya mgogoro; mara ya kwanza wavamizi walivyoingia, Serikali ya Kijiji iliend a ikawaondoa. Wakaingia kwa mara ya pili, Serikali ya Kijiji ikawatoza faini. Wakavamia tena, Serikali ikawapeleka Mahakamani na sasa hivi tunavyozungumza, Serikali ya Kijiji kwa kushirikiana na Mamlaka ya Hifadhi ya Ziwa Manyara, inaendelea kulinda eneo hilo. Ndiyo kusema kwamba, Serikali haijakaa kimya hata kidogo, hata Serikali ya Kijiji ni Serikali, Halmashauri ni Serikali, nao Hifadhi ya Manyara ni sehemu ya Serikali.

Kwa hiyo, suala kwamba tumekaa kimya mpaka Wananchi wanajichukulia hatua siyo la kweli, tumekatazwa kusema ni uongo, siyo la kweli kwa sababu mwenyewe ni shahidi kwamba, hatua zinachukiliwa na hata tunapozungumza hilo eneo linaendelea kulindwa.

Mheshimiwa Spika, suala la Mahakama siwezi kulitolea kauli, lakini nina imani kabisa kwamba wanasikia na nina imani kabisa kwamba hukumu itatolewa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mchungaji Mwanjale; leo Wachungaji tu.

**MHE. MCH. LUCKSON N. MWANJALE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi. Nauliza swali moja dogo.

Kwa kuwa vijiji vingi vinazungukwa na misitu; je, Serikali ina mpango gani wa kusaidia kuwapatia bonasi ili waweze kuitunza hii misitu?

**SPIKA**: Umelielewa swali au arudie?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mchungaji Luckson Mwanjale, kama ifuatavyo:-

Vijiji vyote vinavyozunguka katika hifadhi za misitu na hata hifadhi ya wanyama, upo utaratibu ambao huwa wanapata gawio lao kila mwaka. Pia upo utaratibu wa ujirani mwema ambao zile hifadhi huwa zinasaidia Vijiji ambavyo vinawazunguka.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Kwa kuwa tatizo la Misitu limekuwa kubwa ambalo ni pamoja na Msitu wa Kazimzumbwi ulioko Kisarawe ambako kuna uharibifu mkubwa sana watu wamevamia. Serikali inasemaje kuhusu kuuokoa ule Msitu?

**SPIKA**: Mheshimiwa Waziri wa Nchi, sijui unafahamu?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mchungaji Msigwa, kama ifuatavyo:-

Kweli tunayo matatizo katika Misitu yetu na ndiyo maana Serikali ili kuhakikisha inanusuru Misitu hiyo, imechukua hatua ya kuanzisha Wakala wa Misitu. Lengo ni kuhakikisha misitu hiyo inalindwa, ukiwepo Msitu wa Kazimzumbwi, Mkoa umechukua hatua na Wakala wa Misitu nao unachukua hatua.

**SPIKA**: Ahsante, ngoja twende Wizara ya Katiba na Sheria. Mheshimiwa Rosweeter Kasikila, atauliza swali hilo.

Na. 110

**Mashauri ya Ukatili Dhidi ya Wanawake, Watoto na Walemavu**

**MHE. ROSWEETER F. KASIKILA** aliuliza:-

Kumekuwepo na matukio mengi ya ukatili dhidi ya Wanawake, Watoto na Walemavu wa Ngozi:-

(a) Je, ni mashauri mangapi ya ukatili huo yamepelekwa Mahakamani?

(b) Je, ni mashauri mangapi yamepatiwa ufumbuzi?

(c) Je, ni watu wangapi wamefungwa kwa kufanya ukatili huo?

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Roseeter F. Kasikila, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c), kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, makosa yatokanayo na ukatili dhidi ya wanawake na unyanyasaji wa watoto, husajiliwa Mahakamani kama makosa mengine ya jinai. Hivyo, hakuna mfumo mahususi uliopo wa kuyasajili pekee na hivyo kupata takwimu sahihi.

Mheshimiwa Spika, jumla ya matukio 60 ya mauaji na kujeruhiwa kwa watu wenye ulemavu wa ngozi, yameripotiwa katika vituo mbalimbali vya polisi nchi nzima tangu mwaka 2007. Kati ya mashauri hayo, 35 yalifikishwa Mahakamani na 25 watuhumiwa hawajakamatwa hadi sasa. Kati ya mashauri 35 yaliyofikishwa Mahakamani, ni mashauri 12 ambayo yanaendelea kusikilizwa katika Mahakama mbalimbali, mashauri 9 yamemalizika na washtakiwa kuhukumiwa adhabu mbalimbali na mashauri

*Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

14 yaliyosalia yaliondolewa Mahakamani kwa kukosa ushahidi.

Mheshimiwa Spika, napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba, Serikali itaendelea kuchukua hatua thabiti za kupambana na matukio ya ukatili dhidi ya Wanawake, Watoto na Watu wenye ulemavu wa ngozi, ikiwa ni pamoja na kuwakamata na kuwafikisha Mahakamani na kushughulikiwa kwa mujibu wa Sheria.

**MHE. ROSWEETER F. KASIKILA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana.

Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri na takwimu nzuri hizi alizotupa, inaonesha kwamba, kazi ya kuwafuatilia hawa wakatili inafanyika.

(i) Sasa swali langu ni kwamba, je, Serikali haioni kwamba, ni bora Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora iendelee kutoa taarifa ya kila mwaka ya kuonesha ni jinsi gani udhibiti unafanyika tuweze kujua kama tatizo linaendelea, linapungua au liko palepale?

(ii) Imekuwa ni dhahiri kwamba, hawa watu wenye ulemavu wa ngozi hasa watoto ndiyo waathirika zaidi. Je, Serikali haioni kwamba ni vyema ikawatengea Kijiji ambacho wataishi hapo waweze kupata huduma mbalimbali za kijamii na ili waweze kupata ulinzi madhubuti?

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA**: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Roseeter Kasikila, kama ifuatavyo:-

Kwanza kabisa, Tume ya Utawala Bora na Haki za Binadamu, imekuwa ikitoa elimu kwa umma, kuelimisha jamii kuepukana na vitendo vya ukiukaji wa haki za binadamu. Pia nimwelimishe Mheshimiwa Mbunge kuwa, katika mwaka huu ni matukio matatu tu ambayo yaliripotiwa ya ukatili dhidi ya *albino* yaliyotokea Tabora na Sumbawanga. Kwa

*Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

hiyo, utaona kwamba, hatuwezi kusema tunavikubali vitendo, lakini hatua zinachukuliwa na ndiyo maana wimbi hili kidogo limeanza kupungua.

Kuhusiana na swali lake la pili, kwamba, Serikali haioni kuna haja ya kutenga kijiji maalum cha kuweka watoto hawa wenye matatizo ya ulemavu wa ngozi, lakini pia ili kuhakikisha kwamba wanapata ulinzi. Kwanza kabisa, siyo sahihi kutenganisha watoto hawa na familia zao, lakini pindi inapobidi Serikali imekuwa ikichukua hatua na wapo watoto ambao wamekuwa wakitafutiwa sehemu maalum kwa ajili ya hifadhi na kupewa ulinzi maalum inapohitajika.

**MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba niulize swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa ukatili dhidi ya walemavu wa ngozi umekuwa ukiendelea mwaka hadi mwaka; na kwa kuwa adhabu ya kifo bado ipo; na kwa kuwa kulitolewa hukumu ya baadhi ya watu ambao wamefanya ukatili dhidi ya walemavu wa ngozi, hukumu ya kifo:-

Je, watu hawa hukumu ile wamepatiwa au haijatolewa hadi leo na kama haijatolewa hatuoni kama ukatili dhidi ya watu ambao wana ulemavu wa ngozi utazidi kuendelea? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Kombo Khamis Kombo, kama ifuatavyo:-

Adhabu ya kifo bado ipo na napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa, hadi hivi sasa takribani watuhumiwa wanane wamehukumiwa adhabu ya kunyongwa hadi kifo. Ahsante.

**SPIKA**: Mheshimiwa Silinde, aaah ngoja, hapana hapana; Mheshimiwa Barwany, nimefanya upendeleo mnisamehe.

**MHE. SALUM K. BARWANY:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa upendeleo maalum ambao umenipa.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri, anatuambia hapa kwamba, kwa mujibu wa maelezo yake bado mwendelezo wa mauaji ya *albino* yanaendelea katika Taifa letu. Amesema kwamba ni walemavu wa ngozi watatu tu ambao wameripotiwa kuuawa katika nchi hii. Je, Serikali haoni kwamba, bado mauaji ya *albino* yanaendelea kufanyika katika nchi hii hata kama Mheshimiwa Waziri ametuambia kwamba ni watatu tu? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Barwany, kama ifuatavyo:-

Sijasema ni matatu tu, kana kwamba hatutambui; kwa takwimu ambazo zipo hadi hivi sasa kwa matukio ambayo yameripotiwa katika mwaka huu kuanzia mwezi Januari, ni matukio matatu na tumechukua hatua. Katika matukio hayo, moja lilikuwa linamhusisha Maria Chavanenge, lingine lilikuwa linamhusisha Mwingulu Matonange na lingine lilikuwa linamhusisha Lugololo Bunzali. Hayo ndiyo matukio ambayo tunayo hivi sasa na tunachukua hatua.

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. Kwa kuwa swali la msingi lilikuwa linaelezea ukatili kwa wanawake, watoto na walemavu wa ngozi. Nilitaka nifahamu kwamba, dhana ya kupiga wanawake vijijini imekuwa kubwa na ukatili kwa wanawake vijijini si tu katika kupiga pekee, vilevile umekuwepo ukatili wa namna ya kurithi mali.

Sasa nilitaka Serikali itueleze ni mkakati gani maalum wa kuwasaidia wanawake vijijini waweze kufahamu haki zao na kupata haki zao kama ilivyo katika maeneo ya mjini? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Silinde, kama ifuatavyo:-

Kwanza kabisa, nipende tu kusema kwa niaba ya Serikali, tunakemea vitendo vyote vya unyanyasaji dhidi ya wanawake, vipigo na kwa yeyote mwenye taarifa ya vitendo vya aina hii, kwa mujibu wa Katiba yetu na kwa mujibu wa Sheria za nchi, anatakiwa kutoa taarifa. Ukiwa unashuhudia vitendo vya aina hii vinatokea na ukakaa kimya na wewe unashiriki katika kitendo hicho. Kwa hiyo, nitoe tu rai kwa Watanzania wote ambao wamekuwa wakiona ndugu zao, jamaa na majirani wakifanyiwa vitendo vya aina hii, waweze kutoa taarifa katika vyombo vya dola ili Sheria iweze kuchukua mkondo wake.

Kuhusiana na elimu kiasi ambayo tumetoa kwa wanawake vijijini, niseme tu kwamba, tulikuwa tukijitahidi kutoa elimu kwa wanawake vijijini, lakini pia kwa wanawake wa mjini. Hivi sasa kupitia Mfuko wa Huduma za Msaada wa Kisheria *(Legal Service Facility),* tumekuwa tukiongeza fedha katika Mashirika yanayotoa huduma za msaada wa kisheria ili yaweze kufika mijini na vijijini. Pia tumejitahidi kuongeza idadi ya takribani Mashirika mbalimbali ya wasaidizi wa kisheria kama 84 ili waweze kufikia sehemu mbalimbali ambazo hatuwezi kuzifikia.

Na. 111

**Kutokomeza Vifo vya Watoto Wachanga**

**MHE. LETICIA M. NYERERE** aliuliza:-

Ripoti ya Shirika la Afya Duniani *(WHO)* kupitia *Global Action Report* imedhihirisha kuwa kati ya watoto kumi wanaozaliwa kabla ya wakati, mtoto mmoja hupoteza maisha kwa kukosa huduma na kinga stahiki:-

(a) Je, Serikali inachukua hatua na tahadhari gani kutokomeza vifo vya watoto hao?

*[MHE. L. M. NYERERE]*

(b) Je, Serikali inatumia utaratibu gani wa kutekeleza maamuzi ya kimataifa ikiwemo kulinda haki na kuepusha vifo vya watoto?

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Leticia M. Nyerere, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, kati ya watoto kumi wanaozaliwa kabla ya wakati, mtoto mmoja hupoteza maisha kwa kukosa huduma na kinga stahiki. Kulingana na takwimu za mwaka 2010, matatizo ya kuzaliwa kabla ya wakati, yanachangia kwa asilimia 25 ya vifo vya watoto wachanga.

Kutokana na takwimu hizi, Wizara inafanya juhudi kubwa katika kutokomeza vifo vya watoto wachanga kwa kuanzisha huduma ya matunzo ya mtoto mchanga kwa kumbeba kifuani ngozi-kwa-ngozi *(Kangaroo Method*). Huduma hii inapunguza vifo na imeanzishwa katika Hospitali zote za Mikoa na baadhi ya Hospitali za Wilaya na Vituo vya Afya vipatavyo 35 hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kutekeleza afua mbalimbali za kupunguza vifo vya watoto wachanga, ikiwa ni pamoja na kuboresha mwongozo wa jinsi ya kuwahudumia watoto wachanga na kuokoa maisha yao kwa kutekeleza "Huduma Muhimu kwa Mtoto Mchanga" *(Essential Newborn Care Package).*

Miongozo mingine ya matibabu kwa watoto imeboreshwa ili kuwapatia watoa huduma, elimu na ujuzi unaoendana na miongozo ya Shirika la Afya Duniani kama matibabu ya mtoto anayeharisha kwa kutumia *ORS* na vidonge vya *Zink*, ulishaji na unyonyeshaji kwa mtoto aliyezaliwa na mama mwenye maambukizi ya VVU, na kuhakikisha upatikanaji na matumizi ya dawa kutibu nimonia ya *amoxicilini*.

Matarajio ya Wizara ni kuhakikisha mtoto anapatiwa haki zake na huduma stahiki ili aendelee kuishi na kukua vizuri.

**MHE. LETICIA M. NYERERE:** Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Waziri, kwa majibu yake, pamoja na kwamba hayalengi maandalizi ya uhai wa mtoto kabla hajazaliwa. Tatizo la vifo kwa watoto wachanga limekuwa kubwa sana nchini hususan Kwimba. Kufuatana na tatizo hili lilivyo, ningependekeza Serikali ilete mpango madhubuti wa kutatua tatizo hilo. Ili kufanya hivyo, kuna mambo ya kuzingatia yafuatayo:-

Nchi zilizoendelea na hata zinazoendelea, zimekuwa na mpango unaitwa *Special Supplimental Nutrition Program*. Programu hii humuwezesha mama mjamzito...

**SPIKA:** Wanasema swali na siyo kuhutubia.

**MHE. LETICIA M. NYERERE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunikumbusha.

Ninachosema, Serikali sasa ianze mpango huo wa kuhakikisha akina mama wajawazito na watoto wa chini ya miezi sita wapatiwe lishe stahiki. Kwa hiyo, tuanze mpango madhubuti na tuanze kampeni madhubuti itakayoitwa UHURU WA MTOTO KWANZA, badala ya KILIMO KWANZA. *(Kicheko)*

Swali la pili, kulingana na uzito wa tatizo hili, ninamwomba Mheshimiwa Waziri aongozane na mimi twende mpaka *Clinic* ya Ngudu, afanye tathmini, hatimaye Serikali ije na mpango madhubuti ili iweze kutatua tatizo hili. Ahsante sana. *(Kicheko/Makofi)*

**SPIKA**: Ahsante. Lakini si mmeamka, kawaamsheni, vizuri. *(Kicheko)*

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Leticia M. Nyerere, kama ifuatavyo:-

Swali lilihusu huduma kwa watoto wanaozaliwa kabla ya muda na ndiyo maana tukatoa majibu yanayohusu watoto wachanga. Laiti kama Mheshimiwa Mbunge angeuliza kuhusu maandalizi wakati wa ujauzito, pia tungempa majibu sahihi. *(Makofi)*

Tunatambua umuhimu wa lishe bora wakati wa ujauzito pamoja na mtoto anapozaliwa, tunatambua kwamba, akina mama wajawazito wanatakiwa wasivute sigara na wala wasitumie pombe kwa wingi. Yote hayo hupelekea watoto kuzaliwa kabla ya wakati. Kwa hiyo, maelezo hayo tunayo na mikakati ipo, siyo kwamba hatuna. Kuhusu utaratibu gani unaotumika kuwasaidia watoto hawa wanaoitwa Njiti; mikakati mikuu ndiyo hiyo miwili niliyoisema. Moja, ni kumbeba mtoto ngozi kwa ngozi (*Kangaroo Method);* imeonekana ina faida kubwa na kwa maana hiyo, tumeanza kutekeleza nchi nzima kama nilivyosema Mikoa yote na tutaendelea kusambaza katika vituo vyote vya afya.

Pili, kuna mkakati wa kumsaidia mtoto kupumua, huo nao umetolewa mafunzo yake kwa watoa huduma na haya mambo mawili ndiyo yanayosaidia kwa kiwango kikubwa kupunguza vifo vya watoto wachanga. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge nataka tu nikwambie kwamba, Wizara inatambua na mikakati ipo na tunafanya kila juhudi ili kupunguza vifo vya watoto wachanga.

Swali la pili, kuhusu kufuatana na Mheshimiwa Mbunge kwenda katika maeneo anayoyazungumzia; nataka niseme tu kwamba, nitakuwa tayari kufanya hivyo. Nimweleze Mheshimiwa Mbunge kwamba, tunatambua na takwimu tunazo za maeneo yote ambayo yana vifo vingi vya watoto, ili mikakati iweze kuchukuliwa hususan katika maeneo hayo kwanza kabla ya kuisambaza nchi nzima. *(Kicheko)*

**MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa hawa watoto wachanga wanakabiliwa pia na tatizo la utapiamlo, wengine wanazaliwa wakiwa na uzito pungufu na wanapokaa hospitali wanakuwa *discharged* kurudi nyumbani na wengi wanatoka vijijini. Je, Serikali imeweka utaratibu gani wa kuhakikisha wanawafuatilia na kuweka mpango wa nuru kwenye ngazi ya kijiji, kuhakikisha hawa watoto uzito unaongezeka na wanaepukana na utapiamlo na tukizingatia kwamba Mkoa wa Iringa na Mkoa wa Njombe ni moja ya mikoa ambayo inakabiliwa na tatizo la utapiamlo?

**SPIKA:** Swali!

**MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O:** Mheshimiwa Spika, KILIMO KWANZA halafu lishe inafuatia ili tuwe na chakula cha uhakika lazima tuzingatie KILIMO KWANZA.

**SPIKA:** Hakuna swali, umejibu mwenyewe! Haya Mheshimiwa Waziri!

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, moja ya tatizo kubwa katika nchi yetu linalowakabili watoto ni la utapiamlo. Takwimu zinaonesha bado tatizo la utapiamlo ni kubwa sana, karibu asilimia 40 mpaka 45 ya watoto wamedumaa. Kwa maana hiyo, kuna kila sababu ya kufanya juhudi za ziada ili kuondoa tatizo hili katika nchi yetu. Hivi tunavyozungumza ni kwamba, tumeanzisha kada ya Maafisa Lishe katika ngazi za Halmashauri.

Nia na madhumuni ni kuwafanya Maafisa Lishe hawa waweze kutoa elimu, waweze kuwapa elimu Wananchi katika ngazi ya jamii ili hatimaye wajawazito na

watoto wachanga, waweze kupata lishe bora, tuondokane na tatizo hili kubwa la kudumaa na utapiamlo katika nchi yetu. *(Makofi)*

Na. 112

**Viashiria vya Maradhi ya Ukoma**

**MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS** aliuliza:-

(a) Je, ni viashiria aina gani vinavyoweza kumfanya mwanamke kujua kwamba ameathirika na maradhi ya ukoma?

(b) Je, kuna watoto wangapi hapa nchini ambao wameathirika na maradhi hayo?

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Fakharia Shomar Khamis, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ukoma ni ugonjwa wa kuambukiza unaosababishwa na vimelea vya bakteria ambavyo hushambulia mishipa ya fahamu na ngozi. Dalili kuu ni pamoja na kuwa na baka au mabaka kwenye ngozi, ambayo hayana hisia ya mguso na wakati mwingine huambatana na gazi kwenye mikono na miguu.

Ukoma huambukizwa kwa njia ya hewa toka kwa mgonjwa ambaye hajagundulika na kuanza tiba. Inachukua muda wa miaka mitano hadi 20 toka kuambukizwa hadi kuanza kujitokeza kwa dalili za awali. Mtu aliyeanza matibabu ya ukoma hata akiwa ana ulemavu hawezi kumwambukiza mwingine. Takwimu zinaonesha kuwa, miongoni mwa wagonjwa wapya, wanawake ni kati ya asilimia 30 hadi 40. Katika kipindi cha 2008 hadi 2013, jumla ya wagonjwa wapya wa ukoma 13,025 waligunduliwa na kuanza matibabu. Kati yao, wanawake

ni 5,185, sawa na asilimia 39.8 na wanaume ni 7,840, sawa na asilimia 60.2.

(b) Mheshimiwa Spika, idadi ya watoto wanaogunduliwa, kutibiwa na kupona ukoma kila mwaka inaendelea kupungua. Takwimu tulizonazo zinaonesha kuwa, mwaka kila 2012 kulikuwa na watoto 156 nchini waliogunduliwa kuwa na ugonjwa wa ukoma. Uwepo wa watoto wenye ukoma katika jamii, unaashiria uwepo wa maambukizi mapya na kuwa bado kuna watu wenye ugonjwa wa ukoma katika jamii ile ambao hawajaanza matibabu. Utambuzi wa watoto walioathirika na ukoma na kuwaanzishia matibabu mapema ni muhimu ili kuzuia athari za ugonjwa huu.

Wizara yangu inaendelea kuwahimiza na kuwashauri Wananchi kuwa, mara waonapo dalili za ukoma nilizozitaja, wafike kwenye vituo vya huduma ya afya kwa ajili ya uchunguzi na tiba sahihi. Napenda kusisitiza kuwa, ukoma unatibika na dawa zipo kwenye vituo vyetu vyote vya huduma za afya na hutolewa bila malipo.

**MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, ambayo yametoa darasa tosha kwa Watanzania wote. Nina maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

(i) Kwa kuwa ugonjwa wa ukoma unawapata vilevile watoto wadogo ambao kwa mfano wanaoishi katika jamii ambayo inazunguka maradhi hayo lakini wao wenyewe, jamii ile kwa kutokujitambua na baadaye watoto nao hupata athari hiyo. Je, Mheshimiwa Waziri umetoa darasa gani kwa jamii kama hizo ili kuzisaidia watoto wasipate maradhi hayo? *(Makofi)*

(ii) Ningelipenda kujua ni nchi gani ambayo ilipata Maradhi ya UKIMWI kwa mara ya kwanza duniani kabla ya nchi nyingine?

**SPIKA:** Ukimwi, ukoma?

**MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS:** Samahani Mheshimiwa Spika, ukoma.

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Fakharia, kama ifuatavyo:-

Kama nilivyoeleza katika jibu langu la msingi, ni kwamba, dalili za ukoma zipo wazi sana, ni dalili ambazo kutambuliwa kwake ni rahisi. Moja, ni mabaka yasiyokuwa na hisia ya mguso katika ngozi; na la pili ni kushambuliwa kwa mishipa ya fahamu na hivyo hukua na kuwa minene zaidi kuliko ilivyo kawaida. Kwa maana hiyo, kunapoonekana dalili kama hizo, ni wajibu wa mhusika pamoja na jamii inayomzunguka, kuhakikisha kwamba, wanampeleka katika vituo vya kutolea huduma za afya ili aweze kupata matibabu.

Wafanyakazi wa sekta ya afya katika ngazi za zahanati na katika ngazi za jamii, wanatakiwa kuendelea kutoa elimu kwa jamii juu ya dalili za ukoma. Nadhani mtakumbuka kwamba, tunapoadhimisha Siku ya Ukoma Duniani, mtaona kuna vipeperushi vinavyotolewa vikiwa vina picha zinazoonesha dalili za ukoma na husambazwa katika jamii.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwamba ni nchi gani iliyoanza kupata maradhi haya kabla ya nchi nyingine, jibu la swali hili kwa sasa sina; lakini nataka nimweleze Mheshimiwa Mbunge kwamba, nitalitafuta na naweza nikampatia baadaye.

**SPIKA:** Hizi mnasoma kutoka kwenye Vitabu Vitakatifu toka enzi hizo. Mheshimiwa Sabreena!

**MHE. SABREENA HAMZA SUNGURA:** Mheshimwia Spika, ahsante. Kwa kuwa hali ya Kituo cha Ukoma Mkoani Tanga ni mbaya; je, Serikali ina mkakati gani wa kuboresha Kituo hiki?

**SPIKA:** Maswali mazuri, Mheshimiwa Waziri umesikia, Kituo cha Tanga?

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Sabreena Sungura, kama ifuatavyo:-

Tatizo la ukoma kama nilivyosema katika jibu langu la msingi, bado lipo nchini mwetu, lakini linapungua na takwimu zipo ninazoonesha kupungua kwake. Haitoshi kupungua kwake tukaacha, ni muhimu tukahakikisha yale maeneo ambayo bado tatizo hili lipo; kwa mfano, kwa sasa Wilaya inayoongoza ni Liwale, karibu asilimia kumi ya wagonjwa wa ukoma nchini mwetu wanapatikana katika Wilaya ya Liwale.

Kwa hiyo, bado juhudi za makusudi lazima zichukuliwe ikiwemo kama anavyouliza Mheshimiwa Mbunge kwamba, Mkoa wa Tanga uweze kushughulikiwa kwa makusudi kabisa, nguvu za ziada zipelekwe ili kuweza kupambana na ugonjwa huu. Kwa hivyo, ninachoweza kumweleza Mheshimiwa Mbunge ni kwamba, tutaendelea kuongeza juhudi katika Mikoa na Wilaya ambazo tatizo hili bado ni kubwa ili kuweza kuutokomeza ugonjwa huu.

**SPIKA:** Alichotaka kusema, sijui kuna kituo cha wakoma pale Tanga ambacho kipo katika hali mbaya.

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, samahani, sikuwa nimelisikia vizuri swali hilo, lakini kama anazungumzia vituo vinavyohudumia walemavu wa ukoma; vituo hivyo vipo vingi na lazima nikiri kwamba, siyo vyote ambavyo vipo katika hali nzuri na hii inasababishwa na upungufu wa bajeti kwenye Idara ya Ustawi wa Jamii. Tatizo tunalijua, tutaendelea kuongeza bajeti ya Idara ya Ustawi

*Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

wa Jamii ili waweze kutoa huduma bora zaidi na kuvikarabati vituo hivyo.

**SPIKA:** Naomba niendelee muda umeisha; Mheshimiwa Riziki Omar Juma, swali linalofuata!

Na. 113

**Watu Wanaopoteza Maisha kwa Saratani**

**MHE. RIZIKI OMAR JUMA** aliuliza:-

Taarifa kutoka Taasisi ya Saratani ya Ocean Road inasema kuwa wagonjwa 100 kila siku hupoteza maisha nchini kutokana na ugonjwa wa saratani:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kupunguza vifo hivyo kwa Watanzania?

(b) Je, ni lini Serikali itatenga fedha za kutosha ili Taasisi hii iweze kutoa tiba iliyo bora zaidi na sahihi kwa wagonjwa wa saratani?

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Riziki Omar Juma, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, ina mipango mbalimbali ya kupunguza vifo vya Watanzania vinavyotokana na ugonjwa wa saratani. Mipango hiyo ni pamoja na kuiongezea Taasisi ya Saratani ya Ocean Road, uwezo na ufanisi wa kukinga, kufanya uchunguzi, kutibu, kufundisha na kutoa matibabu ya tiba shufaa. Aidha, taasisi itaongezewa uwezo wa kufanya tafiti mbalimbali zenye lengo la kutoa huduma bora ili kupunguza idadi ya vifo.

*Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*


(b) Mheshimiwa Spika, Serikali imeongeza Bajeti ya Maendeleo kwa Taasisi ya Saratani ya Ocean Road kutoka shilingi bilioni 3.8 mwaka 2012/2013 mpaka bilioni 8 mwaka 2013/2014 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa tiba. Bajeti ya Taasisi ya Matumizi ya Kawaida imepanda kutoka shilingi bilioni 1.9 mpaka shilingi bilioni 2.2.

Serikali imeona upungufu wa bajeti ya Taasisi kwa miaka iliyopita na hivyo inaahidi kuendelea kuongeza bajeti hii kila mwaka kadiri Bajeti ya Serikali Kuu itakavyoongezeka, kuiwezesha Taasisi kutoa matibabu yaliyo bora na sahihi kwa wagonjwa wa saratani.

Kutokana na ongezeko la Bajeti ya Maendeleo, Taasisi imeweza kujenga jengo jipya lenye vitanda 250, maabara, vyumba vya matibabu na famasi. Aidha, taasisi imetengewa bajeti kwa ajili ya ununuzi wa kifaa cha kutoa tiba kiitwacho *Linear Accellerator* katika mwaka huu wa fedha.

Taasisi imeendelea kushirikiana na Shirika la Nguvu za *Atomic (IAEA)* kununua vifaa tiba vya *CT Simulator* na *Gamma Camera*.

**MHE. RIZIKI OMAR JUMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili ya nyongeza.

(i) Naomba nimshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake, lakini swali langu la kwanza linasema kwamba; ukiangalia jiografia ya nchi yetu na umaskini ambao wanao Watanzania na kwamba hospitali ambayo inahudumia saratani ni Ocean Road peke yake ambayo ipo Mjini Dar es Salaam. Wananchi ambao wapo vijijini hawawezi kuifikia huduma hiyo kwa haraka sana. Je, hatuoni kwamba, kwa kuiangalia hopitali hiyo moja tu Watanzania wataendelea kupoteza maisha kwa ugonjwa huu? *(Makofi)*

(ii) Siku za zilizopita niliiomba Serikali na nikapewa jibu kwamba ipo katika mipango ya kuanzisha hospitali

angalau za Mkoa kwa ajili ya kutoa huduma hizo za uchunguzi ili maradhi haya yaweze kugundulika angalau *stage* ya awali. Mtanzania mpaka anapofika Dar es Salaam, anakuja Ocean Road kumaliza uhai wake tu kutokana na kukosa huduma hiyo ya mapema. Je, Serikali inaonaje mpango huu wa kuongeza bajeti zaidi ili kuanzisha angalau vituo katika Hospitali za Mikoa Wananchi waweze kupata huduma hizo mapema? *(Makofi)*

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Riziki Juma, kama ifuatavyo:-

Lazima tukiri kwamba, huduma za matibabu na uchunguzi wa saratani katika nchi yetu bado hatujaweza kuzisambaza nchi nzima, lakini hatua zimeanza kuchukuliwa. Zaidi ya Taasisi ya Saratani ya Ocean Road, sasa hivi hata Hospitali ya Rufaa ya Bungando inatoa huduma za saratani. Lengo ni kwenda awamu kwa awamu, tumeanza na hospitali hizi tunazoziita Hospitali za Kanda, tutashuka kwenye Hospitali za Mikoa na hatimaye katika Hospitali za Wilaya. Fedha zinahitajika kwa kazi hiyo na ndiyo maana hatuwezi kufanya kwa wakati mmoja maeneo yote.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la pili kwamba, uchunguzi ufanyike katika maeneo yote; nataka kulieleza Bunge lako Tukufu kwamba, uchunguzi unafanyika; kuna Taasisi mbalimbali zisizo za Kiserikali pamoja na za Serikali. Kwa mfano, Ocean Road wenyewe, huwa wanatoka pale walipo wanakwenda Mikoani na Wilayani kufanya uchunguzi wa saratani kwa Wananchi. Kuna Taasisi kama MEWATA, Umoja wa Madaktari Wanawake, nao wanafanya hususan kwa saratani ya matiti. *(Makofi)*

Kwa maana hiyo, ninachoweza kueleza ni kwamba, kampeni hizi za uchunguzi zinafanyika mara kwa mara. Nataka nikiri kwamba, ni muhimu tuweke vituo hivi vya uchunguzi na matibabu sehemu kubwa zaidi ya nchi yetu; tumeanza Ocean Road na Bugando, tutaendelea kufikisha katika maeneo mengine ya nchi yetu. *(Makofi)*

**MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza.

Nilitaka kujua; kwa sababu katika magonjwa ya kansa, mkakati mkubwa unapaswa kuelekezwa katika *prevention* kuliko katika matibabu. Sasa nini mkakati wa Serikali kuwekeza fedha, kwa sababu tunavyojua sasa hivi kuna changamoto kubwa sana ya upatikanaji wa fedha katika sekta hii hususan katika matibabu ya magonjwa ya kansa; nini mkakati wa Serikali kuhakikisha kwamba fedha za kutosha zinatengwa katika sekta ya *prevention* kuliko katika matibabu?

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Ndugulile, kama ifuatavyo:-

Kwanza, nataka nikubaliane naye kwamba, kinga ni muhimu kuliko matibabu, hususan kwa saratani ambapo mtu akishagunduliwa, mara nyingi nafasi yake ya kupona kabisa inakuwa ndogo kutokana na kuchelewa kugunduliwa kwao. Kwa hiyo, tunakubaliana na hili.

Nataka niliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, tunao Mpango Mkakati wa Kukinga Saratani na fedha zipo, zimeanza kuwekwa, tutaendelea kuongeza bajeti ya fedha hizo. Niseme tu kwa ufupi kwamba; kwa mfano, mwaka ujao wa fedha tutaanza kutoa chanjo kwa ajili ya kuzuia saratani ya shingo ya kizazi. Kwa hiyo, huo ni mpango wa kukinga saratani na chanjo hiyo itatolewa kwa watoto wa shule ambao wapo kati ya miaka tisa na kuendelea ili tuweze kuwakinga na saratani ya shingo ya kizazi ambayo ndiyo saratani inayoongoza nchini mwetu.

Vilevile tuna mipango mingine ya kuendelea kutoa kinga kwa saratani hususan za matiti kwa kufanya uchunguzi mapema na tutaendelea kufanya uchunguzi wa saratani ya shingo ya kizazi, ukiacha hiyo chanjo, uchunguzi wa

saratani ya shingo ya kizazi mapema ili kuweza kubaini wale ambao wameathirika waweze kupata tiba mapema.

**SPIKA:** Ahsante. Tumetumia dakika 12 kwa swali hili. Wizara ya Ujenzi, Mheshimiwa Esther Midimu atauliza swali hilo!

Na. 114

**Barabara ya Bariadi - Lagangabilili – Mwandoya – Mwanhuzi – Mto Sibiti – Mkalama – Iguguno**

**MHE. ESTHER LUKAGO MIDIMU** aliuliza:-

Mkoa mpya wa Simiyu haujaunganishwa kwa barabara licha ya Sera nzuri ya Serikali ya kuunganisha Makao Makuu ya Mikoa yote kwa barabara za lami:-

(a) Je, ni lini barabara ya Bariadi – Lagangabilili – Mwandoya – Mwanhuzi – Mto Sibiti – Mkalama hadi Iguguno inayounganisha Mikoa ya Simiyu na Singida itajengwa kwa lami?

(b) Je, ni lini Daraja la Mto Sibiti linaloendelea kujengwa litakamilika?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Esther Lukago Midimu, kama ifuatavyo:-

Barabara ya Bariadi – Ligangabilili hadi Kisesa (km 32) ni Barabara ya Mkoa, inayohudumiwa na Wakala wa Barabara *(TANROADS).* Aidha, sehemu ya Barabara hii kutoka Kisesa – Mwandoya hadi Mwandoya Junction (km 73) ni Barabara ya Wilaya chini ya Halmashauri ya Wilaya ya Meatu. Kutoka Mwandoya Junction – Mwanhuzi – Mto Sibiti (km 79.2) ni sehemu ya Barabara Kuu kutoka Kolandoto – Lalago – Mwanhuzi – Matala – Oldeani Junction (km 328),

ambayo imeanza kufanyiwa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina katika Mwaka wa Fedha wa 2013/2014. Aidha, barabara ya kutoka Mto Sibiti – Mkalama – Iguguno (km 102.5) ipo Mkoa wa Singida na ni Barabara ya Mkoa.

Mheshimiwa Spika, sasa napenda kumjibu Mheshimiwa Esther Lugako Midimu kuwa, Serikali imepanga kukamilisha ujenzi wa Barabara Kuu *(Trunk Roads)* kwanza na kutegemeana na upatikanaji wa fedha, itaendelea na barabara za mikoa ikiwemo ya Bariadi – Ligangabilili hadi Kisesa na ile ya kutoka Mto Sibiti – Mkalama hadi Iguguno.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa Daraja la Mto Sibiti, lenye urefu wa mita 82 na barabara za maingilio zenye jumla ya urefu wa km 25, zinajengwa na Kampuni ya *Hainan International* ya China, kwa gharama ya Shilingi bilioni 16.302 na ujenzi unatarajiwa kukamilika mwezi Juni mwaka 2014.

**MHE. ESTHER L. MIDIMU:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, ninaomba niulize swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa maeneo yaliyopo kando na Mto Sibiti yana ardhi chepe chepe; je, wakati wa ujenzi wa barabara hiyo sehemu hiyo wataijenga ili paweze kupitika? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ujenzi wa Daraja la Mto Sibiti kama nilivyosema, umeshaanza na ndani ya ujenzi wa daraja lile kuna kilometa karibu 25 ambayo ni mbuga. Barabara ile pia itajengwa ili kuwezesha kufika kwenye eneo la daraja. Kwa hiyo, suala la Mheshimiwa Mbunge litazingatiwa wakati wa ujenzi wa daraja hilo.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi. Kwa kuwa zile kilometa 73 ambazo anazizungumza Naibu Waziri za kutoka pale Daraja la Mto Simiyu hadi kwenye Njia Panda ya Ng'oboko, tayari tulishaleta mapendekezo hayo Wizarani kwa ajili ya

*Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

kuipandisha daraja barabara hiyo iweze kuwa ya Mkoa; na kwa kuwa sifa zote ambazo zinatakiwa na Wizara zote zinakidhi ile barabara; ni lini sasa na kwa nini mpaka sasa hivi na tuna zaidi ya mwaka mzima toka tupeleke maombi yetu Wizarani hiyo barabara haijapandishwa kuwa barabara ya Mkoa?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mpina, kama ifuatavyo:-

Barabara hiyo wakati wanaleta maombi Mkoa wa Simiyu ulikuwa haujatangazwa kama ni Mkoa wa Simiyu. Kwa hiyo, ninaamini kabisa, vigezo ambavyo vilikuwepo wakati ule na sasa vitakuwa vimebadilika. Ninamshauri Mheshimiwa Mbunge kwamba, maombi hayo yawasilishwe tena.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ninaomba tuendelee maana tuna maswali zaidi ya muda wetu.

Na. 115

**Usimamizi Thabiti wa Shule za Binafsi**

**MHE. HAROUB MOHAMED SHAMIS** aliuliza:-

Baadhi ya shule maarufu za binafsi hujigamba kuwa zinafaulisha wanafunzi kwa wingi na kwa kiwango cha juu, lakini wanafunzi wengi kutoka shule hizi huwa hawana uwezo wa kitaaluma zaidi ya kujua Kiingereza na kutumia *computer*:-

(a) Je, Serikali inasemaje juu ya tatizo hilo?

(b) Je, Serikali itakuwa tayari kusimamia kwa umakini mkubwa shule hizo namna zinavyofundisha na mitaala yake jinsi ilivyo?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Haroub Mohamed Shamis, Mbunge wa Chonga, lenye sehemu (a) na (b), kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 1995, Serikali hutoa elimu kwa ushirikiano na Taasisi zisizo za Serikali. Mitaala inayotumika katika kutoa elimu ni ya aina moja kwa Shule za Msingi na Sekondari za Serikali na zisizo za Serikali. Mitaala hiyo ni Mtaala wa Elimu ya Awali, Mtaala wa Elimu ya Msingi na *Secondary Education Carriculum.* Aidha, zipo Shule chache za Kimataifa zinazotumia Mitaala ya Kimataifa na kutathminiwa na taasisi husika. Mifano ya Mitaala ya Kimataifa ni kama vile *International Baccalaureate (IB)* na *"Cambridge International General Certificate of Secondary Education (Cambridge IGCSE) Curriculum.*

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi haina uthibitisho wa moja kwa moja wa kuwepo kwa baadhi ya shule maarufu nchini za binafsi, ambazo hujigamba kwa kufaulisha wanafunzi kwa wingi na kwa kiwango cha juu wakati wanafunzi wa shule hizo wakiwa wanajua kiingereza na kompyuta tu.

Kwa mujibu wa matokeo ya Mtihani wa Kidato cha Sita wa mwaka 2013, kati ya shule kumi bora katika kundi la shule zenye watahiniwa 30 na zaidi, shule 5 ni za Serikali zenye jumla ya wanafunzi 612, ikilinganishwa na Shule 5 zisizo za Serikali zenye jumla ya wanafunzi 408 waliofanya vizuri. Hata hivyo, utungaji wa mitihani, ufanyikaji wa mitihani na usahihishaji wa mitihani ya shule za msingi na sekondari, hufanyika kwa pamoja chini ya usimamizi thabiti wa Baraza la Mitihani la Tanzania.

Mheshimiwa Spika, katika kusimamia na kudhibiti ubora wa elimu, shule zote zinazotumia mitaala

inayoandaliwa na Serikali kupitia Taasisi ya Elimu Tanzania *(TET),* hukaguliwa na Idara ya Ukaguzi wa Shule na pia hupimwa na kutathminiwa na Baraza la Mitihani la Tanzania.

**MHE. HAROUB MOHAMED SHAMIS:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, majibu haya ya Serikali yanasikitisha, ni majibu hafifu katika masuala mazito.

Mheshimiwa Spika, kweli zipo shule nyingi za *private* zinazofanya vizuri, lakini zipo baadhi ya shule zina majina makubwa ambazo kazi yao ni kuwapa wanafunzi mitihani na majibu ili wapate kuvutia biashara.

(i) Je, Serikali haioni jambo hilo na inasema haina uthibitisisho; Wanafunzi wanapata *Division One Form Four,* lakini ni mbumbumbu hawajui chochote; kapataje *Division One* hiyo?

(ii) Serikali inasema shule zote zinakaguliwa. Juzi tu hapa nilimwuliza Mheshimiwa Waziri swali la nyongeza kuhusu Idara ya Ukaguzi wa Elimu na akasema haina uwezo wa kukagua vizuri, leo anajibu shule zote zinakaguliwa! Serikali haipo makini juu ya suala la elimu na hii ni hatari kwa Taifa. Serikali inajipanga vipi juu ya kusimamia elimu ya nchi ili nchi isiwe nchi ya mambumbumbu na kuburuzwa katika ulimwengu wa sayansi na teknolojia? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Haroub Mohamed Shamis, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwenye jibu langu la msingi nimesema, Mheshimiwa Mbunge ama mimi au Waheshimiwa Wabunge wengine, hatuna ushahidi wa moja kwa moja kwamba, wanafunzi wanaosoma kwenye shule za binafsi, baadhi yao ama wote kama anavyosema

Mheshimiwa Mbunge kwamba, hawana elimu au elimu yao ni ya kubabaisha. Kama nilivyosema, kipimo chetu sisi kama Wizara, ndiyo maana kuna chombo cha kisheria kinachoitwa Baraza la Mitihani la Tanzania. Chombo hicho kimepewa Mamlaka ya kutoa mitihani.

Walimu baada ya kufundisha, wanafunzi wakishapewa mitihani wakishasahihishiwa vizuri, kwa usimamizi wa Baraza, wanatoka *Division One, Division Two, Division Three* na kadhalika. Sasa ukiniambia tena hawana elimu bali wanajua Kiingereza na *Computer,* sina ushahidi wa moja kwa moja juu ya hilo. Vilevile amesema kwamba, shule nyingi wanafanya biashara na wanaiba mitihani, ndiyo maana nimesema kipimo cha mwisho, hata kama wangelifanya biashara au wanaiba mitihani, lakini kipimo cha mwisho ni mtihani, ambapo walimu wa shule husika huwa hawasimamii mitihani. Wanaosimamia mitihani ni Baraza la Mtihani kwa kuchukua Walimu wa Shule jirani kwenda kusimamia mitihani pale walio waaminifu, lakini kwa kushirikiana na Usalama wa Taifa, Polisi, Maafisa Elimu wa Mikoa na Maafisa Elimu wa Wilaya. Kwa hiyo, tuna uhakika vijana wanaotoka pale wanafanya mtihani ambao haujaibiwa.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, anasema nilipojibu swali la wiki iliyopita nilisema kwamba shule zote zinakaguliwa. Hapa tunaulizwa shule zinazokuwa na mitaala tofauti, Mitaala ya Cambridge au Mitaala mingine inayoendeshwa na *TET;* nimesema huwa inakaguliwa pia na Idara ya Ukaguzi. Hata kama ni Mitaala ya nje vilevile huwa inakaguliwa na Idara ya Ukaguzi kupitia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa suala la udanganyifu katika mitihani ni dhahiri na takwimu zinaonesha jinsi shule mbalimbali husan shule za binafsi zimekuwa zikifanya hivyo. Hivi karibuni Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, ameeleza kwamba, sasa

*[MHE. S. A. J. LYIMO]*
matokeo ya mitihani yatatumia pia *Continuous Assessment (CA).* Ninaomba kumwuliza Mheshimiwa Waziri, kwa kutumia *Continuous Assessment,* Serikali imejipanga kuweka *mechanism* gani kuhakikisha hizo *CA* ni za uhalisi na wanafunzi wamefanya hivyo kweli? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Susan Lyimo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Susan Lyimo, anasema kuna udanganyifu. Nami ninakiri kwamba, katika miaka miwili, mitatu iliyopita, kulikuwa kumekithiri sana udanganyifu kwa Shule za Msingi na Sekondari.

Mheshimiwa Spika, utaona hata kwenye matokeo ya Darasa la Saba mwaka huu, tulikuwa na vijana 9,700 waliokuwa wamedanganya kwenye mitihani mwaka 2011. Mwaka 2012, tukapata vijana kama 230. Kwa matokeo yaliyotoka wiki iliyopita ya darasa la saba, Vijana waliokuwa wamedanganya na wamefutiwa matokeo ni 13 tu. Kwa hiyo, utanona juhudi za Serikali za namna ya kudhibiti udanganyifu kwenye mashule.

Udanganyifu huu siyo kwa shule binafsi peke yake, hata katika Shule za Serikali katika takwimu tunaona bado baadhi ya walimu wenzetu wanakuwa siyo waaminifu namna ya kuendesha mitihani.

Mheshimiwa Spika, kuhusu *CA* anazosema Mheshimiwa Susan Lyimo, ni kweli Sera ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi ya mwaka 1995 na rekebisho lake la mwaka 2005 inasema; *continuous assessment* lazima ziwepo kwa mwanafunzi anayemaliza Kidato cha Nne, kwenye matokeo yake ya mwisho ya Baraza la Mtihani; asilimia 50 *continuous assessment* na asilimia 50 kwenye mtihani wake wa mwisho na sisi tumesema kwamba, tutaanza kutumia 40 kwa 60.

Hizi 40 zitatoka kwenye mitihani ambayo itakuwa inasimamiwa na watu ambao siyo wa pale pale shuleni.

Kwa mfano, Mitihani ya *From II,* huwa inasimamiwa na *External Invigilators,* ambayo itatoa asilimia 15. Mitihani ya *Form Three* muhula wa kwanza na muhula wa pili, tumesema itoke pale kwenye shule, lakini tumeipa *low marks;* asilimia tano muhula wa kwanza na asilimia tano muhula wa pili. Na mitihani ya *Mock* ambayo tumesema Maafisa Elimu wa Mikoa wataisimamia kwa kupeleka *External Invigilators* kwenye kila shule iweze kutoa *CA* kwa asilimia 10 ambapo kwa pamoja imeshakuwa asilimia 40. Ukijumlisha na mtihani wa mwisho inakuwa asilimia 60 ya mwanafunzi.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nina tatizo la muda. Naomba nimwite Mheshimiwa Kapt. John Chiligati!

Na. 116

**Uanzishwaji wa Mafunzo ya Ufundi Wilayani Manyoni**

**MHE. KAPT. JOHN Z. CHILIGATI** aliuliza:-

Mkandarasi Konoike wakati akitengeneza Barabara ya Dodoma hadi Manyoni alijenga Kambi yenye majengo mengi ya kudumu katika Kijiji cha Mwiboo, Kata ya Chikuyu na baada ya Mradi kukamilika mkandarasi alikabidhi majengo hayo kwa Halmashauri ya Wilaya; na kwa kuzingatia kwamba kikao cha Halmashauri ya Wilaya kimeamua majengo hayo yatumike kama Chuo cha Ufundi kwa Vijana:-

Je, Serikali itakuwa tayari kusaidia kuanzishwa kwa mafunzo ya ufundi chini ya usimamizi wa *VETA?*

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Kapt. John Zefania Chiligati, Mbunge wa Manyoni Mashariki, kama ifuatavyo:-

*Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

*[NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI]*

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni ipo katika awamu ya pili ya kujengewa Chuo cha Ufundi Stadi cha Wilaya, yaani *VETA.* Mchakato wa ujenzi wa Chuo cha Ufundi Stadi cha Wilaya hutanguliwa kwanza na zoezi la kutambua stadi zinazohitajika katika eneo husika kwa kushirikisha Uongozi wa Wilaya na wadau wengine. Mwaka 2010, Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni ilifanyiwa zoezi la uchambuzi wa stadi, baada ya zoezi hilo, ziliainishwa stadi za useremala, ufundi umeme, ufundi magari, kilimo na ufugaji. Aidha, mapendekezo yaliyotolewa kuhusu eneo la ujenzi wa Chuo cha Ufundi Stadi cha Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni ni Manyoni Mjini, Mwanzi, Chikuyu, Itigi, Mtowo, Mitoo ya Chini na Mkwese.

Mheshimwia Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Mbunge, kwa jitihada zake alizozifanya mpaka kuonana na mkandarasi na hivyo kuafikiana majengo hayo waweze kuipatia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, kwa ajili ya uanzishwaji wa Chuo hicho. Ninaomba Mheshimiwa Mbunge afanye mawasiliano na Halmashauri ya Wilaya, wafanye utaratibu wa kutuandikia na kukabidhi majengo hayo kwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, ili Serikali kupitia *VETA* iweze kuridhia uanzishwaji na uendelezaji wa Kituo hicho na kuwa hadhi ya Chuo cha Wilaya cha *VETA.* Aidha, Wizara itawaagiza Maafisa wa Ofisi ya *VETA* Kanda ya Kati hapa Dodoma, kufanya tathmini ya majengo na kutoa ushauri wa kitaalam, kwa sababu suala la uanzishwaji wa Chuo cha Ufundi Stadi cha *VETA,* linahusisha upatikanaji wa fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa, zana na kuajiri wafanyakazi (rasilimali watu), wenye sifa na siyo majengo pekee.

**MHE. KAPT. JOHN Z. CHILIGATI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu ya kutia moyo ya Mheshimiwa Waziri, ninayo maswali mawili madogo ya nyongeza:-

(a) Jibu linasema kwamba Wilaya ya Manyoni tumo katika awamu ya pili. Nataka kujua tu hiyo awamu ya pili inaanza lini?

*[MHE. KAPT. J. Z. CHILIGATI]*

(b) Amesema kwamba atawatuma Maafisa wa *VETA,* Kanda ya Kati waje wakague hayo majengo. Pamoja na kuwatuma hao Maafisa; je, yeye mwenyewe Waziri yuko tayari kuongozana na mimi kwenda kukagua majengo hayo mara baada ya Bunge hili kumalizika? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali madogo mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Kapt. John Z. Chiligati, kama ifuatavyo:-

Awamu ya pili ya ujenzi wa Vyuo vya *VETA,* utaanza baada ya kukamilika kwa awamu ya kwanza. Baada ya kupata fedha kumaliza vyuo vile 28, tutakuja kwenye awamu ya pili. Nitoe tu angalizo kwamba, kama mpango huu ambao umeuanzisha Mheshimiwa Mbunge, kwa kushirikiana na Halmashauri utakamilika, maana yake Wilaya hii ya Manyoni Mjini, tutakuwa tumefarijika tumepata *VETA* kabla hata ya awamu ya pili.

Swali la pili, Mheshimiwa Mbunge, ameniomba na mimi mwenyewe nifike pale Manyoni kuangalia majengo haya. Mwaliko huu ni mzuri sana, Singida na Dodoma siyo mbali, kwa hiyo, naahidi kwamba kwenye Bunge lijalo tutakapokuwa hapa Mheshimiwa Kapt. Chiligati tutaongozana tukaangalie majengo hayo mimi na wewe. *(Makofi)*

Na. 117

**Mipango ya Kuupatia Mji wa Nzega Maji**

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA** aliuliza:-

Serikali ilishaahidi kuwa upembuzi yakinifu wa kuleta maji ya Ziwa Victoria Wilaya ya Nzega ungeanza mwezi Oktoba, 2011:-

(a) Je, upembuzi huo ulishafanyika na ni lini Mradi huo utaanza na kama bado ni kwa sababu gani?

*[MHE. DKT. H. A. KIGWANGALLA]*

(b) Je, Serikali iko tayari kuchimba visima virefu vya maji katika maeneo ya Nzega ya Ijanija, Utwigu, Nkiniziwa, Puge, Nizibaziba na Nata kwa kuwa mradi wa awali unachelewa kuanza na pia ule wa Benki ya Dunia unasuasua?

(c) Je, kwa nini Serikali isianzishe mpango wa kununua mashine za kuchimba visima na kuzigawa kwa Halmashauri ili zishirikiane na Wananchi kuchimba visima kuliko kuchimba visima kwa njia ya tenda ambayo huchukua muda mrefu?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (K.n.y. WAZIRI WA MAJI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Hamisi A. Kigwangalla, lenye sehemu (a), (b) na (c), kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli usanifu na uandaaji wa makabrasha ya zabuni kwa ajili ya Mradi wa Maji Safi kutoka Ziwa Victoria hadi Tabora, uliohusisha Miji ya Igunga na Nzega, ulipangwa kuanza mwezi Oktoba, 2011. Kazi hiyo haikufanyika kutokana na kuchelewa kukamilika kwa taratibu za manunuzi ya Mtaalam Mshauri.

Serikali itasaini mkataba na Mtaalam Mshauri mwishoni mwa mwezi Novemba, 2013 ili kuanza kazi hiyo. Muda wa kuanza ujenzi na kukamilika kwa Mradi utajulikana baada ya upembuzi yakinifu na usanifu kukamilika. Hata hivyo, Serikali imeingia makubaliano na Kampuni ya Serikali ya India *(WAPCOS),* kufanya tathmini ya Mradi huo pamoja na gharama za utekelezaji. Kazi hiyo imekamilika na inategemewa kuwasilishwa Serikalini mwishoni mwa mwezi Novemba, 2013.

Mheshimiwa Spika, Programu ya Maji na Usafi wa Mazingira ni ya muda wa miaka 20, ambapo inatekelezwa kwa awamu nne kwa muda wa miaka mitano mitano. Katika Mpango wa Awamu ya Kwanza wa Ujenzi wa Miradi

ya Vijiji Kumi ambao unaendelea sasa, kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Nzega, Vijiji viwili vya Nata na Nkiniziwa ni miongoni mwa vijiji vya kipaumbele vinavyotekelezwa. Mikataba ya ujenzi wa miundombinu ya maji ya vijiji hivyo imesainiwa tarehe 7 Oktoba, 2013. Aidha, Serikali inatekeleza Miradi ya Kuleta Matokeo ya Haraka *(BRN)* katika Vijiji vya Busondo na Upungu vilivyopo katika Kata ya Puge. Vijiji vya Nizibaziba, Utwigu na Ijanija vitaingizwa kwenye utekelezaji wa awamu ya pili ya *WSDP* itakayoanza mwaka 2014/2015. Utekelezaji wa Miradi hiyo ya awamu ya pili utahusisha hatua zote za utafutaji wa vyanzo, uchimbaji wa visima, usanifu na ujenzi wa miundombinu ya maji.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wizara imeweka mpango wa kuimarisha Wakala wa Uchimbaji Visima na Ujenzi wa Mabwawa *(DDCA)* pamoja na Sekta Binafsi ili ziweze kujipanua zaidi nchi nzima kiuwezo na kiteknolojia. Serikali imeendelea kununua vifaa vya uchimbaji wa visima kupitia *DDCA.* Vifaa hivyo vitakuwa vikikodishwa na Halmashauri pamoja na Sekta Binafsi kwa kuufuata utaratibu utakaowekwa.

Wazo la kila Halmashari kuwa na mitambo yake yenyewe ni zuri na Halmashauri zinashauriwa kununua mashine za uchimbaji visima kupitia vyanzo vyao vya mapato. Serikali itaendelea na jukumu lake la kuimarisha Wakala wa Uchimbaji Visima pamoja na kuhamasisha sekta binafsi katika uchimbaji wa visima.

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii. Namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa majibu yake.

(i) Kwa kuwa mwaka 2011, Mheshimiwa Profesa Mwandosya, alipokuwa akiugua Mheshimiwa Stephen M. Wasira, alijibu swali langu kuhusiana na Mradi huu na akaniahidi kwamba upembuzi yakinifu ungelianza Oktoba, 2011; lakini leo hii ni 2013 tunaingia 2014, majibu ya Upembuzi yakinifu bado ni yale yale na upembuzi yakinifu haufajanyika

na hakuna lolote ambalo linaendelea. Kwa kuwa ahadi hii ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, inaelekea kama inachezewa chezewa tu. Nini sasa msimamo wa Serikali wa uhakika, wa uhakika, ninapigia mstari, kuhusiana na suala la kutekeleza Mradi huu, ambao unagusa maeneo makubwa ya Mkoa wa Tabora? *(Makofi)*

(ii) Kwa kuwa maeneo yote ambayo ameyataja Mheshimiwa Waziri katika majibu yake, palichimbwa visima na maji hayakupatikana; na kwa kuwa Jumapili, keshokutwa, nitakuwa na kikao pale Nzega Mjini ambapo ninajua Wananchi wa Nzega wataniuliuza juu ya adha ya maji. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri yuko tayari kuongozana na mimi ili anisaidie kutoa majibu haya kwa Wananchi yeye mwenyewe? *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante, uzuri wake wakati ule yeye huyu alikuwa Naibu Waziri wa Maji. Naomba ujibu!

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla, kama ifuatavyo:-

Kwanza, nampongeza kwa namna anavyofuatilia upatikanaji wa maji katika Wilaya yake ya Nzega.

Suala la ahadi ya Serikali ya kupeleka maji kutoka Ziwa Victoria kwenda Igunga, Nzega na Tabora, lipo palepale na Serikali itatekeleza na ndiyo maana tunasema kwamba, tayari hatua za mwisho tumefikia kumpata Mhandisi Mshauri atakayefanya usanifu wa kina. Usanifu wa awali tayari umeshafanyika na gharama za Mradi zimeshaeleweka, tena inaonekana kwamba tunaweza tukapeleka na maeneo mengine zaidi ya haya anayoyazungumzia. Kwa hiyo, Mradi huu utatekelezwa.

Kuhusu kuongozana na yeye, mimi nakubaliana naye na nitamwambia Mheshimiwa Waziri wa Maji aweze kuongozana na Dkt. Kigwangalla kwenda Nzega. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Tuendelee na Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika; Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim atauliza swali hilo!

Na. 118

**Kubinafsishwa kwa Viwanda vya Korosho**

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM** aliuliza:-

Viwanda vya Korosho vya Mikoa ya Lindi na Mtwara vilibinafsishwa na kupewa wawekezaji ambao wameshindwa kuviendeleza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kutatua tatizo hilo?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tathmini iliyofanyika imebaini kuwa, wawekezaji wengi wa viwanda vya korosho wameshindwa kutekeleza mikataba ya mauzo kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo ukosefu wa fedha za uendeshaji, ukosefu wa umeme wa uhakika na viwanda kutumia teknoloja ya zamani. Aidha, kufuatia tathmini hiyo, Wizara yangu kwa kushirikiana na Shirika Hodhi la Mali za Mashirika ya Umma (*CHC*), pamoja na wadau wengine, inaandaa mapendekezo ya hatua za kuchukua dhidi ya wawekezaji walioshindwa kuendeleza viwanda hivyo.

Mheshimiwa Spika, hatua za kupata ufumbuzi wa suala hili ni hatua inayoshirikisha Idara mbalimbali tofauti za Serikali. Aidha, ikumbukwe pia kwamba, maeneo mengine yaliyobinafsishwa kuna matatizo yanayofanana; hivyo, maamuzi katika masuala haya ni mapana na

yatakuwa na athari kwa wawekezaji wengine ambao hawajakidhi makubaliano ya awali ya uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, mapendekezo ya awali ya Wizara yangu ni kwamba, kama mwekezaji ameshindwa kuendeleza rasilimali aliyokabidhiwa na Serikali kinyume na makubaliano ya mkataba, mali hiyo irudishwe, ifanyiwe tathmini upya na itangazwe ili kupata mwekezaji mahili *(Strategic Investor)* mwingine, mwenye uwezo wa kuendeleza rasilimali husika kwa manufaa ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, azma ya Serikali ni kuhakikisha kuwa, viwanda hivyo vinazalisha kwa ufanisi ili viweze kutoa msukumo kwa Sekta ya Kilimo nchini na kutoa ajira kwa Wananchi wa Mikoa ya Lindi na Mtwara. Aidha, Bodi ya Korosho kwa kushirikiana na wadau wengine, imeandaa mkakati wa ubanguaji korosho nchini, unaolenga ujenzi wa viwanda vikubwa vya korosho katika maeneo ya Tunduru, Mtwara na Pwani na ujenzi wa viwanda vidogo vya ubanguaji wa korosho vya wakulima ili kuhakikisha kuwa korosho inaongezewa thamani na hivyo kuongeza mapato ya wakulima.

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Masoud, maswali ya nyongeza!

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru na nina maswali madogo mawili ya nyongeza.

(i) Kwa kuwa Serikali ilikopa *World Bank* dola milioni 210 kwa ajili ya kufunga mitambo katika viwanda hivyo, lakini viwanda hivi viliuzwa kwa bei ndogo kwa Vigogo wa Serikali chini ya shilingi bilioni moja tu; na katika jibu la msingi Serikali imekiri kwamba, wawekezaji hawa wameshindwa kutekeleza mikataba yao; na kwa kuwa pia Serikali imesema kwamba ipo katika mkakati wa kuweza mali hii kutathminiwa na kurudishwa au kupigwa mnada:-

Je, Serikali haioni sasa ni wakati mwafaka wa viwanda hivi kurudishwa kwa Vyama vya Ushirika vyenye

nguvu mfano *TANECU* na *ILULU* kwa ajili ya kufanya kazi vizuri zaidi?

(ii) Kwa kuwa hadi sasa Serikali imelazimisha wakulima wa korosho kuuza korosho zao katika mfumo wa stakabadhi ghalani, jambo ambalo linaleta manung'uniko makubwa, lakini Sera ya Nchi na Sera ya Serikali ni soko huria. Hamwoni mnawadanganya Wananchi na mnaendelea kuwadhoofisha na kuwanyonya Wakulima wa Korosho hasa kwa kuzingatia kuwa korosho ni yao? Tabia hii lini mtaacha na lini mtarekebisha? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, naomba nimjibu Mheshimiwa Masoud Salim, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, mimi nadhani nifafanue kwamba, huu mkopo wa World Bank anaouzungumzia kwa ajili ya kuboresha viwanda hivi; viwanda hivi vyote kwa ujumla vilijengwa baina ya mwaka 1976 na 1980, wakati huo mkakati wa Serikali ulikuwa kujenga viwanda hivi kwa sababu miaka ya 1973, Tanzania ilifikia uzalishaji wa tani 140,000 ambao ndiyo ulikuwa uzalishaji mkubwa dunia nzima; kwa hiyo, ikaonekana busara ya kujenga viwanda vile. Katika miaka ya 1980 mpaka 1990, uzalishaji wa korosho ukafika mpaka tani 20,000, kwa hiyo, uendeshaji wa vile viwanda ukawa hauna tija tena ukasababisha viwanda vile kufa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nilitaka kumsisitizia tu kwamba, wakati wa ubinafsishaji mwaka 2004/2005, maamuzi ya kubinafsisha viwanda hivi yalitokana na kwamba vyenyewe vilikuwa havijiendeshi.

Kwa hiyo, ni kweli kwamba, tulipowapa viwanda hivyo wazalishaji hawa, nadhani ni kama viwanda vitatu tu ambavyo vilijaribujaribu kidogo, lakini hata teknolojia inayotumika sasa hivi kwenye viwanda hivyo imepitwa na wakati sana. Kwa hiyo, ndiyo maana nimesema kwamba, pamoja na kutambua uhalisia wa matatizo waliyokuwa

nayo, lakini kama Taifa tunahitaji kuwa na mkakati mpya wa kubangua na ndiyo maana tunaliangalia upya suala hilo kwa kutafuta wawekezaji wapya.

Mheshimiwa Spika, swali la pili hili la kurudisha viwanda kwenye Vyama vya Ushirika kama *TANECU* na *ILULU,* hiyo *TANECU* yenyewe na *ILULU* ambavyo ni Vyama Vikuu, tayari mkakati wa kuvipasua katikati unafanyika sasa hivi. *ILULU* wanajitenga wanakwenda kuwa *LUNALI,* kuwa na Rwanga, Nachingwea na Liwale kuwa na chama chao na *TANECU* pia Tandahimba wanakwenda kivyao na Newala wanakwenda kivyao. Kwa hiyo, nadhani kidogo upo nyuma na taarifa hizo.

Mkakati ni kwamba, kwa sababu ya matatizo yaliyojitokeza ya vyama hivyo kushindwa kusimamia Stakabadhi Ghalani, ndiyo maana tunavivunja vyama hivi kwani vimekuwa vikubwa mno, viwe vidogo na viwe na ufanisi zaidi viweze kuhudumia wakulima kwa ukaribu zaidi, kwa zao hili muhimu ambalo linazidi kuwa soko la dunia kwa maana ya kwamba lina nafasi kubwa kwa Wakulima wa Korosho.

**SPIKA:** Ahsante. Naomba tuendelee na Viwanda na Biashara, Mheshimwa Albert Obama Ntabaliba!

Na. 119

**Soko la Mnanila**

**MHE. ALBERT OBAMA NTABALIBA** aliuliza:-

Katika bajeti ya mwaka 2011/2012 na 2012/2013; Soko la Mnanila ni moja ya masoko saba ya mipakani yaliyopangwa kutekelezwa:-

Je, ni lini utekelezaji huo utafanyika?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Albert Obama Ntabaliba, Mbunge wa Jimbo la Manyovum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Soko la Mnanila lililopo katika Wilaya mpya ya Buhigwe ni moja kati ya masoko saba ya mpakani, ambayo Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika na Halmashauri husika, iliweza kuhamasisha kutengwa kwa maeneo hayo na kufuatilia hatua mbalimbali za utekelezaji wake.

Mheshimiwa Spika, zabuni ya ujenzi wa Soko la Mnanila imefunguliwa tarehe 30 Septemba, 2013 pamoja na ile ya Soko la Mutukula (Missenyi), ambapo tathmini ya zabuni hizo imekamilika na mawasilisho ya kuomba idhini ya kuendelea na ujenzi yamewasilishwa Benki ya Maendeleo ya Afrika *(ADB),* ambapo wanafadhili Mradi huo. Hivyo, hatua ya kuwapata wakandarasi kwa ajili ya ujenzi wa masoko haya mawili itakamilika mwezi Novemba mwaka huu na ujenzi utaanza mara moja na unatarajiwa kukamilika mwezi Februari, 2014.

Mheshimiwa Spika, maandalizi ya ujenzi wa masoko mengine ya mpakani ya Nkwenda (Karagwe), Kabanga (Ngara), Sirari (Tarime), Murongo (Karagwe) na Busoka (Kahama), mikataba yake imeshasainiwa na ujenzi unaendelea.

**MHE. ALBERT OBAMA NTABALIBA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niulize maswali ya nyongeza.

Kwanza, nampongeza Waziri kwa majibu yake sahihi, lakini naomba niulize maswali mawili madogo ya nyongeza.

(i) Ili haya masoko yaweze kuendelea na masoko mengine yaliyoko katika sehemu nyingine mbalimbali yatahitaji miundombinu ya barabara, maji na umeme; je,

Serikali imejiandaa vipi ili hayo masoko yatakapokamilika yaweze kuanza mara moja?

(ii) Kwa sababu haya ni masoko ya mipakani, yanahitaji elimu ya ndani na nje; je, Serikali imejipanga vipi kutoa elimu Tanzania na nchi za jirani?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Kwanza kabisa, masoko haya ikiwemo Soko la Mnanila na masoko mengine ya mipakani, yakishakamilika ipo changamoto ya miundombinu kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge kwamba, barabara, maji, umeme na mingine kama Ofisi za TRA, Uhamiaji vinatakiwa. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na Wananchi wote kwamba, Serikali imejipanga sawasawa kwa kushirikiana na Wizara nyingine husika, kwa maana ya Wizara ya Nishati, kwa maana ya umeme, Wizara ya Maji, kwa ajili ya maji na hata Wizara ya Miundombinu kwa ajili ya barabara, tutashirikiana ili tuweze kufanya kazi ambayo ina kipaumbele cha kuweza kuyaweka masoko haya ya mipakani yaweze kufanya kazi ipasavyo.

Kuhusu elimu ambayo inakusudiwa kutolewa ni kwamba, ipo mikakati kwamba masoko yote ya mipakani, ambayo tayari yameshabainishwa, yapo kama 48 hivi, tunataka tufanye eneo lote la mipakani ambapo kuna sehemu ya uchumi masoko yaweze kujengwa.

**SPIKA:** Ahsante. Naomba tuendelee na swali la Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia; Mheshimiwa Tauhida Cassian Galos, atauliza swali hilo; kwa niaba yake Mheshimiwa Kabati!

Na. 120

**Mkongo wa Taifa**

**MHE. RITTA E. KABATI (K.n.y. TAUHIDA CASSIAN GALOS NYIMBO)** aliuliza:-

Mkongo wa Taifa umeunganishwa mpaka Tanzania Zanzibar:-

Je, Mradi huu ni Mradi wa pamoja kati ya Serikal ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar au ni hisani tu kutoka Serikali ya Muungano?

**WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Tauhida Cassian Galos Nyimbo, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano unatekelezwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia na umeunganishwa mikoa 24 ya Tanzania Bara. Aidha, Zanzibar imeunganishwa na Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano kupitia waya wa umeme uliojengwa kati ya Dar es Salaam na Unguja na uliokamilika Aprili, 2013 na kwa upande wa Pemba kupitia waya wa umeme kati ya Tanga na Pemba. Ufungaji wa mitambo (*Transmission and Power Equipment*), utafanyika wakati wa utekelezaji wa ujenzi wa mkongo wa awamu ya tatu, ambayo utekelezaji wake umekwishaanza. Mara baada ya kazi hii kukamilika, Mkongo wa Taifa utaanza kufanya kazi kwa upande wa Zanzibar.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, naomba kuuliza maswali mawili kama ifuatavyo:-

*[MHE. R. E. KABATI]*

(i) Je, katika Mradi wa Mkongo wa Taifa; Zanzibar ina mchango kiasi gani katika ujenzi huo?

(ii) Kwa kuwa yapo matatizo makubwa sana ya mawasiliano katika baadhi ya vijiji vyetu vya Wilaya ya Kilolo, Mufindi na Iringa Vijijini katika Mkoa wetu wa Iringa; ni lini Serikali itakamilisha ujenzi huo ili kuondoa adha ya mawasiliano katika Mkoa wetu? *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ritta Kabati, kama ifuatavyo:-

Kwa upande wa Zanzibar, Mkongo wa Zanzibar umegharimu karibu Dola za Kimarekani milioni 20 ambazo ni mkopo kutoka *Exim Bank* ya China.

Swali la pili, kuhusu lini itakamilika kupeleka mawasiliano katika Wilaya ya Kilolo na Wilaya nyingine za Iringa; mpaka hivi sasa hivi Mkongo wa Taifa tumeshaweka kwenye Wilaya 59 na Wilaya zilizobaki ikiwemo na Kilolo, zitakamilika ifikapo mwishoni mwa mwaka 2014.

**SPIKA:** Engineer Mnyaa, niahidi litakuwa swali fupi!

**MHE. ENG. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza.

Kwa kuwa Watanzania sote tulifarijika Serikali iliposema italeta hii mikongo kwa sababu ya urahisi wa mawasiliano ya kawaida pamoja na *database* kurahisisha kazi zake na gharama kupungua sana; lakini hadi hivi leo

pamoja na kwamba baadhi ya sehemu fulani Mkongo wa Taifa unatumika lakini bado Wananchi hawaja-*realise* au hawajaona lile punguzo na gharama kupungua:-

Je, Mheshimiwa Waziri upo tayari kutuletea faida gani tumepata au gharama zimepungua kiasi gani baada ya kuunganisha mikongo hii?

**WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mnyaa, ambaye ni kaka yangu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mkongo wa Taifa ulianza kujengwa mwaka 2009, kabla ya hapo bei ya mtandao hasa kwa *1GB* ilikuwa karibu shilingi 100,000. Mwaka 2010 baada ya kujengwa Mkongo wa Taifa, bei ya *1GB* ilikuwa shilingi 30,000, lakini leo hii tunavyozungumza, bei ya *5GB* ni karibu shilingi 27,000. Kwa vile Mkongo wa Taifa umeleta faida kubwa kwa Watanzania na bei hiyo itazidi kuendelea kushuka, tunategemea mwakani itakuwa *1GB* utanunua kwa karibu shilingi 3,000 au 5,000.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda umekwisha na leo tuna shughuli nyingi. Kwanza, naomba nitambue wageni waliopo, ambapo kuna wanafunzi wanane kutoka Chuo cha Biashara *CBE* Mwanza. Naomba wasimame walipo; karibuni sana!

Tuna Walimu wanane kutoka *Tanzania Nursery Teachers Organisation (TNTO),* naomba wasimame popote walipo. Ahsante sana, ni *rare profession.*

Vilevile tuna wageni saba kutoka Shirikisho la Watu Wenye Ulemavu Tanzania, wakiongozwa na Ndugu Jonas

Lubago. Naomba wasimame popote walipo kama wapo. Ahsanteni na karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wanafunzi 40 kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma; nao wako wapi? Nadhani wamekosa nafasi.

Pia, tuna wanafunzi 14 na Walimu watatu kutoka Shule ya Msingi ya Heka Manyoni wakiongozwa na Mwalimu Silvanus Waziri. Karibuni sana, lakini pia nawaomba msome vizuri.

Tuna Mchungaji Clement Aloyce Matwiga kutoka Kanisa la *Tanzania Assemblies of God Arusha*; karibu sana Mchungaji, nadhani utaiombea nchi. *(Makofi)*

Tunao wageni 14 ambao ni Madiwani na Wenyeviti wa Serikali za Vijiji kutoka Wilaya ya Ulanga, wakiongozwa na Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Ulanga, Mheshimiwa Furaha Ilongeli. Wageni wetu Madiwani karibuni sana na ahsanteni sana. *(Makofi)*

Tunao wanafunzi watano kutoka Chuo Kikuu Huria; hawa wako wapi?

Tuna wageni wanaotoka Nyamongo na Nyabasi, nadhani hawajaingia.

Wageni wengine wote mnakaribishwa.

Matangazo ya kazi; Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Dkt. Hamis Kigwangalla, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba, leo tarehe 8 kuanzia saa 7.15 mchana kutakuwa na ziara ya kutembelea Miradi ya Barabara katika Halmashauri ya Manispaa ya Dodoma.

Hivyo Kamati itakutana katika ukumbi wa chini *basement* naona, kwa ajili ya kuanza safari hiyo. Ni saa 7.15 mchana, mtakutana *basement* hapo na mna safari ya kwenda kutembelea barabara katika Mji wa Dodoma.

Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala - Mheshimiwa Pindi Chana, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba, leo hii saa 7.00 mchana watakuwa na kikao katika Ukumbi Na. 231.

Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa - Mheshimiwa Edward Lowassa, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati hiyo kwamba leo saa 7.00 mchana watakuwa na kikao katika Ukumbi wa Pius Msekwa. Kamati hiyo pia itakuwa na kikao cha pamoja na Kamati ya Bunge ya Ulinzi na Usalama.

Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira - Mheshimiwa James Lembeli, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba, leo Saa 7.30 Mchana watakuwa na kikao katika Ukumbi Na. 227.

Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI - Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba, leo saa 7.00 mchana watakuwa na kikao katika chumba Na. 219.

Waheshimiwa Wabunge, huo ndiyo mwisho wa matangazo, tuendelee na kazi, Katibu!

## MWONGOZO WA SPIKA

**SPIKA:** Ndiyo, Mheshimiwa Rajab Mbarouk.

**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Naomba Mwongozo wako kama Kanuni yetu ya 68(7) inavyotuelekeza tufanye ili tuweze kuomba Mwongozo.

*Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*



Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Maswali na Majibu, wakati Mheshimiwa Waziri anayeshughulika na mambo ya TAMISEMI anajibu swali Na. 108 la nyongeza ambalo nilimwuliza, alitoa kauli ya kwamba, mimi sijui na ni vyema niende ofisini kwake nikajifunze.

Mheshimiwa Spika, imekuwa ni kawaida ya baadhi ya Mawaziri ambao hawako makini wanapokuwa na majibu mepesi kwa Wabunge, na kuona njia ya kukwepa maswali ni kuwaambia Wabunge waende wakajifunze ama kusoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi kama Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa, niliuliza swali lile kwa kujua kinachoendelea, na kwa bahati nzuri kwa sababu Waziri hayuko *serious* na Wizara yake, Kamati yangu iliishakwenda pale kujifunza mfumo huu wa *EPOCA* na ndiyo maana tukauliza lile swali.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba Mwongozo wako juu ya Mawaziri wanapojibu maswali au pale wanapotaka kukwepa maswali. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Sasa unajua ukikaa kwenye Kiti hapa siyo rahisi kujua kama anakwepa, ama hajui. Maana yake mimi nilifikiria kwamba kama kuna uzuri wa kuona hicho kitu kinafanyaje kazi, ingekuwa vizuri. Najua wengi hatufahamu, labda wewe mwenyewe ulikosea kutosema kuwa wewe ni Mwenyekiti, kusudi tujue kama ni Mwenyekiti unajua haya mambo.

**MBUNGE FULANI:** Kwani Waziri hajui?

**SPIKA:** Aah, siyo lazima ajue. Kwa hiyo, na maswali ya nyongeza faida yake ndiyo hiyo. Kwa hiyo, nafikiri ule utaratibu ni vizuri na sisi wengine tukaujue. Lakini kwa Mwenyekiti kama ulijua, basi tunafurahi sana, unaweza kulileta tena swali letu vizuri zaidi, labda halikueleweka. Katibu.

*Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

**MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

**KAMATI YA BUNGE ZIMA**

***Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2013 [The Written Laws Miscellaneous Amendment) (No. 3) Bill, 2013]***

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, jana tulipokuwa tunaendelea na vifungu mbalimbali mtakumbuka kwamba Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe, alitoa rai kuhusu matatizo ya wale ma-*pilots*. Sasa wakati ule nikauliza hii ipo au haipo? Kwa hiyo, baada ya kuangalia upya ikaonekana kwamba kidogo haikuwa vizuri. Sasa naomba turudi kifungu cha 10 tupate maelezo ya Mwanasheria Mkuu.

**SCHEDULE OF AMENDMENT TO BE MOVED BY THE HON. FREDERICK M. WEREMA, THE ATTORNEY GENERAL AT THE SECOND READING OF A BILL ENTITLED "THE WRITTEN LAWS (MISCELLANEOUS AMENDMENTS)" (NO. 3) ACT, 2013"**

*Made under S. 86(10)(b)*

A Bill entitled "The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.3) Act, 2013" is amended generally as follows:

**F:** By deleting Clause 10.

Dodoma, ..............................., 2013

**FMW**
AG

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba Mheshimiwa Dkt. Harrison Mwakyembe, alizungumzia marekebisho yaliyoko kwenye Jedwali la Kumi la Muswada ambalo msingi wa kwanza ulikuwa ni kwamba tunafuta kifungu cha 32 kilichoko kwenye Sheria ya *Civil Aviation* kinachowazuia watendaji pamoja na *Board Members* wa Bodi ile kutoajiriwa katika sekta zinazofanana na sekta hiyo hadi watakapomaliza miezi 18.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo ya Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe ni kwamba yale mawazo ya mwanzo ya Serikali na kama ninavyoendelea kusema ni kwamba Muswada huu wa Marekebisho wa Sheria Mbalimbali, unatokana na tunavyoona matumizi ya sheria hiyo. Tumeona kwamba yale masharti ya kuwazuia wale wafanyakazi kutoajiriwa katika sekta hizo kwa muda huo hayana maana.

Kwa hiyo, anachopendekeza Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe na ambacho nakubaliana nacho ni kwamba yale marekebisho yaliyoletwa mwanzoni na Serikali kwenye Muswada yaendelee kuwa hivyo.

Kwa hiyo, jedwali la Serikali linalofanya marekebisho katika eneo hilo liondolewe na kifungu kibaki kama kilivyokuwa kwenye Muswada.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 23

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Tundu A. Lissu. Leo nataka niende kwa utaratibu kabisa, watu wenye mawazo yao waseme kabla sijahoji.

**SCHEDULE OF AMENDMENTS TO BE MOVED BY HON. TUNDU A.M. LISSU, THE MEMBER OF PARLIAMENT FOR SINGIDA MASHARIKI CONSTITUENCY AT THE SECOND READING OF A BILL ENTITLED "THE WRITTEN LAWS (MISCELLANEOUS AMENDMENTS) (NO.3) ACT, 2013"**

*(Made Under Kanuni ya 86(11) of the Kanuni za Kudumu za Bunge, 2013)*

A Bill entitled "The Written Laws (Miscellaneus Amendments) (No.3) Act, 2013 is hereby amended as follows:

C: In clause 23, by deleting the full stop and the inverted coma in item (ix) and adding a new item (x) as follows:

(x) Two members representing students from publicly-owned institutios of higher learning and privately-ovened institutions of higher learning respectively."

Dated at Dodoma this 6th day of November, 2013

..........................
Tundu A.M. Lissu
Member of Parliament

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika aya ya 23 ya Muswada nimependekeza kwamba iongezwe aya mpya ya 10 ambayo inasema: "*two members representing students from publicly-owned institutions of higher learning and privately-owned institutions of higher learning respectively*."

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia *composition*, muundo wa Bodi ya *TEA* kama inavyopendekezwa kwenye aya ya 23 utakuta kwamba katika Wajumbe wote hakuna

uwakilishi hata kidogo wa wanafunzi katika Bodi inayopendekezwa katika Mamlaka ya Elimu. Taasisi nyingine zimewakilishwa lakini wanafunzi ambao ndio wadau wakubwa wa elimu ya juu hawana uwakilishi kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii inapingana na mapendekezo yaliyoko katika aya ya 29 ya Muswada ambayo inazungumzia *composition* ya Bodi ya Mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu na utaona katika mapendekezo ya aya 29 kuna uwakilishi wa wanafunzi wawili wanaowakilisha Vyuo Vikuu vya Umma na vya binafsi. Sasa ili tuwe *consistent* ni busara katika chombo ambacho kitakuwa kinatoa fedha kama inavyopendekezwa kwa wanafunzi wa elimu ya juu, vilevile uwakilishi wa wanafunzi uwepo kama ilivyo katika Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa elimu ya juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri pendekezo hili halitakuwa na upinzani kwa Serikali. Hilo ndiyo pendekezo langu.

**MWENYEKITI:** Mwanasheria Mkuu. *(Kicheko)*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kumshukuru Mheshimiwa Tundu Lissu kwa maneno aliyotumia ya *consistency* na leo naona amevaa vizuri kuliko magandwa, nafikiri tungekuwa *consistent* hivyo hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kuna tofauti kati ya Wajumbe wa Bodi ya *TEA* na ile ya *higher learning*. Kwa sababu gani? Kinachowaunganisha wanafunzi ni mikopo, *whether* wako kwenye *private or public.* Mahitaji ya wanafunzi *whether private or public are the same*, wanahitaji mikopo. Hapa tunachozungumzia ni watu wanaofanya kazi ya kutafuta fedha kwa ajili ya kwenda kwa wale wanafunzi. Kwa hiyo, hapa wanafunzi hawahitajiki na ndiyo maana hawakuwekwa. Siyo kwamba tume-*omit* kwa makusudi, tumefanya hivyo *consciously* kwa sababu bado siyo sehemu yao bado, hii ni sehemu ya kutafuta fedha.

*[MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI]*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Tundu Lissu, nafikiri utashukuru kwa *complements* za mwanzo. *(Kicheko)*

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, eeh, nilitaka kusema hivyo kwamba Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali huwa hana maneno mema ya kuniambia, lakini angalau leo ameanza, nashukuru kwa hilo. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasikitishwa kidogo na hoja ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwamba wanafunzi hawahitajiki katika Bodi ya Mamlaka ya Elimu kwa sababu hiyo Bodi ni ya kutafuta fedha tu.

Kama nilivyosema jana, hizi kauli ni rahisi mno. Bodi ya Mamlaka ya Elimu haina jukumu la kutafuta fedha peke yake.

Vilevile inazigawa hizo fedha! Muswada huu unapendekeza kwamba ichukue fedha za *Skills Development Levy (SDL)* tulizozipigia kelele sana jana, izipeleke kwenye Bodi, halafu izi-*disburse*.

Kwa hiyo, kazi siyo tu kukusanya fedha, vilevile Bodi hii inagawa hizo fedha kwa Bodi ya Mikopo, Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi, *commission* ya Vyuo Vikuu na kwa Taasisi nyingine. Kama Bodi inagawa fedha kwa Taasisi za elimu ya juu, inakuwaje isiwe busara kuwa na uwakilishi wa wanafunzi katika Bodi hiyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachelea kusema kwamba kwa kweli hoja ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali haina mashiko.

Kwa hiyo, naomba pendekezo langu likubaliwe ili wanafunzi wawe na *representation* katika chombo muhimu hiki kinachopendekezwa kitakacho-*deal* moja kwa moja na maslahi ya wanafunzi wa elimu ya juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni hayo tu.

**MWENYEKITI:** Hivi pale si kuna *formula* ya namna ya kugawa fedha zile?

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli Serikali imekaa, imefanya uchambuzi, imeona hakuna haja ya kuweka wanafunzi hawa hapa na ndiyo pendekezo letu lililoko Mezani. Wanafunzi waende kwenye zile *institutions* zinazogawa fedha zao kwenda kwao. Lakini hapa zinagaiwa *institutions* tu peke yake.

Kwa hiyo, *representation* ya wanafunzi haina maana, siyo kwamba tu haifai, haina maana hapa, na kazi ya wanafunzi ni kusoma na siyo kuja kukaa hapa na kuanza kushughulikia haya mambo ya sera.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua *constituency* ya wapiga kura wanafunzi, lakini nafikiri tusichanganye. Tusiwafanye wanafunzi wakafanya vitu ambavyo hawastahili kuvifanya. Kazi yao ni kusoma!

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, bado niko kwenye msimamo kwamba kifungu kama kilivyo kwenye mapendekezo yetu kiwe hivyo hivyo.

**MWENYEKITI:** Sasa nafikiri leo tufanye uamuzi haraka.

*(Hoja ya Mheshimiwa Tundu Lissu iliamuliwa na Kukataliwa na Kamati ya Bunge Zima)*

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 24 …..

**SCHEDULE OF AMENDMENTS TO BE MOVED BY HON. TUNDU A.M. LISSU, THE MEMBER OF PARLIAMENT FOR SINGIDA MASHARIKI CONSTITUENCY AT THE SECOND READING OF A BILL ENTITLED "THE WRITTEN LAWS (MISCELLANEOUS AMENDMENTS) (NO.3) ACT, 2013"**

*(Made Under Kanuni ya 86(11) of the Kanuni za Kudumu za Bunge, 2013)*

A Bill entitled "The Written Laws (Miscellaneus Amendments) (No.3) Act, 2013 is hereby amended as follows:

D: In clause 24, by deleting that clause in its entirety;

Dated at Dodoma this 6th day of November, 2013

……………………..
Tundu A.M. Lissu
Member of Parliament

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye jedwali langu la marekebisho nimependekeza hicho kifungu cha 24 kifutwe kabisa. Pendekeo langu lina-*flow* moja kwa moja kutoka kwenye mapendekezo yangu kwamba fedha za wanafunzi ambazo wanazipata kutokana na *skills development levy* zisipelekwe katika mamlaka ya elimu.

Sasa kama hoja yangu muhimu ya jana ilivyo, ni kwamba fedha za wanafunzi wa elimu ya juu ambazo tulizipitisha mwaka jana 2012, ambazo zinatokana na *skills and development levy* zisiguswe, maana yake ni kwamba hakutakuwa na haja ya kuwa na huo mgao uliowekwa katika jedwali linalopendekezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua sasa ni vigumu kwa sababu zile hoja zilikataliwa, lakini hoja yangu ilikuwa hiyo

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)



kwamba kama fedha za wanafunzi zitabaki mahali zilipo maana yake hakutakuwa na hili jedwali. Lakini kwa vile hiyo hoja yangu ya msingi ilishakataliwa, nafikiri hii hoja *is purely of academic interest.* Naomba kuifuta.

**MWENYEKITI:** Ahsante, umekuwa *very honesty* kwa kweli. Mheshimiwa Halima Mdee.

**SCHEDULE OF AMENDMENTS TO BE MOVED BY HON. HALIMA JAMES MDEE MEMBER OF PARLIAMENT FOR KAWE CONSTITUENCY AT THE SECOND READING OF A BILL ENTITLED "THE WRITTEN LAWS (MISCELLANEOUS AMENDMENTS) (NO.3) ACT, 2013"**

*[Made Under Standing Order 86(11) and 88(2])*

A Bill entitled "The Written Laws (Miscellaneous Amendment) No.3 Act, 2013" is amended as follows:-

E: In Clause 24 by deleting the proposed THIRD SCHEDULE and replacing it with the following:

THIRD SCHEDULE

Formula for allocation of funds

Made under section 6(i)

| Na. | Institution | Percentage |
|---|---|---|
| 1. | Higher Educations Students Loan Board | 50% |
| 2. | Primary Level | 20% |
| 3. | Secondary Level | 14% |
| 4. | National Council for Technical Education | 3% |
| 5. | Tanzania Commission for Universities | 3% |
| 6. | Tanzania Education Authority | 10% |

Dodoma

..................

Halima James Mdee
Member of Parliament

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilileta hili jedwali kwa madhumuni ya kuweza kuzitambua shule za msingi na sekondari na mgao wake ambao ulikuwa hauko wazi. Sasa jana wakati wa marekebisho ya kifungu cha 20 ambacho kilirekebisha kifungu cha sita (6) cha Sheria mama, Serikali ilikubaliana na hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapendekeza kwamba katika muktadha huo huo wa jedwali ni kweli kabisa fedha ambayo inaenda kwenye mamlaka ya elimu ile *thirty percent* (30%) nusu yake inaenda kwenye *basic* na *secondary*. Sasa nilikuwa naitaka Serikali, katika hiyo nusu ya *basic* na *secondary* zianishwe hapa kama ambavyo nimependekeza.

Sasa nimefanya mbadiliko kwa muktadha kadhaa. Kwanza jana iliibuka hoja ya *disability* ambayo alii-*raise* Mheshimiwa Manyanya. Kwa hiyo, mapendekezo yangu ni mabadiliko haya kama ilivyo kwenye jedwali. *Higher learning* iwe *sixty four percent* (64%) kama ambavyo iko. Jedwali lielekeze kabisa *primary level* kwa sababu ya uhitaji wake ipate *eight percent* (8%), *secondary level* ipate *five percent* (5%) huu ni mgawanyo wa ile *fifteen percent* (15%) na mgawanyo mwingine wa ile *fifteen percent* (15%) ni *two percent* (2%) kwa ajili ya *disability* ambayo yenyewe ita-*cut across*. Halafu *National Council for Technical Education (NACTE*) ipate *three percent* (3%) na Tanzania *Commission for Universities* ipate *three percent* (3%) kama mlivyopendekeza. Vilevile *TEA* ipate *fifteen percent (15%)*. Hii itakuwa imefanya ule mgawanyo uwe wazi na itakuwa imetimia 100% kama ambavyo Serikali ilikuwa imependekeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiacha hivi na tusipoainisha kabisa *primary* itapata nini, *secondary* itapata nini na watu wenye ulemavu watapata nini, tunaweza tukatoa mamlaka kwa watu kuamua kupendelea upande mmoja, kitu ambacho kinaweza kisiwe sahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mapendekezo yangu ni madogo tu, kwa sababu Serikali iliishazitambua hizi, ni muhimu sasa tuziweke rasmi kwenye jedwali kama

*Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*



ambavyo tuliweka hawa watu wengine ambao wana-*benefit* na huu mfuko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namwelewa Mheshimiwa Halima Mdee anachosema, lakini naomba tuseme haya marekebisho kwa jinsi ambavyo vifungu vinakutana na vinaachana. Mapendekezo hayo yanahitaji kufanyiwa kazi ili ku-*align* hizo *percentage.* Ni wazi! Lakini ukiangalia kwenye Ibara ya 20 ukurasa ule wa 12 kwenye (f) unaona kuna ile *requirement* ya kufanya *periodic review*; ile *periodic review* ndiyo itakayoishia kubadilisha hili jedwali.

Kwa hiyo, nafahamu kwamba ni vizuri kuonyesha zile *percentage, disabilities* ngapi na hizo nyingine ngapi. Lakini tunaomba kwamba tuanze kwa hivi, halafu atakapokuwa anafanya hizi *periodic review* wata-*review* hata hili jedwali. Haya ninayoyasema ya Mheshimiwa Eng. Stella Manyanya nafikiri sisi tulikubali *principle* ile ya Mheshimiwa Eng. Stella Manyanya.

Mheshimiwa Mwenyekiri, kwenye hili ambalo linahitaji sasa *arithmetic or mathematics or calculations or logarithms whatever,* inahitaji kufanyiwa kazi kitaalam zaidi. Lakini *concept* yake nafikiri wataalam wapo wananisikia; *concept* yake itakuja kuwa *covered* kwenye *20 (f)* itakapokuwa Sheria, watakapokuwa wanafanya zile *periodic review* na kwa sababu kuna *requirements* sasa kwamba katika kufanya hivyo wafikirie *students with disabilities* na wale ambao wana *special needs* hiyo *formula* yao wataiweka. Ni vigumu sana, nadhani Bunge halina *data* kwa sasa kuweka hiyo *formula*.

**MWENYEKITI:** Kwa sababu tulishakubaliana kwamba maneno yaliyoletwa na Mheshimiwa Eng. Stella Manyanya yaingie, nadhani tukiingia kwenye *details* hizi tutapata matatizo. Mheshimiwa John Mnyika.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Jana wakati naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Eng. Stella Manyanya, nilisema kwamba kwa kuridhia huo uamuzi wa kuweka kwenye malengo, itahitaji kwenye kifungu cha 24 ambacho ndiyo tunakijadili sasa kwenye mgawanyo, tufanye marekebisho.

Nimesikiliza majibu ya Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Hapa tunatunga Sheria, *periodic review* ama tathmini tu ya hivyo vipindi ni kwa ajili ya wakati wa utekelezaji. Hapa tukishaitunga hii Sheria na tukakubali jedwali likawa kama lilivyo kwenye ukurasa wa 14 ya kwamba elimu ya juu asilimia 64, kwa upande wa *Tanzania Education Authority* asilimia 30, na hawa wengine tatu, tatu, hatutakuwa na haki yoyote juu ya utekelezaji wa malengo mengine yoyote ambayo jana tuliyapitisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kufanya marekebisho ya Sheria siyo kitu rahisi sana. Tukiitunga Sheria hivi sasa tunavyoitunga itakuwa muda mrefu sana kwa Sheria kurudishwa tena kufanyiwa marekebisho baada hiki alichokiita Mwanasheria Mkuu wa Serikali *periodic review. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa ili tuwe na uhakika ya kwamba malengo yametimia, mimi naamini watalaam wa Serikalil wapo hapa, Serikali ipo hapa na suala hili la mgawanyo wa viwango wamelifanyia kazi vya kutosha sana. Tungependa tu pendekezo la Mheshimiwa Halima Mdee likubalike la kwamba Elimu ya Juu iwe asilimia 64%, Elimu ya Msingi iwe asilimia 8%, Elimu ya Sekondari asilimia 5%, *NACTE* asilimia 3% na Tanzania *Commission* kwa maana ya *TCU* asilimia 3%, *Tanzania Authority* ama *TEA* (Mamlaka ya Elimu) asilimia 15% na kwa upande wa walemavu asilimia 2%. Sasa kama Serikali inakataa hili pendekezo, Serikali itoe majibu

*[MHE. J. J. MNYIKA]*

mbadala ya jedwali tofauti ili tunapoipitisha hii Sheria tuipitishe ikiwa na jedwali, *periodic review* ziwe ni sawasawa tu na *review* za ndani za kiutendaji, lakini mwongozo utolewe kwa mujibu wa jedwali hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mimi pia ninapata tatizo kwamba tunaweza kuja hapa na *figures* ambazo *justification* zake anazijua yule aliyeleta, lakini wengine wote tuseme ndiyo tu. Mimi inanipa shida hii. Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naelewa *concern* ya Waheshimiwa Wabunge. Kwa kweli kwa kaiwada haya mambo ya majedwali mara nyingi sana yanakuwa ni ya utendaji. Kwa sababu Mheshimiwa John Mnyika, nafahamu ndugu yangu Mbunge wa Ubungo, nafahamu kwamba katika kufanya maamuzi ambayo yanaamua *percentage;* hivi kwa nini unasema mbili, isiwe tano? Hivi kwa nini isiwe kumi? Hizo *facts* Bunge sasa hivi halina. Kwa hiyo, tufanye maamuzi hayo ambayo *rule of thumb* kwa kweli ni *very subjective.* Ni *very subjective* na uendeshaji wa mambo haya unastahili kuwa *objective.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nashauri kwamba kwa sasa tubakize jedwali kama lilivyo, tuwape wataalam nafasi ya kufanya *periodic review* na kupitia hizo hesabu kusudi waje sasa na hizo *data*. Tukiona kuna umuhimu hili jedwali tutalileta. Naahidi sasa kwamba nitawabana wataalam wafanye hiyo *formula* kuhakikisha wale watoto ambao wana *disabilities* na wenyewe wanaingia, kama mnaona kwamba hiyo inaweza kutusaidia kwenda mbele.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa mimi kama nasimamia hapa, napata tatizo sana kukubali hizi hesabu. Maana mimi nikipenda kitu changu nang'ang'ania iwepo. Lakini tuna *argument* gani ya kutu-*convince* sisi wote? Kwa hiyo, nasema kwamba Serikali iende ikafanye hii kwa sababu tunarudi

*Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*



tarehe 3 Desemba tuletewe hapa. Lakini kusema tufanye hesabu hapa tutakuwa hatujitendei haki sisi wenyewe. *(Makofi)*

Kifungu kinaafikiwa?

**WAHESHIMIWA WABUNGE:** Ndiyo!

**SPIKA:** Kifungu kinaafikiwa kukiwa na makubaliano kwamba jedwali hili litafanyiwa kazi tena.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima kukiwa na makubaliano kwamba jedwali hilo litafanyiwa kazi tena)*

Ibara 25

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Tundu Lissu. Sasa hawa watakuwa wanabadilisha yale mabadiliko ya Serikali.

**SCHEDULE OF AMENDMENTS TO BE MOVED BY HON. TUNDU A.M. LISSU, THE MEMBER OF PARLIAMENT FOR SINGIDA MASHARIKI CONSTITUENCY AT THE SECOND READING OF A BILL ENTITLED "THE WRITTEN LAWS (MISCELLANEOUS AMENDMENTS) (NO.3) ACT, 2013"**

*(Made Under Kanuni ya 86(11) of the Kanuni za Kudumu za Bunge, 2013)*

A Bill entitled "The Written Laws (Miscellaneus Amendments) (No.3) Act, 2013 is hereby amended as follows:

E. In clause 26, by deleting that clause in its entirety;

Dated at Dodoma this 6th day of November, 2013

..........................
Tundu A. M. Lissu
Member of Parliament

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, aya 25 na 26 inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Filamu na Michezo ya Kuigiza kwa kuongeza adhabu kwa makosa mbalimbali kwa Mujibu wa Sheria hiyo kutoka Sh. 5,000/= kwa Sheria ya sasa hadi milioni tatu, na vilevile kuongeza adhabu ya kifungo kutoka miezi 12 kwa mujibu wa sheria sasa hadi miaka miwili inayopendekezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na faini. Ongezeko la faini peke yake itakuwa ni asilimia 300,000. Faini inaongezeka kwa asilimia 300,000. Tukienda kwa mara ngapi faini inaongezeka mara 600 kutoka Sh. 5,000/= kwa mujibu wa sheria ya sasa mpaka Shilingi milioni tatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema jana, Sheria ya Filamu na Michezo ya Kuigiza ni moja ya mabaki ya aibu katika mfumo wetu wa Kisheria, mabaki ya ukoloni katika mfumo wetu wa Kisheria. Sheria hii ilitungwa kwa ajili ya kudhibiti uhuru wa watu wa kutoa mawazo yao na fikra zao kwa njia ya sinema na kwa njia ya michezo ya kuigiza. Ni Sheria ya kikoloni, ni Sheria ya kikandamizaji imependekezwa mara nyingi ifutwe, bado ipo kwenye utaratibu wetu wa kisheria. Leo hii inapendekezwa adhabu iongezeke mara 600.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, tangu Sheria hii ilipotungwa mwaka 1976 hakuna hata mtu mmoja ambaye ameshtakiwa na Serikali hii kwa kuvunja Sheria hii; hakuna mtu amepatikana na hatia chini ya Sheria hii hata mmoja; hakuna mtu amepigwa faini kwa Sheria hii hata mmoja! Leo hii kuna sababu gani ya kuongeza faini kwa asilimia 300,000, kuongeza faini kwa mara 600 kama siyo kutisha watu, kama siyo kuingiza Sheria za kidikteta katika mfumo wetu wakati tunatengeneza Katiba Mpya, ni nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, napendekeza mapendekezo haya katika kifungu hiki yakataliwe. Hatuwezi tukawa na Sheria za aibu namna hii. Itakuwa ajabu Serikali ambayo haijawahi kushitaki mtu yeyote kwa kukiuka Sheria hii, leo inaleta Sheria inayosema adhabu iongezeke mara

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)



600. *What is the rational? What is the basis?* Nani ambaye amevunja Sheria hii mkampata na hatia mkaona adhabu hii ni ndogo? Nani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, napendekeza pendekezo hili la kuongeza adhabu bila sababu yoyote ya msingi likataliwe na Bunge hili liondolewe. Itakuwa ni aibu, nchi za watu zinatajirikia filamu, sisi tunapendekeza kuwaadhibu watu, kuongeza faini mara 600, hata aibu hatuna!

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Kwanza kabisa naomba radhi, hicho anachoki-*discuss* Mheshimiwa Tundu Lissu ni kifungu cha 26. Sasa mimi Ibara ya 25 sijawahoji ambacho hakina mabadiliko ya mtu yoyote. Sasa nitaihoji.

Ibara ya 25

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 26

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo, yeye Tundu Lissu alikuwa anazungumzia Ibara ya 26 ambayo sisi tulitaja. Naomba maelezo, Mheshimiwa Ester Bulaya.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, inawezakana tu kwa sauti halisi kuongea kwa ukali na maneno yake mengine ambayo hayana ushirikiano, inaweza isionekane mantiki ya hoja katika hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sipingani kabisa kuwa adhabu kwa watu ambao watakiuka utaratibu katika masuala ya filamu. Lakini na mimi naiona hoja kwamba adhabu ambayo tunaiongeza ni kubwa sana ukilinganisha na maisha halisi ya wasanii wetu. Hivyo hivyo kwa kududuliza, leo hii tunawaona akina JD wanaanza kupata mafanikio.

Sasa tuanze kuwabana hata kwa kile kidogo wanachopata bila kuwaandalia mazingira bora kwa ajili ya kuweza kunufaika na kazi yao ya filamu!

Sasa mimi nilikuwa naiomba Serikali, inawezakana wasifutwe, lakini wakapunguza adhabu, basi wakatoka Sh. 5,000/= mpaka Sh. 500,000/= siyo mbaya kuliko ambavyo hiyo imeenda. Nilikuwa naomba sana Mwanasheria Mkuu wa Serikali baba yangu uliangalie hili kwa kina. Kwa sababu wengi wao ni vijana wenzangu, ndio wameingia kutokana na matatizo makubwa ya ajira. Nilikuwa naomba sana Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi iliangalie kwa kina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mnyika, lakini muwe mnazungumza siyo mna-*shout*. Mheshimiwa Mchungaji Mnyika. *(Kicheko)*

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa John Mnyika naomba ukae. Mheshimiwa Mchungaji Msigwa, pole unafanana na mchungaji mchungaji hivi.

**MHE. MCH. PETER MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Tundu Lissu kwa sababu moja kubwa. Viongozi tupo kwa ajili ya kuwafanya watu bora wale tunaowaongoza. Kwa hiyo, kwa sababu ya kazi kubwa na mapato ambayo yanaweza kupatikana katika eneo la filamu, ni vizuri tukawatengenezea mazingira mazuri hawa vijana wetu wakafaidika na hii *industry* badala ya kuweka Sheria ambazo ni kandamizi ambazo mwisho wa siku hata zile *potentials* walizonazo tunakwenda kuziua.

Kwa hiyo, wajibu wa kwanza wa uongozi ni kuinua *values* za watu, ni kukuza viwango vya watu. Kwa hiyo, hizo Sheria ambazo kimsingi watu hawajawahi kupata nazo taabu, tukiendelea kuwakandamiza, tutakuwa tunawaumiza.

*[MHE. MCH. P. MSIGWA]*

Kwa hiyo, naunga mkono kwamba hicho kifungu kiondolewe ili tuweze kukuza hizo *potentials* ambazo vijana wetu wanazo ziweze kukua kwa sababu kimsingi hatujawaandalia mazingira yaliyo bora ya kuwafanya waweze kuibuka na *potentials* zao katika jamii yetu ya Kitanzania.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa John Mnyika.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwa mujibu wa hotuba ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali wakati anawasilisha maelezo kuhusu kifungu hiki, nitanukuu: "Sehemu ya tano inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Filamu ya Michezo na Kuigiza, Ibara ya 26 inapendekeza kuwa kifungu 24 kirekebishwe ili kuongeza adhabu ya mtu atakayetenda kosa chini ya Sheria hiyo ikiwemo kutoa filamu au mchezo wa kuigiza wenye lugha ya uchochezi." Lakini ukiangalia katika Sheria yenyewe, makosa yapanuliwa sana. Makosa ni pamoja na kutuhumiwa kwamba wametoa filamu yenye matusi au yenye lugha ambayo pengine Serikali imeona haistahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mazingira haya ya wigo huu mpana, naungana mkono na Mheshimiwa Tundu Lissu kwamba marekebisho haya yaondolewe kwa sababu yanaweza kutumika vibaya sana kuminya Tasnia ya Filamu na Tasnia ya Michezo ya Kuigiza Nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naelewa kwamba katika majumuisho ya hoja jana Mwanasheria Mkuu wa Serikali alionesha kama vile Serikali ina mashaka juu ya mambo mbalimbali na akasema kwamba Sheria huwa zinatungwa kutokana na matukio. Sasa ningeomba Mwanasheria Mkuu wa Serikali atueleze ni matukio yapi hasa yaliyoisukuma Serikali kuanza kutunga Sheria za namna hii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vyovyote vile, matukio ambayo Serikali inayatumia kama visingizio hayawezi kuhalalisha kutunga Sheria ambayo itakwenda kusababisha, badala ya kuwa na Matokeo Makubwa Sasa, kutakuwa na

*Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*



Matokeo Mabaya Sasa, yaani badala ya *Big Results Now* kwenye Sekta ya Filamu na Michezo kutakuwa na *Bad Results.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi siungi mkono kabisa hii Sheria kwa sababu italeta Matokeo Mabaya Sasa *(Bad Results Now)* kinyume kabisa na lugha ambazo Serikali inazungumza humu Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kumshauri Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kweli, ni vizuri Serikali isiendeshwe na matukio. Kama tutaendesha Serikali na matukio, maana yake Serikali itakuwa inatunga Sheria kwa kutazama hasira zake na fikrsa zake jambo ambalo litaingiza nchi kwenye matatizo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naunga mkono kwamba kifungu hiki kiondolewe kabisa kwa ujumla wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge wanasahau tu. Iliundwa Kamati ya Bunge hapa na Azimio likatoka hapa Bungeni na ilikuwa tarehe 8 Mei, 2013, tuwe na kumbukumbu. *Let us not shout, let us argue*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Kabwe Zitto alisema maneno haya, naomba niwie radhi kwa ufupi kabisa ni-*quote.* Alikuelekeza na akasema tungependa kuongeza katika Azimio hili kwamba: "kwa kuwa ni dhahiri kabisa na kama tulivyozungumza siku chache zilizopita kwamba hivi sasa kuna nyufa katika Taifa letu, nyufa ambazo ni rahisi sana kutumiwa na maadui wa Taifa letu ili waweze kutugawa na kuliparanganisha Taifa; na kwa kuwa moja ya sababu ya nyufa hizi ni lugha ya uchochezi *(hate speeches)*; na kwa mujibu wa mazungumzo ya Waheshimiwa Wabunge katika

*[MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI]*

Bajeti katika Wizara ya Mambo ya Ndani, ilipendekezwa kwamba tuweze kuuona utaratibu ama Sheria za kuweza kuzuia lugha za chuki, yaani *hate speeches* na kupiga marufuku lugha hizi; ningependa tuongeze katika Azimio hili kipengele hicho ili Bunge liangalie, lipitie Sheria zote za Jinai tulizonazo na kama hazitoshelezi tuweze kutunga Sheria za kuwazuia watu wa Tanzania kutoa lugha ambazo zinaweza kutugawa kama Taifa kwa maana ya *hate speeches* ili tuweze kuhakikisha kwamba tunabakia kama wamoja." Na mkapiga makofi, ipo kwenye *Hansard!*

Sasa hatutungi Sheria tunabadilisha adhabu. Adhabu ni *deterrence,* kuzuia watu waogope, watu waogope! Ndiyo maana ya Serikali. Siyo Serikali ya kuchekeachekea watu, watu wanaandika vitu, wanafanya michezo ya kuigiza ya Pwagu na Pwaguzi ambayo inawagawa Watanzania. Haiwezekani!

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuna *exceptions*. Naomba kujua *exceptions* ya Waandishi wa Habari na amemtaja mwanangu Jay Dee, hana tatizo. Kuna *exceptions* kwamba kuna mambo ambayo ukifanya hata kama itaonekana yanachukiza Serikali hayamo, wewe yafanye tu. Kwa mfano, Sheria hii ya *Penal code* inasema, kama unaonesha kwamba Serikali imefanya mambo ovyo ovyo ruksa. Kama unaonesha makosa ya Serikali kwenye mambo ya Sera, ruksa. Kama unawahamasisha Watanzania wachague Serikali makini, ruksa. Ipo kwenye Sheria. Usichoruhusiwa ni ile michezo utakayoiweka ambayo inaharibu Utanzania wetu; inaharibu usalama wa nchi yetu; inafanya watu wachukie Serikali yao; inawafanya watu wachukiane; inafanya binadamu wachukiane na watu pia wanachukiana. *(Makofi)*

Jana nilitumia maneno haya na siyatumii kwa bahati mbaya. Katiba inazungumza "watu" na inazungumza "binadamu".

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunacholenga hapa, kama unatoa *plays ya* kudhihaki watu wa aina fulani au wanadamu

wa aina fulani au unamdhihaki mtu ambaye aidha ni kiongozi au ni mtu wa kawaida, au ni mfanyabiashara, au ni mkulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, sheria ina kinga na marekebisho haya yanaletwa kwa mtu mwovu. Hatuna tatizo na akina Jay Dee ambao inaonesha wanatii Sheria. Atakayekamatwa hapa, mimi nasema sijui kuna *Big Results Now* sasa haitapata madhara; *what kind of an argument is that?* Mimi nategemea kwamba *we have brains here all of us, we have brains we can use our grey materials* kwenye vichwa vyetu ambavyo tunafugia nywele na tunafikiria. Hii ni *medium* sasa kuna *argument* gani unaleta?

Mheshimiwa Mheshimiwa Zitto Kabwe alisema na nyie mkapiga makofi. Sasa sisi tumefanya tathmini na mimi jana nimesema zipo Sheria nyingi sana. Moja ya kufanya, aidha itungwe Sheria mpya au kubadilisha vifungu vya Sheria ulizonazo. Sheria kuwa nzee kwani imetungwa siku nyingi, ukuukuu wa kamba siyo upya wa ukambaa. *(Kicheko/Makofi)*

Narudia, ukuukuu wa kamba siyo upya wa ukambaa. Kinachofanya Sheria iwe mbovu ni kupitwa na muda. Adhabu hii kwenye somo hili imepitwa na muda. Nani asiyeona? Imepitwa na muda! Matendo ya watu wanafanya hivi kwasababu wanajua tutafanya hivi na tutalipa faini kidogo. Kwa hiyo, wanafanya makusudi

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nilikuwa naomba Waheshimiwa Wabunge, nafahamu *sensitivity.* Sisi kulipendekeza adhabu ya Shilingi milioni tatu. Tuko tayari kurudi kwenye Shilingi milioni tatu. Lakini Kamati ya Bunge ikasema bwana hili ni tatizo, tukakubaliana nao tukafanya Shilingi millioni tano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tukisharudi tena tunasema kwamba Serikali ndiyo imeleta na inawagandamiza, nyinyi hamwoni tatizo? *You don't see the problem really?* Nasema ukuu ukuu wa kamba sio upya wa ukambaa.

*Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Tundu Lissu.

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwanasheria Mkuu wa Serikali amesema *we should argue and not shout. I agree entirely.*

Mheshimiwa Mwenyekiti hoja ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ni hoja ambayo haina msingi wowote Kisheria. Wala kiukweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria tunayoibishania hapa ni Sheria ya filamu na michezo ya kuigiza ya mwaka 1976. Sheria yote, sheria hii yote hakuna mahali ambapo imepiga marufuku uchochezi, *hate speeches* au mambo yote anayosema Mwanasheria Mkuu wa Serikali hapa. Haijapiga marufuku chochote anachosema Mheshimiwa *Attorney General*. Kwa hiyo, anazungumza vitu ambavyo havipo kwenye Sheria ambayo tunaizungumza. Havipo! Sheria hii lengo lake kama lilivyo kwenye vifungu vyote na kama lilivyozungumzwa mwaka 1976 wakati inatungwa, ni kuhakikisha kwamba tunadhibiti wanaotengeneza filamu, wanaouza filamu, wanaoonyesha filamu, ni *thought control.* It's all about *thought control.* Hakuna chochote anachosema ambacho hakipo kwenye Sheria hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile *AG* amemzungumzia Mheshimiwa Zitto Kabwe, sitaki kumjibia Mheshimiwa Zitto Kabwe. Sio jukumu langu kumjibia. Lakini kama kungekuwa kuna tatizo kwenye Sheria hii kama ilivyo, Mwanasheria Mkuu wa Serikali angetoa mfano mmoja wa mtu aliyepatikana na hatia chini ya Sheria hii tangu mwaka 1976 ilipotungwa, akatozwa faini, ikaonekana ndogo, akarudia kosa. Hawezi akasema hivyo kwasababu hawajawahi kumshtaki mtu hata mmoja. Kwa sababu sababu yenyewe ya Sheria kuwepo, *actually, is questionable,* kwa ushahidi huo. Sheria haina makosa wanayoyasema, hakuna ambaye amewahi kupatikana na hatia hata siku moja; hakuna ambaye amewahi kulipishwa faini hata mmoja *in 37 years.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, unaletaje Muswada unaosema tuongeze adhabu ya Sheria hii mara 600 kwa asilimia 300,000? *You can not be serious!* Unataka uonekane unafanya kazi; *this is not the best way of showing productivity* kama Mwanasheria Mkuu wa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa adhabu imepitwa na wakati. Imepitwaje na wakati kama haijawahi kutumika hata mara moja?

Waheshimiwa Wabunge, kama haijawahi kutumika hata siku moja, *how can you argue* kwamba imepitwa na wakati? *How can you* piga makofi kwa hoja ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kwa hoja ya aina hii? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusitunge Sheria ili kuonekana tu tunatunga Sheria. *We should not waste our Parliamentary time*, kwa hoja zisizokuwa na mashiko kama pendekezo la Muswada huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba kwa dhati kabisa. Naomba Waheshimiwa Wabunge Sheria hii; hivi hamjawahi kusikia *Hollywood*? Hamjawahi kusikia *Bollywood*? Hamjawahi kusikia *Nollywood*? Watu wanatengeneza *billions of dollars out of film industry* sisi tunasema tufunge watu.

*(Hapa kengele ililia kuashiria muda wa Mzungumzaji kwisha)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lissu, hii kengele ilikuwa yako.

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Haya tumemaliza. Maana yake adhabu inatolewa kwa yule ambaye ametenda kosa, siyo kwa mtu ambaye hatendi kosa. Sasa tunafanya nini? Sasa napenda kuwahoji maana tutaendelea kubishana mpaka na sisi tutatumia muda vibaya. Bado tunaendelea kuna

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)



amendment ya Mheshimiwa Halima Mdee. Katika *amendment* na wewe ulileta *amendments*. *Okay* tukiifuta hii tukiikataa tunabakia na *original*.

*(Hoja ya Mheshimiwa Tundu Lissu iliamuliwa na Kukataliwa na Kamati ya Bunge Zima)*

**MWENYEKITI: Mheshimiwa** Halima anabadisha kifungu hicho.

**MHE. HALIMA J. MDEE**: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sigombani sana na hoja ya Mheshimiwa Lissu, na ameieleza sana katika muktadha wa Sheria.

**MWENYEKITI:** Hoja ya Mheshimiwa Lissue imeondoka, wewe sema ya kwako.

**MHE. HALIMA J. MDEE**: Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo nakuja huko, si ndiyo kifungu kilikuwa kimoja?

Mapendekezo yangu mimi ni kufuta neno "*five million"* na kubadilisha kwenda kwa 500,000. Sababu yangu moja ni kwamba, kwanza Serikali haijatengeneza mazingira yoyote ya kuhakikisha kwamba kazi za wasanii wetu wa filamu zinalindwa. Mwanasheria Mkuu wakati anajibu hoja ametumia "*hate speeches*," ambayo haiko kabisa kwenye Sheria ya filamu. Kwenye hiyo Sheria ambayo imerejewa, imeundwa Bodi ya Filamu.

Bodi ya Filamu majukumu yake pamoja na mambo mengine ni kuhakiki kazi za wasanii. Sasa Serikali badala ya kuhakikisha kwamba vyombo ambavyo vyake ambavyo vinaundwa kisheria vitekeleze wajibu wake wa kukagua hizi kazi ambazo zinatolewa kwa vijana wetu kuhangaika wenyewe, pasipo msaada wowote wa Serikali; kitu pekee kinachofikiriwa ni kuongeza faini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi kwa nia njema kabisa na kwa kumtaka Mwanasheria Mkuu wa Serikali afute ile kauli ya kusema kwamba, "lugha ya uchochezi" ama lile

*[MHE. H. J. MDEE]*

Azimio, kile kipengele cha Lugha ya Uchochezi; kuna uhusiano wowote na hili suala la filamu hapa. Tusitake kupotosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kama kweli tunajali vijana wetu ambao wanahangaika wenyewe pasipo msaada wa Serikali, nyongeza hii ya faini; wakati Mwanasheria Mkuu anajua kabisa Kamati tulimwuliza: "Hebu tupatie mifano ya kesi gani ambazo zimezidi kipimo, ambazo zimepelekea Serikali kufanya hii adhabu imekuwa kubwa hivi?" Tukauliza katika vikao viwili, kwasababu huwezi kuongeza adhabu bila sababu? Walishindwa kutuletea ushahidi hata mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa katika mazingira kama haya, hatuwezi kuongeza faini tu kwa sababu Serikali imejisikia kufanya hivyo kwa sababu ya hofu wakati vyombo vimepewa dhamana kwa ajili ya kufanya udhibiti ya kuangalia hizi filamu zinaenda kwa mujibu wa matakwa ya Sheria za Filamu havitekelezwi wajibu wake. Lakini zaidi, ni lini Serikali imechukua muda kwenda kuwafundisha hawa vijana kupitia vyombo ambavyo viko kisheria ili filamu wanazozitoa ziende sambamba na matakwa ya kisheria? Sasa badala ya kuongeza faini, ninachoishauri Serikali, kwanza kwa Sheria hii hii ambayo nadhani imepitwa na wakati, wahakikishe vile vyombo vinasimamia hii sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vyombo vikiisimamia hii Sheria hizi hofu ndogo ndogo hazitakuwepo, kwa sababu filamu zitachujwa kupitia njia hiyo hiyo ya hivyo vyombo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni rai yangu kwa Bunge lako Tukufu kuungana na mapendekezo yangu haya yakupunguza faini kwasababu hii faini ni kandamizi, haimsaidii msanii, ambapo wasanii wengi wanaganga njaa; Serikali iimeshindwa kuwatafutia soko; Serikali imeshindwa kulinda hati miliki zao, lakini Serikali hiyo hiyo inatumia rungu lake la Sheria kutaka kuja kumminya kwa kuleta faini kandamizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, maoni yangu katika kifungu hichi cha (a) ni itoke Shilingi milioni tano, irudi

*Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

Sh. 500,000/=, tujenge mazingira ya vijana wetu kwanza ndipo tutoze faini nzito. Siyo tutoze faini nzito halafu wakimbie kutafuta pesa hapa za haraka haraka kiujanja ujanja.

**MWENYEKITI:** Kengele imegongwa. Sasa namwita Mheshimiwa Anna Abdallah. Walioongea kifungu cha namna hiyo hiyo hawapati nafasi.

**MHE. ANNA M. ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Mimi baada ya kuyasikiliza yote haya, kwa kweli Mheshimiwa Halima Mdee anaunga mkono suala la kutoza faini liwepo, hajakataa. Liwepo. Kwa hiyo, hiyo ya kusema tuondoe na nini halipo. Anakubali kwamba hili jambo linahitaji adhabu. Hili ni jambo moja zuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nilikuwa nashauri, kwa kuwa Serikali ilipoleta Muswada huu waliandika Shilingi milioni tatu, ndio sisi huku kwenye Kamati ndio tukasema iende Shilingi milioni tano. Kwanini tusirudi kule kule ambapo Serikali ilisema yenyewe Shilingi milioni tatu ambapo hilo linawezekana. Mimi nafikiri twende tu huko. Jambo zuri hapa ni kwamba hili suala la adhabu linakubalika na wala tusingoje mpaka mtu akose. Hili ni marekebisho ambayo tunataka kuboresha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilikuwa nashauri, pendekezo la Mheshimiwa Mdee nadhani twende kule kule kwenye *original*. Maana tungekuwa tuna-*argue* na *original* ingekuwa vizuri. Kwa kuwa hili lilitokana na sisi Wabunge kwenye Kamati zetu, basi tuliondoe kwakuwa ni sisi wenyewe tuliamua. Tulirudishe vile vile lilivyokuja kutoka Serikalini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mama Anna Abdallah hatuwezi kuendelea kujadili hili. Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sitaki kugombanisha Wabunge na Kamati, lakini mimi nilishakubaliana na maamuzi ya Kamati. Lakini Kamati naomba mnielewe, mimi ni msuluhishi, naomba turudie ile tuliyopendekeza Shilingi milioni tatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba kusema, hatuwezi kuulizwa kwanini tunanunua ndege za kivita wakati hatujawahi pigana vita. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, nimeona umuhimu wa kugawa fedha za Elimu. Nimeona *kuna mis-sharp missing links of analytical skills.* Tanacholenga hapa ni mwovu, basi. Mtu mwovu, ashakum si matusi; tukisema wazinzi wote tutawafunga miezi sita, kama wewe sio mzinzi, unaogopa nini? *(Makofi)*

Kwa hiyo, Mheshimiwa Mwenyekiti nakubaliana na wazo la Mheshimiwa Anna Abdallah. Kwamba pale badala ya kusomeka Shilingi milioni tano, iwe Shilingi milioni tatu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Hatubishani, nimesema Mheshimiwa Halima tu basi; si ndio mjibu hoja Mheshimiwa Halima?

**MHE. HALIMA J. MDEE**: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni rai yangu kwamba hii faini ipunguzwe. Lakini kama imeweza kupunguzwa kutoka *five million*, kwa sababu mapendekezo ya Serikali yalikuwa *three million* ikaja, *five million* Kamati ikasemekana ikapendekeza *ten million*, Serikali ikabaki na *five million;* sasa kama tumekubaliana tunapunguza *two million out of five million,* ibaki *three million, then* nakubaliana na hayo mapendekezo. *(Makofi)*

*(Hoja ya Mheshimiwa Halima J. Mdee iliamuliwa na Kuafikiwa na Kamati ya Bunge Zima)*

*Ibara ya 27*

*[MHE. H. J. MDEE]*

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 28

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 29

**SCHEDULE OF AMENDMENT TO BE MOVED BY THE HON. FREDERICK M. WEREMA, THE ATTORNEY GENERAL AT THE SECOND READING OF A BILL ENTITLED "THE WRITTEN LAWS (MISCELLANEOUS AMENDMENTS)"(NO. 3) ACT, 2013"**

---

*Made under S. 86(10)(b)*

---

A Bill entitled "The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.3) Act, 2013" is amended generally as follows:

**N:** In Clause 29, by deleting the proposed subsection (1) and substituting for it the following:

"(1) The Board shall consist of the following members:
(a) a Chairman;
(b) the Director of Higher Education;
(c) a member from Treasury;
(d) a member representing the Ministry responsible for finance in the Revolutionary Government of Zanzibar;
(e) one student representing students of higher learning institutions;
(f) a State Attorney of rank of senior or above representing the Office of the Attorney General;

*Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*



(g) a member representing the National Council for Technical Education;
(h) a member representing the Tanzania Education Authority;
(i) a member representing the Tanzania Commission for Universities,
(j) one member representing the Association of Tanzania Employers;
(k) one member representing financial institutions; and
(l) one member representing higher learning institutions."

Dodoma,

**FMW**

................................, 2013 AG

**SCHEDULE OF AMENDMENTS TO BE MOVED BY HON. LETICIA NYERERE, MEMBER OF PARLIAMENT (SPECIAL SEATS), AT THE SECOND READING OF A BILL ENTITLED "THE WRITTEN LAWS (MISCELLANEOUS AMENDMENTS) (N0.3) ACT, 2013.**

---

*[Made Under S.O. 86(9) and (11)]*

A Bill entitled "The Written Laws (Miscellaneus Amendments) (No.3) Act, 2013" is amended as follows:-

B: In Clause 29, by deleting item (d) and substituting for the following:-

"(d) three members representing the Minister responsible for finance in the Revolutionary Government of Zanzibar,"

.......................................
Dodoma
HON. LETICIA NYERERE (MP)
1st November, 2013
**SPECIAL SEATS**

**MHE. LETICIA M. NYERERE:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Katika kifungu hiki cha 29, nimeleta mapendekezo kama ifuatavyo:-

*"In Clause 29 by deleting item (d) and substituting for the following:*

*(d) three members representing the Minister responsible for finance in the Revolutionary Government of Zanzibar.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimependekeza hivyo kwa sababu kwanza uwiano uliopo wa *Members* wa Bodi haujitoshelezi. Kuchukua *member* mmoja kutoka Zanzibar kwa kweli uwakilishi huo hautoshi kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia kwamba masuala ya elimu ya juu yapo ndani ya masuala ya Muungano, na tunapoweka Mwakilishi mmoja kutoka Zanzibar kwakweli bado hatutendi haki kwa wenzetu Wazanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini na natambua kwamba Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali ni mhanga mkubwa wa kupigania Muungano wetu. Sasa kwa leo katika kipengele hiki simtarajii Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu kupinga hili kwasababu kupinga hili ni kusababisha kulegalega kwa Muungano wetu.

**MWENYEKITI:** Hebu tunga sheria. Mheshimiwa Leticia!

**MHE. LETICIA M. NYERERE**: Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatambua kuwa kumekuwa na matatizo mengi na malamiko mengi...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Leticia, ni hisia. Wewe sema unachotaka kusema, hizo hisia nyingine hazina haja. Ehe!

*Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

**MHE. LETICIA M. NYERERE**: Ahsante Mheshimiwa Mwenyekiti. Kwa hiyo, naomba tafadhali marekebisho ambayo nimeyaleta, badala kuwa na Mwakilishi mmoja kutoka Wizara ya Fedha Zanzibar naomba wawe Wawakilishi watatu kutoka Zanzibar. Hata kama Mwanasheria Mkuu ana mpango wa kunikatilia hili, basi naomba bado kuwe na Wakilishi zaidi ya huyo mmoja haijalishi atawatoa wapi, jinsi itakavyompendeza yeye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani unaposema *proportional representation*; kwa mfano wewe umekuja kwenye kura za *proportional representation,* ni kura ambazo ziko *related* na watu waliopiga kura. Kwa hiyo, unapokuja na suala hilo kwenye sheria hii ni lazima uniambie pia hiyo *proportional representation* kati ya Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar. Kwa hiyo *argument* hiyo siyo kweli. Kwa hiyo, unachopendekeza wewe ni kwamba Waziri wa Elimu toka Serikali ya Mapinduzi Zanzibar awakilishwe na watu watatu. Mimi sioni *argument,* kwa sababu mapendekezo yetu ni kwamba awakilishwe na mtu mmoja. Sasa wewe unasema awakilishwe na watu watatu, sisi mapendekezo hayo kwa kweli hatuyakubali. Tunaomba iendelee kuwa hivyo hivyo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Leticia hana majibu zaidi. Ni kwamba tuendelee.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Amekubali.

**MWENYEKITI:** He, amekubali? Mheshimiwa Leticia.

**MHE. LETICIA M. NYERERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sijakubaliana na Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Bado nasisitiza ombi langu kwamba Wazanzibar hawajapata uwakilishi wa haki kwenye hii Bodi. Naomba bado uwiano uongezeke. Mheshimiwa *Attorney General* anafahamu kwamba uwiano uliopo sasa hivi haujitoshelezi kwa Zanzibar kama nchi ambayo ina Katiba yake.

**MWENYEKITI:** Jamani, hiyo ni Bodi. Mkishaweka watu wengi, inakuwa tena siyo Bodi, inakuwa ni mkutano wa hadhara.

*(Hoja ya Mheshimiwa Leticia M. Nyerere iliamuliwa na Kukataliwa na Kamati ya Bunge Zima)*

**MWENYEKITI:** Mabadiliko hayo hayajakubalika.

Mheshimiwa Rashid Abdallah.

**SCHEDULE OF AMENDMENT TO BE MOVED BY THE HON. RASHID A. ABDALLAH THE MEMBER OF PARLIAMENT FOR TUMBE CONSTITUENCY AT THE SECOND READING OF A BILL ENTITLED "THE WRITTEN LAWS (MISCELLANEOUS AMENDMENT) (NO.3) ACT, 2013**

*[Made under Standing Order 86(1) and 88(2)]*

---

A bill entitled "The written Laws (Miscellaneious Amendment (No. 3) Act 2013 is hereby amended as follows:-

**A:** In Clause 29(1)(f) by inserting immediately after the words "Attorney General" by the following phrase "from Tanzania Mainland and Tanzania Zanzibar."

HON. RASHID A. ABDALLAH
**MEMBER OF PARLIAMENT FOR TUMBE CONSTITUENCY**
7/11/2013

**MHE. RASHID ALI ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti ahsante sana. Mimi pia nipo kwenye Ibara ya 29(1) (f). Kipengele cha (f) kinaelezea kwamba kutakuwa na *members* kutoka Ofisi ya *AG* lakini haiku-*specify*. Kwa sababu hiki ni kitengo cha Muungano, hatujui *member* huyu kutoka Ofisi ya *AG* ni Zanzibar au ni Tanzania Bara. Sasa nilikuwa na pendekezo kwamba kuwepo na mwakilishi mmoja kutoka kwa *AG* Tanzania Bara na kuwepo na mwakilishi mmoja

*Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*



kutoka kwa *AG* Tanzania Visiwani. Kwa hiyo, hili ni pendekezo langu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni suala la Muungano, hebu tujaribu kufanya hivyo ili kuondoa ule ukakasi wa kuleta hoja ambazo hazina msingi. Baada ya maelezo hayo, naomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali mnayo yale mapendekezo yake?

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwanasheria Mkuu anayetajwa hapa ni Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano, aliyetajwa kwa mujibu wa Ibara ya 59 ya Katiba. Nashauri kwamba mapendekezo yalivyo katika hiyo Bodi yabaki kama yalivyo. Sisi wenyewe tutakuwa na utaratibu wetu wa kushauriana na Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar.

**MHE. RASHID ALI ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, huyu Mwanasheria Mkuu wa Jamhuri ya Muungano ni yupi? Huyu anawakilisha Jamhuri ya Muungano; kule kuna *AG* wake na Jamhuri ya Muungano, sasa hii haileti *balancing,* inaleta mashaka. Mimi sikubaliani na hoja hii ya *AG* kwamba katika fedha, yupo mtu ambaye anashughulikia fedha kule Zanzibar; na haya mambo ya sheria ni vizuri, haya ni mambo ya Muungano bwana aje kutoka Zanzibar. Mimi sikubaliani na hoja ya *AG*.

**MWENYEKITI**: Hii ilikuwepo katika sheria *original*? Sheria ya awali ilisemaje? *Principal law*!

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *principal law Higher Education* haina Mwanasheria wa Zanzibar, kwa sababu ukiangalia kwenye jedwali lile utaona; samahani nitasoma kama ifuatavyo:-

Sorry! *(Makofi)*

*[MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI]*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimewahi kuwa Mwalimu, nimewahi kuwa Jaji, kwa hiyo, hata ukipiga makofi hayo hayanibabaishi. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ni Chairman; pili, ni *Director of Higher Education;* tatu, ni *one member representing the Ministry responsible for education in the Revolution Government of* Zanzibar, *one member from the Treasury*, *the Director of Technical Education* na hawa wanaweza kuwa ni Wazanzibar pia; *legally qualified member from the Attorney General Chambers, one member representing the Employers Association of Tanzania, one member from the Financial Institutions, one member nominated by an organ representing Public Higher Education Institutions, a member nominated by an organ representing Private Higher Education Institution, a member representing the Ministry of Education and Culture, and one member representing the Ministry responsible for Finance in the Revolutionary Government of Zanzibar, and one student representing Public Higher Education Institutions and a student representing Private Higher Education Institutions.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hapa unachoweza kufikiria ni yule anayewakilisha *Finance*, lakini *AG* hakuwepo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hamad Rashid.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Hoja ya Mheshimiwa Rashid nafikiri ina-*stand* hasa ukiona orodha aliyoisoma *AG* ambayo na mimi bahati nzuri ninayo, inaonesha wazi kwamba hawa wote waliotajwa wapo kwenye Makao Makuu ya Muungano. Sasa kama hawaku-*specify* kwamba huyu atatoka Zanzibar utakuta katika Bodi nzima hii hawatazidi watu wawili ambao watatoka Zanzibar. Kwa sababu iliyobaki hapa ni utashi wa mteuzi tu kama sheria haikusema. Kwa hiyo, nilifikiri Mwanasheria Mkuu ungekubaliana na hili pendekezo angalau kuwa na hakika kuna watu wawili wametajwa ndani ya sheria. Ningeomba ukubaliane na hili pendekezo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mwanasheria Mkuu, ukimweka inakuwaje?

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nina marafiki zangu wengi sana Zanzibar kule, lakini hapa tunatunga sheria. *Concept* mimi naiona, falsafa naiona, lakini *interest* hapa ni nini? Ni kwenye elimu. Kwenye elimu, tayari ina mtu anayetoka kwenye Wizara ya *Finance in the Revolutionary Government of* Zanzibar.

Kwenye marekebisho sijui kama yapo, 29 tumeweka: "*a member representing the Ministry responsible for the Finance in a the Revolutionary Government of Zanzibar.*"

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi bado nafikiria kwamba hiyo ingetosha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Rashidi, mara yako ya mwisho kusema.

**MHE. RASHID ALI ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli Mwanasheria Mkuu anasababisha mgogoro baina Zanzibar. Kwanini akataja kwenye *Finance* kwamba huyu ni kutoka Zanzibar? Basi na hii aifute, asitaje kabisa kutoka Zanzibar. Sisi tunasema, Wazanzibar haturidhiki kama hatujawekewa Mwanasheria pale ambaye amekuwa *specified* kutoka Zanzibar. Huyu ndiye anayesababisha migogoro yote, na ndiyo matatizo yote ya Muungano yanatoka hapa. Kwanini hawezi kuitaja? Kuna tatizo gani? Unaogopa nini?

**MWENYEKITI:** Jamani, mnapozungumza humu ndani jamani zungumzeni hoja msiwe mnaanza kutetemeka. Mwanasheria Mkuu tukiweka inaharibu nini?

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri kama unavyosema, unajua hatuwezi kufanya hivi kwa sababu tunataka kuharibu Muungano au vipi.

*[MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI]*

Mheshimiwa Rashid mimi na wewe tunaheshimiana sana na siwezi kuisaliti Zanzibar hata siku moja na unajua ni kwa sababu gani. Lakini hapa tulichokuwa tunazungumza...

**WAHESHIMIWA WABUNGE:** Hatusikii!

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Sasa kama hamsikii, sikilizeni basi!

**MWENYEKITI:** Sauti inakuwa ndogo kidogo.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Hawasikii! Wasikilize!

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashauri kwamba kwenye (f*) tuseme, two State Attorneys of rank of senior or above representing the Office of the Attorney General, one in Mainland the second one from Zanzibar.* Tutaandika vizuri kwa lugha nzuri. Usikasirike sana ndugu yangu. *(Makofi)*

*(Hoja ya Mheshimiwa Rashid Ali Abdallah iliamuliwa na Kuafikiwa na Kamati ya Bunge Zima)*

**MWENYEKITI:** *Okay.* Kwa hiyo, tumeikubali hoja ile kwamba tuongeze hivyo.

Ibara hii ina mtu mwingine, Mheshimiwa Mnyika.

**SCHEDULE OF AMENDMENTS TO BE MOVED BY HON JOHN JOHN MNYIKA, MEMBER OF PARLIAMENT FOR UBUNGO CONSTITUENCY AT THE SECOND READING FOR THE BILL ENTITLED THE WRITTEN LAWS (MISCELLANEOUS AMENDMENTS) (NO.3) ACT, 2013**

**Made under standing order 86(11) and 88(2)**

A bill entitled **"THE WRITTEN LAWS (MISCELLANEOUS AMENDMENTS) (NO.3) ACT,** 2013" is amended as follows:

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

*[MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI]*

**A:** In Clause 29 as amended by Government schedule sub section 29(1) (e) by deleting the word ***"one"*** and substituting it with the word ***"two".*** Also inserting the words ***"private and public"*** between the words ***"of and higher"***

……………………………….
**JOHN JOHN MNYIKA (MP)**
**UBUNGO CONSTITUENCY**

**06.11.2013**

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nina marekebisho kwenye kifungu cha 29 1(e) halafu baadaye nitaomba nafasi kwa ajili ya marekebisho ya kifungu cha 29 1(l).

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na 29 (1), (e) ambayo katika Muswada tunaoujadili ilikuwa inatamka" "*two students representing public and private Higher Learning Institutions."*

Kwa hiyo, sheria ilivyoletwa kwa maana ya Muswada kwenye ujumbe wa Bodi ya Mikopo ilikuwa ni wanafunzi wawili wanaowakilisha Vyuo vya Umma na Vyuo Binafsi, na marekebisho haya yalikuwa yanaendana na sheria ilivyokuwa mwaka 2004 kama ambavyo Mwanasheria Mkuu wa Serikali ameisoma hapo awali. Lakini cha kushangaza kumewasilishwa jedwali la marekebisho na Serikali ambalo kwenye *clause* (n) ukurasa wa tatu wa jedwali kuna mapendekezo ya mgawanyo mpya wa hii Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu ambapo sasa Serikali inapendekeza kwenye kifungu (e) "*one student representing students of higher learning institutions."* Kwa hiyo, mwanafunzi mmoja wa kuwakilisha wanafunzi wa elimu ya juu tofauti na sheria ilivyokuwa mwaka 2004 na tofauti na Muswada ulivyo hivi sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kupendekeza kwamba tufanye marekebisho ili kurejesha hali ilivyokuwa kama mwanzoni katika sheria ya mwaka 2004 na kama

ambavyo Muswada ulivyokuwa ili kuwe na wanafunzi ndani ya Bodi ya Mikopo, mmoja akiwakilisha Vyuo vya Umma, mwingine akiwakilisha Vyuo vya Binafsi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mahitaji ya Vyuo Vikuu yanatofautiana baina ya Vyuo Vikuu vya Umma na Vyuo Vikuu vya Binafsi.

Matatizo ya mikopo yanatofautiana baina ya Vyuo Vikuu vya Umma na Vyuo Vikuu vya Binafsi. Nikitolea mfano mdogo tu, Jimboni kwangu kuna Chuo cha Binafsi kinaitwa *St. Joseph University* kipo pale Kibamba, kiwango chao cha ada ukilinganisha na viwango vya ada katika Vyuo vya Umma ni tofauti. Mkopo akipewa mwanafunzi, akifika pale kwa viwango vya ada vilivyopo pale anashindwa kumudu masomo na hatimaye anashindwa kusoma pamoja na kuwa wote wamepewa mikopo kwa ajili ya elimu moja ya Sayansi ukilinganisha na yule aliyepo Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mazingira haya yapo kwenye maeneo mbalimbali katika Majimbo ya Wabunge mbalimbali yenye Vyuo vya Binafsi na Vyuo vya Umma. Sasa ili kuwe na uwakilishi wa maslahi ya pande zote, maslahi ya wanafunzi wa Vyuo Binafsi na maslahi ya Wanafunzi wa Vyuo vya Umma basi ni muhimu katika nyakati hizi ambapo kuna matatizo makubwa ya mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu kuwe na wanafunzi wa Vyuo vya Binafsi na Vyuo vya Umma kwenye uwakilishi wa Bodi ya Mikopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja na ninaamini Serikali itaikubali hoja hii. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mlata.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niunge mkono hoja ya Mheshimiwa Mnyika kwa sababu tunaowatetea hapa ni watoto wetu, vijana wetu ambao tunakutana nao kule Majimboni. Wanapokuwa wamepata nafasi, wanakosa nafasi kwenye Vyuo vya Serikali; wakipata nafasi kwenye Vyuo Binafsi utata unakuja pale

*Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*



wanapokwenda kupata ile mikopo. Kwa hiyo, kunakuwa na tatizo kubwa sana. Kwa hiyo, kama watapata uwakilishi wa kutosha ndani ya ile Bodi, naamini mambo yote yatawekwa vizuri. Kwa hiyo, naunga mkono hoja hiyo. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikuwa tumeshakubaliana kwamba irudi kama ilivyokuwa kwenye Muswada. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo, hiki kipengele tunarudisha kama ilivyokuwa kwenye *original* Muswada.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ila nafikiria Waziri wa Elimu yupo, napata taarifa hapa ambazo zinatakiwa zifanyiwe kazi.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikubaliane na Muswada kama ulivyokuwa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, hili limekubalika kwamba linabakia katika *original form* ya Muswada.

*(Hoja ya Mheshimiwa John J. Mnyika*
*iliamuliwa na Kukubaliwa)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mnyika hii imekubalika tuende ya pili.

**SCHEDULE OF AMENDMENTS TO BE MOVED BY HON JOHN JOHN MNYIKA, MEMBER OF PARLIAMENT FOR UBUNGO CONSTITUENCY AT THE SECOND READING FOR THE BILL ENTITLED THE WRITTEN LAWS (MISCELLANEOUS AMENDMENTS) (NO.3) ACT, 2013**

**Made under standing order 86(11) and 88(2)**

*Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*



A bill entitled **"THE WRITTEN LAWS (MISCELLANEOUS AMENDMENTS) (NO.3) ACT,** 2013" is amended as follows:

**B:** In sub section 29 (1) (l) by deleting the whole sub section and substituting with the new sub section: "l" ***two members representing public and private higher learning institutions"***

**.....................................**
**JOHN JOHN MNYIKA (MP)**
**UBUNGO CONSTITUENCY**

**06.11.2013**

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwa mwelekeo ule ule ukiangalia jedwali la Serikali ukurasa wa tatu kipengele (n) kifungu cha 29 sehemu (l) kinasema *one member representing higher learning institution.* Hapa ni uwakilishi wa vile Vyuo sasa, siyo wanafunzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya Mheshimiwa Rais kuunda Tume iliyokwenda kuchunguza masuala ya Bodi ya Mikopo, ripoti ile ya Tume pamoja na kuwa imefanywa kuwa siri, nilipata wasaa wa kuona sehemu ya matokeo ya ripoti ya ile Tume. Kati ya mambo yaliyoainishwa na ripoti ya ile Tume ni mazingira ya utofauti wa utawala wa Vyuo katika usimamizi na ufuatiliaji wa masuala ya mikopo. Kufuatia ripoti ile ya Tume, Serikali ilibadili mfumo wa utoaji wa fedha za mikopo. Badala ya Bodi kupeleka fedha kwa wanafunzi moja kwa moja kukawa na mfumo unaohusisha vilevile Vyuo katika mchakato wa utoaji wa mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu.

Kwa hivi tunavyozungumza, Vyuo mbalimbali vinahusika kwa namna moja au nyingine katika mchakato wa utoaji wa mikopo ya wanafunzi inayohusu Vyuo vyao. Katika mazingira kama haya, mazingira ya utawala wa Vyuo Binafsi yanatofautiana na mazingira ya utawala wa vyuo vya

umma, na mahitaji ya kiutawala ya Vyuo Vikuu vya Umma yanatofautiana na mahitaji ya Vyuo Vikuu Binafsi. *(Makofi)*

Hii Bodi ya Mikopo ukiondoa suala la kusimamia suala la kusimamia mfumo wa utoaji wa mikopo kwa wanafunzi, Bodi hii ndiyo inafanya vile vile maamuzi juu ya viwango juu ya madaraja na juu ya mfumo mzima wakati ambapo ada ya Vyuo vya Umma na ada za Vyuo Binafsi zinatofautiana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mazingira kama haya, pendekezo langu ni kwamba badala ya kuwa na mwakilishi mmoja peke yake anayewakilisha Vyuo Vikuu kwa maana siyo ya Serikali za wanafunzi sasa; ni kwa maana ya utawala wa Vyuo Vikuu; kuwe na Wawakilishi wawili ili kuwe na Mwakilishi wa Vyuo Vikuu vya Umma kwa ajili ya kuwakilisha mazingira ya Vyuo Vikuu vya Umma ndani ya Bodi ya Mikopo, na kuwe na Mwakilishi wa Vyuo Vikuu Binafsi kwa maana ya kuwakilisha mazingira ya Vyuo Vikuu Binafsi ndani ya Bodi ya Mikopo wakati wa kufanya maamuzi juu ya madaraja, juu ya viwango, juu ya mfumo mzima wa utoaji wa mikopo nchini kwa Sekta ya Umma na Sekta Binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini kwa *spirit* ile ile ya maamuzi ya kwanza, uamuzi huu vilevile Mwanasheria Mkuu wa Serikali atauunga mkono. Nashukuru sana.

**MWENYEKITI:** Mwanasheria Mkuu wa Serikali au Waziri wa Elimu! Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri kama tumeikubali *concept* ile ya *private* na *public institutions, it goes by saying* na hapa pia tufanye hivyo. Lakini nilikuwa natahadharisha kwamba unajua ukubwa wa Bodi na wenyewe unaweza ukawa ni tatizo. Naichukua hoja lakini ukubwa wa Bodi na wenyewe unaweza ukawa ni hoja.

Kwa hiyo, ile ya (i) tuweke: "*two members, one from Public University and the other one from Private University*."

*Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

**MWENYEKITI:** Kwenye marekebisho pale tunaweka (l). Umesema ni (l)? Kwa hiyo, mapendekezo ya Mheshimiwa Mnyika yamekubalika. Tunaendelea.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Mhe. John J. Mnyika)*

Ibara ya 30

**SCHEDULE OF AMENDMENTS TO BE MOVED BY HON. LETICIA NYERERE, MEMBER OF PARLIAMENT (SPECIAL SEATS) AT THE SECOND READING OF A BILL ENTITLED "THE WRITTEN LAWS (MISCELLANEOUS AMENDMENTS) (NO. 3) ACT, 2013"**

[Made Under S.O. 86(9) and (11)]

A Bill entitled "The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 3) Act, 2013" is amended as follows:

C: In Clause 30, by-

(a) Deleting the proposed paragraph (u);
(b) Renaming the proposed (v) as paragraph (u); and
(c) Renumbering paragraph (u) as paragraph (v).

Dodoma ……………………………
1st November, 2013 HON. LETICIA NYERERE (MP)
SPECIAL SEATS

**MHE. LETICIA M. NYERERE:** Ahsante Mheshimiwa Mwenyekiti. Nimependekeza marekebisho kama ifuatavyo:-

*In clause 30, by- (a) deleting the proposed paragraph (u); (b) renaming the proposed paragraph (v) as paragraph (u); and renumbering paragraph (u) as paragraph (v).*

*[MHE. L. M. NYERERE]*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimependekeza mabadiliko hayo kwanza kwa sababu kubwa kabisa; *function* ya Bodi hii ni kutoa mikopo na wala siyo kutoa *grants na scholarships.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba niainishe *functions* za Bodi; *to assume responsibility for the control and management of any loans funds as vested in the Board under this Act.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa hakuna *grants* wala *scholarship. (b); "To formulate the mechanism for determining eligible students for payment of loans under the Act*." Sijaona *grant* wala *scholarships. (c); "To administer and supervise the whole propose of payment and repayment of loans.* Hapa wanazungumzia *loans* bado Mheshimiwa Mwenyekiti. *Next; to keep the register and other records of student's loan beneficiaries under the Board.* Bado sijaona *scholarships* wala *grants. Next; to advice the Minister on matters of policy and of the Law concerning provisions and recovery of loans to students under this Act. Again* hatuna *grants* wala *scholarships. To establish operational link with higher education institutions with student loan beneficiaries for facilitating a small efficient and effective administration of the Loan Funds.* Hatuna *grants* wala *scholarship.*

*Next; to establish operational link with employer's of loan beneficiaries for the purpose of facilitating the recovery of loans to students under this Act.* Hakuna *grant* wala *scholarship.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani maelezo haya yanajitosheleza kabisa na naamini Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, ameona kwamba kuchomekea *grants* na *scholarship* kwenye *loan*, kwenye shughuli za mikopo, utaleta mkanganyiko. Katika *functions* za Bodi haya mambo hayapo, hawazungumzii sehemu yoyote kuhusu *grants* wala *scholarships.*

*[MHE. L. M. NYERERE]*

Tatizo lingine ni kwamba, tunapochanganya vitu hivi viwili, Bodi itashindwa kufanya kazi yake kwa usahihi na kwa uaminifu, ikizingatiwa kwamba, kutakuwa na *criteria* kwa ajili ya *loans na criteria* kwa ajili ya *grants and scholarships.* Sasa nani anapewa *scholarships;* nani anapewa *grant*; nani anapewa *loan?* Naomba mabadiliko haya yakubalike na *I don't expect a silence.*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Kengele imegonga.

**MHE. LETICIA M. NYERERE:** *Okay.*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu, nadhani hoja yake umeisikia?

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Sheria na sijui unasoma Sheria gani, kwenye Sheria, kifungu cha 7 kimetoa *powers of the Board* na nitaeleza. Tunachofanya sasa ni kuipa Bodi, mamlaka ya hayo mambo ambayo unasema yasiwekwe na ni kwa ajili ya fedha ambazo zimetolewa na Wizara kwa kazi hizi. Tungeweza kutoa *grants.* Sasa najua umeishi Marekani pale; *without scholarship what do you expect for the education?* Kwa sababu Bodi inaweza kuona kuna watu wana vipaji maalum, wakawapa *scholarship* kwenda kufanya kitu kingine.

China inapeleka Marekani wanafunzi laki tano kila mwaka. Sasa ukiondoa hiyo ukisema tusiwape hayo mamlaka sielewi una maana gani! *Grants* inawezekana kutolewa, kwenye Sheria ya sasa, ukiangalia kwenye 7*(g)* ilivyo sasa inasema; *to grant loan money to students. We have been granted such loan in accordance with the provision of the Act*.

Sasa *grants* ndiyo hizo na kuna *grants extra* pia. Kama fedha ipo na watu wanaomba na wanastahili

kupata, *why not?* Tunachofanya hapa ni kuipa mamlaka zaidi, kuipa vitu ambavyo inaweza kufanya bila kuvunja Sheria. Kwa hiyo, nadhani siyo vizuri kuifuta. Kwa hiyo, ile amri yako kwamba nikubali, kwa kweli hapana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Leticia kwa kifupi!

**MHE. LETICIA M. NYERERE:** Ahsante Mheshimiwa Mwenyekiti. Kutokana na maelezo ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, katika uelewa wangu nikupe mfano wa Amerika; *student's loan is a student's loan, student's aid and grant is a student's aid and grant, you can never mix the two. Therefore,* napendekeza ili tuondoe *confusion* ya kuwawekea kiini macho Watanzania wasielewe nini anastahili kupata mkopo, nini anastahili kupata *scholarship* au *grants* kwa nini tusiwe wazi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuainishe kama ni Bodi ya Mikopo iwe ya mikopo kama ni ya *student aids* na *grant* iwe kwa ajili hiyo. Kubabaisha kwamba sijui inaweza ikawa na *funds;* kwa nini isitoe kwenye *grants* au *scholarship* na wakati huo huo ikafanya mambo ya *loan*? Mimi simuelewi kabisa Mheshimiwa *Attorney General.* Namheshimu sana, ni shemeji yangu, lakini kwa hili naomba aangalie upya na bado nina-*insist* kwamba, iwe *specified* kama hii Bodi ni kwa ajili ya mikopo isemekane ni kwa ajili ya mikopo na si vinginevyo. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** *Practically* ikoje sasa hivi? Inafanyika vipi; Naibu Waziri au nani anahusika inavyofanyika sasa hivi?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Bodi hii Sheria ilivyo ni kwa ajili ya mikopo. Sasa pale tulipokuja na neno vipaumbele hasa vya masomo ya udaktari, ndipo ilipoonekana kwamba, wale wanaosomea udaktari wapewe *grants;* ni katika utendaji wa kuangalia vipaumbele. Kwa hiyo, tunatoa

*grants* na *scholarship* kwa udaktari kwa masomo ya vipaumbele.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati tunaifanyia marekebisho Sheria ya Mikopo hii ya Wanafunzi, tuliweka vigezo kwamba ni akina nani watapata kwa asilimia ngapi. Pia kuna kozi tulizitaja kwamba wao watapata *grant* moja kwa moja ikiwepo madaktari na fani zinazohusiana na sayansi. Ilisemwa kabisa kwamba, watapewa *grant* na wanafanya hivyo.

**MWENYEKITI:** Sipendi tuendelee kubishana sana maana muda wenyewe umeisha. Mheshimiwa Engineer Manyanya, nilikuona kwa muda mrefu umesimama!

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti. Mimi nadhani kwa jinsi ambavyo mchango wa mtoa hoja ulivyokuwa, imeonekana kweli inaweza kukatokea *confusion* kama hizi. Bado nakubaliana kwamba, kuna umuhimu mkubwa sana kwa Serikali kuona maeneo ambayo yana umuhimu wa kutoa *grants.*

Naamini kwa leo nasimamia lile lile, kwa mfano, hata kama ni walemavu au wale ambao hata kulipa bado kuna kazi ngumu. Pia kuna kozi ambazo ukiziangalia hata kusoma kwake ni gharama kubwa kiasi kwamba hata huyo aliyesoma kuja kuilipa peke yake inakuwa ni kazi kubwa; lakini Serikali inamhitaji huyu mtu katika kuwezesha shughuli za kitaifa. Kwa hiyo, hapo inabidi Serikali yenyewe itoe kama *subsidy* ili kumwezesha huyu mtu kusoma na kuweza kutumika katika nchi kwenye suala kama hili. Kwa hiyo, mimi naona kwamba utata upo na umuhimu upo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *(Makofi)*

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Hoja hii ni ya msingi sana na mimi nakubaliana na maelezo ya Naibu Waziri na ya mtoa hoja. Kifungu kilivyo hapa ni kipana, hakisemi hayo ambayo anayasema

*[MHE. FELIX F. MKOSAMALI]*

Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba, ni kwa wanafunzi wa sayansi au hao wenye *special needs* peke yao. Kinaeleza tu kwamba ni Bodi ndiyo itakuwa inaamua yenyewe kutoa hizi *grants* na *bursaries.*

Tumeona kumekuwa na matatizo makubwa sana kwenye hii mifumo ya mikopo. Kwa kutoweka utaratibu ukawa unajulikana ni akina nani hao ambao wanapewa hizo *grants* na siyo mikopo, akina nani wapewe misaada na ni akina nani wapewe *scholarships*, tutaongeza matatizo makubwa sana kwenye Bodi ya Mikopo, ambayo imekuwa inalaumiwa kushindwa kupanga viwango vizuri.

Kwa hiyo, nashauri tu kama wanasema Bodi iwe inatoa hizi *grants, bursaries* na *scholarships,* waongeze hiki kifungu, lakini watuambie ni kwa utaratibu gani na kwa vigezo gani.

Nikumbushe tu Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili liliwahi kuletwa kwenye Bunge hili tukalikataa. Lililetwa Kamati ya Huduma za Jamii, moja ya mambo tuliyokataa na hili jambo ni moja ya mambo tuliyoyakataa. Tuliyakataa kwenye Kamati ya Katiba na Sheria tulipokutana, siku hiyo ilikuwa inaongozwa na Mheshimiwa Ndugulile. Moja ya mambo ambayo tuliomba ufafanuzi ili yapite vizuri yasije yakaleta *confusion* ni hili. Kwa hiyo, naomba hoja hii itazamwe kwa umakini zaidi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu, kuna wasiwasi lakini.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sijui hofu ni nini! Tunachofanya hapa, Sheria ilivyo sasa ndugu zangu, inatoa *powers to the Board.* Tunachofanya kwenye marekebisho haya tuliyoleta sisi ni kuongeza katika zile *powers* za Bodi kuiongezea *power* moja hiyo ya kutoa *grants* na mimi sioni tatizo. Tatizo linakuja kwenye *implementation, operationalization* ya *power* za Bodi.

*Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

*[MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI]*

Sasa pendekezo lililoko mezani ambalo limetoka kwa Mheshimiwa Nyerere, siwezi kumkana, ni kwamba; hizo *powers* zifutwe. Sasa ukizifuta Bodi hata ukitaka kuja kufanya utafanyaje; si lazima ziwepo kuiwezesha Bodi iweze kuifanya hiyo kazi? Hoja iliyoko kwamba zile zifutwe, ukishaamua zifutwe ina maana kama Bodi haitakuwa na *powers* za kutoa *scholarship,* za ku-*grant* na haya mambo mengine. Mimi naona kama nitakuwa sifanyi kazi yangu ya Unasheria Mkuu, kuwashauri kwamba hilo mtakuwa mmefanya kosa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vizuri kuweka *powers* ili Bodi ikitaka kufanya, kwa utaratibu ambao Wabunge lazima, kama anavyosema Mheshimiwa Mkosamali, ni lazima Wabunge wa-*supervise* kwamba huu utaratibu kwa sababu nao pia unaweza kuleta matatizo na hiyo *fear* ya matatizo ndiyo ambayo mimi ninajua kwamba Wabunge wanaifikiria.

Kwa hiyo, kwa msingi huo, nashauri Waheshimiwa Wabunge, mnikubalie kwa sababu Muswada wangu huu; kwamba, hii Bodi ipewe hizo *powers.* Sawa? Kwenye *implementation* na Waziri yuko hapa anasikiliza, ni lazima tutakapokuwa tunaleta, nafikiri Muswada utakuja, Wabunge washiriki, kama ni kupitia kwenye Kamati inayohusika, washiriki na wakati mwafaka kama ni kwa kupitia Sheria hii tena, mimi nina-*undertake* kwamba, nitafuatilia Sheria iletwe Bungeni.

Kwa sasa tunachofanya ni kutoa *powers* ambazo kwa sasa hawana. Sasa tunawapa kwamba ukitaka kutoa *scholarship* unaweza. Kwa utaratibu gani? *Let us adjoin that* kwa sababu nafikiri ndiyo *speed*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kuwa *very democratic.* Nia yetu ni hiyo na Mheshimiwa Leticia Nyerere ameweza kuiondoa na nafikiri amekubali kwamba ibaki lakini tuwe makini kwenye *operationalization.*

**MWENYEKITI:** Haya Mheshimiwa Leticia Nyerere, dakika mbili tupe uamuzi. Baada ya maelezo yote haya kwamba, *scholarship* hatukatai, *grant* hatukatai, lakini hofu ilikuwa *how do you mix the two?* Nadhani ndiyo ilikuwa hoja?

**MHE. LETICIA M. NYERERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo lililopo ambalo mimi pamoja na Wabunge wengine tunahofia ni ule utaratibu watakavyofanya, jinsi ya kutoa mkopo au *grants.* Mtoto wa nani ambaye ata-*qualify grants* na mtoto wa nani hata-*qualify* ata-*qualify for a loan.* Hili ndiyo tatizo kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo ya *AG* nakubaliana nayo, lakini ninachomwomba kama anaamua kutokubaliana na hoja yangu, alete *amendment* nyingine itakayozungumzia hizo *grants* na *scholarships* na aeleze ni Bodi ya aina gani, itafuata utaratibu gani, katika kutoa *scholarships* na *grants* na si vinginevyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Naomba tuendelee, eenh Mwenyekiti wa Kamati ya *Social Service!*

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi nami nichangie kama ifuatavyo:-

Ninakubaliana na pendekezo la Mwanasheria Mkuu wa Serikali, baada ya kuelewa maelezo aliyokuwa anazungumzia Mheshimiwa Leticia Nyerere. Nakubaliana na pendekezo, kwa sababu huwezi kufafanua yote, itategemea Bodi kwenye vikao vyao watakavyoamua. Pia nategemea kwamba, baada ya Sheria kutakuwa na Kanuni ambazo zitasaidia kufafanua. *(Makofi)*

Kwa hiyo, nakubaliana na pendekezo la Mwanasheria baada ya ufafanuzi wa Mheshimiwa Leticia Nyerere.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kukataliwa)*

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo, pendekezo limeondolewa, tunaendelea na kifungu kinachofuata.

Ibara ya 31

**SCHEDULE OF AMENDMENT TO BE MOVED BY THE HON. FREDERICK M. WEREMA, THE ATTORNEY GENERAL AT THE SECOND READING OF A BILL ENTITLED "THE WRITTEN LAWS (MISCELLANEOUS AMENDMENTS)" (NO. 3) ACT, 2013"**

*Made under S. 86(10)(b)*

O: In Clause 31 by deleting the proposed paragraph (b) and substituting for it the following:

"(b) deduct from the basic salary of every employee who is the loan beneficiary such percentage as the Board may from time to time determine."

Dodoma, **FMW**
..............................., 2013 AG

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Halima Mdee! Leo mpaka tumalize hapa hatutoki. *(Kicheko)*

**SCHEDULE OF AMENDMENTS TO BE MOVED BY HON HALIMA JAMES MDEE, MEMBER OF PARLIAMENT FOR KAWE CONSTITUENCY AT THE SECOND READING OF A BILL ENTITLED "THE WRITTEN LAWS (MISCELLANEOUS AMENDMENTS) (NO. 3) ACT, 2013**

Made Under Standing Order 86(11) and 88(2)

A Bill entitled "The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 3) Act, 2013" is amended as follows:

G: In Clause 31 by deleting the words "such percentage as the Board may from time to time determine" appearing after the word "beneficiary" as proposed in paragraph (b) and substituting it with the words "such sums not exceeding eight per centum of the monthly salary."

Dodoma ...........................

Halima James Mdee
Member of Parliament

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Mimi naleta mapendekezo katika Ibara ya 31 kwa madhumuni ya kurekebisha Kifungu cha 20(1)(b) kama kilivyopendekezwa cha Sheria ya Bodi ya Mikopo. Ukiangalia hii Sheria kama ilivyokuwa mwanzo, ilikuwa inatoa jukumu la mwajiri kukata kiasi fulani cha fedha kwa mtu ambaye ni *beneficiary* wa mkopo uliotolewa na Bodi ya Mkopo kwa mujibu wa Sheria ambavyo ilikuwa imetaja.

Sasa hiki Kifungu kipya ambacho kimeletwa leo mapendekezo yangu ni katika *clause* hii kwa ku-*delete the words "such percentage as the Board may from time to time determine" appearing after the word "beneficiary" as proposed in paragraph (b) and subtituting it with the words "such sums not exceeding eight per centum of monthly salary."*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivi kwa sababu tukiacha Kifungu hiki kama mabadiliko yalivyoletwa na

*[MHE. H. J. MDEE]*
Mwanasheria Mkuu wa Serikali, tafsiri yake ni nini? Sheria imetoa wigo mpana wa Bodi ya Mikopo kuamua ni kiwango gani cha fedha kitatengwa katika mshahara wa mtu ambaye ame-*benefit* kutoka kwenye ule mkopo. Sasa tukiacha kipengele kikae na ombwe mpana hivi, tutatoa *room* kwa watu ambao wamepewa dhamana ku-*abuse.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo yangu ni kwamba, hii *percent* iwe na *limit* na isi-*exceed eight percent,* ili kutoa *room* sasa kwa Bodi ya Mikopo ambayo ina dhamana hiyo, kucheza kati ya moja na nane, kuangalia itamtoza mtu asilimia gani ya mshahara wake kutokana na ajira na kiwango cha mshahara ambacho analipwa na ni utaratibu ambao ulikuwa unatumika mwanzo.

Mwanasheria Mkuu wa Serikali atakumbuka alituambia hata sisi kwenye Kamati kwamba, *proposal* yao ya mwanzo ilikuwa isizidi asilimia nane ili kuweza kucheza hapo. Kwa sababu tunafahamu kwamba, kuna makato mengi sana kwenye mshahara wa mfanyakazi, sasa tukiacha mamlaka haya makubwa, unaweza ukakuta Bodi ikaagiza mwajiri akate fedha kubwa sana ambayo mwisho wa siku ikawa haimsaidii huyu mfanyakazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mapendekezo yangu ni kuitaka Serikali kusiwe hakuna mwisho wa mamlaka ya Bodi kukata *percent,* ila wawekewe ukomo. Sasa wao wawe wanacheza katika huo ukomo kutokana na mahitaji na vilevile kwa sababu Sheria inaruhusu mtu kama yuko kwenye nafasi nzuri ya kuweza kulipa mkopo wake kwa haraka aweze kufanya hivyo. Tusitengeneze Sheria ambayo inaweza ikawa kandamizi na ikawa ni mwiba kwa hawa vijana wetu ambao wanamaliza shule na wanaanza maisha.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo ni kwamba, unajua huna *basis* ya kusema *between one and eight.* Tusiwe *prescriptive,* kama unasema unatunga Sheria unasema mtu akiumwa malaria

akifika Hospitali basi Daktari amchome kuanzia *cc* mbili mpaka nne. Mimi ninafikiri kwamba, haya kwenye *composition* ya Bodi, naona tumekuwa makini sana kwenye *composition* ya Bodi; tunafikiri hawa *Board Members* watakuwa na uwezo wa ku-*determine* wakifikiria mazingira yaliyopo kuliko kuweka *percentage* kwenye Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huo ndiyo wasiwasi wangu tu, lakini kama unasema *five percent*, *eight percentage*, *I have no problem;* isipokuwa *what is the basis of eight? Why not ten? Why not 15?* Mishahara hii inatofautiana, *what will happen to those who are not working* ambao wanakuwa *self employed* na *fluctuation* za *income* yao zipo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri tukubaliane na mawazo haya ya Serikali. Sisi tulivyokuwa tumependekeza vile tulikuwa na sababu, lakini sasa zile sababu baada ya kukaa tukaona hakuna *basis,* kwa sababu huwezi ku-*determine* kitu kama huna *data,* huna *facts.* Ni vizuri tuiachie Bodi hayo mamlaka, *we should not be too much prescriptive,* tutakuwa tunatunga Sheria ambazo baadaye hazitekelezeki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri tuiache hivyo, tuipe mamlaka hiyo Bodi ku-*determine* hiyo *rate*. Sidhani kama hiyo Bodi itakuwa *very unreasonable* na Waziri yupo anayesimamia Bodi hiyo, aone hizo asilimia zimekuwa *so much high.* Mimi nafikiri Mheshimiwa Mdee, tukubaliane kwamba hiyo iwe kama ilivyo.

**MWENYEKITI:** Jamani *to make progress.* Mheshimiwa Mdee, baada ya maelezo haya?

Mkumbuke tumeongeza wanafunzi wawili kwenye Bodi; *from higher* na nini, tumeongeza na wengine taasisi.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachosema hapa ni kwamba, Sheria hii inasema pamoja na mambo mengine, *as the Board may determine from*

*time to time.* Kitu ambacho nimependekeza na ambacho Mwanasheria Mkuu wa Serikali anafahamu, mapendekezo ya mwanzo ya Serikali, mwanzoni kabisa na yeye mwenyewe alikiri kwenye Kamati yetu kwamba, walikuwa wanafikiria kuweka kiwango kisichozidi asilimia nane, ili kuiwezesha Bodi sasa wakati inapanga iangalie nani ambaye atatozwa nini na kwa kiwango gani kutokana na mahitaji ama kutokana na aina ya kazi ama kutokana na kipato ambacho anakipata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ukiacha wigo mpana kama huu, ni kweli kabisa Bodi ina uwakilishi wa wanafunzi wawili, lakini uwakilishi wa wanafunzi wawili kati ya Wajumbe wa Bodi 14, inawezekana yakafanyika maamuzi ambayo hayataangalia masilahi ya hawa watu ambao mwisho wa siku wao ni wanafunzi, lakini baadaye ndiyo wanaingia kwenye soko la ajira, kisha wanatakiwa walipe huu mkopo. Nami pendekezo langu la kuweka hii asilimia isizidi ni kwa kuzingatia kwamba, ukiangalia *salary slip* ya mfanyakazi yeyote, kuna makato mbalimbali zaidi ya matano. Sasa kama kuna makato hayo mbalimbali wanatumia vigezo gani kuhakikisha kwamba, pamoja na hayo makato hii Sheria isitoe rungu kwa mtu ambaye anaweza akatumia vibaya kuathiri yale makato mengine?

Kwa hiyo, katika muktadha uleule ambao Serikali mlifikiria asilimia nane, ndiyo maana nimelirejesha kwamba, kwa sababu ninyi hamuwezi kuwa mlifikiria wakati hamkufanya utafiti. Kwa hiyo, lengo ikiwa ni kuweka *balance* ili watu ama Bodi isipewe mamlaka ambayo yanaweza yasitumike vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Bunge lako Tukufu, kwa kuzingatia kwamba, vijana ambao ni *beneficiary* wa hii mikopo wapo kwenye Majimbo yetu na ni vijana ambao wanahangaika na kazi hizi za kushikashika zisizokuwa na mshahara wa kutosha, tuwatetee ili tuweze ku-*limit* mamlaka ya Bodi.

**MWENYEKITI:** Hivi ninyi mnafikiri asilimia nane ni ndogo hiyo; ni kubwa siyo ndogo! *(Kicheko)*

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, asilimia nane ni *maximum.* Ndiyo maana nimesema *not exceeding.* Kwa hiyo, wao watakuwa wanacheza pale katikati kutokana na mahitaji, wanaweza wakaweka asilimia mbili, asilimia moja, asilimia tatu, lakini isizidi. Sasa usipoweka ukomo anaweza hata akaamua asilimia ishirini au asilimia thelathini kwa sababu mmewapa *discretion.* Sasa *as long as* mmewapa *discretion,* wakiamua mtakujaje kupingana nao wakati mkopo ni maridhiano na Bodi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapendekeza hilo.

**MWENYEKITI:** Mimi pia sipendi maana tunachukua muda mrefu kwa mambo madogo sana. Mheshimiwa Waziri wa Nchi (TAMISEMI)!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani tumeichagua Bodi na tumeiongezea watu wengi sana. Tungeiamini hiyo Bodi, kwa sababu tukiweka kitu kwenye Sheria hapa, maana yake tunaifunga Bodi isiweze kufanya marekebisho yoyote kwa kuwa tayari wakitaka kufanya chochote ni lazima turudi tena hapa tufanye *amendment.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini anayesema asilimia nane ni kubwa sana, Bima ya Afya yenyewe tunatoa asilimia tatu tu, lakini ukiangalia ni kiasi kikubwa sana kinachokatwa. Kwa hiyo, naomba hebu tuamini kwamba, huko kwenye Bodi kuna watu wenye akili timamu, wenye busara na wenye uwezo wa kufikiri pengine kutushinda sisi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Chenge!

Mitambo katika sehemu ile haifanyi kazi kwa asilimia kubwa, sijui kwa nini!

**MHE. ANDREW J. CHENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Naishukuru Serikali kwa maelezo mazuri. Nataka nitumie uzoefu wangu mdogo kwa kuonesha tu maana ya uzuri wa mapendekezo ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, chukua baadhi ya hawa vijana waliochukua mikopo, wataajiriwa na Serikali na Taasisi zake. Sasa hivi ipo Sheria ambayo inasimamia kiwango ambacho mwajiri anaweza akamkata mwajiriwa kama amechukua mkopo. Huwezi ukamkata mwajiriwa zaidi ya theluthi moja ya mshahara wake.

Sasa unataka uiachie Bodi iwe na unyumbulifu wa kuyafahamu haya, inapopanga itazingatia na ninajua Waziri mwenye dhamana atakapotengeneza hata Kanuni kuielekeza Bodi kwamba, mnapopanga zingatieni haya, ndiyo mambo yatakavyofanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba tuyachukue mapendekezo ya Serikali, twende mbele. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ni kweli kwamba, hatufuti Sheria nyingine; mtu akichukua mkopo katika hali ya kawaida huwezi kumchukulia mpaka zaidi ya *one third* ataishije. Sasa tuyafanyie uamuzi mapendekezo ya Mheshimiwa Halima Mdee.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja ya Mhe. Halima J. Mdee iliamuliwa na Kukataliwa)*

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo, mapendekezo ni ya Serikali.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 32

**SCHEDULE OF AMENDMENT TO BE MOVED BY THE HON. FREDERICK M. WEREMA, THE ATTORNEY GENERAL AT THE SECOND READING OF A BILL ENTITLED "THE WRITTEN LAWS (MISCELLANEOUS AMENDMENTS)" (NO. 3) ACT, 2013"**

_____________

*Made under S. 86(10)(b)*

______________

A Bill entitled "The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 3) Act, 2013" is amended as follows:

P: In Clause 32, by deleting paragraph (c) and substituting for it the following:

"(c) such sums accrued from the repayment of loans granted and interest thereof;"

Dodoma **FMW**
..............................., 2013 AG

**MWENYEKITI:** Kifungu cha 32?

Wewe una maneno? Enhee, Mheshimiwa Mnyika?

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ufafanuzi kutokana na Jedwali lililowasilishwa na Serikali. Jedwali hili ambalo ukurasa wa 4 linatamka...

**MWENYEKITI:** Kifungu cha 32?

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha 32 hicho, Jedwali la Serikali. Kifungu hiki kinazungumzia *information of loan beneficiaries; 32(a)(1)* inayotaka kuingizwa sasa inasema; *"Every institution or company, whether public or private, shall at request of the Board, furnish to the Board information relating to loan beneficiaries who are employed in such institutions or company."*

*[MHE. J. J. MNYIKA]*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *section two* yake inasema; *"A person who fails to comply with the requirement of sub-section (1), commits an offence and the penalty prescribed under sections 21 and 23 shall apply."* Kwa hiyo, Kifungu hiki kinataka Bodi ikitaka taarifa, mwajiri au taasisi atoe taarifa na ambaye hatatoa taarifa kuhusu mwajiriwa, basi anafanya makosa kwa mujibu wa Kifungu cha 21 na 23 cha Sheria Mama.

Ukija kwenye Kifungu cha Sheria Mama sasa cha 21, kwanza kinahusu *penalty for delayed remmitence.* Kwa hiyo, kinahusu adhabu kwa kuchelewa kupeleka marejesho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hapa Kifungu hicho cha adhabu ya kuchelewa kupeleka marejesho kinataka kutumika kwenye adhabu ya kuchelewa kupeleka taarifa; yaani marejesho ya fedha sasa hukumu hiyo hiyo inakuwa sawasawa na kuchelewa kuleta taarifa. Kikubwa zaidi ni *sub-section two* ya *section 21(2),* hii ya *21* inasema; *"Where an employer fails without reasonable excuse to notify the Board that he has in his employment a students loan beneficiary within a specified period, that employer commits an offence and is liable on conviction to a fine not less than one million shillings."*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kama mwajiri akichelewa kutoa taarifa kwa Bodi bila sababu za msingi kwamba, ana mtu aliyenufaika na Bodi ya Mikopo aliyeajiriwa kwenye taasisi yake, anastahili kupewa hukumu ya *fine* isiyopungua shilingi 1,000,000. *Fine* isiyopungua shilingi 1,000,000, kwa hiyo, inaweza ikawa *fine* ya milioni 10, milioni 50. *Fine* isiyopungua milioni moja kwa kuchelewa kutoa taarifa kwamba, umemwajiri mtu ambaye amenufaika na Bodi ya Mikopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitendo cha kuhamisha hukumu hii kwenye Kipengele cha sasa Kipya, ambacho hakihusu suala la kwamba, umemwajiri au haujamwajiri mtu aliyenufaika kwa Bodi ya Mikopo bali taarifa yoyote ile. Kwa mfano, mwajiri anaandikiwa barua ya kuulizwa mfanyakazi

wako anapokea mshahara kiasi gani, ili Bodi ya Mikopo ifanye uamuzi. Mwajiri akichelewa kutoa hiyo taarifa, maana yake ni kwamba, huyo mwajiri anaweza kuhukumiwa kulipa *fine* isiyopungua milioni moja, inaweza ikawa milioni tano, kumi au milioni 50.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa misingi ya Kifungu kilivyo wazi hivi, kwa kuwa sina jedwali katika hiki Kifungu, ningependa kupata ufafanuzi kwa Serikali; ni kwa nini imeamua kuhamisha masharti yanayohusiana na mambo mengine kuyatumia kwenye Kifungu kinachohusu masharti ya mawasiliano ya kitaarifa baina ya mwajiri pamoja na Bodi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ni kwa nini Serikali imeamua kuendeleza mtindo wa hukumu zinazoweka ukomo wa chini na zinaacha ukomo wa juu? Hukumu ambazo zinatoa *discretion* kubwa ya hukumu kutolewa kubwa kuliko kiwango hata cha makosa yenyewe?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeomba ufafanuzi kutoka kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali na kama ufafanuzi hauridhishi basi Mwanasheria arekebishe mwenyewe hivi Vifungu kuondoa huo utata uliopo. Nashukuru sana. *(Makofi)*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *too much talking,* lakini nafikiri *issue* tunayopendekeza ni nini?

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

**MWENYEKITI:** Naomba ukae kwanza. Tunataka kusikiliza, msituchanganye na maneno. Hebu eleza Mheshimiwa.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachosema, Kifungu cha 32 kipo wazi; kule kuhakisha sijui kutoa wapi kwenda huku, sisi tunaona ndivyo

*Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

*[MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI]*
ilivyo. Sasa kama ulikuwa na hoja, ungeleta *Schedule of Ammendment* kusudi tujadili *Schedule of Ammendment* yako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sioni kama kuna tatizo; kinachosemwa pale *32(a)(1),* Kifungu Kipya kwamba, *institution* au kampuni, *whether public or private,* unapoombwa utoe taarifa za Bodi kuhusu watu uliowaajiri ambao ni *beneficiaries* wa mikopo hii, utoe, usipotoa unafanya kosa la jinai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama ni kosa la jinai si lazima kuwe na adhabu, ndiyo adhabu hiyo inakuwa *prescribed* hapo. Sasa kama ulikuwa unafikiri adhabu ni kubwa zaidi, ungeleta *Schedule of Amendment.*

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 33

**FURTHER SCHEDULE OF AMENDMENT TO BE MOVED BY THE HON. FREDERICK M. WEREMA, THE ATTORNEY GENERAL DURING THE SECOND READING OF A BILL ENTITLED "THE WRITTEN LAWS (MISCELLANEOUS AMENDMENTS) (NO. 3) ACT, 2013"**

(Made Under S.O. 86(10)(b))

A Bill entitled "The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 3) Act, 2013" is amended as follows:

C: By-

(a) adding immediately after Clause 32, the following new Clause:

Amendment of Section 27

33. The Principal Act is amended in section 27 by adding immediately after subsection (2) the following new subsection:(3) All funds granted to, ro received by any higher learning institution pursuant to this Act shall be

Cap. 418 audited and reported upon by the Controller and Auditor General in accordance with the Public Audit Act."

(b) renumbering Clauses 33 to 77 accordingly

Dodoma FMW
7th November, 2013 **AG**

*(Ibara mpya iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 34

**SCHEDULE OF AMENDMENT TO BE MOVED BY THE HON. FREDERICK M. WEREMA, THE ATTORNEY GENERAL DURING THE SECOND READING OF A BILL ENTITLED "THE WRITTEN LAWS (MISCELLANEOUS AMENDMENTS) (NO. 3) ACT, 2013"**

(Made Under S.O. 86(10)(b))

A Bill entitled "The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 3) Act, 2013" is amended as follows:

Q: By deleting Clause 33 and substituting for it the following:
"33. The principal Act is amended by deleting section 32A and substituting for it the following:

"Information of loan beneficiaries

32A.-(1) Every institution or company, whether public or private, shall at the request of the Board, furnish to the Board information relating to loan beneficiaries who are employed in such institution or company.

(2) A person who fails to comply with the requirement of subsection (1), commits an offence and the penalty prescribed under sections 21 and 23 shall apply."

Dodoma FMW
7th November, 2013 **AG**

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 35

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 36

**FURTHER SCHEDULE OF AMENDMENT TO BE MOVED BY THE HON. FREDERICK M. WEREMA, THE ATTORNEY GENERAL DURING THE SECOND READING OF A BILL ENTITLED "THE WRITTEN LAWS (MISCELLANEOUS AMENDMENTS) (NO. 3) ACT, 2013"**

(Made Under S.O. 86(10)(b))

A Bill entitled "The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 3) Act, 2013" is amended as follows:

R: By deleting Clause 36.

Dodoma — FMW
7th November, 2013 — **AG**

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilifutwa)*

Ibara ya 37

**FURTHER SCHEDULE OF AMENDMENT TO BE MOVED BY THE HON. FREDERICK M. WEREMA, THE ATTORNEY GENERAL DURING THE SECOND READING OF A BILL ENTITLED "THE WRITTEN LAWS (MISCELLANEOUS AMENDMENTS) (NO. 3) ACT, 2013"**

(Made Under S.O. 86(10)(b))

A Bill entitled "The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 3) Act, 2013" is amended as follows:

S: In Clause 37, by deleting paragraph (d) and substituting for it the following:

"(d) such funds as may be received from the Higher Education Students' Loans Board for purposes of quality assurance of the learning process and standards of institutions within its mandate."

Dodoma FMW
7th November, 2013 **AG**

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 38

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 39

**SCHEDULE OF AMENDMENT TO BE MOVED BY HON. PETER JOSEPH SERUKAMBA, A MEMBER OF PARLIAMENT FOR KIGOMA URBAN CONSTITUENCY AT THE SECOND READING OF A BILL ENTITLED "THE WRITTEN LAWS (MISCELLANEOUS AMENDMENTS) (NO.3) ACT, 2013"**

[*Made Under S. 0. 86(9) & (11)*]

A Bill entitled "The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 3) Act, 2013" is amended as follows-
By deleting part VIII containing clause 39, 40 and 41.

PETER JOSEPH SERUKAMBA (MP)
KIGOMA URBAN CONSITITUENCY
07/11/2013

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye *amendment* yangu nimeomba *part* yote ya (80 kwa maana ya aya ya 39, 40 na 41 ifutwe. Sababu zangu za msingi za kuleta hii, wakati nachangia juzi nilisema kwamba, mimi sipingi hata kidogo adhabu iliyowekwa hapa. Ninachokipinga mimi, ninataka Sheria yote ya Magazeti iletwe hapa ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua jana tumeambiwa ambao wanapinga hili siyo wazalendo, lakini mimi ninaamini uzalendo wa mtu haupingwi kwa kusema tofauti na anavyoamini mwingine. Jana tumeambiwa *Passport* zetu ziangaliwe kwa sababu tunapinga hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kurudia, kazi tunayofanya hapa ni ya kutunga Sheria...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Serukamba, naomba tutunge Sheria; vinenoneno hivi vinaletaga maneno. Wewe *argue* Kisheria.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa ndiyo nina-*argue.*

**MWENYEKITI:** Sasa vinenoneno, vipasipoti, viko wapi hapa? Aah.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimesema naiomba Serikali na suala la Sheria ya Magazeti, huu ni mwaka wangu wa nane Bungeni tunaambiwa inakuja mpaka leo haijaja. Niwaombe Waheshimiwa Wabunge, tukifanya maamuzi leo, tukaondoa aya hizi tatu, nina hakika Bunge lijalo Sheria ya Magazeti itakuja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sipingi hata kidogo, haya yote mnayotaka kuyafanya, yafanywe kwenye Sheria nzima ya Magazeti. Hata yanayofanyika mengine kwenye magazeti kila mtu yanamkera kama yanavyomkera *AG.* Ninachokiomba, naomba sana Waheshimiwa Wabunge

*Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*



wote, tuungane kwenye hili tuitoe ili Serikali iende ikamalizie Muswada wake ambao ninaamini upo tayari, naomba sasa uje Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niunge mkono. *(Makofi)*

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namheshimu sana Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**MWENYEKITI:** Sasa kumheshimu, endeleeni kusema. *(Kicheko)*

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo tunaendelea kusema hivyo. Utaratibu wa kujenga hoja kwa mtindo wa Kibunge, ndiyo unakuwa na vionjo vya namna hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Maendeleo ya Jamii. Kamati yangu imefanya kazi kwa muda mrefu sana, tena kwa maagizo yako Mheshimiwa Spika. Kwa kutambua kwamba, upo ukiukwaji mkubwa kweli ama wa kimaadili ama wa namna moja au nyingine kwenye tasnia nzima ya habari. Lakini kwenye tasnia hii ya habari, si kipengele hiki tu cha adhabu ndicho ambacho kinaweza kuwa ni kikwazo cha maadili ya tasnia nzima ya habari katika nchi yetu ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ulitupa kibali, Kamati imekwenda mpaka India kujifunza ni namna gani tunaweza kuzuia uhalifu anaousema *AG*. Tunaweza kuwazuia waandishi wa habari wenye nia mbaya kama anavyosema *AG* na tunaweza kutengeneza Sheria ambayo italeta heshima ya tasnia ya habari katika nchi yetu ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli tunaenda ku-*impose* hii adhabu, nakubaliana kabisa na waandishi

*Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*



ambao hawana nidhamu; nakubali kabisa. Wizara tumeihoji kwenye Kamati na imetuambia Muswada upo tayari; tunapata kigugumizi gani kuleta Muswada wa Habari toka mwaka 2006, tunang'ang'ania kuleta Kifungu hiki kidogo? Kwa nia hiyo nzuri, mimi nakubali kabisa ni nia nzuri kabisa inayoletwa na Serikali katika Kifungu hiki. *(Makofi)*

Tumekuwa na Waziri Mkuchika ameonesha nia hiyo ya Muswada wa Habari, naye yupo hapa ni shahidi, kwenye Kamati yangu tumefanya kazi ya kutosha. Tumekuwa na Mheshimiwa Emmanuel Nchimbi, Muswada upo tayari, tumekuwa na Mheshimiwa Dokta Fenella, ameiarifu Kamati Muswada upo tayari; tatizo ni nini tung'ang'anie Kifungu hiki ambacho kweli ni sahihi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini tusilete Muswada huo tukaangalia masilahi ya Wanahabari hawa ambao wanapewa fedha ili wasaliti uzalendo kwenye nchi yao? Tukiendelea na hivi vi-*piecemeal* hatutibu matatizo, tunaangalia tulipoangukia badala ya tunapojikwaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana tukiondoa hii leo, Serikali mwezi wa 12 ituletee huo Muswada mzima tufanye kazi ya kutosha hapa. Naomba sana Serikali yangu sikivu, katika hili namuunga mkono Mheshimiwa Peter Serukamba na simuungi mkono kwa maana sitambui madhara, natambua madhara ni makubwa. Sasa je, wale ambao wanapata yale madhara mtu ukiandikwa ovyo na wewe unapata fidia gani basi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mukangara, tunataka Sheria hata mimi naitaka Sheria. *(Makofi)*

**WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami niseme tu kwamba, Muswada upo katika hatua ya *Cabinet*

*[WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO]*
*Secretariat,* umerudia Wizarani tunafanya *polishing* halafu tutaurudisha tena *Cabinet Secretariat* kwenda *MTC* na kuna uwezekano kama tukijipanga vizuri, kuweza kuuwasilisha hapa. Pamoja na kusema haya, niseme haya mabadiliko yanayotakiwa kufanyika sidhani kama yataweza kuzuia huo Muswada kuletwa. *(Makofi)*

*(Sehemu iliyotajwa hapo juu (Clause 39, 40 na 41) iliondolewa na Kamati ya Bunge Zima)*

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo, *part* hii mnataka tuhesabu?

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tuite majina.

**MWENYEKITI:** Tuhesabu?

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Ndiyo.

**MWENYEKITI:** Hujaungwa mkono.

Waheshimiwa Wabunge, sisi tunajua, sasa naomba niseme katika eneo ambalo tumefanyiana utani ni katika Sheria hiyo tunayoisema. Tumefanyiana utani sana, kila siku tunasema mpaka tunaleta ugomvi leteni sheria hapa, leteni sheria na yote yaingie. Tunaendelea, Katibu. *(Makofi)*

Ibara ya 42

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 43

**SCHEDULE OF AMENDMENTS TO BE MOVED BY THE HON. TUNDU A. M. LISSU, THE MEMBER OF PARLIAMENT FOR SINGIDA MASHARIKI CONSTITUENCY AT THE SECOND READING OF A BILL ENTITLED THE WRITTEN LAWS (MISCELLANEOUS AMENDMENTS) (NO. 3) ACT, 2013**

(Made under Kanuni ya 86(11) of the Kanuni za Kudumu za Bunge, 2013)

G. In Clause 43, by deleting the clause aforesaid in its entirety;

Dated at Dodoma this 6th day of November, 2013.

……………
Tundu A. M. Lissu
Member of Parliament

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Jedwali langu la Marekebisho nimependekeza kwamba, mapendekezo ya aya ya 43 ya Muswada yafutiliwe mbali. Mapendekezo ya aya hiyo yanataka Jaji Mkuu, Jaji Kiongozi na Majaji wa Mahakama za Rufaa na Majaji wa Mahakama Kuu, wawe wanakula Kiapo cha Utii kwa Rais. Nimesema napendekeza kifungu hicho kifutwe kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria, tuanze na Katiba, katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano haijaelekeza; inaelekeza kwamba, Majaji wa Mahakama Kuu, Ibara ya 111 na Majaji wa Mahakama ya Rufani, Ibara ya 121, watakula Kiapo cha Utii kwa mujibu wa Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria yetu ya Viapo hii *Official Oaths Act* inasema kwamba, Jaji wa Mahakama Kuu atakula kiapo mbele ya Rais. Sheria hiyo hiyo kifungu cha nane inasema kwamba, Spika wa Bunge hili utakula Kiapo cha Utii mbele ya Bunge hili, ndani ya Bunge hili kwa

sababu unaongoza Mhimili ulio huru, unaojitegemea. Jaji Mkuu anaongoza Mhimili kama unavyoongoza wewe Mhimili na Majaji wa Mahakama ya Rufani na Majaji wa Mahakama Kuu wanafanya kazi katika Mhimili huo.

Sasa mapendekezo ya Muswada huu ni kuwafanya Majaji wa Mahakama ya Rufani, Jaji Mkuu, Majaji wa Mahakama ya Rufani, Majaji wa Mahakama Kuu, wawe wanakula kiapo kwa Mheshimiwa Rais. Mkuu wa Mhimili mwingine, ambao wewe Mheshimiwa Spika huli kiapo mbele yake, sisi Wabunge hatuli kiapo mbele yake, lakini Majaji wanatakiwa wale kiapo mbele yake.

Uhuru wa Mahakama ndiyo hoja yangu hapa; kwa nini Majaji wale Kiapo cha Utiifu kwa Rais? Inasema nini juu ya Uhuru wa Mahakama, ndiyo maana kwenye Bunge letu Tukufu kuna Nembo ya Taifa pale. Ukienda kwenye Mahakama zetu kuna picha ya Rais inamkodolea Jaji macho hivi! Tuna *undermine Judicial Independence* kwa masharti ya Kifungu hiki katika Karne hii ya 21 nchi inayotengeneza Katiba mpya hawafai kuwepo ni aibu. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, napendekeza hayo mapendekezo ya aya ya 43 ya kuwafanya Majaji wetu wakale kiapo cha kumtii Rais, tukimshitaki huku amekula kiapo cha kumtii tutapata haki? Hayo mapendekezo yaondolewe hayana maana yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemaliza.

**MWENYEKITI:** Haya Mwanasheria maana wewe ulikuwa Jaji!

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikwenda shule na tulipokuwa na *arguments* tulikuwa tunasahihishwa, wapo waliokuwa wanapata A, wapo waliokuwa wanapata F, *grade* yangu mimi naijua. Hii *argument* ya Bwana Tundu Lissu ni ya ovyo kwa sababu

gani? Sikilizeni, kama hamsikii sikilizeni basi, sasa nitafanyaje nimepewa *mike* ya kuzungumza hii hapa!

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivi; Spika anachaguliwa na Wabunge, Jaji Mkuu anachaguliwa na Majaji Wakuu, Majaji wengine wa Mahakama ya Rufani. Sasa tunazungumzia Katiba tuliyonayo siyo Katiba ijayo, hizi *arguments* za shule, tuna Katiba, Jaji Mkuu hachaguliwi na Majaji wa Mahakama ya Rufani na anapokwenda kwa Rais unajua neno Rais ni la Kiarabu, Rais *is an Arabic word* maana yake ni nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, huyu Rais ni Mkuu wa nchi na ashakum si matusi, anayevaa nguo ya mama yako ndiyo baba yako. Kwa hiyo, Rais anayo mamlaka na tunachofanya kwenye Sheria, kwa sababu Sheria ilikuwa haitamki Majaji wa Mahakama ya Rufani, sasa tunaiandika vizuri, mapendekezo yetu ndiyo hayo. Ninawaomba Waheshimiwa Wabunge, pamoja na kwamba mmenikatalia ile ya magazeti hata wangu wamenikataa, basi niungeni mkono kwenye hili. *(Makofi)*

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ningetaka kupata ufafanuzi kutoka kwa Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, ambaye ni Mshauri wa Sheria hapa, kwa uzoefu wake atusaidie uzoefu wa nchi zenye mfumo unaofanana na wetu, juu ya kiapo cha Majaji, Jaji Mkuu kula Kiapo cha Utii kwa Rais, ambaye wote hatuna mashaka kwamba ndiye Mkuu wa Nchi na hatuna mashaka kwamba yeye ndiye anayeteua kwa mujibu wa Katiba tuliyonayo. Nataka kujua anapokula Kiapo cha Utii kwa Rais na asipokula Kiapo cha Utii kwa Rais anapungukiwa nini?

Kwa sababu hofu yangu ni kwamba, tuna Mihimili mitatu kwa mujibu wa Katiba yetu na Mihimili huru kabisa na hata sisi tunapokuja hapa hatuli Kiapo cha Utii kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kama Mhimili unaojitegemea. Mheshimiwa Spika huli Kiapo cha Utii kwa Rais wa Nchi na bado Rais ni Mkuu wa Nchi.

*[MHE. C. O. OLE-SENDEKA]*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kujua athari; tutakachopungukiwa sasa kwa Majaji hao kutokula Kiapo cha Utii kwa Rais wa Nchi na itaongezeka nini watakapokula Kiapo cha Utii kwa Rais wa Nchi? Maana hofu yangu ni kwamba, sasa kama watakula Kiapo cha Utii kwa Rais maana yake kwa namna moja au nyingine, kwa tafsiri yangu mimi ambaye ni *layman* siyo Mwanasheria, inaweza kuleta taswira ya kuwafanya Majaji hawa kutii amri ya Rais; Rais ambaye anatokana na chama fulani cha siasa. Kwa maana hiyo, inaweza kuathiri utaratibu na ndiyo maana Rais anapata mamlaka ya kuwateua Majaji, lakini hana mamlaka ya kuwaondoa mpaka utaratibu wa majopo ya Majaji wengine uliowekwa kwa mujibu wa Sheria utakapofuatwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba ufafanuzi katika hoja hii kabla hatujaiunga mkono.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nadhani vitu vingine vinapaswa kuja katika mabadiliko ya Katiba mpya. Nami kwa uelewa wangu mdogo siamini kwamba, Jaji kwenda kuapa kwa Rais, inaingilia uhuru wa Mahakama; hiyo siamini. Kiapo kile ni cha kumfanya yeye atimize wajibu wake bila upendeleo, haihusiani kabisa na suala zima la kuingilia Mahakama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naunga mkono hoja ya Mwanasheria Mkuu, tuache kama ilivyo mpaka tutakapofanya mabadiliko ya Sheria ya Katiba mpya.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, sina hakika kama tuna-*define* vizuri maana ya Rais. Rais siyo mtu, Rais ni mamlaka, unaitii mamlaka. Rais ni jina la mamlaka ya juu ya utawala wa nchi. Sasa hoja hapa ni rahisi tu kwamba, kama mnakubali ateue, unakataaje kumkubalia mtu aseme atatii mamlaka na inayeteua Jaji Mkuu ni mamlaka na ile mamlaka ndiyo inayotakiwa kutiiwa na Rais amechukua mamlaka ya sisi Watanzania wote akaiweka pale yeye ni nembo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kuapa kule hoja ingekuwa ya maana kama tungeanzia kwamba, asiteue. Hiyo siyo hoja hapa, hoja hapa ni kuapa. Mimi ningeomba sana kwa sasa, kwa Katiba hii ya sasa, tukikubaliana na hoja nzuri tu ya Tundu Lissu, ila mazingira yake si haya, tutakuwa tume-*create contradiction.* *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa Kifungu cha 28(2) cha Kanuni, naongeza nusu saa mpaka tumalize kazi hii.

Mheshimiwa Tundu Lissu!

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwanasheria Mkuu wa Serikali amesema kuna baadhi ya waliosoma wamepata F. Sasa sitampeleka huko, kwa sababu hoja haijibiwi kwa kejeli na kama anataka kujua nimefanyaje shule aje nitamweleza tu.

**MWENYEKITI:** Endeleeni kujibu hoja.

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya msingi hapa ipo hivi; hii Sheria ya Viapo ilitungwa mwaka 1962, miaka 51 iliyopita, haijawahi kuweka masharti ya Jaji Mkuu, Jaji wa Mahakama ya Rufani, kula kiapo kwa Rais. Haijawahi na ndiyo maana wanaweka mapendekezo hayo. Kwa hiyo, Kisheria na Kikatiba, Jaji Mkuu, Jaji wa Mahakama ya Rufani, hatakiwi kula kiapo kwa Rais, kwa sababu Sheria haisemi hivyo. Sheria hii iliyotungwa miaka 51 iliyopita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa *Attorney General* amekuwa mwanasiasa sijui hasomi Sheria! Hoja ni kwamba, Rais sasa hivi hana mamlaka ya kumlisha kiapo Jaji Mkuu. Hoja ni kwamba, Rais sasa hivi hana mamlaka ya kumlisha kiapo Jaji wa Mahakama ya Rufaa. Sasa najua wanakula

lakini kama kawaida yetu ni uvunjaji wa Sheria tu, uvunjaji wa Katiba tu. *(Makofi)*

Tunafanya mambo kwa mazoea badala ya kufanya mambo kwa kufuata Sheria. Kama hii hoja Mwanasheria Mkuu wa Serikali ni yenye mashiko, swali linabaki kwa nini imewachukua miaka 51 kugundua kwamba Jaji Mkuu hatakiwi kula kiapo kwa Rais? Ni kwa sababu hawasomi wanatukana watu kirejareja tu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mmezowea kutukanana kirejareja tu, endelea.

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ni hiyo; Majaji wetu uwekwe utaratibu wale kiapo kwa namna itakayolinda uhuru wa Mahakama na hizo picha za Rais za kuwakodolea Majaji Mahakamani zitoke, iende Nembo ya Taifa, kwa sababu Mahakama zetu zipo huru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pendekezo lililoletwa la Serikali halina mashiko, itakuwa aibu itabidi muwaeleze Watanzania miaka yote hii mlikuwa mnafanya nini hamkugundua kwamba Majaji hawatakiwi kula kiapo kwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja hii iondoke inatutia aibu hapa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Sasa nitawahoji tuiamue hoja ya Mheshimiwa Tundu Lissu.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja ya Mhe. Tundu A. M. Lissu iliamuliwa na Kukataliwa)*

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 44
Ibara ya 45

Ibara ya 46

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara 47

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilifutwa)*

**SPIKA:** Imeshafutwa haipo.

Ibara ya 48

**SCHEDULE OF AMENDMENT TO BE MOVED BY THE HON. FREDERICK M. WEREMA, THE ATTORNEY GENERAL DURING THE SECOND READING OF A BILL ENTITLED "THE WRITTEN LAWS (MISCELLANEOUS AMENDMENTS) (NO. 3) ACT, 2013"**

(Made Under S.O. 86(10)(b))

A Bill entitled "The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 3) Act, 2013" is amended as follows:

U: In Clause 48, by deleting the word "years" appearing at the end of that Clause and substituting for it the word "year".

Dodoma FMW
7th November, 2013 **AG**

*(Ibara iliyotajwa hapo ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 49

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 50

*Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

**ADENDUM TO**
**SCHEDULE OF AMENDMENT TO BE MOVED BY HON. MOSES JOSEPH MACHALI A MEMBER OF PARLIAMENT FOR KASULU URBAN CONSTITUENCY AT THE SECOND READING OF A BILL ENTITLED "THE WRITTEN LAWS(MISCELLANEOUS AMENDMENTS) (NO.3) ACT, 2013"**

[*Made Under S. 0. 86(9) & (11)*]

---

A Bill entitled "The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 3) Act, 2013" is amended as follows-

In clause 50

By deleting the words "one year" and replacing them by the words "three months"

---

HON. MOSES JOSEPH MACHALI (MP)
KASULU URBAN CONSITITUENCY
07/11/2013

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kimsingi, katika mapendekezo yangu naiomba Serikali iangalie busara ya kupunguza adhabu au umri wa adhabu ambao unapendekezwa na Serikali, ambapo ukiangalia wao wanataka kuongeza kutoka kifungo cha miezi sita kwenda mpaka mwaka mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu hata juzi wakati nachangia kuhusiana na hoja mbalimbali ambazo zimejitokeza kwenye Muswada huu, nilisema kwamba, ukienda katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu, watu mbalimbali wamefungwa, wengine kwa kuonewa, Magereza yamejaa na nikashauri ni vyema tukaangalia jinsi tunavyoweza tukaanza kuondokana na adhabu za vifungo.

Wengine tukasema inawezekana Muswada huu umetungwa watu wakiwa na hasira dhidi ya watu fulani

fulani. Vilevile michango ambayo imeendelea hapa tangu asubuhi wakati tunaendelea na Muswada huu, imeonesha wazi kwamba, Serikali wakati mwingine inatunga sheria kuendana na matukio au kutokana na matukio ya wakati uliopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naiomba Serikali ione sababu ya msingi ya kupunguza adhabu ambayo inapendekezwa kutoka mwaka mmoja na iwe miezi mitatu kama ambavyo nimependekeza ili tupunguze msongamano wa watu kwenye magereza yetu. Tunazidi kuongeza gharama za kuwahudumia watu hawa, ambapo watakuwa pengine wamekutwa na makosa halafu wapo magereza. Badala yake, tuanze kufikiria kuwa na adhabu mbadala, badala ya kuona kwamba kufunga mtu ndiyo kumfundisha. Tunaweza tukawafundisha watu kwa namna nyingine na hasa hili suala la kuendelea kuongeza adhabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nalomba Serikali ione umuhimu wa kukubaliana kwamba iwe miezi mitatu badala ya mwaka mmoja. Sasa ilikuwa miezi sita, unatoa miezi sita unapeleka mwaka mmoja, lengo ni nini hapa? *AG* nakuomba ukubaliane na suala hili.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mamlaka ya kuamua kama mtu anakwenda nje atapewa adhabu, lakini atatumikia kifungo nje ni ya mahakama. Tunachofanya, kama mahakama itaona kosa lile ni kubwa halistahili miezi sita na kama mahakama inaona anastahili kwenda jela, atakwenda mwaka mmoja. Pia akiona amefanya kosa, amepatikana na hatia anaonywa, kwa sababu sheria inaruhusu kutumikia kifungo nje, lakini usifanye kosa kwa muda fulani, inawezekana pia.

Sisi tunafikiri kwamba, pale ambapo anaona kosa ni kubwa, basi kifungo kina kipande toka miezi sita mpaka

mwaka mmoja. Hayo ndiyo mapendekezo ya Serikali na ambayo nayasimamia na naomba Waheshimiwa Wabunge, muunge mkono.

**MWENYEKITI:** Jibu Mheshimiwa Machali!

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali inishawishi, sikatai adhabu kutolewa. Pengine sasa Serikali ieleze ni sababu gani ambayo imeonekana miezi sita haitoshi sasa adhabu iongezwe kutoka kwenye miezi sita na kuwa mwaka mmoja, badala ya kusema kwamba sasa tuangalie namna gani kwa nini isipungue adhabu hii?

Kama kuna sababu ambazo zimepelekea, mimi binafsi sijashawishika ni kwa nini tumeongeza adhabu badala ya kufikiria jinsi gani ya kuweza kupunguza adhabu. *AG* akiweza kunishawishi basi nitakubaliana naye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Nawahoji juu ya pendekezo la Mheshimiwa Machali.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja ya Mhe. Moses J. Machali iliamuliwa na Kukataliwa)*

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

**MWENYEKITI:** Pendekezo la Machali limeondoka. Mmeshampigia kura. Tunaendelea, Katibu hatua inayofuata.

Ibara ya 51

**ADENDUM TO**
**SCHEDULE OF AMENDMENT TO BE MOVED BY HON. MOSES JOSEPH MACHALI A MEMBER OF PARLIAMENT FOR KASULU URBAN CONSTITUENCY AT THE SECOND READING OF A BILL ENTITLED "THE WRITTEN LAWS(MISCELLANEOUS AMENDMENTS) (NO.3) ACT, 2013"**

[*Made Under S. 0. 86(9) & (11)*]

_________

A Bill entitled "The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 3) Act, 2013" is amended as follows-

In clause 51

By deleting the words "...is guilty of a misdemeanor" and substituting for them the words "...commits an offence and upon conviction may be liable to a fine of one million or imprisonment for a term of 3 months..."

____________________________

HON. MOSES JOSEPH MACHALI (MP)
KASULU URBAN CONSITITUENCY
07/11/2013

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha 50 pia hii Ibara ya 51, maelezo yake ni sawasawa na maelezo ambayo nilikuwa nayatumia kwenye Kifungu hicho cha 50. Kwa hiyo, naiomba Serikali ieleze ni kwa nini inaongeza adhabu badala ya kupunguza adhabu?

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI**: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nafikiri tuchukue maneno yako ambayo unatuambia kila wakati kwamba, pengine kabla hatujaja hapa kama una marekebisho na wengi wanafanya hivyo, Mama Leticia Nyerere amekuja na nafikiri asubuhi nilizungumza na Mheshimiwa Serukamba, tunajadiliana kama tukielewana tusipoteze muda wa Bunge.

*[MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI]*

Napata shida sana kwenye Jedwali la Marekebisho la Mheshimiwa Machali, kwa sababu ukisoma pale anachozungumzia ni *Clause 55,* kwenye Muswada 55 anayozungumzia haipo kwenye Muswada wangu. Sasa kwenye Kanuni za Bunge ambazo unazo, ile Kanuni ya 86(9) na (11), hakuna kitu kinaitwa *addendum*. Nauliza hii *addendum* imekuja kwa utaratibu gani; ndiyo napata shida? Nafikiri tuwe na utaratibu wa kuendesha Bunge kwa viwango; hii *addendum* inaletwa kwa msingi upi? Ndiyo maana nasema nimeletewa *document* hapa lakini sijui imetoka wapi, hakuna utaratibu wowote wa kwenye Kanuni!

Naangalia neno hili ambalo umetumia, *addendum* siyo neno hilo, neno sahihi ni *addendum* na kwenye Kanuni hakuna addendum. Nikujibu swali lako labda kwa sababu lipo, kama lipo sasa tutafanyaje? Unajua kwa nini tunaongeza adhabu na watu wanafikiri kwamba huu ni ukandamizi? Adhabu hizi kama Mheshimiwa Tundu anavyosema, Sheria zimetungwa siku nyingi zimepitwa na wakati na tunazipa mahakama mamlaka ya kuamua pale inapothibitika kwamba kosa hili linastahili adhabu hii. Pia hatuzuii mahakama kutoa adhabu kwa makosa hayo hayo, kutoa adhabu tahafifu, kumwambia mtu nenda kafagie barabara ukimaliza nenda nyumbani; inawezekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hii *addendum* ya Mheshimiwa nafikiri ndiyo nimejibu hivyo. Siku nyingine Mheshimiwa Machali ni vizuri tukutane, najua tunafahamiana, tuzungumze kama hiki kinafaa au hakifai.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, labda pengine nimpe taarifa Mheshimiwa *AG*, hii *addendum* imefuata utaratibu wote na ndiyo maana ina muhuri wa Katibu wa Bunge. Kwa hiyo, kama unayo nyingine, nafikiri huenda hiyo umetengeneza wewe siyo mimi ambaye nimetengeneza. Nimetengeneza na imethibitishwa na Ofisi ya Katibu wa Bunge.

**MWENYEKITI:** Naomba utulie kwanza. Anachokisema ni kwamba, sasa sijui kama ni pale ofisini kwangu au ni nani; hizi zote zinaitwa *Schedule of Amendment* siyo *addendum.* Neno *addendum* linakuwa kama unaongeza habari katika habari uliyokuwa nayo. Sasa hili ndiyo kosa; umeona kuna maneno yanaitwa *addendum, so,* kama ni ofisi yangu sijui lakini siyo *correct,* ilikuwa hizi ni *Schedule of Amendment* siyo *addendum*. Tumeelewa sasa tuendelee.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, bado nasema kwamba, marekebisho ambayo niliyafanya ni Ofisi ya Katibu wa Bunge ndiyo ambayo imeandika hapo juu...

**MWENYEKITI:** Tumeelewa hivyo, lakini *addendum* wenzako wote haipo, hii ni *Schedule of Amendment*. Unajua *addendum* na *Schedule of Amendment* ni tofauti. Endelea tu.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa narekebisha kwanza ndiyo maana kuna neno hapo juu na wameandika Ofisi ya Katibu wa Bunge, ambao ni Wanasheria kama *AG* siyo mimi.

**MWENYEKITI:** Nimekwambia ofisi yangu imekosea hiyo siyo sahihi sasa tuendelee, kama ni ofisini kwangu ni kosa, kama wamekosea ofisini kwangu wamekosea.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Niseme tu kwamba, kama msimamo wa Serikali ni huo, nadhani hoja ihitimishwe tu. Ahsante.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 52
Ibara ya 53

Ibara ya 54

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 55

**SCHEDULE OF AMENDMENT TO BE MOVED BY HON. MOSES JOSEPH MACHALI, A MEMBER OF PARLIAMENT FOR KASULU URBAN CONSTITUENCY AT THE SECOND READING OF A BILL ENTITLED "THE WRITTEN LAWS(MISCELLANEOUS AMENDMENTS) (NO.3) ACT, 2013"**

*Made Under S. 0. 86(9) & (11)*

*PART X*

Amendment of the penal code

(cap. 16)

A Bill entitled "The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 3) Act, 2013" is amended as follows-

In Clause 55(1) by adding the word "intentionally" immediately after the suggested phrase "Any person who-"

There after in Sub-clause 1(a – e) by deleting the word "to" appearing at the beginning of each of the mentioned sub-clauses and adding the following words after all sub-clauses "Commits an Offence and upon conviction is liable to imprisonment for a term of six months."

---

HON. MOSES JOSEPH MACHALI (MP)
KASULU URBAN CONSITITUENCY
07/11/2013

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo hii *addendum* ambayo nilifanya katika *Schedule of Amendment.* Marekebisho ambayo nilifanya, tayari vifungu vyangu vyote nilikuwa nahoji kikiwemo Kifungu cha 47, vipo ndani ya hii ya pili.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 56
Ibara ya 57
Ibara ya 58
Ibara ya 59
Ibara ya 60

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 61

**SCHEDULE OF AMENDMENTS TO BE MOVED BY HON. JOHN JOHN MNYIKA, MEMBER OF PARLIAMENT FOR UBUNGO CONSTITUENCY AT THE SECOND READING FOR THE BILL ENTITLED THE WRITTEN LAWS (MISCELLANEOUS AMENDMENTS) (NO. 3) ACT, 2013**

Made under standing order 86(11) and 88(2)

A Bill entitled "THE WRITTEN LAWS (MISCELLANEOUS AMENDMENTS) (NO. 3) ACT, 2013" is amended as follows:

C: In Clause 61 adding the subsection "f" after subsection "e".

(f) two members representing self employed members and informal sector members.

………………….
JOHN JOHN MNYIKA (MP)
UBUNGO CONSTITUENCY
06.11.2013

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Ibara hii inahusu marekebisho kwenye Mamlaka ya Hifadhi ya Jamii kwa maana ya *SSRA,* kwenye kifungu cha (7) kinachohusu Muundo wa Bodi. Marekebisho yanayopendekezwa na Serikali yanalenga kuingiza Wawakilishi wawili wanaowakilisha Vyama vya Waajiri. Tasnia ya Hifadhi ya Jamii imepanuka, dhana ya awali ya Hifadhi ya Jamii ya kwamba ni waajiriwa ambao wanawakilishwa na Vyama vya Waajiriwa na Waajiri ambao wanawakilisha Vyama vya Waajiri, ni dhana ambayo imebadilika kidogo baada ya Sekta Isiyo Rasmi nayo kuingia kuwa sehemu ya Hifadhi ya Jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi hapa tumepitisha Sheria ya *GEPF Retirement Benefit Fund* na kwa mujibu wa Sheria ile tuliyopitisha, Sekta Isiyo Rasmi na watu waliojiajiri nao ni sehemu ya watu ambao wanaweza kuwa Wanachama wa Hifadhi ya Jamii. Vilevile siyo tu katika Sheria tuliyopitisha juzi, Mifuko mbalimbali ya Hifadhi ya Jamii hivi sasa inaanza kuanzisha *voluntary schemes,* mifumo ya hiari ya watu waliojiri wenyewe au walio kwenye Sekta Isiyo Rasmi kuwa sehemu ya Wanachama wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Wanachama hawa wana mahitaji maalum na mazingira maalum…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Pindi Chana na kundi lako, mnapiga kelele! Mheshimiwa Mnyika endelea!

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Wanachama hawa wana mahitaji maalum tofauti na waajiriwa na wala hawahusiani na Vyama vya Waajiri. Kwa sababu hiyo basi, nimependekeza kwamba, kwenye Mamlaka ya Hifadhi ya Jamii, tuongeze sasa baada ya kifungu (e) kilichopendekezwa na Serikali, napendekeza kuongezwe kifungu kingine cha (f) ili vilevile kuwe na wawakilishi wawili wa watu waliojiajiri na watu wanaotoka kwenye Sekta Isiyo Rasmi ili nao wawe na wawakilishi wawili kwenye hii Mamlaka ya Udhibiti wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii.

Mamlaka hii, Bodi yake inapokaa hufanya maamuzi ya udhibiti wa Mifuko mbalimbali katika masuala yanayogusa masilahi ya watu waliojiajiri wenyewe; iwe ni wakulima, iwe ni wamachinga, iwe ni mama lishe, iwe ni watu mbalimbali, basi vilevile waweze kuzingatia masilahi ya watu ambao wamejiajiri wenyewe na ambao wapo kwenye Sekta Isiyo Rasmi, ambayo kitakwimu Sekta Isiyo Rasmi ndiyo imeajiri zaidi ya asilimia 80 ya Watanzania nchini. Kwa hiyo, tukiweza kuifanya Sekta Isiyo Rasmi na watu waliojiajiri wakijihisi ni Wadau Wakuu kwenye masuala ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, tutaweza kuongeza mwamko wa watu waliojiajiri na walio kwenye Sekta Isiyo Rasmi kujiunga na Mifuko mbalimbali ya Hifadhi ya Jamii na hatua hii itafanyika kama tutawawezesha kuwa na uwakilishi kwenye Mamlaka ya Hifadhi ya Jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba kutoa hoja kwamba, pendekezo hilo likubalike ili Kipengele cha (f) kiongezwe. Ahsante sana.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nami nikubaliane kabisa na hoja ya Mheshimiwa Mnyika kwamba, mara nyingi kwa siku za nyuma tulikuwa tumezowea wanaotoa *contribution* ni hao wafanyakazi ambao wapo katika Sekta Rasmi hasa Serikalini na kwenye Mashirika ya Umma. Katika upana huu na ikizingatiwa kwamba hata juzi tulikuwa tumepitisha kifungu kinachompa madaraka Mheshimiwa Waziri, kuweza kuweka hata nafasi ya mchango kadiri atakavyoona inafaa, kutokana na mazingira yatakayokuwepo mbali ya zile asilimia ambazo zingekuwa zimeshawekwa pale kisheria. Kuna lilijitokeza lilijitokeza hivi karibuni kwamba, wafanyakazi wote ambao ni wa *private* wale wa kima cha chini angalau iwe ni laki tatu na ishirini na tano.

Hiyo ilipelekea waajiri wasio waaminifu na utu, wakaamua kuwashusha mishahara wale ambao walikuwa na mishahara mikubwa kama *operators* wa magari na kuwapandisha kidogo wale waliokuwa chini na kuwapa wote *flat rate,* kiasi kwamba, hata wao wanauliza sasa

jamani kambare wote tuna ndevu sawa. Kwa hiyo, wakishiriki hawa watu katika Bodi kama hizi, wataweza kushauri na kuisaidia sana Serikali katika mipango mbalimbali na ikizingatiwa kwamba sasa hivi tunapozungumzia kazi au ajira, hatuangalii tu Serikali bali tunaangalia pia hata *Private Sector* na watu waliojiajiri binafsi. Nashukuru ila jinsia pia izingatiwe, isiwe tu wanaenda wawakilishi wawili bila kujali wanawake na wanaume, kwa sababu mazingira yao ya kazi yako tofauti. Ahsante.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, marekebisho tuliyoleta sisi na nia yetu ilikuwa kufuta Kifungu cha 7(1)(c) ili kuondoa maneno yale *Trade Unions Congress of Tanzania* na badala yake iwe *the most representative employers organization* kwenye *possessive*. Sasa haya mengine anayoyasema sisi hatukuyaleta. Sisi tumeleta hapo kuondoa *Trade Union Congress of Tanzania* na badala yake kuweka *two members representing the most representative employers organization.*

Sasa ukisema *private sector, public sector, let us go one* by *one,* tuangalie hivi hawa *Tanzania Employers Association* wanaotajwa kwenye (d) ni akina nani. Hawa siyo wafanyakazi, hawa ni watu wa *private sector* pamoja na *public sector.* Ukienda kwenye (f), *one member from amongst persons who possess knowledge and experience in social security matters.* Hawa wanatoka wapi kwenye *private sector.* Kwa hiyo, *argument* kwamba kuwe na *balance* na nini, *private sector* na *public sector,* siyo *issue* yetu sisi. *Issue* yetu tuliyosema ni kwamba, tuondoe ile (c) ambayo inasema *two representative from the Trade Unions Congress of Tanzania,* tuweke *two members representing the most representative employers organization*. Kwa hiyo, ukifanya hivyo, utakuta kuna *mix* ya *private sector* na *public sector.* Hii ya *gender balance* na mimi nasema siyo *gender balance, gender parity,* inategemeana na *appointing authority.* Hili siyo jambo la kwenda kujaza, hili sasa tufuate hata wakiwa wanawake wote sijui nusu, hapa ni *issue* ya *brain,* kama mtu anajua ile *sector* aidha ni mwanamke au mwanamke *it doesn't matter.*

*[MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI]*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi pendekezo letu ni kuondoa ile (e) na kuweka hii (e) mpya tunayoi-*propose*, *we are not doing anything there*. Sheria ilivyo ni hako ka sehemu kamoja tu tunakopitia na naomba mapendekezo tunayofanya Serikali yakubalike.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mnyika umeelewa hapo kwamba pendekezo lako halihusiani na *amendment* ya Serikali?

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi si-*amend amendment* ya Serikali na wala sina tatizo na *amendment* ya Serikali. Kwenye *principal legislation*, Sheria yenyewe mama, kipengele (e) kilisema *two representatives from Trade Unions Congress of Tanzania*, wawakilishi wa *TUCTA* na sehemu (d) ilisema *two representatives from the Tanzania Employers Association*, wawakilishi wa TEA. Stahili hii ya kutaja *TEA* kama taasisi, *TUCTA* kama Taasisi ni *style* ya zamani ya uandishi wa sheria wakati huo. *ILO Conversion* imekuja na dhana kwamba, Vyama vya Waajiri na Vyama vya Wafanyakazi kwa sheria kwenye nchi mbalimbali viitwe tu, *the most representative*.

Kwa hiyo, *regardless the name* ya hiyo taasisi inaingia, mimi sina tatizo na hiyo *amendment* ya Serikali kabisa. Tatizo langu na ndiyo msingi wa pendekezo langu ni kwamba, kwenye tasnia ya hifadhi ya Jamii sasa hivi ni zaidi ya wafanyakazi walioajiriwa na ni zaidi ya waajiri waliowaajiri hao wafanyakazi. Kwa hiyo, *principle* ya utatu sasa hivi, siyo tu mwajiriwa, mwajiri na Serikali, *tripartite* iko hivyo kwa hao walioajiriwa.

Sisi sasa hivi tunafikiria, ili Watanzania wengi wanufaike na hifadhi ya jamii, ni lazima tuwafanye watu ambao wamejiajiri wenyewe na wenyewe waingie kwenye hifadhi ya jamii. Tuwafanye watu ambao wako kwenye *sector* isiyo rasmi na wenyewe waingie kwenye hifadhi ya jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninachopendekeza ni nini? Ukiondoa mwakilishi wa wafanyakazi walioajiriwa, iwe ni *TUCTA* iwe ni nani. Ukiondoa mwakilishi wa watu waliowaajiri

wafanyakazi, kuwe na wawakilishi wa watu waliojiajiri wenyewe ili na wenyewe wawe na wawakilishi kwenye hii mamlaka ndiyo pendekezo langu. Kwa hiyo, naungana kabisa na pendekezo la Serikali, lakini napendekeza kiongezwe kifungu kingine cha hawa wawakilishi.

Sasa Mwanasheria Mkuu, uko hapa kutusaidia kutunga sheria, kama *argument* yako ni kwamba, isiwe kwenye kifungu (f), maana yake ni nini? Utushauri na naamini huo ushauri utatuelekeza hivyo, kwamba, kwa kuwa kwenye *principal legislation* inaishia kwenye (g), ambayo inasema:

"*The Director General who shall ex-officio member,* ama kabla ya huyu *Director General* au baada ya *Director General* kuingiza sasa *provision* ambayo sasa ina maneno ambayo nimeyapendekeza hapa inasomeka: "*Two members representing self employed members and informal sector members,* basi.

Kwa hiyo, Mwanasheria Mkuu wa Serikali unatakiwa utushauri tu kwamba; sasa hicho kifungu kwa sababu kina dhamira sahihi, basi kiingie sehemu hii, ndiyo ambacho natarajia kutoka kwako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie tu, siku chache zilizopita juzi tumepitisha sheria ya *GEPF,* tumeingiza kifungu kama hiki cha wawakilishi wa *self employed members* na wawakilishi wa *informal sector members*. Kama tumepitisha kwenye sheria ya *GEPF* na Mifuko mingine nayo sasa inaanza kuwa na *voluntary schemes* za watu wanaojiajiri wenyewe. Ni kwa nini kusiwe na wawakilishi wao kwenye Mamlaka inayodhibiti Mifuko yote, ili maslahi ya watu waliojiajiri na watu walio kwenye *sector* isiyo rasmi yazingatiwe. Hilo ndiyo pendekezo langu.

**MWENYEKITI:** Naomba tumalize, Mheshimiwa.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Unajua utungaji wa sheria, hautaki *heat of passion*, yaani mawazo yanayotoka ghafla, halafu unasema unatunga sheria. *Process*

yetu hii toka kwenye Kamati, hakuna wazo hilo, hakuna mdau aliyekuja akatuambia tuweke pale...

*(Hapa baadhi ya Wabunge walikuwa wanaongea ongea kuonesha kutokubaliana na Mwanasheria Mkuu wa Serikali)*

**MWENYEKITI:** Jamani eee! Kwa nini mnapiga kelele, kila mtu ana nafasi yake.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** *No, no!* Kwanza hii siyo *fund*, hii ni Mamlaka na wazo lako hilo...

*(Hapa Mheshimiwa John J. Mnyika alionekana kutokubaliana na Mwanasheria Mkuu wa Serikali)*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Si umesema nikushauri.

**MWENYEKITI:** Nawaomba mumsikilize.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Si umesema nikushauri na kazi yangu ni kushauri, ndiyo niliyosomea. Nakushauri hivi; wazo lako hilo zuri, lakini kwa mapendekezo haya yaliyoko hapa nalikataa, kwa sababu, kwanza halijachujwa katika Kamati ya Bunge. Pili, halijachujwa na wadau wa Mifuko hii. Tatu, hao *self-employed persons* hawana *structure,* kwa hiyo, tusubiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unajua Sheria hatutungi *cuts and stones*, kuna siku nyingine tena itakuja. Ikifika wakati huo, tukiwa na hiyo *structure* yote tutaweka, lakini kwa sasa, nafikiri kwa niaba ya Serikali, mapendekezo ya Mheshimiwa Mnyika yasikubalike.

**MWENYEKITI:** Naona tuendelee. Mheshimiwa Mnyika sema tumalize.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tupige kura kwa sababu jambo hili liko wazi sana.

**MWENYEKITI:** Unajua...

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Juzi tumepitisha sheria na tukakubali watu ambao ni *self employed* wana-*represent* kwenye *GEPF*; Mwanasheria Mkuu wa Serikali akaunga mkono, hakusema kwamba hawana mfumo wa wawakilishi, hakusema kwamba hawana taasisi zao. Leo inapokuja suala la Mamlaka sasa ambayo ndiyo inatengeneza mfumo mzima, *Voluntary scheme* ziweje na utaratibu mzima uweje, kinakuja kisingizio ambacho hakina msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tupige kura ili umma wa watu waliojiajiri. Sasa hivi nchi yetu ni asilimia sita tu chini ya Serikali ya CCM ndiyo wako kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, tunafikiri kuingiza watu wengi zaidi kwenye mifuko; watu wengi wako kwenye sekta isiyo rasmi. Leo tunakataa *representation* ya sekta isiyo rasmi, tupige kura umma unaona.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa kwa nini unapiga kelele jamani? Hapa ni mfumo, kwa hiyo anayekwenda pale ni mtu mmoja mmoja, anakwenda mtu na hela yake kwa ajili ya akiba yake. Sasa hapa nani atakwenda, haiwezekani kwenda wote. Tuamue!

*(Hoja ya Mheshimiwa John J. Mnyika iliamuliwa na Kukataliwa na Kamati ya Bunge Zima)*

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 62
Ibara ya 63

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 64

**SCHEDULE OF AMENDMENT TO BE MOVED BY THE HON. FREDERICK M. WEREMA,THE ATTORNEY GENERAL AT THE SECOND READING OF A BILL ENTITLED "THE WRITTEN LAWS (MISCELLANEOUS AMENDMENTS)" (NO. 3) ACT, 2013"**

---

*Made under S. 86(10)(b)*

---

**V:** In Clause 64 by-

(a) deleting paragraph (e) and substituting for it the following:

"(e) such funds as may be received from the Higher Education Students' Loans Board for purposes of quality assurance of the learning process and standards of institutions within its mandate."; and

(b) re-numbering Clauses 11-35,37-46 and 48-65 as Clauses 10- 62 respectively.

**V:** In Clause 64 by-

Dodoma, **FMW**
................................, 2013 AG

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 65
Ibara ya 66

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

*Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

*(Bunge lilirudia)*

**Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2913 (The *Written Laws (Miscellaneous Amendment) No.3 Bill, 2013)***

*(Kusomwa Mara ya Tatu)*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 89(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2013, naomba sasa kutoa taarifa kuwa, Kamati ya Bunge Zima imeupitia Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali No.3 ya mwaka 2013 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendment) Bill No*.3, 2013), ibara kwa ibara na imeukubali pamoja na marekebisho yaliyofanyika.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali namba tatu wa mwaka 2013 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendment) Bill,* 2013 kama ulivyorekebishwa katika Kamati ya Bunge Zima, sasa ukubaliwe.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Tatu na Kupitishwa na Bunge)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tumefanya kazi kubwa, lakini nafikiri kwamba, utaratibu mzima wa *amendments* hatufanyi sawasawa. Kwa sababu kila mtu anachomoa kifungu, anapeleka huku, sasa tukienda namna

hiyo, mwisho *distortion* ya sheria nzima inaweza kutokea. Kwa hiyo, kwa mfano, unakuta katika kifungu kimoja kuna watu *severally*, kumbe wangekuwa *coordinated* ingekuwa imefanyika vizuri.

Tatizo lingine ninaloliona ni kwamba, wale *members* wa Kamati wenyewe, hivi kule kwenye Kamati walikuwa wamepeleka *amendments* au hawakupeleka. Maana yake wengine waliokuja hapa *very effectively* ni *members* wa *Committee* na sisi tungetamani sana kazi kubwa ifanyike kwenye Kamati kwa sababu mna uwezo wa kukaa pamoja na kushauriana, mna uwezo mkubwa zaidi kuliko katika ukumbi huu ambao ni mkubwa mno. Hivyo, tunapenda tuwashukuru kwa kazi kubwa mliyofanya na maafisa wahusika katika Miswada mbalimbali kwa kazi mliyofanya.

Kama tulivyosema *we are very serious* kuhusu Sheria ya Magazeti, imechukua *too long* na sababu hakuna. Matokeo yake tusiwalaumu tu, kwa sababu tumewaachia. Kwa hiyo, nadhani tukitunga Sheria ya Magazeti nadhani tutakuwa salama zaidi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nina matangazo mawili; Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Ulinzi na Usalama, Mheshimiwa Anna Abdallah, ameomba niwatangazie wajumbe wa Kamati yake kwamba, saa saba hii kutakuwa na kikao cha Kamati katika ukumbi wa Msekwa *Hall*, nadhani watakutana na wale wenzao niliotangaza asubuhi.

Tangazo lingine kutoka kwa Katibu wa Bunge, anasema niwatangazie wajumbe ambao hawakujaza na kurudisha fomu za Bima ya Afya ya Wabunge, wazirudishe ili zoezi hilo liendelee. Pia wale ambao hawakuchukua fomu, wakachukue katika jengo la utawala. Naomba mfanye hiyo shughuli, sijui kama mliambiwa vizuri.

Pia, kuna tangazo lingine kutoka ofisini hapa kwamba, Wabunge wote wa Mkoa wa Dodoma, baada ya kuahirisha

*Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*


Bunge waende mapokezi, jengo la utawala ili wapate maelezo kuhusu mkutano wa wadau wa Bima ya Afya, Mkoa wa Dodoma, kutoka kwa maafisa wa Bima ya Afya. Nadhani ninaowatangazia wanaelewa.

Waheshimiwa Wabunge, mchana tukirudi tunaingia kwenye Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Mabadiliko ya Katiba wa mwaka, 2013 ambao umekuja *under certificate of urgency*. Kwa hiyo, naomba msikae mbali ili tuweze kufanya kazi inayostahili.

Sasa nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa kumi na moja jioni.

*(Saa 7.30 Mchana Bunge lilisitishwa hadi saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge lilirudia)*

*Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alikalia Kiti*

**SPIKA:** Waheshimiwa tukae. Katibu!

**MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

**Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Mabadiliko ya Katiba wa Mwaka 2013, (The Constitution Review (Ammendment No. 2) Bill, 2013)**

*(Kusomwa Mara ya Pili)*

*Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

**ISSN 0856-035X**

***BILL SUPPLEMENT***

***No. 14*** ***25th October, 2013***

*To the Gazette of the United Republic of Tanzania No. 43 Vol. 94 dated 25th October, 2013*

Printed by the Government Printer, Dodoma by Order of the Government

# THE CONSTITUTIONAL REVIEW (AMENDMENT NO. 2) ACT, 2013

## ARRANGEMENT OF SECTIONS

*Section* *Title*

1. Construction.

2. Amendment of Section 22.

3. Amendment of Section 24.

4. Amendment of Section 26.

5. Amendment of Part VI.

*Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

## NOTICE

This Bill to be submitted to the National Assembly is published for the general information to the public together with a statement of its objects and reasons.

Dar es Salaam
28th October, 2013

**OMBENI Y. SEFUE**
*Secretary to the Cabinet*

**A BILL**
*for*

An act to amend the Constitutional Review Act, Cap. 83.

**ENACTED** by Parliament of the United Republic of Tanzania.

Construction

**1.** This Act may be cited as the Constitutional Review (Amendment No. 2) Act, 2013 and shall be read as one with the Constitutional Review Act, hereinafter referred to as the "principal Act".

Amendment of section 22

**2.** The principal Act is amended in section 22 by:

(a) deleting paragraph (c) of subsection (1) and substituting for it the following:

"(c) two hundred and one members appointed by the President in agreement with the President of Zanzibar as follows:

(i) twenty members from Non-Governmental Organisations;

(ii) twenty members from Faith Based Organisations;

(iii) forty two members from all fully registered Political Parties;

(iv) twenty members from Higher Learning Institutions;

(v) twenty members from groups of people with special needs;

(vi) nineteen members from Trade Union Organisations;

(vii) ten members from an association representing livestock keepers;

(viii) ten members from fisheries association;

(ix) twenty members from agricultural associations; and

(x) twenty members from any other groups of persons having common interest;

(b) deleting subsection (2A) and substituting for it the following:

"(2A) The President shall invite each group specified under subsection (1)(c) from both sides of the union to submit to him a list of not less than six names and not more than nine names for consideration of appointment, provided that, the list shall-

(a) for every name proposed, indicate the age, gender, experience, qualifications and place of abode for that person;

(b) take into consideration gender balance."

*Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

Amendment of section 24

**3.** The principal Act is amended in section 24 by:

(a) adding immediately after subsection(1) the following new subsection:

> "(2) Subject to the provisions of subsection(1) and without prejudice to the provisions of this section, the Clerk of the National Assembly and the Clerk of the House of Representatives shall make necessary preparations for the better carrying out of the Constituent Assembly business."

(b) renaming subsections(2) to (6) as subsections (3) to (7);

(c) deleting the word "secondment" appearing in the renamed subsection (6) and substituting for it the word "attachment.

Amendment of section 26

**4.** The principal Act is amended in section 26 by deleting subsections (3), (4), (5), (6) and (7).

Amendment of Part VI

**5.** The principal Act is amended in Part VI by:

(a) deleting the whole heading;

(b) repealing sections 31 to 36;

(c) renumbering sections 37 and 38 as sections 31and 32 respectively.

Dar es Salaam,
*28th* October, 2013

**MATHIAS M. CHIKAWE**
*Minister for Constitution and Legal Affairs*

*Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

## OBJECTS AND REASONS

The Bill proposes to amend the Constitutional Review Act, Cap. 83 by deleting and re-writing paragraph(c) of section 22(1) for the purposes of increasing the number of the members of the Constituent Assembly to be appointed by the President in agreement with the President of Zanzibar from the current number of 166 to 201.

In addition, it is proposed that subsection (2A) of section 22 be deleted and substituted with intent to set the minimum and maximum number of persons to be proposed by each group mentioned in that section and to be submitted for appointment to the President for consideration of appointment. Currently, the law only provides for a maximum number.

Section 24 of the Act is proposed to be amended by adding a new subsection (2) which will allow the Clerks of the National Assembly and the House of Representatives to make necessary preparations to enable the Constituent Assembly to carry out its business efficiently. This provision is new.

Section 26 is amended by deleting subsections (3) to (7) with an intent to allow the Constituent Assembly to prescribe its own Standing Orders which will guide voting procedures in the Assembly and how to reach consensus when deliberating on matters before it.

The heading of Part VI is proposed to be deleted as well as section 31 to 36 which provides for the procedure of conducting referendum. This is due to the fact that the procedure of conducting referendum will be provided by the Referendum Act to be enacted.

*Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

**ISSN 0856-035X**

***BILL SUPPLEMENT***

***No. 14*** ***25th October, 2013***

*To the Gazette of the United Republic of Tanzania No. 43 Vol. 94 dated 25th October, 2013*

Printed by the Government Printer, Dodoma by Order of the Government

# SHERIA YA MAREKEBISHO (NA. 2) YA SHERIA YA MABADILIKO YA KATIBA YA MWAKA 2013

## MPANGILIO WA VIFUNGU

*Kifungu* *Maelezo*

1. Jina.

2. Marekebisho ya kifungu cha 22.

3. Marekebisho ya kifungu cha 24.

4. Marekebisho ya kifungu cha 26.

5. Marekebisho ya Sehemu ya Sita .

*Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

## TAARIFA

Muswada huu utakaowasilishwa Bungeni unachapishwa ukiwa pamoja na Madhumuni na Sababu zake kwa ajili ya kutoa taarifa kwa umma.

Dar es Salaam — **OMBENI Y. SEFUE**
28 Oktoba, 2013 — *Katibu wa Baraza la Mawaziri*

Sheria itakayofanya marekebisho katika Sheria ya Mabadiliko ya Katiba, Sura ya 83.

**IMETUNGWA** na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Jina

**1.** Sheria hii itaitwa Sheria ya Marekebisho (Na.2) ya Sheria ya Mabadiliko ya Katiba ya Mwaka 2013 na itasomwa pamoja na Sheria ya Mabadiliko ya Katiba ambayo katika Sheria hii itajulikana kama "Sheria kuu".

Marekebisho ya kifungu cha 22

**2.** Sheria kuu inafanyiwa marekebisho katika kifungu cha 22 kwa:

(a) kufuta aya (c) ya kifungu kidogo cha (1) na kuiandika upya kama ifuatavyo:

"(c) wajumbe mia mbili na moja watakaoteuliwa na Rais kwa makubaliano na Rais wa Zanzibar kama ifuatavyo:

(i) wajumbe ishirini kutoka Taasisi zisizokuwa za Kiserikali;

(ii) wajumbe ishirini kutoka Taasisi za Kidini;

(iii) wajumbe arobaini na mbili kutoka Vyama vyote vya Siasa vyenye usajili wa kudumu;

(iv) wajumbe ishirini kutoka Taasisi za Elimu ya Juu;

(v) wajumbe ishirini kutoka katika makundi ya watu wenye mahitaji maalum;

(vi) wajumbe kumi na tisa kutoka Vyama vya Wafanyakazi;

(vii) wajumbe kumi kutoka Chama kinachowakilisha Wafugaji;

(viii) wajumbe kumi kutoka Chama kinachowakilisha Wavuvi;

(ix) wajumbe ishirini kutoka Vyama vya Wakulima;

(x) wajumbe ishirini kutoka makundi mengine yoyote ambayo yana malengo yanayofanana."

(b) kufuta kifungu kidogo cha (2A) na badala yake kuweka kifungu kipya kifuatacho:

"**2A.** Rais ataalika kila kundi lililotajwa katika kifungu kidogo cha (1)(c), kutoka kila upande wa Muungano kuwasilisha kwake orodha ya majina yasiyopungua sita na yasiyozidi tisa kwa ajili ya kufikiriwa kwa uteuzi, isipokuwa kwamba, orodha hiyo itaonyesha katika-

(a) kila jina linalopendekezwa umri, jinsia, uzoefu, sifa na mahali anapotoka mtu huyo;"

(b) itazingatia usawa wa jinsia;

Marekebisho kifungu cha 24

**3.** Sheria kuu inafanyiwa marekebisho katika kifungu cha 24 kwa:

(a) kuongeza, mara baada ya kifungu kidogo cha(1), kifungu kidogo kifuatacho:

"(2) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu kidogo cha (1) na bila kuathiri masharti mengine ya kifungu hiki, Katibu wa

Bunge la Jamhuri ya Muungano na Katibu wa Baraza la Wawakilishi watafanya maandalizi muhimu kwa ajili ya utekelezaji bora wa shughuli za Bunge Maalum."

(b) kubadilisha kifungu kidogo cha (2) mpaka cha (6) kuwa kifungu kidogo cha (3) mpaka cha (7);

(c) kufuta maneno "katika masharti ya kuazimwa" yanayoonekana katika kifungu kidogo kipya cha (6) na badala yake kuweka maneno "wameazimwa".

Marekebisho ya kifungu cha 26

**4.** Sheria kuu inafanyiwa marekebisho katika kifungu cha 26 kwa kufuta vifungu vidogo vya (3), (4), (5), (6) na (7).

Marekebisho ya sehemu ya sita

**5.** Sheria kuu inafanyiwa marekebisho katika sehemu ya sita kwa:-

(a) kufuta kichwa chote cha habari;
(b) kufuta vifungu vya 31 mpaka 36;
(c) kuvipa namba upya vifungu vya 37 na 38 kuwa 32 na 33.

---

**MADHUMUNI NA SABABU**

---

Muswada huu unapendekeza kufanyia marekebisho Sheria ya Mabadiliko ya Katiba kwa kufuta na kuandika upya aya ya (c) ya kifungu cha 22(1) kwa madhumuni ya kuongeza idadi ya wajumbe wa Bunge Maalum ambao wanateuliwa na Rais kutoka katika idadi iliyopendekezwa ya wajumbe 166 kuwa 201.

Aidha, kifungu kidogo cha (2A) cha kifungu cha 22 kinapendekezwa kufutwa na badala yake kuwekwa kifungu kipya. Mabadiliko haya yamekusudia kuweka kiwango cha chini na cha juu cha wajumbe ambao wanapendekezwa kutoka katika Taasisi zilizotajwa katika kila Taasisi na kupelekwa kwa Rais ili awafikirie kwa uteuzi. Kwa sasa, Sheria inaainisha idadi ya juu tu.

Katika kifungu cha 24 marekebisho yanayopendekezwa ni kwa kuongeza kifungu kidogo cha (2) ambacho kinawaruhusu Katibu wa Bunge la Jamhuri ya Muungano na Katibu wa Baraza la Wawakilishi kufanya maandalizi muhimu ambayo yatawezesha Bunge Maalum kufanya shughuli zake kwa ufanisi. Masharti haya hayakuwa yamewekwa katika Sheria kama inavyosomeka sasa.

Kifungu cha 26 kinafanyiwa marekebisho kwa kuvifuta vifungu vya (3) hadi (7) kwa madhumuni ya kuruhusu Bunge Maalum kutunga Kanuni zake ambazo zitaainisha utaratibu wa upigaji kura kwa ajili ya kuipitisha Katiba inayopendekezwa na namna ya kufikia muafaka wakati kikao kinaendelea.

Kichwa cha habari sehemu ya sita kinafutwa sambamba na vifungu vya 31 hadi 36 ambavyo vinatoa utaratibu wa

kuendesha kura ya maoni. Kufutwa kwa vifungu hivi kumesababishwa na ukweli kwamba masuala haya yatawekwa kwenye sheria ya kura ya maoni itakayotungwa.

Dar es Salaam,
28 Oktoba, 2013

**MATHIAS M. CHIKAWE**
*Waziri wa Katiba na Sheria*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mtoa Hoja.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 86 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Mwaka 2013, naomba kutoa hoja kwamba Muswada uitwao Sheria ya Marekebisho ya Mabadiliko ya Katiba ya Mwaka 2013 *(The Constitutional Review (Amendment No. 2) Act, 2013)* sasa usomwe kwa mara ya pili na Bunge lako Tukufu liujadili na hatimaye liupitishe kuwa Sheria ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kutoa maelezo kuhusu Muswada huu, napenda kumshukuru sana Dkt. Pindi Hazara Chana, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala; Mheshimiwa William Mganga Ngeleja, Makamu Mwenyekiti wa Kamati hiyo na kupitia kwao naomba niwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati hiyo kwa kazi kubwa waliyoifanya katika kutoa maoni na ushauri uliowezesha kuboresha Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu ni mfupi sana, una vifungu vitano tu, lakini ni Muswada muhimu katika mchakato mzima wa upatikanaji wa Katiba yetu Mpya. Aidha, Muswada huu unaletwa mbele ya Bunge lako Tukufu chini ya utaratibu wa Hati ya Dharura. Ni nadra sana kwa Serikali kuleta hapa Bungeni Miswada chini ya utaratibu huu, lakini tunauleta Muswada huu kwa njia hii ya hati ya dharura ili kuonesha unyeti na uharaka wa Muswada huu katika mchakato mzima wa kupata Katiba mpya.

Mheshimiwa Spika, madhumuni ya marekebisho ya sheria hii ni kukidhi maamuzi ya Serikali yaliyofikiwa baada ya Mheshimiwa Rais kukutana na Wenyeviti wa Vyama vya Siasa vilivyo na uwakilishi hapa Bungeni. Marekebisho haya yanalenga kuondoa upungufu uliobainishwa katika kikao tajwa, kabla ya kuanza kwa utekelezaji wa baadhi ya masharti yaliyomo katika sheria hii ili kusaidia utekelezaji madhubuti wa sheria.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee, naomba kumshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano

wa Tanzania, Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete kwa busara alizotumia kuwaalika na kuongea na Wenyeviti wa Vyama vya Siasa vyenye Wabunge Bungeni ili kuangalia maeneo ambayo yalikuwa yanalalamikiwa katika Sheria hii.

Mheshimiwa Spika, ni kutokana na busara zake, Serikali iliweza kukutana na Vyama hivyo vya Siasa na kujadili kwa kina na kuafikiana juu ya marekebisho ambayo yanapendekezwa katika Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kuvishukuru pia Vyama vyote vya Siasa kikiwemo Chama changu cha CCM ambavyo tulishirikiana navyo katika majadiliano ya jinsi ya kuboresha Muswada huu katika vikao vitatu.

Mheshimiwa Spika, marekebisho yanayopendekezwa katika Muswada huu ni mwendelezo wa nia ya dhati ya Serikali hii ya CCM ya kupata muafaka wa Kitaifa katika mchakato wa kutunga Katiba mpya. Ni imani yetu kuwa marekebisho tunayoyapendekeza yatakubaliwa na Bunge lako Tukufu ili kutuwezesha kuingia katika hatua nyingine ya uundwaji wa Bunge Maalum la Katiba na hatimaye kuifikisha Rasimu ya Katiba kwa Watanzania ili waitolee uamuzi katika kura ya maoni.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza awali, Muswada huu unapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Mabadiliko ya Katiba kwa lengo la kuondoa upungufu ambao umeonekana na kutoa ufafanuzi wa ziada kwenye vifungu kadhaa ili kuondoa utata katika matumizi ya sheria hii.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu unapendekeza kukifanyia marekebisho kifungu cha 22(1)(c) kwa kukifuta na kuandika upya aya (c) ya kifungu hicho. Madhumuni ya mapendekezo hayo ni kuongeza idadi ya wajumbe wa Bunge Maalum ambao wanateuliwa na Rais kwa makubaliano na Rais wa Zanzibar kutoka idadi iliyokuwepo ya wajumbe 166 hadi kufikia wajumbe 201. Idadi hii imetokana na mapendekezo ya Kamati ya Kudumu ya

Katiba, Sheria na Utawala ambayo iliwahi kuyatoa wakati tukijadili Sheria namba (6) ya 2013. Aidha, idadi hii ni sehemu ya maridhiano baina ya Serikali na Vyama vya Siasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuongeza idadi ya wajumbe wa Bunge Maalum, marekebisho yanayopendekezwa katika aya (c) ya kifungu cha 22(1) yamekusudia pia kutaja idadi ya wajumbe watakaoteuliwa na Rais kutoka kila kundi lililotajwa katika aya hiyo. Sheria ilivyo sasa haitaji idadi ya wajumbe watakaoteuliwa kutoka katika kila kundi lililotajwa.

Mheshimiwa Spika, aidha, Muswada huu unapendekeza kukifuta kifungu kidogo cha (2A) cha kifungu cha 22 na kuwekwa kifungu kipya. Mapendekezo ya mabadiliko haya yamekusudia kuweka kiwango cha chini na cha juu cha majina ya watu yatakayowasilishwa kwa Rais na taasisi mbalimbali kwa ajili ya uteuzi wa wajumbe wa Bunge Maalum.

Mheshimiwa Spika, mapendekezo ya Marekebisho haya pia yanaweka sharti kwamba, pindi kila kundi lililotajwa katika aya (c) linapowasilisha majina ya watu wanaopendekezwa kwa ajili ya kuteuliwa na Rais kuwa wajumbe wa Bunge Maalum, lazima kundi husika kuzingatia jinsia, uzoefu, sifa na jiografia na mtawanyiko wa watu katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa sasa Sheria inatoa tu idadi ya juu ya majina yanayopaswa kuwasilishwa kwa Rais na taasisi mbalimbali kwa ajili ya uteuzi wa wajumbe wa Bunge Maalum.

Mheshimiwa Spika, Muswada unapendekeza marekebisho katika kifungu cha 24 kwa kuongeza kifungu kidogo cha (2) ambacho kinawaruhusu Katibu wa Bunge la Jamhuri la Muungano wa Tanzania na Katibu wa Baraza la Wawakilishi kufanya matayarisho muhimu ambayo yataliwezesha Bunge Maalum kufanya shughuli zake katika namna bora. Masharti haya hayakuwepo katika Sheria kama

*Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*


ilivyo sasa na kimsingi mambo yoyote ikiwemo manunuzi ya vifaa muhimu yanaweza kuwa batili kama kifungu hiki hakitawekwa.

Mheshimiwa Spika, Muswada unapendekeza marekebisho katika Kifungu cha 26 kwa kufuta vifungu vidogo vya (3) hadi (7) kwa madhumuni ya kuruhusu Bunge Maalum kutunga Kanuni zake ambazo zitaainisha utaratibu wa upigaji kura na namna ya kufikia muafaka wakati kikao kinaendelea. Kimsingi maamuzi yote ya kupitisha vifungu vya Katiba Mpya yatafanywa kwa kura itakayozingatia upatikanaji wa theluthi mbili ya kura za wajumbe kutoka Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar kwa kila kundi kupiga kura peke yake. Utaratibu wa kupiga kura kwa utaratibu wa *simple majority* sasa unaondolewa kabisa.

Mheshimiwa Spika, mwisho, lakini sio kwa umuhimu, Muswada unapendekeza kufuta kichwa cha habari cha Sehemu ya Sita ya Sheria sambamba na vifungu vya 31 hadi 36 ambavyo vinatoa utaratibu wa kuendesha kura ya maoni. Kufutwa kwa vifungu hivi kumesababishwa na ukweli kuwa masuala haya yatawekwa kwenye Sheria ya Kura ya Maoni ambayo Bunge lako linatarajiwa kuizungumza hivi karibuni.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya, ni matumaini yangu ya dhati kuwa Bunge litaunga mkono hoja hii kwa vile ni hoja iliyotokana na muafaka uliofikiwa baada ya majadiliano na maafikiano baina ya Serikali na Vyama vyote vya Siasa.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Ahsante, hoja hiyo imeungwa mkono. Sasa nimwite Msemaji wa Kamati iliyopitia Muswada huu, Mheshimiwa Pindi Chana!

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)
*[MWENYEKITI WA KAMATI YA BUNGE YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA]*

**MHE. DKT. PINDI H. CHANA - MWENYEKITI WA KAMATI YA BUNGE YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 86(5) ya kanuni za kudumu za Bunge, Toleo la Aprili, 2013, naomba kuwasilisha maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusu Muswada wa Sheria ya Mabadiliko ya Katiba, Muswada Na. 2 wa mwaka 2013 *(The Constitutional Review (Amendment) Bill No.2, 2013).*

Mheshimiwa Spika, Muswada huu uliwasilishwa kwanza kwenye Kamati ya Uongozi mnamo tarehe 6 Novemba, 2013 kwa hati ya dharura kwa mujibu wa Kanuni ya 80(5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Aprili, 2013.

Baada ya Kamati ya Uongozi kuridhika kuwa unastahili kuwasilishwa kwa dharura, Kanuni ya 84(1) ilizingatiwa. Kwa msingi huo, Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala ilikutana tarehe 7 Novemba, 2013 katika Ukumbi Na. 231, Ofisi ya Bunge, Dodoma ili kufanya uchambuzi wa kina. Lengo la uchambuzi huo lilikuwa ni kuona kama kweli kuna haja ya marekebisho hayo na mapendekezo yanaweza kukidhi haja.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Muswada, kama nilivyotangulia kusema, Muswada huu umeletwa kwa hati ya dharura na kwamba Kamati ya Uongozi imeridhika kuwa, kwa namna ulivyo unafaa kuzingatiwa katika hali hii. Kamati ya Katiba Sheria na Utawala mara baada ya kuupokea, ilikuwa na jukumu la kuuchambua na kuona kama mabadiliko hayo yana tija au la na vilevile kama umezingatia mambo ya msingi katika utungaji sheria.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza jukumu hilo lenye umuhimu mkubwa kwa mustakabali wa taifa letu, umakini mkubwa ulihitajika. Kamati ilipokea maelezo ya serikali kuhusu mantiki, sababu, madhumuni, mpangilio na maudhui kwa kulinganisha hali ilivyo kwa sheria zilizopo na inavyoweza kuwa baada ya kupitisha sheria hii.

Mheshimiwa Spika, aidha, upembuzi wa faida na madhara kutokana na Bunge kupitisha au kutopitisha

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Muswada huu ni moja ya mbinu iliyotumika wakati Kamati ilipokutana. Jambo lingine muhimu llililozingatiwa na Kamati ni uzito wa upungufu na namna inayofaa kurekebisha kwa mustakabali wa Taifa.

Mheshimiwa Spika, kama ilivyo kawaida ya majadiliano yoyote, si rahisi kukosa kutofautiana kwa hoja ingawa baadaye hutokea kukubaliana. Napenda kuliarifu Bunge hili kuwa, tulikuwa na mijadiliano yenye mvutano mkali kuhusu mambo makubwa matatu:-

(1) Idadi ya Wajumbe wa Bunge Maalum;

(2) Idadi ya chini na ya juu ya wajumbe wanaopendekezwa kwa Rais kwa ajili ya uteuzi; na

(3) Ukomo wa uhai wa Tume ya Mabadiliko ya Katiba.

Mheshimiwa Spika, tofauti hizo zinatokana na kutofautiana kimitazamo hususan kuhusu idadi ya wanasiasa katika Bunge Maalum la Katiba dhidi ya idadi ya wajumbe wengine. Aidha, wapo waliotumia misingi kulenga kufanikisha dhamira njema ya mchakato wa Katiba.

Mheshimiwa Spika, mambo hayo yote yasingeweza kuepukika kwa kuwa suala la mchakato wa Katiba linagusa mambo mengi ya kiutawala, kisiasa na uendeshaji wa nchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilizingatia umuhimu wa mambo ya msingi na hatimaye kufikia uamuzi kwa njia ya makubaliano na kupiga kura.

Mheshimiwa Spika, jambo lolote linalolenga kustawisha misingi ya nchi na kuzingatia tunu za Taifa, halipaswi kupingwa kwa vyovyote vile.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naomba kutoa taarifa kuwa, Kamati ilichambua Ibara zote tano (5)

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

za Muswada. Katika uchambuzi huo, Kamati ilibaini mambo makuu matano (5) yanayojitokeza katika mapendekezo haya ya Serikali. Mambo hayo ni:-

(1) Pendekezo la kuongeza Idadi ya Wajumbe wa Bunge maalum kutoka 166 hadi 201;

(2) Kuweka kiwango cha chini na cha juu cha idadi ya watu wanaopendekezwa kwa ajili ya kuteuliwa na Rais;

(3) Kutoa ruhusa kwa Katibu wa Bunge la Jamhuri ya Muungano na Katibu wa Baraza la Wawakilishi kufanya maandalizi yote muhimu kwa ufanisi wa Bunge Maalum la Katiba. Hata hivyo, Kamati imebaini kwamba, Ibara ya 22(a) ya Sheria ya Mabadiliko ya Katiba, Sura namba 83 ya mwaka, 2011 inatamka kwamba, Katibu wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Katibu wa Baraza la Mapinduzi, watasimamia mchakato wa kumchagua Mwenyekiti wa muda wa Bunge Maalum;

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri kwamba, kwa kuwa sheria ilikusudia kumtaja Katibu wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar na siyo Katibu wa Baraza la Mapinduzi, Serikali ifanye marekebisho ili kuondoa dosari hiyo;

(4) Kuliachia Bunge Maalum kuweka utaratibu wake wa kupiga kura na kufikia makubaliano wakati wa majadiliano; na

(5) Kuondoa utaratibu wa kura ya maoni juu ya Katiba kutoka katika sheria hii.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mambo hayo, ziliibuka hoja mbalimbali wakati wa majadiliano. Hoja hizo zilihusu:-

(1) Mantiki ya kupendekeza ongezeko la idadi ya Wajumbe wa Bunge Maalum watakaoteuliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kushirikiana na Rais wa Zanzibar, kutoka Wajumbe 166 hadi 201.

(2) Utaratibu utakaotumika kuzingatia uwakilishi kutoka Zanzibar na Tanzania Bara katika kupata idadi hiyo ya Wajumbe 201 inayopendekezwa.

(3) Vile vile yaliyokuwa Makubalino ya Vyama vya Siasa kuhusu sheria inayopendekezwa.

(4) Mantiki ya kuwa na Wajumbe arobaini na mbili (42) kutoka vyama vyote vya siasa vyenye usajili wa kudumu.

(5) Sababu ya kuweka kiwango cha chini na cha juu cha idadi ya Wajumbe wa Bunge Maalum watakaoteuliwa na Rais.

Mheshimiwa Spika, maelezo ya Serikali kuhusu hoja hizo yaliiridhisha Kamati na kuafiki kuwa, kimsingi mapendekezo haya ya Serikali yanapaswa kuungwa mkono kwa ujumla wake. Uamuzi huu ulifikiwa katika kikao cha Kamati, kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 117(11).

Mheshimiwa Spika, zipo sababu za msingi zilizoifikisha Kamati katika uamuzi huu. Naomba kulijulisha Bunge lako Tukufu baadhi ya sababu hizo kama ifuatavyo:-

(1) Mapendekezo hayo yanazingatia maridhiano na mashauriano miongoni mwa wananchi wa kawaida pamoja na makundi na asasi/taasisi mbalimbali nchini. Mambo haya ni muhimu kwa mustakabali wa Taifa.

(2) Muswada umeandaliwa kwa kuzingatia namna ya kuongeza ufanisi wa Bunge Maalum.

Kwa mfano, si rahisi kutokubali pendekezo linalotolewa katika Ibara ya (3) ya Muswada ambalo linajielekeza kwenye umuhimu wa maandalizi yatakayowezesha ufanisi wa Bunge Maalum.

(3) Sheria inayopendekezwa kutungwa inatatua tatizo la baadhi ya mambo yaliyoonekana kuwa na utata

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

na kurahisisha matumizi ya sheria hiyo kwa namna ya utekelezaji bora wa sheria.

Mheshimiwa Spika, pamoja na maelezo yaliyotangulia, matarajio ya Bunge lako Tukufu kwa Kamati hii ni maoni na ushauri wa Kamati baada ya uchambuzi. Naomba kutoa maoni hayo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, maoni kuhusu wataalam; wakati wa uchambuzi wa Muswada Kamati iliona upo umuhimu wa kuweka utaratibu wa Bunge Maalum la Katiba kuwaalika Wataalam wa Masuala ya Katiba pale watakapohitajika.

Mheshimiwa Spika, hii ni kutokana na ukweli kwamba suala la Katiba, pamoja na kwamba ni mchakato wa kisiasa, lakini ipo haja ya kuwaalika wataalam ili kuweza kutoa ufafanuzi katika maeneo fulani fulani. Kwa kuwa utaratibu huu haujawekwa kwenye sheria hii, basi uangaliwe uwezekano wa kuuweka kwenye kanuni za Bunge Maalum la Katiba.

Mheshimiwa Spika, maoni kuhusu uandishi; Kamati ilibaini kuwa, Ibara ya 2(a)(vii), (viii) na (ix) zinahitaji kuangaliwa kwa namna inayofanana. Wakati neno *association* katika Ibara 2(a)(vii) na (viii) limetumika katika hali ya umoja *(singular)*, kwenye fasili hiyo, fasili ndogo ya kirumi (ix) neno hilo limetumika katika hali ya uwingi *(plural)*. Kamati inashauri kuwa, katika fasili ndogo ya (7) na (8) neno *association* liongezwe herufi S ili liwe katika wingi *(plural)*.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwa katika tafsiri ya sheria haitakuwa na madhara, lakini haipendezi kuwa na tofauti ya uandishi wa Muswada ulio katika Kiswahili ikilinganishwa na ule ulio katika Kiingereza. Ibara ya 2 (a) kwenye Kiswahili imeishia Kirumi (iv) na kisha kuanza herufi (a) hadi (f), wakati ibara hiyo katika Kiingereza imeanzia fasili ya kwanza hadi (x). Kamati inashauri kuwa, ili kuweka uandishi vizuri zaidi, kasoro hiyo ifanyiwe kazi na kulinganisha rejea kwa watu watakaotumia lugha hizo mbili tofauti.

Mheshimiwa Spika, mbali na maoni kuhusu uandishi, Kamati pia ina maoni na ushauri kuhusu Ibara za Mswada huu. Pamoja na kuridhika na mapendekezo ya Serikali, Kamati inashauri kuwa Ibara ya 2(b) kwenye kifungu cha 2(a) kinachopendekeza kuongezwa kwenye Sheria, neno la tatu katika mstari wa nne lisomeke *for* badala ya *six*. Sababu ya ushauri huo ni kuzingatia maoni ya Vyama vya Siasa na mchakato wa matayarisho ya Muswada huu. Aidha, ushauri huu unatokana na kurejea chimbuko la hoja ya Muswada unaojadiliwa leo.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kuipongeza Serikali kwa kuja na Muswada huu ambao msingi wake ni kujenga dhana ya makubaliano ya pamoja *(Consensus)* baina ya Serikali, Vyama vya Siasa na makundi ya kijamii. Aidha, napenda kuwashukuru Waziri wa Katiba na Sheria wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Mathias Chikawe; Waziri wa Katiba na Sheria wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Mheshimiwa Abubakar Khamis Bakar; Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, Mheshimiwa Angela Kairuki pamoja na Watendaji wote wa Serikali katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ufafanuzi wa kina walioutoa kuhusu Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Mabadiliko ya Katiba.

Mheshimiwa Spika, kipekee kabisa nawashukuru sana Wajumbe wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kwa kuuchambua Muswada huu kwa lengo la kuuboresha pamoja na kuandaa taarifa hii, kwa kuzingatia kwamba, Muswada umekuja katika kipindi ambacho Kamati ilikuwa bado inaendelea na kazi ya kuchambua Miswada mingine ya Sheria Mbalimbali *(The Written Laws, (Miscellaneous Amendments) Act, 2013)*na Muswada wa Sheria ya Kura ya Maoni *(The Referendum Act,2013)*. Hata hivyo, kwa kuzingatia maslahi ya Taifa, ilibidi kufanya kazi hadi muda wa usiku.

Mheshimiwa Spika, kwa heshima na taadhima naomba kuwatambua Wajumbe wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kama ifuatavyo:-

*Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

*[MWENYEKITI WA KAMATI YA BUNGE YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA]*

Mheshimiwa Pindi Hazara Chana, Mwenyekiti; Mheshimiwa William Mganga Ngeleja, Makamu Mwenyekiti; Mheshimiwa Gosbert Begumisa Blandes, Mjumbe; Mheshimiwa Abbas Zuberi Mtemvu, Mjumbe; Mheshimiwa Nimrod Elirehema Mkono, Mjumbe; Mheshimiwa Felix Francis Mkosamali, Mjumbe; Mheshimiwa Nyambari Chacha Mariba Nyangwine, Mjumbe; Mheshimiwa Fakharia Khamis Shomari, Mjumbe; Mheshimiwa Rukia Kassim Ahmed, Mjumbe na Mheshimiwa Jaku Hashim Ayoub, Mjumbe.

Mheshimiwa Mustapha Boay Akunaay, Mjumbe; Mheshimiwa Mustapha Boay Akunaay, Mjumbe; Mheshimiwa Ramadhan Haji Saleh, Mjumbe; Mheshimiwa Jasson Samson Rweikiza, Mjumbe; Mheshimiwa Tundu Antiphas Mughway Lissu, Mjumbe; Mheshimiwa Deogratias Aloyce Ntukamazina, Mjumbe; Mheshimiwa Ali Khamis Seif, Mjumbe; Mheshimiwa Mariam Reuben Kasembe, Mjumbe; Mheshimiwa Abdallah Sharia Ameir, Mjumbe; Mheshimiwa Halima James Mdee, Mjumbe na Mheshimiwa Zahra Ali Hamad, Mjumbe.

**SPIKA:** Mheshimiwa hapana, ahsante.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA BUNGE YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA:** Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ndiyo maana linaitwa Bunge la Vijana, mnaweza kufanya kazi mpaka usiku. Msemaji wa Kambi ya Upinzani kuhusu maneno hayo!

**MHE. TUNDU A. M. LISSU - MSEMAJI WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika na mimi sijalala kwa kweli.

**SPIKA:** Unaonekana *(Kicheko)*

**MHE. TUNDU A. M. LISSU - MSEMAJI WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, naomba kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani ya Bunge lako Tukufu, kuwasilisha maoni ya Kambi

Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Mabadiliko ya Katiba (Na. 2) ya Mwaka 2013.

Mheshimiwa Spika naomba kufanya hivyo kwa mujibu wa Kanuni ya 86(6) ya Kanuni za Kudumu za Bunge lako Tukufu za mwaka 2013.

Mheshimiwa Spika, tumerudi kwa mara nyingine tena kutafakari mapendekezo ya marekebisho ya Sheria ya Mabadiliko ya Katiba, Sura ya 83 ya Sheria za Tanzania. Hii ni mara ya tatu kwa Bunge lako Tukufu kufanya hivyo kuhusiana na Sheria hii hii.

Mheshimiwa Spika, kama itakavyokumbukwa, marekebisho ya kwanza yalifanyika mwezi Februari ya mwaka jana, wakati marekebisho ya pili yalifanyika aghalabu mwezi mmoja na nusu uliopita. Mara hii, kama ililvyokuwa kwa Sheria Mama wakati wa Mkutano wa Tatu wa Bunge hili Tukufu mwezi Aprili, 2011, Muswada wa Sheria ya Marekebisho umeletwa kwenye Bunge lako Tukufu kwa Hati ya Dharura ya Mheshimiwa Rais ya tarehe 28 Oktoba, 2013.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu ulichapishwa kwenye Gazeti la Serikali la siku tatu kabla, yaani tarehe 25 Oktoba, 2013. Hii ina maana kwamba, kwa mujibu wa kanuni ya 93(3) ya Kanuni za Kudumu na kwa mujibu wa ratiba mpya ya Mkutano huu wa Bunge lako Tukufu, Muswada huu unatakiwa ujadiliwe na kupitishwa kwa hatua zote tatu katika Mkutano huu.

Mheshimiwa Spika, kama tulivyosema wakati wa kujadili Muswada wa Sheria ya Uendeshaji Mahakama wakati wa Mkutano wa Tatu wa Bunge lako Tukufu, matumizi ya Hati ya Dharura katika utungaji wa Sheria yana madhara makubwa na ya wazi kwa demokrasia yetu na hivi ndivyo tulivyosema, naomba kunukuu.

“Sheria zinazotungwa haraka haraka namna hiyo zinakosa uhalali wa kisiasa kwa sababu ya kukosa ushiriki wa

Wabunge na wadau wengine. Vile vile, sheria hizo zinakuwa na makosa mengi kwa sababu ya kukosekana umakini katika kuzitunga na utekelezaji wake kisiasa na kisheria unakuwa mgumu.

Aidha, sheria za aina hiyo zinafisha demokrasia na uwajibikaji wa Serikali kwa Bunge na kwa wananchi kwa sababu jukumu la Kikatiba la Bunge kama baraza la kutunga sheria na la kusimamia Serikali linageuzwa kuwa ni la kupiga muhuri maamuzi na mapendekezo yanayoletwa na Serikali.

Mwishowe, Bunge la aina hiyo linakosa hadhi na heshima kwa wananchi na hivyo kukaribisha aina nyingine za siasa za nje ya Bunge."

Historia ya miaka miwili ya Sheria ya Mabadiliko ya Katiba inathibitisha ukweli wa kauli hii.

Mheshimiwa Spika, kama ilivyokuwa kwa marekebisho ya kwanza ya Sheria hii, Muswada huu umekuja kufuatia Rais Jakaya Kikwete kuingilia kati kufuatia mtafaruku uliotokea wakati wa na baada ya kupitishwa kwa marekebisho ya pili ya Sheria hii wakati wa Mkutano uliopita wa Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, mara hii Mheshimiwa Rais aliwaita Viongozi Wakuu wa Vyama vya Siasa vyenye uwakilishi Bungeni kwenye majadiliano yaliyofanyika Ikulu, Dar es Salaam, tarehe 15 Oktoba, 2013. Baadaye, kwa maelekezo ya Mheshimiwa Rais, Viongozi Wakuu wa Vyama hivyo walikutana chini ya uratibu wa Kituo cha Demokrasia Tanzania, mnamo tarehe 17 na 20 Oktoba, 2013, ili kukubaliana juu ya maeneo ya Sheria hii yanayohitaji kurekebishwa kwa ajili ya kuyawasilisha Serikalini. Muswada huu ni matokeo ya mchakato huo.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu unapendekeza marekebisho katika vifungu vitatu vya Sheria na Sehemu ya VI ambayo vifungu vyake vikuu vitafutwa na kutungwa upya katika Sheria ya Kura ya Maoni ya 2013.

Mheshimiwa Spika, maeneo yanayopendekezwa kurekebishwa yanahusu idadi ya wajumbe wa Bunge Maalum wasiotokana na Wabunge, mamlaka na utaratibu wa uteuzi wao; mamlaka ya Makatibu wa Bunge la Jamhuri ya Muungano na Baraza la Wawakilishi kufanya maandalizi kwa ajili ya utekelezaji bora wa shughuli za Bunge Maalum na utaratibu wa kufanya maamuzi juu ya Rasimu ya Katiba katika Bunge hilo. Eneo la mwisho linalopendekezwa kurekebishwa ni utaratibu wa uhalalishaji wa Katiba Mpya katika Sehemu ya VI ya Sheria.

Mheshimiwa Spika, idadi ya Wajumbe wa Bunge Maalum, Muswada unapendekeza kuongeza idadi ya wajumbe wa Bunge Maalum wasiotokana na Wabunge na Wawakilishi kutoka 166 walioko kwa mujibu wa kifungu cha 22(1)(c) cha Sheria ya sasa hadi kufikia wajumbe 201. Hili ni ongezeko la wajumbe 35 na litafanya idadi ya wajumbe wote wa Bunge Maalum kufikia 639. Kama ilivyokuwa tangu Sheria hii ilipotungwa mwaka 2011, wajumbe hawa watateuliwa na Rais kwa makubaliano na Rais wa Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, licha ya mabadiliko ya idadi yao, kuna mapendekezo mengine ya marekebisho yanayohusu wajumbe wa Bunge Maalum. Wakati Sheria ilitamka tu kwamba wajumbe hao watatokana na makundi tisa yaliyoainishwa katika kifungu cha 22(1)(c) bila kufafanua taasisi husika za kila kundi wala idadi ya wajumbe kwa kila kundi, aya ya 2(a) ya Muswada inapendekeza idadi ya wajumbe kwa kila kundi lililotajwa katika kifungu hicho. Hivyo, kwa mfano, kundi la taasisi zisizokuwa za Kiserikali litawakilishwa na wajumbe 20; Taasisi za Kidini zitawakilishwa na wajumbe 20 na Vyama vya Siasa vyenye usajili wa kudumu vitawakilishwa na wajumbe 42.

Makundi mengine ni taasisi za elimu ya juu ambazo zitawakilishwa na wajumbe 20; makundi ya watu wenye mahitaji maalum wajumbe 20 na Vyama vya Wafanyakazi ambavyo vitawakilishwa na wajumbe 19. Makundi mengine ni Vyama vinavyowakilisha Wafugaji vitakavyowakilishwa na wajumbe 10; wajumbe 10 kutoka Vyama vya Wavuvi;

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

wajumbe 20 kutoka Vyama vya Wakulima na wajumbe 20 kutoka makundi mengine yoyote ya watu wenye maslahi yanayofanana.

Mheshimiwa Spika, aya ya 2(b) ya Muswada inamtaka Rais kuyaalika makundi hayo kutoka pande zote mbili za Jamhuri ya Muungano kumpelekea orodha ya majina ya watu wasiopungua sita na wasiozidi tisa kwa ajili ya kufikiriwa kuteuliwa kuwa wajumbe wa Bunge Maalum. Kwa kila jina litakalopendekezwa, kutaoneshwa umri, jinsia, uzoefu, ujuzi na mahali anapoishi mhusika. Katika kufanya uteuzi kutokana na majina hayo, Rais atatakiwa kutilia maanani uwiano wa kijinsia.

Mheshimiwa Spika, mapendekezo ya marekebisho haya ni mapya na kwa kiasi fulani ni hatua chanya ikilinganishwa na Sheria kama ilivyo sasa. Kwanza, ongezeko lolote la wajumbe wasiokuwa Wabunge na Wawakilishi linapunguza hodhi ya Vyama vya Siasa kwa mchakato wa Katiba Mpya. Hii ni kwa sababu, sifa mojawapo kuu ya Wabunge au Wawakilishi wa aina zote ni kwamba, wote wametokana na ni wanachama wa Vyama vya Siasa.

Pili, kwa kuweka idadi ya wajumbe watakaowakilisha kila kundi lililotajwa na kifungu cha 22(1)(c) cha Sheria, kuna uwezekano mkubwa zaidi wa makundi hayo kuwakilishwa katika Bunge Maalum kuliko ambavyo idadi ya kila kundi isingewekwa wazi.

Tatu, kwa sababu ya ongezeko la wajumbe wasiokuwa Wabunge na Wawakilishi, kuna uwezekano mkubwa zaidi wa mjadala katika Bunge Maalum kuwa bora zaidi kwa kuingiza sauti na mitazamo isiyotawaliwa na maslahi ya kivyama. Yote haya yanaongeza uwezekano wa kupatikana Katiba Mpya yenye taswira ya Kitanzania zaidi badala ya Katiba mpya yenye taswira ya kivyama zaidi na hayana budi kuungwa mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Hata hivyo, mapendekezo haya bado hayajatosheleza haja ya kuwa na mchakato wa

kidemokrasia zaidi na wenye kujenga maridhiano ya Kitaifa katika kutengeneza Katiba Mpya. Kwanza, kwa kuendelea kumng'ang'aniza Rais kuwateua wajumbe hawa, Muswada huu unaendeleza dhana ya Urais wa Kifalme katika mchakato wa Katiba Mpya.

Mheshimiwa Spika, tumeielezea dhana hii kwa kirefu kuhusiana na mchakato huu kiasi kwamba hatuna haja ya kujirudia rudia hapa. Itoshe tu kukumbushia kwamba hata Chama cha Mapinduzi katika enzi za ujana wake kilikuwa kinatambua hatari ya Urais wa Kifalme katika mfumo wa Kikatiba na kisheria wa nchi yetu. Ndio maana katika Mwongozo wake wa 1981, CCM ililalamika kwamba "madaraka mengi na makubwa yamelimbikizwa katika Ofisi ya Rais."

Mheshimiwa Spika, ukweli ni kwamba, hata Rais Kikwete mwenyewe ameonesha dhahiri kwamba hataki mamlaka haya ambayo Muswada huu unamng'ang'aniza. Katika mkutano wake na Viongozi Wakuu wa Vyama vya Siasa, Mheshimiwa Rais alisema kwamba, alikuwa tayari kuyaachia makundi yaliyotajwa katika kifungu cha 22(1)(c) kuteua wawakilishi wao wenyewe endapo vyama vya siasa vingekubaliana juu ya *formula* ambayo ingehakikisha uwiano mzuri wa jinsia unazingatiwa. Ndiyo maana Vyama vya Siasa vyenye uwakilishi ndani ya Bunge hili vilikubaliana kwamba na naomba kununukuu:-

"Kifungu cha 22(2A) cha Sheria kama ilivyo sasa kifutwe kabisa na kwamba wajumbe waliotajwa katika kifungu cha 22(1)(c) watateuliwa na taasisi wanazoziwakilisha."

Pili, kwa kutaja makundi ya jumla badala ya kutaja taasisi zinazounda makundi hayo, Muswada huu unatoa mwanya kwa Rais kuteua watu anaowataka yeye na kueleza kwamba wametokana na kundi mojawapo ya yale yaliyotajwa katika kifungu cha 22(1)(c) cha Sheria.

Mheshimiwa Spika, kwa kiasi fulani, hivyo ndivyo

ilivyotokea wakati wa mchakato wa kuteua wajumbe wa Tume ya Mabadiliko ya Katiba, kwa kadiri ya taarifa zilizotolewa na wadau mbele ya Kamati ya Kudumu ya Bunge lako Tukufu ya Katiba, Sheria na Utawala wakati wa kujadili marekebisho ya pili ya Sheria hii mwezi Agosti mwaka huu.

Tatu, hata kama majina atakayopelekewa Rais hayatachakachuliwa, mapendekezo ya aya ya 2(b) hayawezi kutekeleza matakwa ya kuwa na wajumbe 201 wanaopendekezwa kwenye aya ya 2(a) ya Muswada huu. Hii ni kwa sababu aya hiyo inapendekeza Rais apelekewe majina yasiyopungua sita na yasiyozidi tisa kutoka kila kundi lililotajwa katika kifungu cha 22(1)(c) kutoka sehemu mbili za Jamhuri ya Muungano.

*Assuming*, kama aya ya 2(b) inavyoashiria, kwamba kila sehemu ya Jamhuri ya Muungano ina makundi yaliyotajwa katika kifungu hicho, kutakuwa na makundi 20 yatakayotakiwa kupeleka majina kati ya sita na tisa kwa Rais kwa ajili ya uteuzi.

Mheshimiwa Spika, endapo kila moja ya makundi hayo litapeleka idadi ya juu kabisa inayopendekezwa na Muswada na endapo wajumbe wote hao watateuliwa kuwa wajumbe wa Bunge Maalum, idadi yao itakuwa 180 tu. Kutakuwa na baki ya wajumbe 21 ambao haijulikani watatoka wapi.

Mheshimiwa Spika, kwa upande mwingine, endapo kila kundi lililotajwa litapeleka idadi ya chini kabisa ya majina kama inavyopendekezwa na idadi hiyo wakateuliwa wote bila kuacha hata mmoja, basi idadi ya wajumbe wa Bunge Maalum wasiotokana na Bunge au Baraza la Wawakilishi itakuwa 120. Kutakuwa bado na akiba ya wajumbe themanini na moja ambao haijulikani watapatikana wapi na kwa utaratibu gani.

Mheshimiwa Spika, kwa vyovyote vile linavyoangaliwa, pendekezo la aya ya 2(b) ya Muswada haliwezi kutekeleza matakwa ya pendekezo la aya ya 2(a)

ya Muswada huu kuhusu idadi ya wajumbe wa Bunge Maalum wasiokuwa Wabunge na Wawakilishi.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapendekeza namna tatu za kutatua tatizo hili. Njia ya kwanza ni kufuta kabisa pendekezo la Rais kupelekewa kati ya majina sita hadi tisa kwa ajili ya uteuzi. Badala yake, aya ya 2(b) ipendekeze kwamba Rais apelekewe na makundi husika majina kulingana na idadi iliyopangwa kwa kila moja ya makundi yaliyotajwa na kifungu cha 22(1)(c) cha Sheria. Hii itahakikisha kwamba idadi ya wajumbe mia mbili na moja inayopendekezwa inafikiwa.

Mheshimiwa Spika, kwa wanaopendekeza kivuli kikubwa cha Rais katika mchakato wa Katiba Mpya kiendelee, pendekezo hili litamwondolea Rais *discretion* aliyo nayo katika kuteua wajumbe hao wa Bunge Maalum. Badala yake, kazi ya Rais itakuwa ni *mere formality* kwa maana kwamba atateua wajumbe kutokana na idadi kamili atakayopatiwa na kila kundi.

Mheshimiwa Spika, namna ya pili ya kutatua tatizo lililoletwa na pendekezo la aya ya 2(b) ya Muswada ni kufanya idadi ya majina atakayopelekewa Rais kuwa kubwa zaidi ya idadi ya wajumbe wa kila kundi. Hivyo, kwa mfano, kundi la taasisi zisizo za Kiserikali au za Kidini, au taasisi za elimu ya juu, litapeleka majina kati ya 30 hadi 40 ili Rais ateue wajumbe 20 wa kundi hilo kama inavyopendekezwa na aya ya 2(a).

Mheshimiwa Spika, aidha, kwa makundi ya Vyama Vya Wafanyakazi au Wakulima au Wafugaji nayo yatapeleka majina mengi zaidi ya mgawo wao ili Rais aweze kuteua idadi ya wajumbe inayotakiwa kwa kila kundi.

Mheshimiwa Spika, pendekezo hili litahifadhi mamlaka *substantive* ya uteuzi aliyo nayo Rais, lakini litathibitisha dhana kwamba wajumbe hao ni watu wa Rais badala ya kuwa wawakilishi wa makundi yaliyowapendekeza.

Mheshimiwa Spika, njia ya tatu ya kutatua tatizo la namna ya kuwapata wajumbe wa Bunge Maalum waliotajwa katika aya ya 2(a) ya Muswada ni kuzitaja taasisi zinazounda makundi hayo na kuzigawia idadi ya wajumbe watakaoteuliwa kutoka kila taasisi.

Mheshimiwa Spika, hapa inawezekana kila taasisi iliyotajwa kupeleka majina kulingana na idadi ya wajumbe iliyotengewa, kama ulivyo msimamo wa Kambi Rasmi ya Upinzani au kupeleka idadi kubwa zaidi ya majina kuliko idadi ya wajumbe wa kutoka taasisi hiyo na hivyo kumpa Rais *flexibility* ya kuteua anavyoona yeye inafaa, kama inavyopendelewa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya kwanza ya pendekezo hili ilikwishakubaliwa na Wakuu wa Vyama vinavyounda *TCD,* lakini ikakataliwa na Serikali. Huu ni wakati muafaka wa kulifikiria tena pendekezo hili.

Mheshimiwa Spika, hoja ya gharama za Bunge Maalum, Serikali hii ya CCM imetumia hoja mbili kukataa kuongeza idadi ya wajumbe wa Bunge Maalum.

Kwanza, inadaiwa kwamba ongezeko la wajumbe kama ilivyopendekezwa na wadau wengi, litaongeza gharama za Bunge Maalum katika nyakati hizi za "Sungura Mdogo" na *economic belt-tightening*.

Pili, inadaiwa kwamba Ukumbi huu wa Bunge lako Tukufu unaotazamiwa kuwa *venue* ya Bunge Maalum hautatosha endapo idadi ya wajumbe itaongezeka kama inavyopendekezwa.

Mheshimiwa Spika, mchakato wowote wa maana wa kutengeneza Katiba Mpya huwa na gharama kubwa. Hii ni kweli kwa nchi zote ambazo zimepitia mchakato huo na itakuwa kweli kwa Tanzania pia.

Mheshimiwa Spika, kama Waheshimiwa Wabunge watakavyokumbuka, tangu mchakato huu uanze kwa uteuzi

wa Tume ya Mabadiliko ya Katiba, mwezi Mei Mosi 2012, Bunge lako Tukufu limekwishaidhinisha zaidi ya shilingi bilioni 74.463 kwa ajili ya shughuli za Tume peke yake. Kwa vyovyote vile itakavyokuwa, shughuli za Bunge Maalum zitakuwa na gharama kubwa pia, kama sio zaidi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na ukweli huu, hoja zote mbili za Serikali hii ya CCM ni potofu. Kwanza, hadi sasa, licha ya kutakiwa kufanya hivyo katika Mkutano wa Kumi na Moja wa Bunge la Bajeti, Serikali haijatangaza na wala Bunge lako Tukufu halijaidhinisha bajeti yoyote ya Bunge Maalum.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu hiyo, hakuna msingi wala ushahidi wowote wa kupima ukweli na uhalali wa hoja ya ongezeko kubwa la gharama linalodaiwa na Serikali hii ya CCM endapo wajumbe wa Bunge Maalum wataongezwa kama ilivyopendekezwa na wadau mbalimbali, wakiwemo Vyama vyetu vya Siasa. Vinginevyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali hii ya CCM ilieleze Bunge lako Tukufu na Watanzania kwa ujumla makadirio ya gharama za shughuli za Bunge Maalum. Aidha, Serikali ieleze gharama hizo zimeidhinishwa na kikao kipi cha Bunge lako Tukufu.

Pili, licha ya ukweli wa gharama kubwa za kutengeneza Katiba Mpya, gharama za mchakato mbovu ni kubwa zaidi. Gharama hizo hazijumuishi fedha, muda na rasilimali nyingine peke yake, bali pia zinaweza kujumuisha uharibifu mkubwa wa mali na uchumi na hata upotevu wa maisha ya watu, endapo maridhiano na muafaka wa Kitaifa havitapatikana na nchi ikaingia katika mtafaruku na machafuko ya kisiasa.

Mheshimiwa Spika, kwenye jambo hili, hatuna budi kujifunza kutoka kwa majirani zetu wa Kenya ambapo Rais wa nchi hiyo na Makamu wake wanakabiliwa na mashtaka ya makosa dhidi ya ubinadamu katika Mahakama ya Jinai ya Kimataifa, *The Hague,* kufuatia vurugu za kisiasa zilizosababishwa na machafuko ya Uchaguzi Mkuu wa Desemba, 2007. Uchaguzi huo ulifanyika baada ya mchakato

wa Katiba Mpya ya nchi hiyo kuvunjika mwaka 2006 pale Rasimu ya Katiba Mpya ilipokataliwa na Wakenya kwenye kura ya maoni.

Mheshimiwa Spika, matokeo yake, maelfu ya watu waliuawa au kujeruhiwa, mabilioni ya fedha na mali kuteketea na Jumuiya ya Kimataifa kuingilia kati kabla Wakenya hawajafunguka macho kwamba kujenga muafaka wa Kitaifa juu ya Katiba Mpya ni gharama nafuu zaidi kuliko kiasi chochote cha fedha!

Tatu, hoja ya udogo wa Ukumbi kwa ajili ya Bunge Maalum ni ya kuchekesha. Kwanza, tangu kuzaliwa kwake zaidi ya miaka thelathini na sita iliyopita, CCM imefanyia Mikutano yake yote Mikuu hapa Dodoma. Hata vyama vya upinzani kama CHADEMA na *CUF* navyo vimefanya Mikutano yao Mikuu au Mabaraza ya Taifa hapa hapa nchini. Mikutano na Mabaraza hayo ina mamia na hata maelfu ya wajumbe na suala la udogo wa kumbi za kuifanyia halijawahi kuizuia isifanyike.

Pili, hoja hii inapingana moja kwa moja na kauli ya Katibu wa Bunge lako Tukufu kwa vyombo vya habari kwamba Ukumbi huu utawekewa viti vingine 750 ambavyo vitatosha ukumbini hapo bila kubanana.

Mheshimiwa Spika, naomba kurudia sehemu hii; pili hoja hii inapingana moja kwa moja na kauli ya Katibu wa Bunge lako Tukufu kwa vyombo vya habari kwamba Ukumbi huu lutawekewa viti vingine 750 ambavyo vitatosha ukumbini hapo bila kubanana. Hata kama bado hautatosha kwa ajili ya idadi ya wajumbe wa Bunge Maalum wanaopendekezwa na wadau, basi ukumbi mwingine mkubwa zaidi unaweza kutafutwa hapa hapa Dodoma na hata nje ya Dodoma kama ikihitajika. Muafaka wa Kitaifa juu ya Katiba Mpya ni muhimu zaidi kuliko gharama za ukumbi wa mikutano.

Mheshimiwa Spika, Makatibu wa Bunge Maalum: Aya ya 3(a) ya Muswada inapendekeza kumpa Katibu wa Bunge

la Jamhuri ya Muungano na Katibu wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar mamlaka ya kufanya maandalizi muhimu kwa ajili ya utekelezaji bora wa shughuli za Bunge Maalum. Katika haraka haraka ya kupitisha marekebisho ya pili ya Sheria hii, suala hili halikuwekwa kwenye Muswada na hivyo halikufikiriwa na Bunge lako Tukufu. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaunga mkono pendekezo hili.

Mheshimiwa Spika, hatma ya Tume ya Mabadiliko ya Katiba; kwa mujibu wa Sheria kama ilivyo sasa, Tume ya Mabadiliko ya Katiba itavunjwa na Rais baada ya kuwasilishwa kwa Rasimu ya Katiba kwenye Bunge Maalum. Hata hivyo, kwa mujibu wa kifungu kipya cha 20(4) cha Sheria: "Katibu wa Bunge Maalum anaweza, kwa kushauriana na Mwenyekiti wa Bunge Maalum, kumwalika Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti au Mjumbe yeyote wa Tume iliyovunjwa ili kutoa ufafanuzi utakaohitajika wakati wa mjadala wa Bunge Maalum."

Mheshimiwa Spika, licha ya matakwa haya ya Sheria kama ilivyo sasa, kifungu cha 33(2) cha Sheria hiyo hiyo kinailazimisha Tume kutoa elimu ya uraia na uhamasishaji juu ya Katiba inayopendekezwa kwa muda usiozidi siku thelathini kuanzia siku ya kuchapishwa (kwa taarifa ya kura ya maoni) katika Gazeti la Serikali. Hii ni kwa madhumuni ya kuelimisha na kuhamasisha wananchi kuhusu kuipigia kura ya maoni Katiba inayopendekezwa. Aidha, sambamba na kifungu cha 33(2) cha Sheria, Bunge lako Tukufu limetenga mabilioni ya fedha kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu haya ya Tume katika mwaka huu wa fedha wa 2013/2014.

Mheshimiwa Spika, pendekezo la kuivunja Tume mara tu baada ya kuwasilisha ripoti yake na Rasimu ya Katiba kwa Rais halikuwa sehemu ya Muswada wa Sheria ya Marekebisho iliyopitishwa katika Mkutano uliopita wa Bunge lako Tukufu. Kwa mujibu wa Taarifa Rasmi ya Majadiliano ya Bunge *(Hansard)* ya tarehe 6 Septemba, 2013, hoja hiyoililetwa Bungeni na Mheshimiwa Selemani Jafo. Katika hoja yake, Mheshimiwa Jafo alidai kwamba pendekezo hilo, nanukuu:

"Ni kutokana na kilio cha Watanzania wengi waliokuwa wanapiga kelele mpaka wengine kuwavunjia heshima wazee wetu ambao kwa kweli wapo tu."

Mheshimiwa Spika, taarifa hiyo ya *Hansard* inaonesha kwamba hoja ya Mheshimiwa Jafo iliungwa mkono na Waziri wa Katiba na Sheria, Mheshimiwa Mathias Chikawe kwa maneno yafuatayo, naomba kununukuu:

"Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hili Mheshimiwa Jafo wala asipoteze nguvu nyingi sana kulisemea, kwa sababu na mimi naliona na nakubali kwa sababu, inawezekana ilikuwa tu ni *oversight* kwa upande wetu tulipokuwa tunatunga hii sheria. Haiwezekani Tume ikaendelea bila kuvunjwa."

Mheshimiwa Spika, taarifa hiyo inaonesha vile vile kwamba, hoja ya Mheshimiwa Jafo iliungwa mkono pia na Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba yake kwa wananchi ya tarehe 4 Oktoba, 2013, Rais Kikwete aliisifu kazi ambayo Tume imeifanya kwa maneno yafuatayo, naomba kununukuu:

"Bahati nzuri (kutengeneza Katiba ya watu wa vyama vyote na wasiokuwa na vyama ambao ndio wengi kuliko wote) ndio sifa kubwa iliyooneshwa na wajumbe wa Tume ya Mabadiliko ya Katiba. Wamewasimamia na kuwasemea watu wote bila ya kubagua. Natambua kuwepo kwa baadhi ya watu ambao hawafurahii msimamo huo na matokeo ya kazi yao. Watu hao kuwalaumu wajumbe wa Tume kwa ajili hiyo ni kutowatendea haki." Mwisho wa kununukuu.

Mheshimiwa Spika, akizungumzia uhai wa Tume, Mheshimiwa Rais alisema yafuatayo, naomba kununukuu tena:

"Katika orodha ya madai ya ndugu zetu wa Upinzani lipo suala la uhai wa Tume ya Katiba. Wanataka usiishe wanapokabidhi rasimu ya pili kwa Bunge Maalum bali waendelee kuwepo mpaka mwisho wa mchakato. Nimeulizia

ilikuwaje? Nimeelezwa kuwa jambo hili halitokani na mapendekezo ya Serikali wala ya Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, limetokana na pendekezo la Mbunge katika Bunge wakati wa kupitia vifungu na kuungwa mkono na Wabunge wengi. Kwa hiyo, kuilaumu Serikali si haki, Serikali inaweza kuwa mshirika katika hoja hii. Nami naiona hoja ya Wajumbe wa Tume kuwa na wajibu wakati wa Bunge Maalum hasa wa kusaidia kufafanua mapendekezo ya Tume."

Mheshimiwa Spika, kama Mheshimiwa Rais mwenyewe anaiona hoja ya wajumbe wa Tume kuwa na wajibu wakati wa Bunge Maalum hasa wa kusaidia kufafanua mapendekezo ya Tume, haitaeleweka endapo Bunge lako Tukufu litakataa kufanya marekebisho ya Sheria hii ili kuiwezesha Tume kuendelea kuwepo kama ilivyokuwa kabla marekebisho ya pili hayajapitishwa. Kwa sababu hizo na kama walivyokubaliana Viongozi Wakuu wa Vyama vya Kibunge, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapendekeza kama ifuatavyo kuhusu hatima ya Tume ya Mabadiliko ya Katiba:-

(a) Kifungu cha 20(4) cha Sheria kifutwe kabisa;

(b) Kifungu cha 22(1) kirekebishwe kwa kuongeza aya ya (d) mara baada ya aya (c) itakayosomeka kama ifuatavyo:

"Wajumbe wa Tume ambao hawatakuwa na haki ya kupiga kura katika Bunge Maalum, yaani watakuwa wajumbe *ex officio* wa Bunge Maalum."

(c) Kifungu cha zamani cha 37(1) kirejeshwe ili kuwezesha uwepo wa Tume hadi baada ya matokeo ya kura ya maoni kutangazwa kama ilivyokuwa kabla ya marekebisho ya pili ya Sheria hii.

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa kupitisha Vifungu vya Katiba Mpya: Aya ya (4) ya Muswada huu inapendekeza kufutwa kwa vifungu vidogo vya (3), (4), (5), (6) na (7) vya

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

kifungu cha 26 ambavyo viliingizwa na marekebisho ya pili. Vifungu hivyo vilikuwa na athari ya kuruhusu Katiba Mpya kupitishwa kwa wingi wa kawaida wa wajumbe wa Bunge Maalum. Mapendekezo ya marekebisho ya kifungu yana athari ya kurudisha *status quo ante*, yaani hali kama ilivyokuwa kabla ya marekebisho ya pili ya Sheria hii.

Mheshimiwa Spika, kwa maana hiyo, endapo mapendekezo haya yatakubaliwa na Bunge lako Tukufu, Katiba Mpya itaamuliwa kwa wingi maalum wa theluthi mbili ya wajumbe wote wa Bunge Maalum wanaotoka Tanganyika na idadi hiyo hiyo ya wajumbe wanaotoka Zanzibar. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inayakubali mapendekezo haya na inawasihi Waheshimiwa Wabunge wote wayaunge mkono.

Mheshimiwa Spika, uhalalishaji wa Katiba mpya; aya ya (5) ya Muswada inapendekeza kufutwa kwa vifungu sita vya Sehemu ya Sita ya Sheria inayohusu uhalalishaji wa Katiba Mpya. Kama tulivyosema awali, vifungu vinavyofutwa vimehamishiwa katika Muswada wa Sheria ya Kura ya Maoni, 2013.

Mheshimiwa Spika, Vifungu viwili vinavyopendekezwa kubaki ni kifungu cha 37 kinachohusu kuvunjwa kwa Tume na ambacho tumekwishakijadili kwa kirefu; na kifungu cha 38 kinachohusu kuanza kutumika kwa Katiba Mpya. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inakubaliana na mapendekezo ya marekebisho haya na inasihi Waheshimiwa Wabunge wote wayaunge mkono.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema yote haya, naomba kuwasilisha na nashukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Nashukuru. Sasa nitawaita wafuatao waweze kujadili, kama mnavyoona muda nilionao ni mdogo. Wachangiaji ni wengi. Kwanza kabisa ataanza Mheshimiwa *Engineer* Mnyaa, atafutiwa na Mheshimiwa Makilagi, halafu tutaona tena kinachofuata baadaye.

**MHE. ENG. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ya kwanza ya kuchangia Muswada huu wa Marekebisho ya Katiba.

Kwanza, niseme tu kwamba, Muswada uliopita. Sheria ilipopitishwa ilileta mzozo hapa Bungeni na ikasababisha sisi wa upande wa Upinzani kutoka nje ya Ukumbi huu.

Mheshimiwa Spika, mtafaruku uliotokea, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, akatumia busara zake akawaita Wakuu wa Vyama na baada ya maagizo yake kupitia Vyama kama *TCD,* vyama vikaweza kutoa mapendekezo.

Mheshimiwa Spika, mapendekezo mengi ambayo ameyazungumza hapa Mheshimiwa Tundu Lissu, yalikuwa ni mapendekezo ya vyama na vyama vile vile vilipokaa kama *TCD,* vikakutana na Serikali. Baada ya kukutana na Serikali, pakajadiliwa ndiyo kufika hatma ya kuletwa Muswada huu leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika majadiliano yote tulikuwa na mambo mengi ambayo tunayahitaji, mengine kama upande wa vyama tukaweza kufanikiwa, mengine hatukuweza kufanikiwa. *Spirit* yoyote ya majadiliano, kwamba ikiwa nina madai 100 nikafanikiwa madai 60, madai 40 sikufanikiwa, upande mwingine wa kiungwana natakiwa niridhike. *(Makofi)*

Kwa mfano, hoja ya *TCD* ya Wajumbe wale kutoka 166, ilikuwa wafike Wajumbe 438, lakini baada ya *TCD* tu Kamati ile ya Ufundi pamoja na Serikali, ikafikia maamuzi Serikali ikakubali kuongeza Wajumbe 35 kutoka 166. Hilo lilikuwa ni makubaliano ya Kamati ile ya Ufundi ya *TCD* na Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo hatukufanikiwa kufika 438, lakini tulifanikiwa kutoka 166, angalau kufika 201. Idadi ile ya 201 kusema kweli iliwahi kupendekezwa katika Kamati

ya Katiba, Sheria na Utawala katika Bunge lililopita. Serikali bila shaka ilitoa sababu na nyingine zinakubalika. Lakini katika *spirit* ya makubaliano *TCD* ilibidi wakubali hoja hii. Yako ambayo *TCD* ilikubaliana kutokukubaliana, lakini ndiyo hali ya *negotiation* ya pande mbili, lazima yapo ya kufanikiwa na yale ambayo hayatafanikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hivyo kwa hili, huu Muswada vifungu vyote vya 22, 24 na 26, kusema kweli vimetokana na makubaliano. Naunga mkono hoja hii, kwa sababu kama tutaendelea kuwa na malumbano ya muda mrefu hatutofika dhamira tunayo kusudia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niseme jambo moja na katika hao Viongozi wa Vyama walipokwenda Ikulu, kuonana na Mheshimiwa Rais, walikwenda na wasaidizi wao, nami nilikuwa miongoni mwao.

Mheshimiwa Spika, Kauli aliyoizungumza Mheshimiwa Rais ni kwamba, katika jambo hili la Muswada huu wa Katiba mpya au kupata Katiba mpya ya Jamhuri ya Muungano, ni lazima tuwe na *spirit* ya kuzungumza na kukubaliana na ikiwa tutazungumza kwanza, nje ya Bunge kama Vyama, Miswada kama hii inapoingia Bungeni inakuwa ni rahisi kupitishwa. Kwa hali hiyo, niseme kwamba Muswada huu, unakubaliana na unakwenda sambamba na makubaliano kwa asilimia angalau 60%. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine katika Muswada uliopita, au Sheria hii iliyorekebishwa, tulilalamika Bunge lililopita kuhusu kuwakilishwa kwa Zanzibar. Pamoja na kwamba Mheshimiwa Makamu wa Pili wa Rais, alithibitisha hapa kwamba, Zanzibar iliwakilishwa, lakini baadaye ilibainika kwamba ushirikishwaji wake haukushirikishwa kikamilifu, kwa sababu vifungu mwanzo vilikuwa vinne, baadaye vifungu vikawa 12. Hilo lilidhihirika.

Mheshimiwa Spika, safari hii, niishukuru Serikali ya Jamhuri ya Muungano, wamefanya juhudi za kushirikisha kikamilifu upande wa Zanzibar. Muswada huu

*[MHE. ENG. M. H. J. MNYAA]*

unazoungumzwa hapa Bungeni leo ni kwamba una baraka kamili za upande wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuvunjwa kwa Tume ya Katiba Mpya. Hili ni suala ambalo *TCD* tulikubaliana kutokukubaliana, lakini baada ya Serikali kutoa hoja na Zanzibar wakafafanua, kwamba chombo kilichotunga Rasimu ya Katiba mpya, halafu tushiriki nacho kuijadili ni mgongano wa maslahi. Lakini Serikali kitendo cha kukubali kwamba Wajumbe aidha, Mwenyekiti, Makamu au mjumbe yeyote kama wataalam katika Bunge jipya la Katiba, Kanuni zile zitatungwa ili kuruhusu watu wale kuja hapa kama wataalam wakati wowote watakapohitajika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa hata kama tulikubaliana kutokubaliana, kile kitendo cha Serikali angalau hawa watu kupatikana, kwa ushauri kwa kutoa Wataalam wakati watakapohitajika, pia hiyo ni hatua mbele ya kushukuru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, bila ya kupoteza muda niseme tu kwamba Muswada huu sasa utatuwezesha sisi, kusonga mbele katika hatua nyingine ya Rasimu mpya ya Katiba na Bunge jipya la Bajeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hayo machache, naomba kuunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

**MHE. AMINA N. MAKILAGI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Haya makofi yaliyotokea hapa yanaashiria kwamba, Mheshimiwa Mnyaa amenifilisi, lakini kwa sababu mimi ni mwakilishi wa wananchi na hasa wanawake, sitakosa jambo la kuzungumza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwanza kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Mohamed Habib Mnyaa, kwa maelezo mazuri ya ufasaha aliyoyatoa. Maelezo ambayo yamesaidia kuwaelimisha Watanzania ili waweze

kuwa na uelewa wa pamoja. Wapi tulipotoka, wapi tulipo na wapi tunapokwenda kwa manufaa ya Watanzania na hasa wanawake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nasema hivyo kwa sababu, ilipotangazwa kwamba itakapofika tarehe fulani itakuwa ni siku ya kutotii sheria bila shuruti, wanawake kule vijijini waliniuliza Katibu Mkuu unasema nini katika hili. Je na sisi tuweke mgomo? Niliwajibu hapana, msiweke mgomo haya mambo yatakwisha.

Mheshimiwa Spika, naomba nianze kabisa kumpongeza sana Mheshimiwa Mohamed Mnyaa kwa maelezo aliyoyatoa hapa, kwamba mkutano wa *TCD* ulishirikishwa na umefanya kazi nzuri sana, naomba niupongeze na naomba uendelee kufanya hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mara baada ya utangulizi huo, naomba sasa niende moja kwa moja kuzungumzia mambo machache ambayo nimeyapanga kuyazungumza na nitajielekeza kabisa katika masuala yanayowagusa wanawake.

Mheshimiwa Spika, kwanza, naomba niunge mkono hoja hii asilimia mia moja kwa mia moja kwa sababu hoja hii imelenga kwa kweli kutupeleka kule tunakohitaji. Ombi langu ni moja tu kwamba, kwenye makundi yaliyoainishwa kwenye Muswada ambao unawasilishwa kwetu, mfano, makundi ya wakulima, wafugaji, makundi yenye mahitaji maalum na hata makundi yenye malengo yanayofanana na makundi mengine, naomba viongozi watakaowateua wazingatie sana usawa wa kijinsia kati ya wanawake kwa wanaume yaani hamsini kwa hamsini ili Bunge la Katiba litakaloundwa na Wabunge watakaoteuliwa angalau tuwe tumeweza kufikia *fifty fifty* kama ambavyo dhamira imeainisha.

Mheshimiwa Spika, pia naomba sasa Muswada huu tunaoutengeneza ili kuweka sawa na kuondoa utata, maana

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)


unapozungumzia usawa wa kijinsia na unapozungumzia uwiano wa kijinsia baadhi ya watu huwa wanaitafsiri tofauti. Ukikuta kuna watu wakandamizaji wanafikiri usawa wa kijinsia au uwiano wa kijinsia ni kuweka wanawake wanne katika watu labda 20 wanaotakiwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ombi langu ni kwamba, naomba katika kifungu kinachozungumzia usawa wa kijinsia, itamke moja kwa moja asilimia hamsini kwa hamsini kati ya wanawake na wanaume. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vile vile katika makundi yaliyoorodheshwa hapa, kuna mahali nimeona inasomeka Vyama vya Wakulima, mahali pengine panasema Chama cha Wafugaji, lakini nashauri kwamba hakuna Chama cha Wafugaji, maana ukisema Chama cha Wafugaji hapa Tanzania huwezi kukipata na hata ukisema Chama cha Wakulima pia huwezi kukipata, nashauri iendelee kusema Vyama vya Wafugaji.

Mheshimiwa Spika, hapa ninachokisisitiza ni kwamba, tusije tukatoa mwanya kwa wale wajanja wajanja wachache wanaokaa Dar es Salaam wanaopiga maneno, ndiyo wakaja kutengeneza hii sheria. Naomba uwiano wa kuwapata wajumbe kupitia makundi maalum utoke katika Mikoa yote 31 ya Tanzania Bara na Zanzibar na hapa nasisitiza kwa sababu wapo wananchi waliopo Tunduru wana mawazo mazuri na hata Kigoma na kadhalika. Kwa hiyo, hizi taasisi zilizopewa fursa na tukisema watoke kila Mkoa katika Mikoa yote 31 tutaweza kupata uwiano ambao tunauhitaji.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naomba kuunga mkono hoja na ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Mbatia, atafuatiwa na Mheshimiwa Mkanga. Mheshimiwa Mbatia!

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi ya kutoa mchango kwenye Muswada uliopo mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, kwanza, nitoe ufafanuzi kwamba tunaposema *TCD, Summit* ya *TCD* inaundwa na Wakuu wote wa Vyama vya Siasa vilivyo na uwakilishi Bungeni na mazungumzo yaliyofanyika tarehe 15/10/2013 yalikuwa ni ya *Summit* ya Viongozi Wakuu wa Vyama tuliyozungumza na Mheshimiwa Rais, vyama vilivyo na uwakilishi Bungeni.

Mheshimiwa Spika, kwa msingi huo, haya mengine ya utekelezaji yanayozungumzwa hapa, yalikuwa kati ya *Technical Committee* ya *TCD* na Serikali na kwa kuwa muda ulikuwa ni mfupi, hatukupata muda wa kutosha, mapendekezo yale kurudishwa kwa Viongozi Wakuu wa Vyama ili kuafikiana kwa pamoja. Kwa hiyo, ionekane wanaochangia hapa wakitumia *TCD* iwe ni *individual parties* na siyo *TCD* kama *TCD* ili tuweze kuendelea vizuri kwa misingi ya maridhiano.

Mheshimiwa Spika, nasema haya kwa sababu bado tuna safari ndefu ya maridhiano na bado tutazungumza na tunatarajia tukutane Vyama vya Siasa na makundi mbalimbali katika jamii ili tuweze kuridhiana na tukawa na muafaka wa Kitaifa kwa misingi ya kuweza kupata Katiba shirikishi na Katiba ambayo itatokana na maridhiano yaani *consensus* ambayo yatashirikisha kila jamii kwa kiasi kikubwa katika Taifa letu la Tanzania.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa ufafanuzi huo, kwanza kabisa nishukuru kwa kuwa tunazungumzia suala la Katiba bahati mbaya sana Mjumbe mmoja katika Tume ya Katiba ambayo ni muhimu katika Tume hiyo ni mwanasheria na ni mtaalam wa masuala ya sheria, alipatwa na tatizo usiku wa Jumamosi, Dkt. Seng'ondo Mvungi na hali yake kusema kweli bado ni mbaya sana na amelazwa katika Hospitali ya Milpack Afrika Kusini, yuko *ICU*.

Mheshimiwa Spika, sasa hii damu ya Watanzania inayomwagika mara kwa mara, inatupa shaka kubwa sana. Kwa kweli hali yake ni mbaya sana, nawaomba Watanzania waendelee kumwombea na tushukuru kwamba, tangu alipopata tatizo hili na kwa kuwa siku zote anatuambia Katiba ni matokeo ya maridhiano, Katiba ni uhai wa Taifa, Katiba ni sheria kuu na Katiba ina ukuu wake.

Mheshimiwa Spika, sasa mtaalam huyu ambaye amefanya kazi ya maridhiano sana katika Taifa hili, akiwa kwenye mchakato ambao hatujaukamilisha amepatwa na tatizo hili, basi Watanzania tuchukue yale mazuri aliyotuambia kwamba, Katiba ni maridhiano, Katiba ni tendo la Kisiasa, ili turidhiane na tuweze kuvuka hapa tulipo kwa sasa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee nimshukuru Mheshimiwa Rais, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano, Makamu wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Makamu wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Viongozi wa Vyama vya Siasa, Tume ya Mabadiliko ya Katiba, Hospitali ya Moi, Mawaziri Wakuu wastaafu Jaji Warioba, Salim, Sumaye, Malecela na Mheshimiwa Edward Lowassa, Waziri Hussein Mwinyi, Waziri Wiliam Lukuvi na Mheshimiwa Benard Membe na watendaji wote kama Balozi wetu Afrika Kusini, Radhia Msuya na viongozi wote wa Vyama vya Siasa na Msajili wa Vyama vya Siasa.

Mheshimiwa Spika, wengine ni viongozi wa Dini BAKWATA, *TEC* na CCT Baraza Kuu, Taasisi za Mashehe na wanazuoni wa Kiislamu, Chuo Kikuu cha Bagamoyo, Sekta ya Sheria nchini Majaji na Mawakili na kwa namna ya pekee Baba Askofu Sendoro, Profesa Sarungi ambaye analia machozi mpaka sasa hivi, anasema nishani tunayompatia ndiyo hiyo; Mama Edith Lusina, Mama Jidawi, vyombo vya habari na baadhi ya Wabunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimesema nitaje orodha hii kwa sababu wote hawa wanatoka kwenye makundi mbalimbali, lakini tunapotapwa na tatizo la kijamii kama hili, tunaridhiana kwa pamoja. Kwa kuwa, Watanzania tunaweka utu mbele

zaidi na ndiyo maana tunataka Katiba ambayo tunaitunga iwe juu kabisa ya Vyama vyote vya Siasa, Katiba ambayo tunaitunga siyo ya Itikadi ya Chama chochote kile cha Siasa kwa kuwa Bunge hili kwa kiasi kikubwa linawakilisha Watanzania.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, inabidi kufikiri kwa mapana ili yale ambayo tunayafanya kwa nia njema na Mheshimiwa Rais ameonesha nia njema na kwa kiasi kikubwa basi wale ambao wanaona kwamba labda wengine wanatoka nje ya Bunge halafu wanakwenda kwa Mheshimiwa Rais, niseme la hasha! Haikufanyika hivyo, Mheshimiwa Rais alikuwa juu kabisa ya itikadi za vyama na ndiyo maana aliwashirikisha wote kabisa kwa umoja wetu kama Taifa la Tanzania ili tuweze kulivusha Taifa letu hapa tulipo leo hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niwaombe basi, viongozi wetu wa Dini wakuu, ukisoma Biblia Takatifu katika Mathayo 5:9 inasema: "Heri wapatanishi maana wataitwa wana wa Mungu."

Qurani Tukufu au Wosia wakati wa Mtume Muhamad *(Swalallah Alayh Wasaalam)* alipokuwa ameona Makabila mbalimbali yanagombana Makka wakati wanataka kuweka jiwe kuu mahali pa kuhiji, sehemu takatifu, aliyaita yale makabila mbalimbali yaliyokuwa yanagombana, akawaambia tulieni, akatumia hekima na busara, hakutumia kanuni wala sheria.

Akavua kilemba chake, akawaambia wekeni jiwe, sasa wawakilishi wa makabila mbalimbali kila mtu ashike kile kilemba aweke kwenye Mimbari na mpaka leo lile eneo limekuwa ni eneo tukufu na ni eneo ambalo ndugu zetu Waislamu wanahiji, alitumia hekima na busara, lilikuwa ni tendo la maridhiano.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niwaombe ndugu zangu kwamba, Katiba ni tendo la maridhiano, Katiba tunayohitaji siyo kwa ajili yetu tu bali ni kwa ajili ya vizazi vijavyo na miaka

50 ijayo mpaka miaka 100 ijayo. Tukubali kwenye *dialogue* au kwenye mazungumzo kuna *give and take*, kuna mengine unapata na mengine unakosa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa kwa msingi huo kuna yale ya msingi ambayo tumekubaliana, basi yakubalike na kuna mengine ambayo upande wa Serikali unasema hapana, lakini mimi binafsi siyo la *TCD*, kuna suala la Tume ya Katiba ina wataalam mbalimbali, tuone utaratibu, niwe mkweli niko *down* sana kwa sababu sikushiriki kwa kiasi kikubwa kuona mchakato huu vizuri zaidi ya wiki nzima, tuone utaratibu ulio mzuri kwa sababu ukiangalia wenzetu wa Uganda, Zimbabwe, Afrika Kusini pia Kenya walikuwa wanashiriki kama *Ex-officials* ambapo panatokea jambo la ufafanuzi wanatoa ufafanuzi.

Mheshimiwa Spika, tofauti na Katiba tunayoitunga sasa na huko nyuma kama niko sahihi, hii inaanzia kwa wananchi kwa kukusanya mawazo yao, yameingia kwenye mabaraza na itahitimishwa na wananchi wenyewe kwenye kura ya maoni.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba tutumie hekima na busara ili tuone namna gani ya kuwashirikisha hasa kwenye ufafanuzi kwa sababu wao ndiyo wenye hoja na ndiyo mtoa hoja ili tuweze kuvusha Taifa na ili tusiunde *centre* mbili, *centre* moja tukawa huku tunazungumza na wengine wameshavunjwa *then* wanakuwa na kauli nyingine nje ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, tujihadhari sana hata kama kuna mtu anatoa kauli ambayo imeudhi, basi tuwe juu ya kauli hizi, tujihadhari sana na kauli za kulipizana kisasi. Tukichukua chuki binafsi nje, halafu tukazileta ndani ya Bunge hili ndiyo maana linaitwa Bunge Tukufu, hatutavuka!

Mheshimiwa Spika, hebu tuwe na *maturity*, tuwe na ukomavu, tuone kwamba maslahi mapana ya Taifa hili inabidi tushirikishane sote kwa nia njema na naamini sheria hii tunayoitunga kwa nia njema tukiweza, tutavuka. Nikiri kwa

asilimia kubwa yale ambayo tulizungumza na Mheshimiwa Rais na tukaafikiana yako kwenye Muswada huu, kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Spika, lakini kuna mengine ambayo japo tulikubaliana, lakini lenye maamuzi ya mwisho ni Bunge hili Tukufu. Kwa kuwa lenye maamuzi ya mwisho ni Bunge hili Tukufu, basi lisitufunge midomo kwa wengine kuweza kutoa na wao mawazo yao ili kuiboresha zaidi kwa sababu huu utakuwa ni Muswada wa Bunge Tukufu. Lakini kwa kiasi kikubwa yale maridhiano tuliyokubaliana kwa kweli naomba tuaminiane ili tuweze kuvuka, tuaminiane ili kesho mtu akitoa kauli yake iwe kwa maneno na kwa matendo tuwe tunaaminiana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kauli hiyo na kwa nafasi hiyo uliyonipatia, nashukuru sana na naomba nikiri kwamba, tupo kwenye mchakato wa maridhiano, tushirikishane wote kwa nia njema. Kwa upande wangu kwa kiasi kikubwa naunga mkono Muswada huu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Margareth Mkanga atafuatiwa na Mheshimiwa Kombo Khamis Kombo.

**MHE. MARGARETH A. MKANGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kusema machache kuhusu Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, kwanza, naunga mkono hoja, hata kama nitayazungumza kama mzungumzaji aliyekaa sasa hivi, labda ni kuendelea kuboresha kwamba twende vipi katika mchakato huu ili kusudi tuweze kuumaliza salama. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, licha ya kuunga mkono kwa ujumla, nimefarijika sana na mawazo, mchango na ushauri uliotolewa na Mheshimiwa Mnyaa na Mwenyekiti Mheshimiwa Mbatia aliyekaa sasa hivi. Kwangu wamezidi kunipa uelewa na hasa yale yaliyopita wiki mbili au tatu,

kumbe yalikwisha vizuri kabisa huko na hayo ndiyo yameletwa hapa ili tu tumalizie na tuendelee kuyaboresha. Ni *spirit* nzuri na nadhani tumeanza vizuri na tutafika salama. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika Muswada huu nimefurahi sana kwamba mawazo ya Kamati iliyochambua Muswada huu ya awali ya kuongeza wajumbe kutoka 166 kufikia 201 wameyarudia na wakayaridhia kwa sababu unaweza ukaona kama umekosea lakini kurudi kwa jema la nyuma ni vizuri sana.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hii imetuonesha kwamba ah! Walikuwa kama vile, lakini wamerudi nyuma na katika kurudi nyuma tumeongeza wajumbe na mgawanyo wake kwa kweli umeeleweka au unaendelea kueleweka.

Mheshimiwa Spika, ningependa katika makundi haya ya mgawanyo wa nani aende hao 20 kama Muswada ulivyopendekeza, sehemu ya kumi ni makundi ambayo yatakuwa na wajumbe wale wenye nia iliyo sawa; hapo pawe na uangalifu na waongezwe na wengine ambao watatoka kwenye kundi lingine ambalo lilifikiriwa hivyo, lakini kwa maoni yangu, naona hilo kundi lililofikiriwa wengine wapungue waje kwenye hili kundi namba 10 ninalolisema.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, Ibara ya 2(c) na kuendelea, (v) kuna watu wenye mahitaji maalum. Naiomba Serikali hapo iendelee kufikiria, hivi hao watu wenye mahitaji maalum ni akina nani na inakuwajekuwaje hapo? Waendelee kufikiria vizuri ili kusudi tuweze kuwa na *clear demarcation* ya nani ni nani katika mchakato huu.

Mheshimiwa Spika, sina mengi ya kuchangia kwa ujumla, lakini nime-*move amendment,* tutakapokuja kwenye vifungu naamini nitapata nafsi ya kuendelea kufafanua nini

hasa ambacho nakipendekeza katika Muswada huu ili kusudi kwa upande wangu twende vizuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunisikiliza hoja yangu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ukiwa na *amendments,* kama ukiweza kuiongelea vizuri sasa, wakati wa *amendments* wenzako watafuatilia vizuri zaidi kwa sababu umeeleza na huzuiwi na muda. Kama una *amendment* hapo, ukipata nafasi ya kuzungumza, basi zungumzia ile *amendment* ili kusudi tuweze kukuelewa vizuri, hata wewe ungeongea.

**MHE. MARGARETH A. MKANGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa sababu muda haujakwisha.

Mheshimiwa Spika, nilidhani napaswa kusubiri kwenye vifungu, lakini kama ruhusa ya kikanuni ni hiyo, haina tatizo!

Mheshimiwa Spika, katika Muswada wetu Ibara ya 2(c) na ndogo ya (5), kwa mapendekezo yangu ninavyoona, haya maneno *special needs* kwamba pawe na wajumbe 20 wa makundi ya watu wenye mahitaji maalum.

Mheshimiwa Spika, napendekeza kabisa kwa heshima napenda tuite kabisa moja kwa moja hapo watu wenye ulemavu na tuondoe *special needs*, kwa nini? *Special needs* kwa sasa hivi watu tunavyozungumza, nadhani kila mtu ana mahitaji yake jamani, sasa tunaposema *needs* ni nini? Ni chakula au mavazi?

Mheshimiwa Spika, hayo ni ya jumla kwa wote, lakini kwa watu wenye ulemavu ni kweli pamoja na chakula na

*Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*


malazi sijui na kitu gani, tuna mahitaji maalum ambayo wengi wanayasahau kwa sababu huwezi kuyaelewa mpaka haya mambo yawe yamekusibu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, napenda kabisa tuweke; 20 *members from people with disabilities*. Hapa Tanzania aina za ulemavu ambazo zinaonekana kwa macho zipo saba na katika hizo saba kila aina ina tatizo la tofauti na la namna fulani ambalo lazima lifikiriwe na kushughulikiwa katika uhai wao.

Mheshimiwa Spika, wengine wanasema wajane ni *special needs,* watoto yatima *special needs* na kadhalika lakini watakutwa huku kwenye namba 10 ya watu wengine wenye *interest* sawasawa kuliko hawa. Tukiliacha hivi mara zote au mara nyingi watu wenye ulemavu wanafunikwa katika maneno hayo bila kuwa *clear*. Hapa napenda pawe *clearly defined,* watu wenye ulemavu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, bila kusahau napendekeza watoke 10 upande wa Zanzibar wake kwa waume, kama mchangiaji mmoja alivyosema; watano wanaume na watano wanawake na Bara watano wanaume na watano wanawake, ishirini waingie humu, wayazungumze haya. Wale akinamama wajane, watoto yatima na kadhalika watakuja kwenye haya mengine, hata kwenye *Government Organization,* huenda utakuta mama mjane ana *NGO* yake huko, lakini hapa kwa nafasi hii tuliyopewa na Taifa hili hebu mtuone kwa mara ya kwanza peupe watu wenye ulemavu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilikuwa kidogo niyanyamazie lakini katika huku kuwaweka wazi kabisa ndiko kutakakotusaidia kujua Wabunge hao watakapoingia humu ndani wanahitaji vifaa gani vya kusikilizia, maana hapa napenda kila aina iingine hapa; wale wa kutafsiri lugha waingie, ndiyo gharama za demokrasia na sisi lazima tuwemo ili tutoe mawazo yetu hapa yote yale. Anayekaa upandeupande, mwandalieni kiti cha kukaa upandeupande, ili mradi ataweza kuchangia mawazo ya kuipeleka nchi yetu hii mbele jinsi tunavyotarajia kwa makundi yote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga tena mkono. Huu Muswada ni mwema na *inshallah* Mungu atuweke hai hilo Bunge bwana tuwemo, litakuwa wapi si kiti ila naamini litakuwepo na tutamaliza salama. Ahsanteni kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Nilimwita Mheshimiwa Kombo Khamis Kombo, halafu nitamwita Mheshimiwa Freeman Mbowe.

**MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Awali ya yote na mimi nishukuru kupata fursa na nafasi hii ya kuweza kutoa mawazo yangu juu ya yale ambayo yameletwa mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, kwa mara ya kwanza niseme kwamba, naunga mkono Muswada huu kwa namna ambavyo ulileṭwa mbele yetu. Kwa sababu ni dhahiri Muswada huu umeshirikisha pande mbili za Muungano kutoka Zanzibar na Tanganyika. *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Spika, sisi Zanzibar tuna uzoefu wa siasa za vurugu. Tuna uzoefu wa siasa za vurugu ambazo kwa kweli zimeshapoteza nafsi za watu walio wengi. Tumefika mahali baada ya kukutana pande mbili, CUF na CCM, tukaweza kuunda Serikali ya Umoja wa Kitaifa na leo hii kukutana kwa vyama vyote na Rais wa Jamhuri ya Muungano, kutokana na vurugu na athari zilizotaka kujitokeza huko nyuma dhidi ya Muswada huu, leo tukafikia mahali tukakubaliana angalau

kwa asilimia sitini (60%), niseme kwamba Watanzania tumepiga hatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata hivyo niseme kwamba endapo ataonekana mmoja wetu akawa na mawazo tofauti dhidi ya kuunga ama kutounga mkono, asionekane adui bali aelimishwe na aelekezwe ili twende sambamba katika kulijenga Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niseme kwamba naungana na idadi iliyotolewa ya watu 201. Hata hivyo, naomba yale ambayo yataamuliwa au idadi hii izingatie uadilifu katika uteuzi wake. Pia si vibaya kama kutoka idadi ya watu 201 ikafika angalau watu 220 mpaka 250, si mbaya. Kama inawezekana basi ifanywe hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile niseme kwamba suala la kuvunjwa kwa Tume ya Katiba si suala ambalo litaanzishwa hapa Tanzania. Wenzetu Zimbabwe walikuwa na Tume ya Katiba lakini katika Bunge la Katiba Tume ile ilikuwa imeishavunjwa. Hata hivyo, nashauri Serikali iunde Kamati ya Wataalam ambao wakati Bunge la Katiba linaendelea basi na Kamati ya Wataalam iwepo ili kuweza kutoa ushauri wa baadhi ya mambo endapo itaonekana kwamba watu wamehitilafiana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia niseme kwamba nimefurahishwa na uwakilishi huu ambao umetaka Wabunge kutoka Tanganyika wapige kura kwa theluthi mbili ($^2/_3$) na Wabunge kutoka Zanzibar wawe na theluthi mbili ($^2/_3$). Hili vilevile ninaliunga mkono. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, niwaambie Waheshimiwa Wabunge, sisi kwenye Quran kuna aya inayosema *Waa taswimu bihabil-llah jamia wala tafarraku*, yaani na shikamaneni katika kamba ya Mwenyezi Mungu wala msifarakane. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, yaliyojitokeza yameishajitokeza, tulipofika tuanze ukurasa mpya wa kujenga nchi. Pamoja

na Mheshimiwa Lukuvi kushika tama lakini nasema tujenge nchi pamoja na *inshallah* tutafika katika safari yetu kwa njia ya kheri. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Freeman Mbowe.

**MHE. FREEMAN A. MBOWE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kunipa nafasi ya kushiriki mjadala huu ambao ni muhimu sana kwa mustakabali wa nchi.

Mheshimiwa Spika, wote tunakumbuka sintofahamu ambayo ilitokea katika Bunge la Kumi na Mbili. Siyo mambo ya kujivunia, wala siyo mambo ya kubezana lakini ni ukweli kwamba hatukulimaliza Bunge lile tukiwa wamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni na mimi nitumie fursa hii kumshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Rais, kwa sababu yeye kwa nafasi yake kama mkuu wa nchi aliona kwamba, nchi yetu haiendi vizuri, Wabunge hatukuweza kuelewana vya kutosha na sintofahamu ile ilikuwa inahamia kwenye umma mpana zaidi wa Watanzania, jambo ambalo kwa kweli wote hatuliombei, lakini lilikuwa ni jambo ambalo lilistahili kiongozi mkuu wa nchi kuingilia kati na ndiyo sababu tunampongeza Rais kwa mkutano ambao tuliufanya tarehe 15 Oktoba, katika ofisi yake Ikulu Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata hivyo pamoja na hayo ni ukweli kwamba, mchakato huu wa Katiba unastahili kuwa shirikishi. Ni mchakato ambao bado tutaendelea kulumbana sana na tutavutana sana, lakini ni rai yangu kwa Wabunge wote wa vyama vyote, wananchi wa vyama vyote bila kujali mtu chama chake ni kipi ama pengine kabila au dini yake ni ipi, sisi wote kama Watanzania tujenge utamaduni wa maridhiano katika mchakato huu wa Katiba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, siamini kwamba kuna mtu yeyote miongoni mwetu humu ndani ambaye anataka mchakato

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)



huu pengine uchafuke, ama pengine kuleta vurugu katika Taifa, lakini pale tutakapokuwa na masikio ya kusikiliza na tukazitumia akili zetu kwa uvumilivu, kwa staha, kwa kuvumiliana hata pale tunapokerana safari yetu itafika salama na tutaweza kumaliza mchakato wa Katiba salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni kweli yako mambo ambayo tuliyadai na sisi tuliyadai siyo kwa ubinafsi wetu, tuliyadai kwa kuangalia kwa upana sana maslahi ya Taifa kwa sababu tuliona mchakato ule ulichukua zaidi msukumo wa kiitikadi tukaacha hata kuangalia mambo mengine ambayo pengine yangetuunganisha zaidi sisi kama Taifa. Kwa hiyo, tulichukua misimamo ile ambayo nina hakika leo imekuwa faida kwa Bunge lako, leo inakuwa faida kwa Taifa letu kwamba tumeweza kuvuka kikwazo kikubwa sana kilichokuwa kinajitokeza kwa sababu tulifanya misimamo ile. Mambo tuliyokuwa tunayapigania mengine leo Serikali imeyaridhia, nina imani kabisa kwamba, hata Wabunge wenzetu wa Chama cha Mapinduzi, nao watayaridhia kwa sababu ya nia njema iliyoko katika jambo hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, yako mambo ya msingi sana tulikuwa tumeyaacha katika Muswada ule. Kwa mfano; hoja ya Makatibu wa Bunge kuanza kufanya maandalizi na kuingizwa na kutambuliwa na sheria, ni mambo ya msingi mno, lakini kwa mazingira yalivyokwenda katika Bunge la Kumi na Mbili, mambo ya msingi kama haya tulikuwa tumeweza kuyasahau, tukayaacha, lakini baadaye tulipopata fursa ya kukaa na kuzungumza tena, tukagundua kwamba tofauti zetu ni ndogo sana, ni tofauti za kimtazamo ambazo tunastahili tuziepuke katika mchakato huu wa kuipata Katiba Mpya.

Mheshimiwa Spika, ni kweli ni lazima yawepo maridhiano katika vyama vya siasa na katika wadau mbalimbali. Vilevile katika *political management, consistency* ni jambo la msingi sana. Mnaweza mkawa na msimamo, wenzenu wakaona hapana msimamo huo haufai, mkaendelea kuwa na msimamo, ukabaki kwenye *record* kwa

[MHE. F. A. MBOWE]

sababu *process* nzima ya kuandika Katiba ni pamoja na kuandika historia ya Taifa kwamba, watu fulani walisimamia jambo fulani mpaka hatua fulani. Hata hivyo, haina maana kwamba hatutaheshimu na hatutambua pale maamuzi yatakapofanywa na wengi na maamuzi ya wengi ni lazima yakubalike kwa sababu ni lazima turidhiane na mwisho wa siku tumalize wote tukiwa salama. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, maamuzi ya kupitisha Katiba kwa *simple majority* yalikuwa ni maamuzi ambayo kwa kweli si mazuri sana. Vilevile yalikuwa ni maamuzi ambayo yanavunja Katiba yetu, lakini watu wamekwenda wamekaa, wameshauriana, busara zimeingia ndani, tukajikuta tunakubaliana wote kwa pamoja kwamba tukubaliane basi iwe ni *two third* (2/3). Kwa hiyo, uamuzi wa kwamba *two third* ya Wabunge wa Bunge la Katiba ndiyo wanaoweza kupitisha vifungu vya Katiba, ni jambo la msingi sana katika *process* ya Katiba na halistahili kufanyiwa utani kwa njia yoyote ile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu Tume ya Mabadiliko ya Katiba. Inaweza ikawa kila nchi ina *experience* ya aina yake lakini napenda kuamini kwamba Tume ya Marekebisho ya Katiba mpaka hatua ya sasa imefanya kazi nzuri. Kwa sababu Tume hii imefanya kazi nzuri na hata Rais akaitambua, kwa vyovyote ina *experience* fulani ambayo sisi Wabunge katika utaratibu wa kawaida hatuna kwa sababu hatukushiriki sana katika hatua za kukusanya maoni ya wananchi. Hili kundi la watu thelathini (30) kuliruhusu likaendelea kuwepo, likaweza kuwa ni *resource group* katika Bunge letu la Katiba, ni jambo la msingi sana. Sioni ni kwa sababu gani inakuwa kama vile tuna ugomvi na Tume ya Katiba. Wana uwezo mkubwa sana wa kutupa mawazo ambayo walikutana nayo kwa wananchi, hawa wamekusanya mawazo ya Watanzania wengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna hoja inatolewa wengine wanasema kwamba, kundi hili ni *interested part*, nani ambaye si *interested part* katika hii *process* ya Katiba? Sisi viongozi wa vyama ni *interested part*, sisi Wabunge ni

*interested part,* Serikali ni *interested part* katika mchakato wa Katiba, iweje Tume ya Katiba ya Warioba ionekane ndiyo *interested part?* Jamani hawa watu wamepata uzoefu mkubwa, wamekusanya maoni ya Watanzania, huu mchakato unaendelea, bado tunawahitaji. Tunawahitaji katika kundi hili kubwa, tunatengeneza kundi kubwa mno halafu tunaacha kundi ambalo limekusanya maoni ya Watanzania wote, tuna maana gani? Sioni sababu yoyote ya hili na ndiyo sababu sisi tulisema pamoja na kwamba Serikali ilionekana kuridhia kufikisha ukomo wa Tume, bado tunaomba busara za Wabunge zitumike na ndiyo *consistency* ambayo mimi ninaizungumza hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, bado tunaomba tusisitize kwamba pamoja na nia njema sana ya maridhiano, mwisho wa siku nina hakika tutaridhiana, lakini ni vyema tukaangalia hii Tume imefanya kazi nzuri, bado tunahitaji watu wa kutuletea mawazo ya watu. Kuna jambo fulani pengine wanaweza wakalitetea katika Katiba au wakatu – *lead* ni nini kiliwapelekea mpaka busara zao zikawafikisha hapo. Hawa ni Watanzania wenzetu, kwa nini tunaona hofu ya kuwa nao kama tunaita makundi mengine ambayo pengine hata hayana *experience* ya chochote kuhusu Katiba, lakini hawa ambao tayari wameishafanya kazi ya msingi kabisa tuwaondoe katika *process*, mimi nafikiri halitakuwa jambo la maana sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika suala la Katiba ndugu zangu tusifanye mambo ya jaziba. Katika suala la Katiba hebu tuone kwamba hii Katiba itaendelea kuishi wakati vyama vyetu pengine Mungu akipenda havitakuwepo. Hebu tuione Katiba hii kama ambayo itaendelea kutumika wakati sisi Wabunge wa leo hatutakuwepo katika maisha haya. Hebu tufikirie *beyond our political parties*. Hebu *tufikirie beyond ourselves*. Tukimzungumza Rais tusiangalie Rais kama Mheshimiwa Jakaya Kikwete, tumuangalie Rais kama mtu mwingine yeyote yule ambaye anaweza kuja kuwepo baada ya miaka hamsini (50) kuanzia leo, ili tuweze kujenga kitu ambacho kinatuunganisha kama Taifa. Tuitumie fursa hii kujenga umoja wetu wa kitaifa. Tutumie fursa hii kumaliza

na kupunguza tofauti zetu. Tusiitumie fursa hii kuongeza tofauti zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri yatakuwepo maneno ya kukerana lakini ili hii *process* iweze kuwa *successful* ni lazima kuwepo na *element* ya kusameheana. Wako watu watabeza wengine, lakini wengine vema watarekebisha na watu watasameheana katika hii *process* ili angalau wote tumalize hii *process* tukiwa Taifa la watu wamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuna matatizo mengi sana hatuwezi kugawana lawama na matatizo, hebu kila mtu awe *sober* katika hii *process*, kila mtu amvumilie mwenzake, kila mtu azungumze kwa hisia lakini hisia zisiwe kali sana. Tuwe na staha, tuwe na kuheshimiana katika hii *process* bila kujali ni chama gani kikubwa ama kipi kidogo ama wangapi, yaani tutafute namna ya kujenga utaifa wetu na umoja wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, CHADEMA hatuna tatizo katika kuunga mkono hoja hii, lakini ambacho napenda kusema tu ni kwamba tutaendelea kujaribu kuomba busara za Wabunge zitusaidie ili tumalize wote tukiwa salama. Katika hatua ya baadaye Mheshimiwa Mnyika ata-*move* hoja ya kufanya *amendments* mbalimbali, hebu naomba tukubaliane kwamba, tunapoweza kurekebisha kidogo tukapata jambo ambalo pengine ni jema zaidi, tusikatae tu kwa sababu za kiitikadi, tukatae kwa hoja, tuijadili, tukiridhiana kuikubali tuikubali, tukiridhiana kuikataa tuikatae, ili tumalize hii *process* tukiwa salama na tumalize Bunge letu la Kumi na Tatu tukiwa salama.

Mheshimiwa Spika, naomba katika hatua hii sasa niseme tunaunga hoja mkono kwa yale yote mema yaliyofanyika na katika hatua ya baadaye ni imani yangu vilevile kwamba, tutaweza kurekebisha pengine tunakoweza kurekebisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninawaomba sana Waheshimiwa Wabunge tumalize hoja hii tukiwa wamoja, tusimalize hoja

hii tukiwa tumetengana. Ahsanteni sana, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Sasa nimwite Mheshimiwa John Mnyika.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Nieleze tu kwamba nimeshiriki majadiliano katika hatua zote za majadiliano na vikao vyote vya majadiliano. Kwenye majadiliano ni ukweli kwamba kuna *spirit* ya *give and take*. Kuna wakati wa kukataa na kuna wakati wa kukubali. Kuna wakati wa kutofautiana na kuna wakati wa kuelewana. Kwa hiyo, kuna mambo ambayo ni wazi kwa pamoja tunakubaliana nayo moja kwa moja. Tunakubaliana kwa pamoja na mapendekezo yaliyoletwa na Serikali ya kurejesha kama ilivyokuwa awali kwamba maamuzi kwenye Bunge la Katiba yafanyike kwa mbili ya tatu ($^{2}/_{3}$) ya pande mbili. Hili ni jambo ambalo naliunga mkono moja kwa moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikubaliane vilevile na mapendekezo ya Serikali ya kutoa majukumu maalum ya maandalizi ya Bunge la Katiba kwa Makatibu; Katibu wa Bunge la Jamhuri ya Muungano na Katibu wa Baraza la Wawakilishi. Hili nalo ni jambo ninalolikubali moja kwa moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini kuna mambo ambayo tunaomba Wabunge wenzetu myatafakari kwa niaba ya Watanzania. Jambo la kwanza, ni idadi ya Wajumbe Maalum katika Bunge la Katiba. Tunatambua kwamba upande wa Serikali na upande na Kamati ya Katiba na Sheria na tunashukuru umekubali kuongeza Wajumbe kutoka 166 mpaka Wajumbe 201. Tunashukuru kwa uamuzi huo wa kuongeza Wajumbe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini uamuzi huu bado hautalivusha Taifa katika mpasuko ulioko nje hivi sasa na mpasuko huu ni mwelekeo wa makundi mbalimbali katika jamii kuona kwamba Bunge la Katiba ni Bunge lililotawaliwa

*[MHE. J. J. MNYIKA]*

na sisi Wabunge na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi ambao tumetokana na Vyama vya Siasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni wazi sisi tumechaguliwa na wananchi na tunaingia Bungeni kuwakilisha na kuwasilisha maslahi ya wananchi lakini tulipochaguliwa, sisi tulichaguliwa na tuliapa kuilinda na kudumisha Katiba iliyopo, hatukuapa na hatukuchaguliwa kwa kazi ya kuandika upya Katiba ya nchi yetu. Natambua nchi mbalimbali zimetumia Wabunge kwenye kuandika Katiba, Zimbabwe jirani yetu wamefanya hivyo na baadhi ya nchi duniani zimefanya hivyo. Hata hivyo, ni ukweli usiopingika kwamba jamii ya nje ya Bunge letu, jamii ya makundi mbalimbali, wakulima, wafanyakazi, Taasisi za Dini, watu wenye mahitaji maalum, wanatamani sana na kama ingekuwa ni ridhaa yao kwa makundi mbalimbali tuliyokutana nao, wanatamani sana kwamba wao wangekuwa wengi katika Bunge Maalum la Katiba*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini inaeleweka kwamba jambo hili lina changamoto zake. Sasa hivi tunavyozungumza, sisi Wabunge pamoja na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwa ujumla tunafikia Wajumbe 438 katika hilo Bunge la Katiba. Kwa hiyo, sisi tutakuwa 438, watu wa makundi mengine wanaoingia kwa ujumla wao kwa Sheria ilivyokuwa ni 166 na kwa mapendekezo ya sasa ni 201 ni sehemu ndogo sana ya sisi wengine ambao ni wengi katika mazingira haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi tulipendekeza kwamba idadi ya makundi haya ya nje, makundi haya mengine katika jamii wawe wajumbe 438 ili iwe sawa na idadi ya Wabunge na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi ilivyo sasa. Hata hivyo, kama tulivyosema majadiliano ni jambo la *give and take*, kuna mambo ambayo unasema, unapendekeza mwenzako anatoa hoja na baadaye mnaona mantiki ya sehemu ya hoja hizo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusikiliza hoja za majadiliano tukaja na pendekezo kwamba idadi hiyo ishuke kutoka 438 mpaka 292. Idadi ya 292 ni sawasawa na $^{2}/_{3}$ ya

438 kwa maneno mengine idadi ya watu wengine wa nje ya sisi Wabunge na nje ya Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi ikiwa ni $^{2}/_{3}$ ya sisi maana yake kunakuwa na hakika ya jamii, kwa sababu Katiba ni zaidi ya Vyama vya Siasa, Katiba ni zaidi ya Wabunge, Katiba ni zaidi ya Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, jamii ya nje ikiwa ni ya $^{2}/_{3}$ kutakuwa na uhakika kwamba tunapoandika Katiba, tunaandika Katiba yenye muafaka wa Kitaifa kwa makundi yote siyo makundi ya watu tu waliotokana na Vyama vya Siasa. Tunaamini jambo hili litajadiliwa na Wabunge wenzetu kwa kulitazama Taifa na siyo kutazama sura ya Vyama vya Siasa. Kuyatazama makundi mengine ya Majimbo mbalimbali tuliyotoka na maeneo mbalimbali tuliyotoka.

Mheshimiwa Spika, hoja ambazo zinatumika kukataa mapendekezo haya ni ukubwa wa Bunge letu kwamba chumba cha kufanyia mkutano kinaweza kisiwepo cha kutosha idadi ya Wajumbe. Hata hivyo, ukijumlisha 438 na 292 inakuja 720 na kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Katibu wa Bunge kwenye vyombo vya habari, Bunge hili vikiondolewa viti hivi vikubwa na vikawekwa viti vya kawaida, litakuwa na uwezo wa kuwa na Wajumbe 750. Tafsiri yake ni kwamba Wabunge hawa watakaoongezeka ambao ni 730 wanaweza kutosha katika Ukumbi huu wa Bunge na bado nafasi 20 zikabaki ndani ya ukumbi huu. Kwa hiyo, tunaamini kwamba hoja ya uKumbi haipaswi kutumika katika kuamua jambo hili nzito kwa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la idadi ya gharama za Bunge hili, sauti ya kupanua wigo wa makundi mbalimbali katika Taifa letu ni sauti iliyotokana na makundi ya nje ya walipa kodi wa nchi hii. Kwa vyovyote vile, makundi haya ya walipa kodi yenye kupaza sauti ya kutaka uwakilishi hayawezi kuwa ya kwanza kupiga kelele pale Bunge litakapofanya uamuzi sahihi wa kuongeza idadi ya Wajumbe kwa gharama za walipa kodi haohao wanaotaka uwakilishi. Makundi haya yanaelewa Taifa hili linahitaji Katiba mpya itakayojenga msingi bora wa Taifa letu kwa miaka mingi zaidi na msingi huu hatupaswi kutazama gharama ya sasa badala

*[MHE. J. J. MNYIKA]*

yake tuepusha gharama za badaye kwa maslahi ya muda mrefu ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo ni la msingi sana katika mapendekezo ambayo bado tunadhani tunahitaji majadiliano. Majadiliano yamefanyike na Serikali, majadiliano yamefanyika na Kamati na sasa tupo ndani ya Bunge kwa sababu Bunge hili ni chombo cha majadiliano. Majadiliano yanaendelea hivi sasa, tunachowaomba wenzetu, bila kujali Vyama, bila kujali itikadi ni kuendeleza majadiliano haya na kufikia hatma, nalo ni suala la ukomo wa Tume ya Mabadiliko ya Katiba.

Mheshimiwa Spika, kwa Mujibu wa Muswada ulio mbele yetu, kuna kifungu cha 5 katika Muswada huu kinachofuta Sehemu ya Sita ya Sheria na kubadili nambari za vifungu vya 37 na 38 na kuvitaja vifungu vya 31 na 32. Katika vifungu hivi, kifungu 37 ni kifungu ambacho vilevile kinahusu masuala ya ukomo wa Tume. Kwa maneno mengine, suala la ukomo wa Tume linajadilika na linaweza kujadilika kwenye Mkutano huu wa Bunge na linaweza kufanyiwa maamuzi kwenye Mkutano huu wa Bunge.

Mheshimiwa Spika, kuna mambo ambayo ni muhimu Wabunge wenzetu wakayatafakari wanapojadili Sheria hii. Tanzania imeandika Katiba kwenye nyakati mbalimbali na mara zote ambazo Tanzania imeandika Katiba, ziwe ni Katiba za mpito za baada ya Muungano au Katiba ya Kudumu ya mwaka 1977, mara zote Bunge la Jamhuri ya Tanzania lilijigeuza kuwa Bunge la Katiba na katika Bunge hilo la nyakati zote hizo, mtoaji hoja wa kuwasilisha Rasimu ya Katiba ndani ya Bunge alikuwa ni Kiongozi wa Shughuli za Serikali ndani ya Bungeni, ndiye aliyekuwa mtoa hoja na ndiye ambaye alihusika kuitetea hoja, kuielezea hoja, kuifafanua hoja mpaka hatua za hoja kuweza kupitishwa.

Mheshimiwa Spika, safari hii tunaenda kwa mfumo tofauti kabisa. Tunaandika Katiba Mpya na tunapoandika Katiba Mpya, Tume kupitia Mwenyekiti wake ndio ambao watakuja ndani ya Bunge kutoa hoja na watawasilisha Ripoti,

watawasilisha Rasimu na watawasilisha Ripoti zote za Timu za Wataalam. Ni wazi, wapo wanaojenga hoja kwamba Tume ikishapeleka ripoti kwa kuwa tayari ina ripoti ya maoni ya wananchi, ina mapendekezo ya Tume, ina ripoti za wataalam, hakuna sababu yoyote ya Tume kuendelea kuwepo kwa sababu tayari maoni ya wananchi yamewasilishwa kimaandishi.

Mheshimiwa Spika, hoja hii bado haijaleta majibu ya masuala ya msingi yanayobaki kama ombwe katika Bunge la Katiba litakapokaa. La kwanza, kama Tume ikishatoa hoja na Tume ikawa imeshavunjwa, wale watu watakaoitwa kuja kutoa ufafanuzi kwa Sheria ya sasa, watakuja wakiwa tena siyo Wajumbe wa Tume. Wakishakuja wakiwa siyo Wajumbe wa Tume, hawawezi kuwa wafafanuaji wa hoja ya Tume kwa kiwango ambacho kama wangekuja wakiwa ni Wajumbe wa Tume. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni wazi kwa mwelekeo ulivyo mpaka hivi sasa, Bunge la Katiba litafanya kwa maridhiano zaidi na mashauriano zaidi kuliko ukumbi wa pamoja. Maridhiano na mashauriano kwenye Bunge la Katiba yatafanyika zaidi kwenye Kamati mbalimbali za Bunge la Katiba ambazo zitakaa wakati Bunge likiendelea. Ni wazi, wafafanuzi wa hoja ndani ya Kamati mbalimbali za Bunge la Katiba wanahitajika kuwa wengi zaidi, hali inayohitaji Tume nzima iwepo, wakiwa ni Wajumbe wasio na kura na maslahi ambao wataweza kulisaidia Taifa letu katika hatua ya Bunge letu kuweza kufanya kazi. Mambo haya yanawezekana kwa sababu tayari ndani ya bajeti yetu tumetenga shilingi bilioni nne kwa ajili ya Tume kuifanya kazi hiyo, tuwawekee utaratibu wa kufanya kazi hiyo kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, kuna jedwali nimeliwasilisha, tukifika kwenye hatua hiyo, tutakwenda kipengele kwa kipengele kwa marekebisho yanayokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Sasa nimwite Mheshimiwa Ole-Sendeka, nawaita wenye majedwali yao waweze kuzungumza tukiwa huru zaidi kusudi tutakapofika kwenye Kamati ya Bunge Zima tuweze kujua nani alikuwa anasema nini? Kwa hiyo, Mheshimiwa Ole- Sendeka atafuatiwa na Mheshimiwa Jenista Mhagama.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi ya kwanza kabisa kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia lakini nikupongeze pia kwa jinsi unavyoliongoza Bunge letu kwa umakini na umahiri mkubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunajadili Muswada huu ukiwa ni matokeo ya busara, hekima, uzalendo wa Rais wa nchi yetu, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, ulio juu ya mipaka na misimamo ya itikadi za vyama. Mheshimiwa Dkt. Kikwete ameweka mbele maslahi ya Taifa letu kama ulivyosema wenzangu walionitangulia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini haya siyo ya leo, moja kati ya vitabu ambavyo huwa ninapenda kutembea navyo nikiacha Mwongozo wa Chama cha Mapinduzi na Biblia ni pamoja na Hotuba hii ya Mheshimiwa Dkt. Kikwete ya tarehe 30 Desemba, 2005 wakati akitoa Dira ya Uongozi anayokusudia au jinsi anavyokusudia kuliongoza Taifa letu. Katika ukurasa wa 15, Mheshimiwa Dkt. Kikwete anasema hivi:-

"Serikali ya Awamu ya Nne inakusudia miongoni mwa mambo mengine kuimarisha utaifa wetu kwa kufanya mambo kumi na mimi nitasoma mawili. La tano, kujenga muafaka baina ya vyama na makundi ya jamii juu ya utambuzi na kuheshimu tunu za Kitaifa kama vile haki, usawa, umoja na mshikamano. Namba kumi, kuimarisha utaratibu wa mazungumzo ili kutatua mapema migogoro katika jamii. Anaendelea kusema zipo sababu kwa nini nchi yetu imekuwa kwa kiwango kikubwa kisiwa cha amani na utulivu katika bahari iliyotibuka. Mojawapo ya sababu hizo kama nilivyosema, ni Sera ambazo kwa makusudi zilijenga hisia za

umoja, hazikuwabagua wala kuwanyima haki Watanzania kwa sababu za kidini, rangi, kabila, jinsia au eneo anakotoka mtu.” Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, tunampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kuamua wa kukaa na wenzetu au Vyama vyetu vya Siasa na kufikia muafaka huu ulio muhimu kwa mustakabali mwema wa Taifa letu. Nachotaka kusema tu kazi iliyopo mbele yetu sasa kama Bunge ni kutimiza wajibu wetu usiokuwa na mbadala wa kutunga Sheria na hii ni kazi iliyopewa Bunge lako Tukufu kwa mujibu wa Katiba. Kwa hiyo, tunapotakafari mambo haya, tunaongozwa na misingi muhimu sana ya kulinda tunu za Taifa letu. Tuna haja ya kutambua kwamba hata tunapozungumza habari ya idadi ya Wabunge au Wajumbe wa Bunge Maalum, tuna kila sababu ya kuangalia uwiano utakaokidhi pande zote mbili za Muungano ili tuhakikishe pia kwamba pande zote mbili zitawakilishwa kwa uwiano mzuri ambao utaweza kujadili maslahi ya pande zote kwa mustakabali mwema wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baadaye nitakapokuwa nikijadili zile nafasi 201, nitakuwa na maeneo ambayo nitayaainisha ambayo ninakusudia kuleta marekebisho ili kuboresha zaidi ili tuweze kwenda vizuri zaidi katika makundi yale ambayo yametajwa katika Muswada wetu.

Mheshimiwa Spika, katika kutazama orodha ile iliyopo kwenye Muswada huu ya makundi yale ambayo yamewekwa hapa, utaona kwamba kuna Wajumbe 20 kutoka Taasisi zisizo za Kiserikali, kuna Wajumbe 42 kutoka Vyama vya Siasa vyenye usajili wa kudumu. Katiba ni mali ya Watanzania wote, kuna makundi mbalimbali yanaendelea kutajwa, lakini napenda kuungana na Wabunge walioeleza bayana kwamba Katiba ni mali ya Watanzania wote, siyo mali ya wasomi na makundi machache ya wanaharakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunapokuja kutafakari baadaye namna ya kupata uwakilishi huu kutoka kwenye Asasi zisizokuwa za Kiserikali, ni lazima tupate sura ya nchi.

*[MHE. C. O. OLE-SENDEKA]*

Lazima tupate watu kutoka kona zote za Tanzania. Lazima tuzingatie kwamba Watanzania asilimia kubwa ni wakulima na wanaishi vijijini hawako Mijini. Lazima Bunge hili Maalum kwa nafasi 201 zitakazoteuliwa ziakisi sura ya Tanzania kwa ujumla wake na zitoe kipaumbele kwa watu waliko huko walio wengi zaidi waliotuleta hata sisi katika ukumbi huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lipo eneo moja ambalo nitalizungumzia baadaye la Wajumbe 42 kutoka vyama vyote vya siasa vyenye usajili wa kudumu. Sina tatizo na idadi ya hii, ninakubaliana nayo lakini nachotaka kusema hapa ni kwamba hapa kuna nafasi 42, vyama vyenye usajili wa kudumu Tanzania vipo 21. Ukichukua vyama 21 ukawapa nafasi moja moja utabaki na nafasi 21. Nafasi 21 zinazobaki, nitapendekeza zigawanywe kwa uwiano wa vyama vyenye Wabunge Bungeni na kwa uwiano wa Wabunge waliopo katika Bunge la Jamhuri ya Muungano. Haiwezekani kama nafasi hizi ni za Vyama vya Siasa ukafananisha Chama kama CCM, CHADEMA, CUF na chama ambacho hakina hata Mwenyekiti wa Kitongoji huko kilipo. Hivi ni vyama ambavyo vimeaminika. Kwa hiyo, tutagawana nafasi 21 kwa uwiano wa Viti vya Wabunge katika Bunge hili la Jamhuri ya Muungano. Wakati huohuo tutaendelea kuzingatia misingi ya Sheria Mama, *Principal Act* ya kulinda maslahi ya uwiano wa upande mbili za Muungano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo hili litakidhi matarajio ya uwakilishi sahihi kulingana na jinsi ukubwa wa vyama vyenyewe vilivyo. Lazima tuwe na *proportion,* hatuwezi tu kukuteua kwa sababu wewe una chama, umesajiliwa watu 200, 200 kutoka katika eneo ukajilinganisha na Vyama vikubwa ambavyo vimepata ridhaa ya nchi kwa sababu tu ya kisingizio kwamba nyie yote mna usajili wa kudumu, hii haiwezekani. Tunajua hata maeneo mengine tumeenda mbali zaidi, baadhi ya wanachama wa chama kimoja wamedhamini vyama vingine vipya wakati wanaendelea kuwa na kadi zao zingine walizonazo. Huko sitaki kwenda zaidi, lakini nitaleta mapendekezo katika eneo hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sina tatizo na wawakilishi kutoka elimu ya juu nafasi zao 20. Tuendelee kuzipata lakini tuhakikishie kwamba tunazitawanya kutoka kwenye Taasisi za Elimu katika Vyuo Binafsi na Vyuo vya Umma. Tunahakikishe sura ya nchi inapatikana. Kwa mujibu wa Sheria hii, mapendekezo haya, bahati nzuri jina la mtu litakuwepo, umri wake utakuwepo, jinsia yake itakuwepo, uzoefu utaonekana, sifa na mahali anapotoka, narudia sifa na mahali anapotoka, hii ni kigezo muhimu sana kwa wale watakaokuwa na dhamana ya kuteua. Lazima tupate sura ya Tanzania katika Bunge la Katiba. Maana mkija tu mkasema mnaenda kwa taasisi za wasomi, mnakwenda kwenye *NGOs*, mnaweza mkajikuta mmeleta Wamasai watupu katika Bunge Maalum badala ya kuwa na sura ya nchi. Tunataka sura ya Tanzania iakisi katika Bunge la Maalum la Katiba. Hii ni mali ya Watanzania wote siyo mali ya wasomi na wajanja wachache ambao wapo kwenye nafasi mbalimbali. Hili lazima tuhakikishe na tumshauri sana Rais na Taasisi yake ya Urais wafanye uchambuzi sana na wawe makini sana katika eneo hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sitaki kuwarudisha nyuma japo sikuridhika sana na idadi ya wawakilishi kutoka kwa wafugaji, wavuvi na wakulima maana ndiyo sehemu kubwa. Hata hivyo, sina tatizo kwa sababu hata hawa wasomi wengine na Taasisi zingine watatoka hukohuko kwa wakulima kama tutahakikisha pia kwamba watapatikana huko na wengine pia watawakilishwa.

Mheshimiwa Spika, nachopendekeza kwa upande wa nafasi ile iliyoandikwa ya wajumbe 10 kutoka chama kinachowakilisha wavuvi, nakubaliana na Katibu Mkuu wa Umoja wa Wanawake wa Tanzania wa CCM, Mheshimiwa Mbunge aliyekuwa amependekeza kwamba tusizungumze habari ya chama, tuzungumze habari ya vyama kwa sababu vyama vya Wavuvi ni vyama, hakuna chama kimoja cha wavuvi, hakuna chama kimoja cha wafugaji. Kwa hiyo, baadaye ni suala tu la kukubaliana, nadhani *Attorney General* atakubali kurekebisha tu pale kidogo ili ionekane kwamba ni vyama na siyo chama.

Mheshimiwa Spika, tukishapitia baadaye katika maeneo hayo, sina tatizo na maeneo yale ila ninaungana na Mheshimiwa Mbunge aliyezungumzia makundi yale ya watu wenye mahitaji maalum kwamba ni vizuri tukaenda kwenye hatua moja mbele ya kuwa wazi kabisa, kama alivyosema Mheshimiwa Margaret Mkanga, mimi nitamuunga mkono kwa asilimia mia kwenye hoja yake anayoipendekeza katika eneo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tukifanya hivi na niwaombe sana wale ambao wanapendekeza tuongeze idadi ya Wajumbe isiwe 201, sisi hapa tukiongeza na wengine 201, tukiwaongeza na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi hata ungeongeza na wengine, mimi nataka kusema kitakachoweza kupatikana kwa Wajumbe hawa 201 ukijumlisha na Wabunge wa Bunge la Jamhuri na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi hakitaweza kupatikana hata ukiongeza hawa 400. Hata hivyo, lazima tuone, kwamba idadi hiyo, unaliongezea pia Taifa mzigo lakini ukweli pia lazima tukubaliane, madhali hutukwenda kuchagua Wajumbe wa Bunge Maalum ili wapate ridhaa ya wananchi, hatuwezi tu tukakaa tukasema teuwa, teuwa mpaka unateuwa wengi kuliko wale waliopata ridhaa ya wananchi, lazima pia twende kwa misingi ya demokrasia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika hili na mimi nitawaomba wenzangu baadaye waniunge mkono kupinga hoja hiyo ya kuongeza Wabunge kwenda idadi hiyo ambayo wengine wamependekeza. Hii ni kwa nia njema tu wala haina ajenda ya siri lakini ni kwa nia ya kulinda maslahi na kufanya kile ambacho kinalinganana na uwezo wa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nina kila sababu tena ya kukushukuru na nitasubiri wakati wangu wa ku-*move amendment* ile, lakini nataka kusema nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Jenista Mhagama.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na mimi kwa kunipa nafasi Ili niweze kuchangia katika hoja hii muhimu sana itakayoipelekea Taifa letu kupata Katiba njema.

Mheshimiwa Spika, nianze kwanza kwa kumpongeza sana Rais wetu, Jakaya Mrisho Kikwete ambaye pia ni Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi. Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete ameonyesha ukomavu na busara ya hali ya juu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo nafarijika Bunge hili limekuwa moja. Watu wote wanaosimama kuchangia Muswada huu, wanaanza na kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu Jakaya Mrisho Kikwete. Hiyo ni faraja kubwa sana kwetu Wabunge wote lakini mimi kama Mbunge wa Chama cha Mapinduzi ni faraja sana kwa Chama changu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la Katiba, ni suala linalopelekea mustakabali wa Taifa. Ninaamini kabisa hakuna kitu chema katika kuendelea na maandalizi haya yatakayotupelekea kupata Katiba nzuri, yenye kukidhi matakwa ya Watanzania kama mijadala yote ndani ya Bunge hili, ndani ya Bunge lijalo la Katiba itaongozwa na hekima na busara na sio jazba, malumbano na mapambano. Hapo kwa kweli nakubaliana na wachangiaji wote waliosema hayo na ninaamini kabisa kwa kufanya hivyo, tutafika mahali ambapo Watanzania waliotupa dhamana, wanatutegemea kuonyesha ukomavu wa kidhamana na kuwarudishia kitu chema kwa maslahi ya nchi yetu na si kwa maslahi ya mtu yeyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema maneno hayo ya utangulizi, kabla sijasahau, ninaunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na kuvipongeza vyama vyote, baada ya jazba nyingi, baada ya malumbano makubwa lakini vyama vyote vilikubali hakuna suluhisho jema bali ni kuketi pamoja, tena kwa kuongozwa na Rais

wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kufikia hitimisho ambalo limeweza kutufikisha hapa tulipo. Nimpongeza Mheshimiwa Mnyaa lakini nimpongeze kwa namna ya kipekee Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni na nimpongeze pia Mheshimiwa Dokta James Mbatia, hawa ni viongozi wakubwa sana katika vyama vyao vya siasa lakini wameelewa umuhimu wa suala hili na mustakabali wa nchi yetu na kukubali haya yaliokwenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa ninayo mambo makubwa mawili katika Muswada huu. Suala la kwanza, nimepokea na kukubali mapendekezo yaliyoletwa katika Muswada huu ya kuruhusu sasa Makatibu, Katibu wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Katibu wa Baraza la Wawakilishi kuanza kazi ya kufanya maandalizi ya shughuli hizi za Bunge la Katiba mapema.

Mheshimiwa Spika, nadhani kuna umuhimu wa kufanya marekebisho kidogo. Pamoja na kwamba Wabunge wote tumekubaliana katika eneo hili lakini vipo vitu ambavyo nadhani kwa maandishi, Wanasheria wapo hapa na hata tukiongozwa na Mwanasheria wetu makini kabisa, mkongwe, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, atatusaidia sana katika jambo hili akiwepo Waziri na Naibu Waziri katika eneo lao hilo la kazi na mimi naamini tutaelewana vizuri.

Mheshimiwa Spika, kwenye ule ukurasa wa 10, kifungu cha 2 cha Muswada huu tumekubaliana na wenzetu Serikali wametuambia wanakuja kuingiza kile kifungu cha 2 kinachosema:-

"Kwa kuzingatia masharti ya kifungu kidogo cha (1) na bila kuathiri masharti mengine ya kifungu hiki, Katibu wa Bunge la Jamhuri ya Muungano na Katibu wa Baraza la Wawakilishi watafanya maandalizi muhimu kwa ajili ya utekelezaji bora wa shughuli za Bunge Maalum".

Mheshimiwa Spika, kifungu hicho cha (1) kinachozungumziwa hapa, ukienda katika Sheria

tuliyoipitisha, kifungu hicho cha 24(1) kimebaki kwa kusema yafuatayo:-

"Mara baada ya Rais kulitangaza Bunge Maalum na kwa kuzingatia masharti ya kifungu kidogo cha (2), Katibu wa Bunge la Jamhuri ya Muungano na Katibu wa Baraza la Wawakalishi kwa mujibu wa Sheria hii, watakuwa Katibu na Naibu Katibu wa Bunge Maalum au kinyume chake".

Mheshimiwa Spika, ukienda kwenye *version* ya Kiingereza, unakuta pia kuna maneno hapo ambayo bado nadhani kama nilivyosema Mwanasheria Mkuu anaweza kutusaidia. Ukurasa wa nne wa sheria ambayo tunaibadilisha, kile kifungu kidogo cha 2 kinasema, *subject to the provision of subsection (1)*. Sasa ukienda kwenye ile *subsection (1)* bado inaendelea ku-*insist*, *immediately after the proclamation* ndipo hawa Makatibu wataanza kazi zao.

Mheshimiwa Spika, sasa mkanganyiko wangu, kuna maneno pale *without prejudice* na huku kwenye mapendekezo haya tunaambia '*shall',* wataanza sasa hivi, nadhani hapo ndipo pana tatizo. Naomba sana Mwanasheria Mkuu atusaidie kidogo ili kuliweka sawa kwa sababu kuna umuhimu sana wa hawa Makatibu wawili kuanza kazi sasa. Mimi nadhani ikiwezekana hata watumishi wa Baraza na Bunge wataanza kusaidia shughuli hizo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hawa Wanasheria wakongwe watatusaidia ili hii mikanganyiko miwili isituharibu na kweli tutoe nafasi kwa Makatibu wetu kuanza kazi. Nimshukuru sana Mwanasheria Mkongwe, Mstaafu, Mheshimiwa Mtemi Chenge kweli kwa pamoja tumelitizama hili tunaona kwamba halijakaa sawasawa. Kwa hiyo, Mtemi nakushukuru sana kwa kuona hili lipo ndivyo sivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukurasa wa nane, kifungu cha 2, unaenda kuangalia ule mgawanyo wa Wajumbe ambao watakuwa wanaingia kwenye Bunge la Katiba. Mimi kitu cha kwanza, niungane mkono na Rais kuachiwa hayo madaraka ya uteuzi, naungana nayo mkono kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, hili la kufikiri kwamba hawa watu wajikusanye tu bila kuwa na utaratibu wowote bado hiyo itakuwa na shida. Tunazo taasisi za dini nyingi, ukienda Mkoa Mbeya peke yake nadhani kuna taasisi za dini zisizopungua hata 500 au 600. Aidha, ukienda kuziangalia *NGOs* zilizokuwa *registered* kwenye Sheria mbalimbali, nafikiri zinafika hata 3000 na kitu, zinazidi hata idadi ya Wajumbe wa hili Bunge la Katiba. Sasa tusipoweka utaratibu wa mgawanyo mzuri na tusipoweka utaratibu wa vyanzo vizuri na mtu mwenye mamlaka ya uteuzi hapo, nadhani tutafikia mahali tutashindwa kufanya uteuzi na Bunge halitaweza kuanza kazi. Kwa hiyo, tumwache Mheshiwa Rais kama ilivyopendekezwa aendelee na kazi baada ya kazi kufanyika na makundi yenyewe.

Mheshimiwa Spika, ninayo hoja nyingine, hivi kwa nini kwenye haya makundi yote tuliyoyaja mfano, Wajumbe 20 kutoka Taasisi zisizokuwa za Kiserikali. Kwa nini Sheria isiseme Wajumbe hao kumi wawe wanawake na kumi wengine wawe wanaume? Wajumbe 20 kutoka Taasisi za Kidini, kwa nini Sheria isiseme angalau kumi wanawake na kumi wanaume. Wajumbe 20 kutoka Taasisi za Elimu ya Juu, kwa nini Sheria isiseme angalau kumi wanawake, kumi wanaume? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naendelea, Wajumbe kumi kutoka vyama vinavyowakilisha wavuvi, angalau kumi wanawake, kumi waume. Wajumbe 20 kutoka makundi mengine yoyote, kumi angalau wanawake, kumi angalau wanaume. Wajumbe kumi kutoka vyama vinavyowakilisha wafugaji angalau kumi wanawake, kumi wanaume hivyo hivyo kwa Wajumbe kutoka Vyama vinavyowakilisha Wakulima. *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Spika, tunakwenda kwenye *spirit* ya 50/50, hamsini kwa hamsini. Mawazo ya wanawake kwenye Bunge la Katiba ni ya muhimu sana. Naamini hata Mheshimiwa Rais kwenye zile nafasi ambazo atapewa kazi hii, akisharahisishiwa hivi, atatuletea 50 kwa 50. *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Spika, wanawake wanaweza na sio lazima wawezeshwe na wanawake ni mhimili imara sana kwa maendeleo ya Taifa hili. Naomba sana Mwanasheria Mkuu, Waziri mwenye dhamana ya Katiba na Sheria na Naibu Waziri, hebu lioneni hili kwa sababu ni muhimu sana sasa hivi tunapoenda kutengeneza Katiba ya nchi yetu na mtaona kazi itakayofanywa na wanawake katika Bunge hili, itakuwa ni kazi ya kutukuka na haitasahaulika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niendelee kuweka mkazo kwenye kifungu kile cha kuwapa mamlaka Katibu wa Bunge na Katibu wa Baraza kuja kuanza kufanya kazi, ni kifungu muhimu sana. Niendelee kusisitiza mgawanyo sawa na niendelee kusisitiza umuhimu wa kumwachia Rais madaraka hayo ya uteuzi baada ya kazi zote kufanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja na nawashukuru viongozi wote wa vyama walioelewa umuhimu wa amani na utulivu wa nchi yetu kama ndio kinga muhimu ya maendeleo ya Taifa la Watanzania.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante, napenda kumwita Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba na Sheria, Mheshimiwa Ngeleja, atamalizia Mjumbe mwingine wa *TCD*, Mheshimiwa Lukuvi.

**MHE. WILLIAM M. NGELEJA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa hii.

Mheshimiwa Spika, kabla sijajikita katika Muswada, naomba nitumie nafasi hii kumshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, kwa hekima na busara zake, pamoja na Serikali yake kwa ujumla kwa jinsi ambavyo waliona ni hekima na busara kukutana na wawakiishi wa wananchi katika mojawapo ya nyanja ambazo ni muhimu sana katika maendeleo ya jamii yetu hasa ya vyama vya siasa.

**SPIKA:** Sijui ungehama mashine hiyo maana tunapata tabu, humu ndani nimetambua watu warefu sana huwa hatuwasikii vizuri. *(Kicheko)*

**MHE.WILLIAM M. NGELEJA:** Mheshimiwa Spika, nilikuwa nasema namshukuru Mheshimiwa Rais, nampongeza na naungana na Watanzania wenzangu hasa kupitia Bunge lako Tukufu kwa jinsi ambavyo alitumia hekima kukutana na viongozi wa vyama mbalimbali vya kisiasa ikiwa ni maandalizi ya Muswada huu uliopo mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, kabla sijajikita katika Muswada, naomba kusema mambo ya msingi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, moja, limesemwa na baadhi ya wasemaji na hasa Taarifa Rasmi ya Kambi ya Upinzani kwamba Miswada inayoletwa kwa utaratibu huu Hati ya Dharura, imeonyesha kwa kadri ambavyo taarifa inavyosemwa, imelifanya Bunge liwe ni chombo cha kupiga mihuri kwa sababu inakosa muda wa kutafakari mambo haya vizuri.

Mheshimiwa Spika, nachotaka kuwakumbusha Watanzania kupitia Bunge lako Tukufu ni kwamba utaratibu wa kuwasilisha Muswada kwa kupitia utaratibu wa Hati ya Dharura, ni jambo la Kikanuni, lina baraka zote, si jambo haramu. Kwa hivi, katika mazingira ambayo yanastahili kufanya hivyo, tunafanya hivyo na sisi wenyewe washiriki katika shughuli hiyo, tunakuwa tumeji-*tune* kulishughulikia kwa kiwango hicho. Kwa hivyo, hili ni jambo halali, si jambo haramu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika amesema maneno kwamba, kwa utaratibu ambao tunaufanya na hasa Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi, inaonekana kama tunamng'ang'aniza Mheshimiwa Rais wetu kufanya mambo na hivyo kurejea ile dhana iliosemwa ya Uraisi wa kifalme. Muswada huu haujafika hapa kwa utaratibu wa dhana hiyo ya kifalme. Tumesikia habari za kushirikishwa *TCD* ambao ni ushirikiano wa vyama ambavyo vinauwakilishi hapa Bungeni lakini pia hili jambo

[MHE.W.M. NGELEJA]

limepitia Kamati ya Bunge. Kwa hiyo, wanavyojaribu kuwaaminisha Watanzania kwamba wakati mwingine utaratibu huu unahalalisha ile dhana ya Urais wa Kifalme sio sahihi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye Kamati tulizungumza mambo mengi na Waheshimiwa Wabunge wamesema lakini mimi naungana na wenzangu wote ambao wameunga mkono Muswada huu na mimi nauunga mkono kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja ya Wajumbe watakaoteuliwa na Mheshimiwa Rais kutoka 201 hadi pendekezo lililowekwa na baadhi ya wazungumzaji hapa kwamba twende kwenye 292, wako wachangiaji ambao wamezungumza kabla yangu wametukumbusha, kwa utaratibu wa kawaida ambao tumejiwekea kama Bunge, Miswada ni lazima ipitie kwenye Kamati. Lilikuwa ni wazo la Kamati ambalo kimsingi tulikubaliana kwamba idadi ya watu watakaoteliwa na Mheshimiwa Rais ambao ni 201, ni muafaka na inakidhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini tunafahamu katika siasa kuna mambo mengi. Kuna dirisha la watu kusema yale ambayo wanakusudia lakini sisi tunajielekeza katika mambo ya msingi kama chombo mahsusi, taasisi inayowakilisha wananchi wa Tanzania. Hili ni wazo sahihi, ni namba ambayo tulikubaliana, tuliichakata vizuri, tukaijadili na tukaitafakari vizuri na tukakubaliana kwamba jambo hili lina manufaa na lina tija. Naomba Waheshimiwa Wabunge wengine tuendelee kuunga mkono Muswada kwa namba hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Muswada huu kama nilivyosema ni shirikishi na tumezingatia kwamba demokrasia pia inatoa fursa kwa wachache kusikilizwa. Mnaofuatilia Muswada huu Mheshimiwa Spika na Watanzania kwa ujumla, ukiangalia sehemu ya mabadiliko, kifungu cha 2A, Serikali ilikuwa inapendekeza kwamba Mheshimiwa Rais katika kila kundi apelekewe idadi ya watu kati ya sita mpaka tisa, lakini

wenzetu Kambi ya Rasmi ya Upinzani walikuja na hoja, wanapendekeza kati ya idadi ya watu wanne mpaka tisa. Sisi tumechukuwa wazo lao la watu wanne mpaka tisa tukitambua kwamba watu wachache nao wanahitaji kusikilizwa. Kwa hiyo, mambo haya kimsingi tumekuwa tukienda kwa kusikilizana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja ya Makatibu wa Bunge na mimi naunga mkono. Tukisoma kifungu cha 24, tumesema kwamba Makatibu wa Bunge hawa wataanza kazi yao hasa baada ya Mheshimiwa Rais kutangaza Wajumbe wa Bunge Maalum lakini kuna kitu nataka niongezee hapo kwamba tukisubiri mpaka Mheshimiwa Rais atangaze, huenda Makatibu hawatapata fursa ya kujiandaa vizuri kwa sababu yapo mambo tumeidhinisha watuandalie ili kujenga msingi wa hiyo kazi itakayofanywa na Bunge Maalum. Mimi naomba Bunge lako Tukufu na nafahamu yapo marekebisho ambayo yataletwa na baadhi ya Wabunge, tuyaunge mkono kwamba hawa Makatibu tuwape *mandate* hiyo ya kuanza kazi mapema kabla ya hapo ili tujijengee utaratibu mzuri wa kufanya hiyo kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, limesemwa suala la ukomo wa Tume na limesemwa na wengi sana lakini na mimi niungane na wale ambao wanaona kwamba sisi kama Bunge, kwa wale ambao tutakuwa Wajumbe wa Bunge Maalum naamini kwamba watakuwa na uwezo wa kuyatafakari mambo yenye maslahi kwa Taifa. Miongoni mwao watakuwa ni Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar, lakini pia na Wabunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na yale makundi ambayo kwa fursa ambayo Watanzania wanapewa, tunaamini kwamba hilo Bunge halitakuwa mahali pa kupeleka watu wanaoenda kufanya majaribio. Watapelekwa watu ambao wanauelewa sawasawa kusaidia kuchambua, kupanga na kutengeneza mustakabali wa Taifa hili. Kwa hiyo, mimi sina mashaka na hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini yamesemwa hapa mambo, utaratibu huu kwa kweli wa Tume hizi zinavyofanya kazi, huwa unatokana na hadidu zake za rejea na watu wasipotoshe

wakadhani kwamba kwa wale wenye maono tofauti, wenye mawazo tofauti, wanaounga mkono kwamba ukomo wa Tume uishie hapa, sio kwa sababu tunaanza leo, zimekuwepo Tume nyingi ambazo zimekuwa zikiteuliwa na mamlaka, lakini kazi yake huwa zinakamilika zinapokabidhi zile taarifa za kazi ilizotumwa kufanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Watanzania wasijaribu kupotoshwa kwamba jambo hili ni kwa dhana pengine ya kuifikiria au kuwa na mtazamo hasi kwenye Tume hii, haiwezekani. Ile ni Tume ya Wazalendo, tunafahamu ni watu waliotumikia Taifa hili. Utakuwa ni mtu wa ajabu sana katika Taifa hili ambaye hatatambua kazi njema iliyofanywa na Tume hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, tunasema, kama ambavyo Kanuni ya 5 ya Kanuni zetu za Bunge, Bunge linaongozwa na Katiba, sheria na *best practices* katika nchi zingine, tunafahamu kazi za Tume zinavyokuwa. Napenda kusikiliza hasa wanaosema kwamba tukiuke taratibu zote hizi kwa ajili tu ya kuonesha kwamba sisi tuna mapenzi muafaka au ambayo yana-*justify* ongezeko la ukomo huu wangetushawishi, kuhusu uhalali wa jambo hilo kisheria, mazoea na hata kuepuka ile *conflict of interest* (mgongano wa kimaslahi). Kwa hiyo, mimi naomba Watanzania waelewe kwamba sisi hatuwezi kuwa watu wa kwanza kuishutumu Tume. Wale viongozi walioteuliwa kwenye Tume ile, Makamishna wale ni watu wanaotambulika na wana heshima zao katika Taifa hili, lakini kama Taifa tusimamie misingi ambayo tumejiwekea kwa ajili ya utawala bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, limesemwa jambo hapa kwamba mambo ya dharura haya yanatufanya wakati mwingine Bunge lako lionekane halifanyi kazi vizuri. Naomba niwarejeshe kwenye Taarifa ya Upinzani, ukurasa wa 11, kuna jambo ambalo si la kweli. Muswada unapoletwa kwa utaratibu wa Hati ya Dharura si kweli kwamba unaweza kusababisha sisi tusifikiri sawasawa. Ni upungufu wa sisi washiriki katika shughuli hii, ndiyo ambao unaweza

kusababisha wananchi kule wakatu-*judge* vingenevyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumeaminishwa hapa na Taarifa ya Kambi ya Upinzani, ukurasa wa 11, aya ya pili, kuna jambo linarejewa ambalo halipo. Aya ya pili inasema licha ya matakwa haya ya sheria kama ilivyo sasa, kifungu cha 32(2) cha Sheria hiyo kinailazimisha Tume kutoa elimu ya uraia na uhamasishaji na kuendelea. Ukisoma marekebisho ambayo yameletwa na Serikali hapa, tumeambiwa kabisa kwamba kifungu hicho hasa ukisoma ile kifungu cha 5 cha marekebisho, kifungu cha 31- 36 vimefutwa. Leo Taarifa ya Kambi Ramsi ya Upinzani inawahutubia Watanzania na ulimwengu mzima kwamba tunafanya jambo ambalo siyo la msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, simwoni Mheshimiwa Mbowe kama Kiongozi wa Kambi ya Upinzani, nataka niseme, Mheshimiwa Lissu ni naogopa, ni rafiki yangu kumwambia aliyoyasema ni mambo ya uwongo. Nachelea kusema kwamba ni upotoshaji kwa Bunge na Taifa kwa ujumla. Mheshimiwa Lissu ni rafiki yangu tulikuwa pamoja shuleni. Kinachonipa faraja, amesema hapa kwamba leo amekesha. Tuwaombe, nilishawahi kuwaonya na kuwakumbusha wenzetu wa Upinzani, mambo haya yanahitaji umakini, kuongoza Taifa ama kujadili mambo ya maslahi ya Taifa yanahitaji umakini na utulivu wa hali ya juu. Nakaribia kusema kwamba hii shughuli kwa baadhi ya Viongozi wenzetu wamekuwa wakifanya kama *one man show*. Haiwezekani Kambi Rasmi ya Upinzani yenye watu zaidi ya 30 inashindwa kutafakari marekebisho yanayoletwa na Serikali yenye vifungu vitano tu.

**SPIKA:** Wapo Wabunge tisini.

**MHE. WILLIAM M. NGELEJA:** Mheshimiwa Spika, wapo 90? Kwa hivyo, Watanzania tusipowakumbusha kwamba hii taarifa na vyombo vya habari mtusaidie, kifungu cha 33 kimefutwa na warejee hivyo. Kwa hiyo, kuwaaminisha Watanzania kwamba kwa sababu kuna kigezo cha kwenda

kutoa elimu ya uraia kwa wananchi, si sahihi kukirejea kabisa hapa ni makosa makubwa. Ni upotoshaji uliokubuhu, lakini kwa sababu tunatambua kwamba katika mambo haya wakati mwingine kuna kupitiwa ndiyo maana nikasema Mheshimiwa Lissu ni rafiki, siwezi kusema kwamba amepotosha Bunge, siwezi kusema kwamba anasema uwongo hapa kwa sababu sitaki kutumia neno la kuudhi lakini ukweli ni kwamba tunahitaji na tuna kila sababu ya kuwakumbusha Watanzania, yapo mambo ambayo tumekuwa tukitumia utaratibu huuhuu wa kutowafikishia ujumbe sahihi na hatimaye Taifa linafikia katika majaribu. Ninaomba sana wenzetu wawe makini katika hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho, Mheshimiwa Mbowe amesema maneno mazuri sana leo. Anafahamu na kutambua msingi mkubwa wa demokrasia kwamba unaachia wengi waamue lakini wachache wasikilizwe. Kauli kama hizi ndiyo tunataka kuzisikia katika mustakabali wa Taifa hili. Ni kipindi ambacho sisi kama Taifa tunatakiwa tusimame juu ya itikadi zetu za kisiasa, itikadi zetu za kidini na tofauti zetu za vipato na mambo mengine yanayofanana na hayo. Viongozi wa Kitaifa kama wataendelea kuwa na misimamo hii, tunahakika kwamba Taifa hili litaendelea kuwa tulivu na kuyafikia ambayo tunakubaliana kwa minajili ya matokeo mapana na faida kwa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, naunga mkono hoja hii, naomba tuendelee kulijenga Taifa letu kwa pamoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Lukuvi. Wazee wa *TCD* hawa. *(Kicheko)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii lakini labda niseme na-*declare interest* kwamba viongozi hawa wanapokutana na Mheshimiwa Rais baada ya hapo hoja zinapelekwa kwenye *Technical Committee* ambayo mimi ndiyo Mwenyekiti na hii ya juzi siyo mara ya kwanza, ni mara tatu nimekaa nao.

**SPIKA:** Hiyo mashine hatukusikii vizuri. Hata ukija hapa mbele sawa ili tusipoteze muda.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Spika, nataka kusema kwamba mimi ndio Mwenyekiti wa *Technical Committee*. Mara ya kwanza tulikutana, tukapitisha ile Sheria lakini baadaye walikuja Ikulu, kwa kawaida Ikulu huwa wanazungumza tu lakini hoja zile zinapelekwa kwa Kamati ya Wataalam. Kwa hiyo, sisi Serikali tuna Kamati yetu na wenzetu wana Kamati yao, tunakutana pamoja lakini mimi ndio Mwenyekiti na ndivyo tulivyofanya sasa.

Mheshimiwa Spika, tulipokutana safari hii, walikuja na hoja walizomwachia Mheshimiwa Rais. Nimeamua nifafanue kidogo kwa sababu kuna upotoshwaji ambao umefanywa na CHADEMA, Kambi Rasmi ya Upinzani. Wamewasilisha, Mheshimiwa Rais akasema utaratibu wetu unajulikana....

*(Hapa baadhi ya Wabunge Walionekana kama Kumpinga Waziri)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Aah, mimi sijui kama...

**SPIKA:** Mheshimiwa Lukuvi, mimi ndiye Mwenyekiti mbona naona unawasikiliza watu wengine?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE:** Basi naomba wanyamaze kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais alisema utaratibu unajulikana, wakakae kwenye *TCD* na *TCD* ina Viongozi wa Vyama vyenye Wabunge Bungeni akiwepo Kiongozi wa Chama cha Mapinduzi. Kwa hiyo, walipokutana walileta maandishi kwangu na yalisainiwa na Mheshimiwa Mbatia ambaye ndiye anakaimu Uenyekiti maana Mwenyekiti ni Mheshimiwa Augustine Mrema ambaye anaumwa.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)


Mheshimiwa Spika, haya maandishi yaliyoletwa na *TCD* ndiyo tuliyokaa kuyafanyia kazi. Huu ndiyo msingi wa kufanyia kazi. Kwa hiyo, naposema wanapotosha ni kwamba sababu za msingi tulizokuwa tunazingatia hoja hadi hoja ni hizi zilizoandikwa lakini tuliposhindana hapa, nashangaa leo wanataja sababu zingine.

Mheshimiwa Spika, kwanza, walizungumza habari ya kuongeza idadi kutoka 166 mpaka 438. Leo kuna marekebisho yanakuja na sababu iliyotolewa hapa ni kwamba kuweka sauti ya watu ambao siyo Wabunge kutoka taasisi za jamii ili kauli zao ziweze kusikika. Hata hivyo, sababu iliyokuwa mezani siyo hiyo! Sababu iliyobeba hoja hii ni kuweka usawa kati ya nchi mbili za Muungano na iko hapa, kwa kuzingatia dhana ya haki na hadhi sawa, ndiyo sababu iliyoletwa. Ndiyo maana walisema wanaomba Wajumbe 438 ili Zanzibar ipate 279, karatasi iko hapa na imesainiwa na Mheshimiwa Mbatia na wote tulikuwa tunatumia.

Mheshimiwa Spika, ndani yake, namshukuru sana Mheshimiwa Jussa nitoleeni salamu, Mheshimiwa Jussa ni muungwana sijawahi kuona. Sisi tukajua sababu iliyobeba Wazanzibar kuwa na hofu na namba hii ni kile kifungu cha upitishaji wa Katiba *(simple majority)*. Walitaka nafasi hizi ziwe nyingi ili angalau wasikwazwe katika kupitisha Katiba kwa *simple majority*. Tulipokuja kuafikiana, tuliposhauriwa na Mwanasheria Mkuu na Mwanasheria wa Zanzibar tuondoe kile kifungu cha *simple majority* tubakize hatua zote kwa *two third,* hii hoja ikaanza kukosa mshiko kwa sababu Wazanzibar waliona kwamba sasa haki yao italindwa kwa *two third*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hoja hii msingi wake ilikuwa ni kuweka nafasi sawa kwa washirika wa Muungano si haya ya leo, tutafute vyama sijui vya kijamii vipate sauti, hii inatungwa hapa. Haya ni mapya, hayakuandikwa hata katika mstari mmoja wa hapa. Mheshimiwa Mbatia yupo hapa na ndiye aliyesaini na Mheshimiwa Mnyika tulikuwa naye, hii ndiyo *document* tuliyoifanyia kazi. *(Makofi)*

*Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*


Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tulipofika mwisho tukakubaliana kama Wazanzibar kinga yao ni *two third* na *two third* inapatikana wakiwa kumi, wakiwa ishirini, wakiwa hamsini.

**MHE. EZEKIA D. WENJE:** Taarifa!

**SPIKA:** Tunataka kusikiliza *continuations* siyo malumbano. Mheshimiwa Wenje, nakuomba ukae kwa sababu tunasikiliza namna wanavyoeleza, ndiyo maana nasema sipendi *disturbance*. Mheshimiwa Waziri endelea.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, nasema hoja hii iliondoka tu kwa sababu Wazanzibar walielewa kwamba wingi si hoja ila kinga yao ni maamuzi na kinga yao ni *two third,* wakiwa ishirini, wakiwa 30, uamuzi wa kila hoja utaamuliwa kwa *two third* siyo kwa wingi wa mmoja mmoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nataka kusema, mwisho japo tulikuabliana kutokubaliana lakini *majority* pale tulikubaliana isipokuwa Mheshimiwa Mnyika, nataka kuwa mkweli. Mheshimiwa Mnyika mimi nampenda tofauti na, Mheshimiwa Tundu Lissu ni rafiki yangu sana nje lakini anayoandika huwa ni tofauti. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mnyika tulikuwa vizuri na ni kweli ndani ya kikao kile Mheshimiwa Mnyika aliondoka akipinga kifungu hiki, lakini makubaliano ya tulio wengi tulikubaliana tuongeze Wajumbe 35. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kimsingi hoja ya kuongeza idadi ilikuwa ni kubeba hoja ya usawa wa nchi mbili siyo hoja hizi zilizotolewa. Hata hivyo, ukitafakari kwa ndani, kuna hofu ya baadhi yetu kwamba kwa kuwa Wabunge wengi ni wa CCM na Baraza la Wawakilishi wengi ni wa CCM, basi hawa jamaa tuwa-*dilute* kwa kuongeza watu wengine huko nje ili angalau tuwe na uwiano, kuna

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)


hofu hiyo, haisemwi lakini ndiyo hofu yenyewe, haisemwi waziwazi.

**WABUNGE FULANI:** Aaaah!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Spika, sasa hiyo hatuwezi kulaumiwa sisi, walaumiwe watu waliotuweka hapa, waliopiga kura. Maana hatuwezi kulaumiwa sisi, hatukujiweka, leo tupo wengi, kesho tunaweza kuwa wachache, ndiyo misingi itaendelea kutumika hiyohiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka kusema kwamba tulifanya mkutano Dar es Salaam siku mbili, tukaafikiana ingawa Mheshimiwa Mnyika aliweka *scenario* yake, ilishuka kutoka 348 mpaka hii aliyoleta leo. Sisi watu wa Serikali tulikubaliana na walio wengi kwamba tuje na hii *scenario* ya 201.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuiandika, tulitumia uungwana tena, nikaona mmh, hawa jamaa tukipeleka huu Muswada bila ku-*proofread,* tukaitana wote Jumapili iliyopita. Tulipofika kwenye kikao, niliwagawia huu Muswada wa leo. Hawa *Members* wa *TCD* wakasema hapana, wewe Serikali ndiyo umeleta, acha sisi tuzungumze peke yetu. Wakakaa wenyewe kwenye chumba cha mikutano cha Waziri Mkuu, wakakubaliana waliyokubaliana. Tukaitwa watu wa Serikali, *Chief Whip* wa CUF akaanza kutusomea makubaliano, yote yaliungwa mkono isipokuwa mawili ambayo walishindana, walikuwa wawili kwa wanne. Walipiga kura wenyewe na hili ninaweza kulithibitisha kwa sababu ninayo *CD* ya mazungumzo yao. *(Makofi)*

**WABUNGE FULANI:** Aaah!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kusema tumejitahidi sana kufuata uungwana wa majadiliano ya pamoja. Sishangai kutofautiana, hili ni jambo la kawaida

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)


na simshangai Mheshimiwa Mnyika kuendelea kushikilia hoja yake kwa sababu ni kweli ameendelea kushikilia mpaka dakika ya mwisho lakini kama ilivyo kwenye majadiliano wengi wape. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, suala hili lilishakufa. Kwanza Mheshimiwa Jussa palepale alishaliua baada ya kuondoa ile *simple majority,* hii hoja ya kuwabeba Wazanzibar kwa idadi ikawa haina nguvu na ndiyo hoja iliyotumika.

Mheshimiwa Spika, hoja ya pili, ni kwa Tume. Tulikubaliana pale kwa sababu hata hapa inaonekana kana kwamba Bunge lile litakuwa kama kongamano hivi, kutakuwa na mtoa hoja halafu kutakuwa na mtu wa kutoa majumuisho. Sisi tukasema hakuna majumuisho kwenye Bunge, kila sura na kila hoja itaafikiwa kwa *two third*, kwa kura. Hawa wanakuja kutoa hoja ya nini hapa, hakuna majumuisho kwamba aje mtu wa Tume hapa atuambie *consensus* kwamba sisi tunavyoona ilikuwa hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tukakubaliana pale kwamba Bunge hili la watu 600 lina watu wenye uwezo kwa sababu hata hawa 30 wametoka miongoni mwa hao Watanzania na tumewaacha watu wengi sana kwa sababu watu walioomba pale walikuwa zaidi ya 500 na wakapatikana 30. Wapo watu wenye uwezo sana ambao wanaweza wakakaa, wakatafakari maoni ya wananchi. Tume hii ukisoma Sheria ilipewa kazi ya kukusanya maoni ya wananchi, haikupewa kazi nyingine zaidi ya hapo. Wamepita huko, wamerekodi, wametafsiri waliyotafsiri. Tukakubaliana pale hakuna sababu ya kuja hawa kutukalia shingoni kwamba lazima msome, tuwafundishe mpaka mfaulu huu mtihani, sisi siyo wanafunzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tukakubaliana kwamba Kanuni za Bunge, kwanza Bunge lenyewe linaweza likasema hatuwataki kaeni nje, lakini sisi tukakubaliana kwamba endapo watatakiwa wataitwa kwa ratiba itakavyokubalika kwa mujibu wa Kanuni za Bunge. Hapa tunamaanisha

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)


kwamba katika Bunge lile, uzoefu utakaotakiwa si kwa hawa Tume ya Tanzania tu, pengine Bunge lile linaweza likamtaka hata Prof. Shivji, mtu aliyebobea katika mambo ya Katiba yupo ndani ya nchi, kupata uzoefu labda Mwenyekiti wa Tume aliyesimamia mchakato kama huu Kenya au Zimbabwe, kwa nini tujifunge kwamba wasomeshaji wa Katiba hii ni lazima iwe Tume iliyovunjwa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tukakubaliana pale kwamba si lazima lakini kwa sababu kifungu kinaruhusu kuwaita baadhi yao na kwa kweli hata ukiangalia utakuta kwamba katika Tume ile ya watu thelathini, kuna watu ambao walikuwa *key* katika kutengeneza hii, si wote. Kwa hiyo, Bunge litaamua nani na nani limwalike kwa hoja gani, siyo lazima wote waje wakae hapa. Hata hivyo, sheria inatambua kwamba nyaraka zote za Tume zitakabidhiwa kwenye Bunge Maalum, vielelezo vyote, *recordings* zote, picha, *everything* vinakabidhiwa hapa. Hakuna sababu ya kufikiri kwamba hatutakuwa tunajua waliendeleaje kwa sababu vile vyote walivyotumia vinakuwa mali ya Bunge na sheria hii inakubali kwamba Watumishi wa Umma ndiyo watakaokuwa Sekretarieti. Maana yake ni pamoja na hata sehemu ya Sekretarieti ya Tume yenyewe, watatufunulia hivyo vitabu, kwa hiyo hoja ikafa.

Mheshimiwa Spika, nilitaka nisemee hizi hoja mbili lakini niwashukuru sana Viongozi hawa wa vyama, Mheshimiwa Mbowe nakushukuru sana, uliniona hapa nilikuwa na mashaka kidogo. Mheshimiwa Mnyaa nakushukuru sana lakini kwenye kikao kile namshukuru na Mheshimiwa Jussa. Mheshimiwa Mbowe unafanya vizuri sana kumtuma Mnyika, ni mtu ambaye anazungumza kwenye kinywa lakini lugha ya kiungwana. Nakushukuru sana Mheshimiwa Mbatia, nawashukuru sana viongozi wote walioshiriki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Rais kwa kukubali haya, nawapeni pole sana Wabunge na hongera maana tulipoachana hapa mmeitwa majina mengi lakini

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)


tupo hapa kutekeleza hili jukumu kubwa. Nawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nachotaka kumalizia ni kwamba wameuliza habari ya bajeti, fedha hizi zipo *budgeted*, ukiniambia leo kwamba hujui Mfuko Mkuu uko wapi na bajeti haipo, ipo! Tumepitisha hapa Mfuko Mkuu, zipo fedha nyingi lakini siyo kapu lisilo na matumizi, ni Mfuko Mkuu lakini una matumizi. Serikali inajua ni kiwango gani cha pesa zimetengwa kwa Bunge la Katiba na ndiyo maana tunafikiri haiwezekani kwenda zaidi ya 635 kwa sababu uwezo huo hautakuwepo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa msifikiri kwamba Mfuko Mkuu ni pesa huwa zinawekwa tu, hazijulikani kazi yake, hapana! Bajeti ipo, tukisema bajeti haitoshi, imepangwa kwa ajili hiyo na kweli ilipangwa kwa ajili ya watu 166 lakini kwa sababu ya *consideration* ya kujenga umoja wa nchi ndiyo maana Mheshimiwa Rais sisi tulimuona akakubali akaridhia kuongeza wajumbe 35. Kwa hiyo, tunamshukuru Rais hata kwa kuongeza idadi ya watu 35. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kulishawishi Bunge lako, ziko *amendments* hapa hazina mashiko kwa sababu, sababu zilizotolewa kwao hazifanani na sababu za msingi zilizoletwa kwenye vikao. Hoja ya kuongeza idadi kwa kutafuta huko watu ambao hawana dhamana ya watu, haina mshiko. Watu wana dhamana ya watu ambao wataulizwa na kuadhibiwa na kupongezwa kwenye Majimbo yao ya uwakilishi ni Wabunge, wapo hapa. Zoezi hili la kuandika Katiba, nani asiyejua ni la kisiasa, hivi tusipoandika sisi Wanasiasa, zipo nchi nyingine ambazo Mabunge peke yao bila ya kuongeza hata mtu mmoja wa nje wanatunga Katiba. Leo sisi tumefanya uungwana kuongoza watu 201! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la mwisho, nataka niwatoe hofu Mheshimiwa Ole-Sendeka na wengine kwamba tafsiri ya kikundi hiki, vikundi hivi si vyama, si chama kimoja kimoja au kundi, ni taasisi zinazofungamana katika eneo hilo yaani

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)


fungate hilo. Kwa sababu wenzetu katika ambatanisho lao walitaka tuteue katika taasisi 142, ndiyo kiambatanisho walicholeta. Sisi tukawaambia tumesajili taasisi 15,000, je, hawa wengine wakishtaki kwamba Rais amewaalika 142 na kuwaacha wengine itakuwaje? Hoja ikafa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana tukawa-*cluster* wale, lakini ile ni *cluster* ila mwaliko utatolewa kwa taasisi mojamoja. Tunaposema Taasisi za Elimu ya Juu au *NGOs* siyo kwamba zitakutana halafu ziteue watu wa kuomba, kila *NGO* na kila Taasisi ya Elimu ya Juu na kundi wataomba wenyewe. Tunazo Taasisi zilizosajiliwa Kiwilaya, Kimkoa, Kitaifa, mialiko itatolewa, Taasisi hizi zitatolewa, isipokuwa Taasisi zinazofanana kwa malengo yao ndiyo zitachambuliwa na kutolewa idadi iliyobaki.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na naomba Waheshimiwa Wabunge wote muunge mkono hoja hii. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwanza kabisa, napenda nitumie Kanuni ya 28(5), inayoniambia kama nitaongeza muda. Naongeza muda kwa sababu mbili. Kwanza, naomba hoja ya kwamba kesho tuweze kumalizia kazi hii lakini ya pili, tuna maelezo ya binafsi ya Mheshimiwa Zambi.

Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu hiyo, naomba niongeze kwa mujibu wa Kanuni ya 28(5). Kwanza, Mheshimiwa Waziri wa Nchi!

## HOJA YA KUTENGUA KANUNI ZA BUNGE

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 28(3) na (7), naomba kutoa hoja ili Bunge lako Tukufu liahirishwe kabla ya muda uliopangwa.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**WABUNGE FULANI:** Aaah!

**SPIKA:** Iko hiyo, lakini iko ile ya kwamba kesho tufanye kazi kwa kuwa ni siku ya Jumamosi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Waheshimiwa Wabunge, kama alivyosema Mheshimiwa Spika na kama alivyoelekeza, naomba kutoa hoja ili Waheshimiwa Wabunge mkubali Bunge lako Tukufu liweze kufanya kazi siku ya Jumamosi ili kukamilisha kazi iliyobaki.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Kwa hiyo, kesho tutafanya kazi na kama nilivyosema Muswada huu umeletwa kwa *Certificate of Urgency* lakini Muswada huu tuna mambo maalum ambayo tulifikiri katika *Certificate of Urgency* yaingie. Kwa hiyo, kesho si-*entertain* mtu mwingine kuzungumza, tunaingia moja kwa moja kwenye vifungu na wale wenye *amendment* zao wafanye kazi zao, tutaingia huko, hatuna sababu ya kupanua mazungumzo kwa sababu wale ambao tulitegemea walileta *amendments* zao wamepewa nafasi ya kuzungumza hapa lakini kesho tutaingia kifungu kwa kifungu. Kwa hiyo, tutaanzia hapo kesho, hatuendelei tena na mjadala.

Waheshimiwa Wabunge, sasa namwita Mheshimiwa Zambi kwa dakika kumi na tano.

## MAELEZO BINAFSI YA MBUNGE

### Maelezo Binafsi ya Mhe. Godfrey W. Zambi Kuhusu Bei Kubwa za Mashine za Kutolea Receipts' (*Electeronic Fiscal Devise Machines - EFDS*) Pamoja na Kero Nyingine Zinazosababishwa na Mashine hizo na Kero Kuhusu Kodi Nyingi

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kunipa nafasi ili niweze kutoa Maelezo yangu Binafsi mbele ya Bunge lako.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni 28(8) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Aprili, 2013, napenda kutoa maelezo binafsi kuhusu bei kubwa za mashine za kutolea risiti yaani *Electronic Feasical Device Machines* pamoja na kero nyingine zinazosababishwa na mashine hizo na kero kuhusu kodi kuwa nyingi na nalisema hili Mheshimiwa Spika, kwa sababu hali hiyo imejitokeza kule Mbeya na kulikuwa na vurugu sana ambazo zilijitokeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lengo la maelezo yangu ni kuitaka Serikali kwanza isitishe uuzwaji wa mashine hizo kwa bei za sasa na suala hilo liweze kuchunguzwa vizuri. Pili, kuwe na elimu ya kutosha kuhusu matumizi ya mashine hizo kwani inaonekana pia wafanyabiashara wengi hawajui matumizi mazuri ya mashine hizo kwa sababu ya kutokufundishwa vizuri. Katika maelezo yangu, naitaka Serikali ipitie upya Sheria zote za kodi ili kufanya marekebisho katika Sheria zitakazoonekana zina upungufu.

Mheshimiwa Spika, naomba ieleweke kwamba wafanyabiashara Mkoani Mbeya hawagomi kulipa kodi maana watu wanaweza wakatafsiri hivyo. Tatizo lililopo ni kwamba wafanyabiashara wale wanapinga bei kubwa ya mashine hizo lakini pia hawana elimu ya kutosha kwa ajili ya kutumia mashine hizo.

Mheshimiwa Spika, msingi wa maelezo yangu unatokana na hali iliyojitokeza Mkoani Mbeya mwanzoni mwa mwezi wa kumi mwaka huu na kwamba mnamo

tarehe 2/10//2013, wafanyabiashara wa jijini Mbeya, walikuwa wamepanga kufanya kikao katika Viwanja vya CCM pale Ilomba Mbeya na baadhi ya mambo yaliyokuwa yamepangwa kuzungumzwa ni haya yafuatayo:-

(i) Kujadiliana wao wenyewe na kupeleka Serikalini bei kubwa za mashine hizi za kutolea risiti hizi;

(ii) Gharama kubwa ya uendeshaji wa mashine hizo;

(iii) Elimu ndogo ya watumiaji wa *EDFs* hizo; na

(iv) Malalamiko ya kwamba kuna kodi nyingi wanazotozwa wafanyabiashara Jijini Mbeya.

Mheshimiwa Spika, hata siku moja kabla ya mkutano huo wa wafanyabiashara ambao ulikuwa umepangwa ufanyike tarehe 1/10/2013, Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Ndugu Abbas Kandoro aliitisha mkutano wa wafanyabiashara wa Mkoani Mbeya katika ukumbi wa *Mtenda Sunset*. Katika mkutano huo, Mkuu wa Mkoa pamoja na mambo mengine aliyozungumza na wafanyabiashara hao, bado hawakuweza kufika muafaka. Hivyo, Mkuu wa Mkoa aliwaahidi kwamba atayafikisha madai yao kwa Waziri Mkuu ili yatafutiwe majibu. Hivyo, Mkuu wa Mkoa aliwataka wafanyabiashara hao kutoendelea na mkutano wao uliokuwa umepangwa kufanyika siku ya tarehe 2/10/2013, kama nilivyosema hapo awali.

Mheshimiwa Spika, mkutano huu wa wafanyabiashara ambao ulikuwa na kibali cha Polisi uliahirishwa chini ya saa 12 tu. Hivyo wafanyabiashara hao walikubaliana kwamba mkutano wao uendelee kama ulivyokuwa umepangwa. Hivyo, siku ya tarehe 2/10/2013 maduka karibu yote hasa eneo la Mwanjelwa yalifungwa na wafanyabiashara wakaanza kuelekea eneo la mkutano kama walivyokuwa wamekubaliana.

Mheshimiwa Spika, kwa mshangao mkubwa sana, vilijitokeza vikosi vya Polisi na FFU wakaanza kuwatawanya wafanyabiashara hao, mabomu ya machozi yalitumika, kukatokea vurugu kubwa sana. Katika vurugu hizo, mtu mmoja aliumizwa sana, aidha, watu/wafanyabiashara 105 walikamatwa. Baada ya mahojiano, watu 59 waliachiwa na 46 walifikishwa Mahakamani na kesi bado iko Mahakamani. Kati ya watu 46 waliofikishwa Mahakamani, watu watatu walikosa dhamana na bado wako mahabusu na 43 wako nje kwa dhamana.

Mheshimiwa Spika, hapa si nia yangu kuzungumzia jambo ambalo liko Mahakamani ila nataka nitoe picha juu ya jambo hilo lilivyoshughulikiwa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, ni kweli Mkuu wa Mkoa alikutana nao akazungumza nao, lakini nao wakaona ni vizuri waendelee na mkutano kama walivyokuwa wamepanga. Kwa bahati mbaya sana, Serikali ya Mkoa ambayo ilikuwa imetoa kibali cha kufanyika mkutano huo iliamua tena ghafla kuahirisha mkutano huo! Unajiuliza hivi kama wangeachwa waendelee na mkutano wao hayo yaliyotokea yangetokea? Jibu ni rahisi tu yasingetokea.

Mheshimiwa Spika, huku ni kujenga mahusiano mabaya na jamii ya wafanyabiashara bila sababu. Katika hili Chama cha Mapinduzi kinalaumiwa bila sababu kwa maamuzi mabaya yanayofanywa na Viongozi wa Serikali bila kuzitafakari athari za maamuzi yao.

Mheshimiwa Spika, katika vurugu hizo pia mali ya baadhi ya wafanyabiashara pale Jijini Mbeya ziliibiwa. Pia matairi ya magari yalichomwa barabarani na hivyo kusababisha shughuli nyingi za kiuchumi kusimama. Aidha, maduka karibu yote ya Mwanjelwa na maeneo mengine Mkoani Mbeya yalifungwa kwa siku mbili yaani tarehe 2-3/10/2013. Hii ina maana kwamba hata nchi ilipoteza mapato, wafanyabiashara walipoteza mapato pamoja na kuwapoteza wateja wao. Hasara hii si ndogo ni kubwa na ambayo kama nilivyosema hapo juu ingeweza kuepukwa.

*[MHE. G.W.ZAMBI]*

Mheshimiwa Spika, mashine za kutolea risiti, *EDFs* huko nyumba zilikuwa zinauzwa Sh.2,000,000 kwa wafanyabiashara ambao mzunguko wa biashara zao unafika Sh.14,000,000 kwa mwaka na hii ni kwa mujibu wa Sheria. Hata hivyo, wafanyabiashara walikuwa wakilalamikia bei hizo na kwamba ni kubwa. Baada ya malalamiko ya muda mrefu, *TRA* ilipunguza bei hizo hadi kufika Sh.800,000. Msingi wa malalamiko ilikuwa ni kwamba huko zinakotoka hususan China, Dubai na Japan, zinauzwa kati ya dola za Kimarekani 60 hadi 150 wastani wa shilingi 75,000 hadi 300,000 za Kitanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kuthibitisha kwamba mashine hizo zina bei kubwa kwa Tanzania, *TBC Taifa* (Redio ya Taifa) kupitia kipindi chake cha asubuhi hii kilichoendeshwa na Ndugu Lutengano Haonga, tarehe 6 mwezi Novemba, Watanzania wengi waliopiga simu walalamikia bei kubwa za *EDFs* hizo pamoja na elimu ndogo kwa watumiaji wa mashine hizi yaani wafanyabiashara. Nina hakika baadhi ya Wabunge mlisikia kipindi hicho, Watanzania wengi wakilalamikia mambo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa nini uhalali wa kuuza kwa Sh.800,000/= hadi 1,500,000/= za Tanzania! Je, kama siyo kuwaibia wafanyabiashara wa Tanzania, bei hizo zinatoka wapi? *(Makofi)*

Mheshimmiwa Spika, baada ya kupata malalamiko ya wafanyabiashara wa Mbeya ambayo naamini pia ni malalamiko ya Watanzania wengi wafanyabiashara, niliamua kuutafuta ukweli. Mwishoni mwa mwezi uliopita nilisafiri kwenda Dubai na namshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu aliniteua nikaongozana naye na China; ambako nilikuta mashine hizo *(EFDs)* zinauzwa kwa USD 60-150 kutegemeana na aina ya mashine na ubora wake. Hapa niliamini kwamba malalamiko ya wafanyabiashara ni halali kabisa na yana msingi. Kwa vyovyote vile kwa kuwa hao Wazabuni wa *TRA* wanapoagiza mashine hizo huchukua mashine hizo kwa wingi na kwa vyovyote vile hununua chini ya bei hizo. Sasa unamuuzia Mtanzania huyu kwa bei hizo

kubwa, nataka niamini huku ni kuwaibia Watanzania hawa maskini wafanyabiashara ambao kimsingi walipaswa wauziwe kwa bei nzuri. Najiuliza chombo kinachojiita rafiki wa wafanyabiashara kwa nini kifanye mambo hayo? Mimi nadhani hapa siyo urafiki bali *TRA* inajenga mahusiano mabaya na wafanyabiashara. Kwa kweli huu ni wizi mkubwa na wizi wa waziwazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni vizuri pia tuelewe kwamba Wazabuni hao kwa habari zilizopo ni kwamba hawatozwi kodi wanapoingiza mashine hizo nchini. Kwa maana hiyo, wao hupata faida ya wastani wa Sh.500,000 kwa mashine moja tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, yapo maneno kwamba iko *syndicate* kati ya baadhi ya wafanyakazi wasiowaaminifu wa *TRA* walioungana na wazabuni wa mashine hizo katika kuiibia Serikali. Siyo kwamba *TRA* imetoa zabuni hizo bila kujua bei za mashine hizo, wanajua ila wanatumia nafasi hiyo kuhujumu uchumi wa nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivi ninavyoleta maelezo haya, *TRA* imetoa *ultimatum* kwamba wafanyabiashara wote ifikapo tarehe 15/11/2013 lazima wote wawe wamefunga mashine hizo kwa bei hizohizo vinginevyo biashaa zao zitafungwa na wanalazimisha kwa sababu nataka niamini kwamba wanaona wanapata faida na wao kwenye mashine hizo.

Mheshimiwa Spika, ziko gharama pia kubwa sana za kuendeshaji wa mashine hizo. Kwa mfano, mashine inapoharibika anapoitwa fundi aliyeifunga lazima alipwe Sh.25,000/= na hizi hulipwa na mfanyabiashara. Pili, karatasi ambazo hutumika kwa ajili ya mashine hizo kutolea risiti moja tu, karatasi *peace* moja tu ambayo inatoa wastani wa risiti 12 inauzwa Sh.2,000. Kwa maana hiyo, kama mfanyabiashara huyu atapata wateja mathalani 48 kwa siku maana yake atahitaji karatasi za A4 sita mara shilingi hizo 2,000 kwa muda wastani wa siku 22 anazofanya biashara kwa mwezi, atalazimika kutumia Sh.264,000 kwa ajili ya

kununua karatasi za risiti peke yake. Hii ni gharama ya karatasi peke yake bado mashine hizo hutumia wino na bado hizo ni gharama zingine. Unajiuliza wafanyabiashara wangapi wanafanyabiashara kwa faida?

Mheshimiwa Spika, mawakala wa *TRA* wanaofundisha wafanyabiashara namna ya kutumia mashine hizi hupata mafunzo kwa wastani wa miezi mitatu hadi sita. Hata hivyo, wafanyabiashara hufundishwa matumizi ya mashine hizo kwa muda wa kati ya siku mbili hadi tatu. Yaani ukipewa hiyo mashine unafundishwa matumizi yake kwa wastani wa siku mbili au tatu wakati mawakala wa *TRA* wanaowafundisha wao hupata mafunzo kwa wastani wa miezi mitatu hadi sita. Tunategemea nini hapa? Watapatauelewa wa kweli katika mazingira hayo? Hivyo unaona kabisa muda wa kufundishwa matumizi ya *EFDs* hautoshi.

Mheshimiwa Spika, mfanyabiashara anapokosea kuandika risiti, risiti moja tu unapoikosea kwa mfano risiti ya shilingi elfu moja ikaandikwa vibaya, mfanyabiasara anapigwa faini ya shilingi milioni tatu. Sina hakika kama Bunge lilitunga Sheria hiyo ambayo kosa na adhabu haviendani kabisa. Sheria za namna hiyo, haziwezi kujenga urafiki wa *TRA* na mlipa kodi hata siku moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hapa kuna mambo mawili, moja elimu zaidi itolewe kwa wafanyabiashara wanaotumia mashine hizo. Pili, Sheria zote ambazo zinajenga mahusiano mabaya kati ya *TRA* na mlipa kodi ziwe zinaangaliwa mara kwa mara.

Mheshimiwa Spika, yapo malalamiko pia makubwa kwa wafanyabiashara wa Jijini Mbeya kuhusu kodi nyingi wanazotozwa. Kwa mfano, kodi chache tu:-

(i) Kodi ya leseni (kwa mfano Fundi Cherehani hulipa Shs 80,000/= kwa leseni, bado hajalipa kodi ya mapato).

*[MHE. G.W.ZAMBI]*

(ii) Kodi ya Mapato.
(iii) Kodi ya Taka.
(iv) Kodi ya *Fire extinguisher.*
(v) Kodi ya Service Levy.
(vi) Kodi ya TFDA.
(vii) Kodi ya mabango.
(viii) Kodi ya maneno n.k.

Mheshimiwa Spika, hapa nisikitike sana kwa mfano kodi ya maneno yanayoandikwa ukutani mwa duka, zipo taarifa kwamba neno moja linatozwa ada ya shilingi elfu moja, neno moja. Kwa hiyo, ina maana kama umeandika maneno 50 kwenye duka lako maana yake utalipa kodi ya Sh.50,000.

Mheshimiwa Spika, hizo ni baadhi ya kodi ambazo mfanyabiashara hulipa. Unajiuliza je mfanyakazi wa Serikali, Wabunge na kadhalika hukatwa kodi nyingi hivyo kwenye mapato yao? Kwa vyovyote vile wafanyabiashara wa Mbeya wanayo hoja ya msingi.

Mheshimiwa Spika, yafuatayo ni mapendekezo yangu:-

(i) Serikali iagize *TRA* isimamamishe mara moja zoezi la kuwauzia wafanyabiashara mashine za *EDFs* kwa bei za sasa kwani ni kubwa sana ukilinganisha na bei za kule zinakotoka. Hivyo badala ya kufunga biashara zao kwa wale ambao watakuwa hawajafunga *EDFs* ifikapo tarehe 15 Novemba, 2013 kama walivyoagiza *TRA* basi utaratibu wa kulipa kodi wa zamani uendelee kutumikia hadi hapo suala la bei kubwa za *EFDs* litakapokuwa limetafutiwa ufumbuzi. *(Makofi)*

(ii) Serikali ichunguze kwa nini *TRA* inaingia mikataba inayotia mashaka kama mikataba ya ununuzi wa *EFDs* na ilete taarifa Bungeni mapema inavyowezekana.

(iii) TRA yenyewe inunuwe mashine hizo na kuwapa wafanyabiashara ili wazitumie kukusanya pesa ya

Serikali badala ya kuwatumia wazabuni ambao wanaziuza kwa bei kubwa sana.

(iv) TRA ifanye mchakato wa kutosha kujua ni nani hasa anayestahili kuwa na mashine za *EFD's*. Kwa mujibu wa Serikali anayestahili kutumia mashine hizo ni yule ambaye mzunguko wa fedha kama nilivyosema hapo awali unafika Sh.14,000,000 kwa mwaka. Jambo hili lilishtua wafanyabiashara wengi Mkoani Mbeya, akina mama lishe, wamachinga, akina mama wauza mchele na kadhalika, kwani kwa maelezo ya *TRA* ni kama wote mzunguko wa biashara yao unafika Sh.14,000,000, ni jambo ambalo sitaki kuamini. Hivi mama anayeuza mchele mashineni mwenye mtaji wa shilingi milioni moja ukimtaka alipe shilingi laki nane kwa ajili ya *EFD's* anabaki na nini? *(Makofi)*

(v) Itolewe elimu ya kutosha kwa wafanyabiashara ambao wanatumia *EFD's* na wale watakaozitumia baadaye, elimu isiwe ya siku mbili tu.

(vi) Sheria zote za kodi pamoja na adhabu zake zitazamwe upya lakini pia Maafisa wa *TRA* waache kauli za kejeli kwa Bunge kwani kila wafanyabiashara wanapohoji kuhusu Sheria mbalimbali za Kodi hujibu kwamba hilo ndiyo Bunge lenu linavyotunga Sheria na sisi kazi yetu ni utekelezaji. Hali hii hujenga chuki kati ya wananchi na Bunge lao na hali hii imenikuta mimi kwani kuna Maafisa wa *TRA* ambao walisema Sheria zinatungwa na Bunge kwa hiyo sisi kazi yetu ni utekelezaji.

(vii) Viongozi wa Serikali katika ngazi mbalimbali kuanzia Wilayani, Mkoa na Taifa wawe makini katika kutoa matamko yanayoweza kuleta madhara katika jamii. Hali iliyojitokeza Mbeya tarehe 2/10/2013 iliyolazimisha Jeshi la Polisi kutumia nguvu kubwa kuwatawanya wafanyabiashara haikuwa na sababu. Madhara yaliyojitokeza yangeweza kuepukwa kama wafanyabiashara wangeachwa waendelee na mkutano wao kwani haukuwa na madhara yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 28 (8) ya Kanuni za Bunge Toleo la Aprili, 2013, Serikali hailazimiki kujibu maelezo yangu. Hata hivyo, kutokana na hali halisi ilivyo Mbeya leo yaani mahusiano mabaya ya wafanyabiasha na Serikali/TRA na naamini wafanyabiashara wengine nchini kote na kwa kuwa Serikali ya CCM ni sikivu kwa wanachi wake basi nashauri Serikali ijibu maelezo yangu ili wafanyabiashara waweze kufanya biashara katika mazingira ya utulivu zaidi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**WABUNGE FULANI:** Safi sana.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nina matangazo mawili. Kwanza kabisa Waziri wa Maji alikuwa ameahidi kwamba kabla hatujaondoka atatoa kijitabu ambacho kitaelezea miradi yote ambayo ilipitishwa na Bunge wakati wa Bajeti. Sasa, tutaweka kwenye *pigion holes* maana tunajua kuna wengine wanachukua kuna wengine wanaacha. Afadhali mkiacha kwenye *pigion holes* tutazikusanya wenyewe tutaviweka, maana ni vitabu vizuri tu, kuliko mchukue hapa mkaviacha mahali popote, hapana. Kwa hiyo, tutaviweka kesho asubuhi, mtu yeyote anayetaka atakiona kwenye *pigion holes* yake, kitabu kama hiki. Tunavyo vitabu 450, vitatosha kwa Wabunge wote kwa sababu tutaweka kimoja kimoja. Kwa hiyo, kesho msiondoke bila kuviona kwenye *pigion holes* zenu.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Aaah, tafadhali naomba, tafadhali mimi nazungumza.

Halafu kesho pia tunangaza kwamba imeandaliwa tafrija kwa Wabunge wote na wafanyakazi ili kutafakari zaidi masuala mtambuka baada ya kumaliza mkutano wa kumi na tatu wa Bunge. Tafrija hiyo itafanyika kesho tarehe 9/11/

2013, saa 12.30 katika viwanja vyetu vya Bunge. Kwa wale ambao mtakuwa hamjasafiri basi mnakaribishwa. *(Makofi)*

Halafu tuna tangazo lingine, Wabunge ambao wanatoka kwenye Mikoa inayolima pamba, nimeagizwa nitangaze kwamba watakuwa na kikao chao baada ya mimi kuahirisha hapa. Mikoa yote inayolima pamba mtakuwa na mkutano Pius Msekwa na Waziri wa Kilimo atakuwepo. Mtajadiliana naye kuhusu mustakabali wa mambo mnavyofanyia kazi.

Mheshimiwa Ole-Sendeka!

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kuniona. Nimesimama kuomba Mwongozo kwa mujibu wa Kanuni ya 68(7) na Kanuni ya 5. Kanuni ya 5 inasema, katika kutekeleza majukumu yake yaliyotajwa katika Ibara ya 84 ya Katiba, Spika ataongozwa na Kanuni hizi na pale ambapo Kanuni hazikutoa Mwongozo basi Spika atafanya kazi kwa kuzingatia Katiba, Sheria nyingine za nchi, Kanuni nyingine zilizopo, maamuzi ya awali ya Maspika wa Bunge pamoja na mila na desturi za Mabunge mengine yenye utaratibu wa Kibunge unaofanana na utaratibu wa Bunge la Tanzania.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa naweka msisitizo tu, maamuzi ya Maspika wa Bunge pamoja na mila na desturi, hasa maamuzi ya Maspika.

Mheshimiwa Spika, nimesema nisimame kukuomba kwa ajili ya hoja iliyokuwa imewasilishwa na Mheshimiwa Godfrey Zambi kwamba kwa mujibu wa Kanuni zetu huwezi kuendelea kuijadili hoja ile. Hata hivyo, kuna hoja ya msingi yenye maslahi kwa Taifa ambayo imewasilishwa hapa na kwa uzoefu wa Bunge hili katika hoja iliyokuwa inahusu Maelezo Binafsi ya Mheshimiwa Kaika S. Telele ilikuwa imewasilishwa hapa ndani ya Bunge, tuliomba Spika atumie mamlaka yake ili kuielekeza Kamati ya Kisekta na wakati ule Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira kulitazama jambo lililokuwepo katika operesheni iliyofanyika kule Loliondo.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)


Mheshimiwa Spika, kwa kuwa jambo hili ni jambo la msingi na Bunge lako linaahirishwa kesho, nilikuwa naomba utumie mamlaka yako uliyonayo ikiwezekana kutoa maelekezo kwa Kamati ya Kisekta kushughulikia jambo hili la msingi alilolizungumza Mheshimiwa Godfrey Zambi, ili kuweka uwazi zaidi katika mambo hayo ambayo yamezungumzwa na hasa kufichua ufisadi ulioko *TRA* ambao ni mzigo mkubwa kwa taifa letu na ikibidi Kamati ya Kisekta baada ya kubaini ukweli, iweze kutoa maelekezo, ushauri kwa Wizara husika kuchukua hatua stahiki ili kunusuru hasara kubwa na chuki inayoaanza kujengeka miongoni mwa wananchi, wafanyabiashara na Serikali yao.

Mheshimiwa Spika, naomba tu Mwongozo wako kama unaweza kutumia nafasi yako. *(Makofi)*

**SPIKA:** Kabla ya Maelezo Binafsi ya Mheshimiwa Zambi, kulikuwa na mashauriano makubwa sana na Serikali na ndiyo maana tukakubali kwamba hili suala alitoe na mimi binafsi nimeshaelekeza Kamati yangu ya Bajeti kwa sababu vitu kama hivi vinaweza kupunguza mapato na kupunguza imani ya watu, kwa hiyo, nayo pia itafanya kazi hiyo. Kwa hiyo, hili suala tutalifanyia na nimeshawaandikia. Kuna mambo mengi kuhusiana na kutumia haya masuala ya *electronics,* yanaleta matatizo katika *revenue.* Kwa hivyo, ndivyo itakavyofanyika. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hivyo, nashukuru kwa kazi nzuri mliyofanya na mimi nimeamini kwamba Wabunge mkipenda, mnaweza kufanya kazi kubwa sana hasa katika suala zima la kuliongoza Taifa katika amani na utulivu. Maana mambo yote yanalipukaga humu. Nasema Mwenyezi Mungu katujalia sisi tumeweza kufika hapa. Tumechaguliwa na wananchi wengi tu, sidhani kama kuna mtu kachaguliwa na chama chake hapa, tumechaguliwa na wananchi kwa imani. Kwa hiyo kwa imani hiyo hiyo, kweli nasema tumwogope na Mwenyezi Mungu. Tuibebe katika shughuli nzima ya mchakato wa Katiba mpaka mwisho kusudi Watanzania wapate kitabu chao ambacho watakiamini. Mimi nasema kama mtaweka

mambo yenu ya hisia ya vyama, mtakosea na mtakuwa mmewakosea Watanzania. Wanaamini kabisa waliowachagua hapa ninyi wote ni *brain* kama ni *brain* tuandike Katiba sio vinginevyo. Mimi kubishana mpaka asubuhi sioni tatizo, maana ndiyo uhai wenyewe, mnabishana vizuri kwa heshima. Sio kubishana mnarushiana maneno aaah siyo sahihi.

Kwa hiyo, mimi naamini kabisa kesho tutaendelea na Muswada wetu vizuri, mshauriane na msiondoke na chuki kwa sababu ya maneno ya humu ndani. Mtu hapa ana haki, amesimamiwa na Katiba, Ibara ya 100 anaweza akasema mradi huvunji sheria, mkitoka hapa wengine wanaanza kununiana nje, *why?* Hiyo ni upungufu wa kisiasa. Hamwezi mkafanya mambo huku mkaenda kukunjana miguu huko nje, siyo sahihi. Kwa hiyo, zungumzeni kwa upendo hata kama una nguvu sana kwenye kutoa hoja ni sahihi tu lakini kwa upendo kwa kuwa tuna nia yetu ya kuwa na kitabu chetu kimoja, Katiba ambayo itapendwa na Watanzania.

Namshukuru sana Mheshimiwa Mbowe, umeonyesha *leadership.* Namshukuru Mheshimiwa Mnyaa, mmeonyesha *leadership*. Mheshimiwa Mdogo wangu Mbatia nakushukuru, umeonyesha *leadership* na ndiyo tunavyotakiwa tufanye. Kweli kabisa tutoe heshima kwa nchi yetu, hatuna sababu ya kuingia kwenye mikorogano yoyote ile. Tunapobishana tubishane tu, ndiyo maana ya Bunge. Bunge ni kubishana kwa hoja tu basi ndiyo maana ya Bunge. Nawashukuru, leo nimeridhika sana, nimefurahi sana.

Kesho tutaendelea kama nilivyoeleza, hatutafungua mjalada. Mtoa hoja atafunga kwa kuhitimisha hoja yake halafu tutaingia kwenye vifungu kwa sababu tuna kazi nyingine zitakazofanyika kesho.

Baada ya kusema hayo, naomba kuahirisha kikao cha Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi. *(Makofi)*

*(Saa 2.01 Usiku Bunge liliahirishwa Mpaka Siku ya Jumamosi, Tarehe 9 Novemba, 2013, Saa Tatu Asubuhi)*